**19 APRILI, 2024**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Kumi – Tarehe 19 Aprili, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Maswali, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Nicodemas Maganga.

Na. 118

### Ujenzi wa Barabara Zinazofadhiliwa na Benki ya Dunia – Mbogwe

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA** aliuliza:-

Je, lini barabara za lami zinazofadhiliwa na Benki ya Dunia zitaanza kujengwa Mbogwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ambazo zitajengwa kwa kiwango cha lami kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia Mradi wa *RISE* katika Wilaya ya Mbogwe zina jumla ya urefu wa kilometa 102. Barabara zitakazojengwa kwenye Mradi huo ni Masumbwe – Iponya - Nyashimba (kilometa 20), Lulembela – Kiseke – Isebya (kilometa 17), Mkweni – Nhomolwa - Nyanhwiga (kilometa 21), Ishigamva – Busabaga – Ilolangulu (kilometa 14) na Ivumwa – Ushirika - Shibutwe (kilometa 30).

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huu utafanyika kwa awamu, ambapo awamu ya kwanza itahusisha ujenzi wa Barabara za Masumbwe – Iponya – Nyashimba (kilometa 20), Lulembela – Kiseke – Isebya (kilometa 17), Ishigamva – Busabaga – Ilolangulu (kilometa 14) na Mkweni – Nhomolwa – Nyanhwiga (kilometa 21). Aidha, kazi za usanifu wa barabara za awamu ya kwanza zilianza Januari, 2024 na zinatarajiwa kukamilika Agosti, 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kazi ya usanifu wa barabara kukamilika Serikali kupitia *TARURA* itatangaza zabuni na kumpata mkandarasi wa kujenga barabara za awamu ya kwanza kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maganga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Swali la kwanza; kwenye Wilaya ya Mbogwe kuna hizo barabara alizozitaja Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna madaraja ambayo hayapitiki kabisa sasa hivi pamoja na kwamba nashukuru kwa majibu ya Serikali. Je, Serikali ina mpango gani wa kulitengeneza na Daraja la Ikalanga – Ilangale kwa sababu sasa

hivi haipitiki na wakulima wamelima mazao mengi ambayo yanatarajiwa kutoka huko?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; mpango wa Serikali wa kuunganisha kwa kiwango cha lami wilaya na mkoa. Je, ni lini sasa Serikali itaitimiza ahadi hii ili kuunganisha Wilaya ya Mbogwe na Geita kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la kwanza Mheshimiwa Mbunge, naomba nitumie nafasi hii kumwagiza Meneja wa *TARURA* katika Wilaya ya Mbogwe ili aweze kwenda kufanya tathmini na kubaini kwamba barabara hiyo inahitaji kupatiwa fedha za dharura kwa ajili ya kuirekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili la kuunganisha wilaya na mkoa, tutaendelea kufanya tathmini na kuzingatia uhitaji na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Atupele Mwakibete, kwa niaba yake Mheshimiwa Chumi.

Na. 119

**Ujenzi wa Daraja la Nsanga – Kiteputepu Busokelo**

**MHE. COSATO D. CHUMI K.n.y. MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja la Nsanga – Kiteputepu katika Kata ya Ntaba – Busokelo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja la Nsanga linaunganisha Kata ya Ntaba upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo na Kata ya Ipinda upande wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela. Daraja hilo hutumiwa na wakulima wa mpunga na kokoa kutoka mashambani kwenda kwenye masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali kupitia *TARURA* imetenga shillingi 500,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa daraja la kudumu la zege katika sehemu hiyo ambapo kwa sasa kuna kivuko cha waenda kwa miguu ambacho kinatumika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Mwakibete, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; tunaishukuru Serikali kwa kutenga fedha hizo kwa ajili ya kujenga daraja hili, lakini kutenga ni jambo lingine, kuanza ujenzi ni jambo lingine. Je, lini ujenzi utaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa katika Halmashauri ya Mji wa Mafinga kuna daraja kama hilo kutoka upande wa Isupilo kwenda Itimbo kufupisha njia ya watu wanaokwenda Iringa na kusafirisha mazao ya misitu. Je, Serikali iko tayari wakati ujao kututengea fedha ili na sisi tujenge daraja hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza ni kwamba, fedha imetengwa na dhamira ya Serikali ni kutekeleza miradi kwa kadiri bajeti inavyokuwa imetengwa. Kwa hiyo kwa kadiri fedha itakapokuwa inapatikana daraja hili litajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili la kuhusiana na daraja katika jimbo lake. Nimwambie pia kazi kubwa ya *TARURA* ni kufuatilia na kuangalia sehemu zenye mahitaji na kupanga vipaumbele. Kwa hiyo kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha na kwa kuzingatia vipaumbele daraja hilo litajengwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa daraja linalounganisha Kata ya Nkilizya na Kata ya Bukongo Jimboni Ukerewe limekuwa ni kilio cha muda mrefu na limekuwa linaathiri sana uchumi wa wananchi wa maeneo haya. Je, ni lini sasa daraja hili litajengwa kupitia Kijiji cha Msozi na Nkilizya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa miundombinu hii na kwa kuzingatia vipaumbele na upatikanaji wa fedha Serikali itajenga miundombinu hii kwenye jimbo la Mheshimiwa Mbunge. Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri Daraja hili la Kiteputepu ni daraja ambalo linatumia mbao, linacheza na maji ni mengi sana. Wamesema kwamba wametenga na wataweka bajeti ili waweze kulifanyia kazi. Tunaomba Serikali ifanyie kazi haraka kwa maana wanawake wengi wanazama katika daraja hili pale Ntaba.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napokea maombi ya Mheshimiwa Mbunge, tutayachakata na nitarudisha mrejesho kwake Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

Na. 120

**Kutumia Wataalamu kwenye Miradi ya *Force Account***

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kutumia wataalam wa ujenzi kwenye Miradi ya *Force Account* hata ikiwa kwa mikataba?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inazingatia miongozo iliyopo kwenye kutekeleza kazi za ujenzi wa miradi kwa kutumia njia ya *force account* ili miradi hiyo iweze kutekelezwa kwa ubora na ufanisi mkubwa. Aidha, Serikali imekua ikiwatumia wataalamu wa ujenzi kwa mikataba na waajiriwa wa halmashauri ili kuhakikisha miradi inayojengwa kwa *force account* inakua bora na imara.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kaijage.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, je, Serikali sasa haioni kuwa kuna haja ya kutumia wahitimu waliohitimu ufundi katika Miradi ya *Force Account?*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Serikali haioni kuwa, kuna haja ya kushirikiana na taasisi za ufundi ili kusimamia miradi ya *force account* badala ya kutumia watumishi ambao hawana fani hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokea mawazo ya Mheshimiwa Mbunge, tutachakata maoni yake na tuone tunaweza vipi kuboresha ufanisi katika utekelezaji wa miradi hii.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga.

Na. 121

**Mpango wa Kuanzisha Vituo Maalum vya Uwekezaji na Masoko ya Wanawake**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanzisha utekelezaji wa mpango wake wa kuanzisha vituo maalum vya masuala ya uwekezaji na masoko kwa wanawake kila kata?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya *EPZA* imetenga maeneo kwa ajili ya kuanzisha kanda maalum za kiuchumi katika mikoa mbalimbali nchini. Lengo kuu la kuanzisha maeneo haya ni kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya kuongeza thamani mazao mbalimbali yanayozalishwa nchini na kukuza mauzo ya nje ya bidhaa za viwandani na pia kuzalisha bidhaa zinazoagizwa nje kwa soko la ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza maeneo haya kuna sehemu zitatengwa kwa ajili ya wajasiriamali wadogo na wa kati *(SME's)* wakiwemo wanawake na vijana ili waweze kuanzisha viwanda vya kuchakata na kutengeneza bidhaa mbalimbali kwa ajili ya soko la ndani na nje. Aidha, maeneo haya yatatumika

kama *incubators* kwa maana ya atamizi ili kukuza wajasiriamali wadogo. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Elias.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali haioni umuhimu wa kuwasaidia wanawake wajasiriamali wanaofanya biashara pembezoni mwa barabara hususan wale wanaokuwa na watoto wadogo kwa kuwatafutia maeneo ya muda wa kati wanasubiri kuwatengea maeneo husika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, ni lini sasa kituo cha uwekezaji kitaona umuhimu wa kuwasaidia kutengeneza program ndogondogo kwa ajili ya wajasiriamali wadogo hususan wanufaika wa mikopo ya Serikali ili fedha zile ziweze kurudi kwa kuwekezwa sehemu sahihi na kuwaonesha fursa zinazowazunguka katika maeneo yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna changamoto kubwa ya maeneo ya ufanyaji biashara hasa kwa akinamama wajasiriamali wadogo na vijana ambao wanauza biashara ndogondogo na wengi wanatumia maeneo ya barabarani au kando ya barabara kuuza bidhaa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshaanza kutenga maeneo kwenye halmashauri na miji ambako tunahamasisha hawa akinamama na wengine ambao hawana maeneo maalum ili waweze kufanya biashara zao katika maeneo hayo ambayo ni salama na sahihi kulingana na ubora hasa kwenye vyakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kituo chetu cha uwekezaji kimekuwa kikitoa vivutio maalum kwa Watanzania na hasa kikilenga wajasiriamali au wafanyabiashara wanawake na vijana. Ndiyo maana kupitia *program* hii ya kuwezesha akinamama na vijana, Mheshimiwa Rais ameanza kuja na mpango maalum ambao kupitia mikopo hii ya 10% itakuwa ni sehemu ya kichocheo cha kuwasaidia akinamama hao ili wapate fursa za kuwekeza na kukua zaidi katika biashara zao. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Oran Manase Njeza.

Na. 122

**Fursa na Changamoto za Biashara ya Kaboni**

**MHE. ORAN M. NJEZA** aliuliza:-

Je, kuna fursa na changamoto gani kwa Tanzania kushiriki kwenye biashara ya *carbon*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna fursa kubwa ambayo Tanzania inanufaika katika biashara ya kaboni. Fursa ya kwanza ni uhifadhi wa baioanuai na pili, ongezeko la pato la Taifa. Hivi karibuni halmashauri mbalimbali zimepokea fedha zilizotokana na

biashara ya *carbon* kutoka katika kampuni mbalimbali ambazo zinatumika kujenga miundombinu ya kusaidia jamii katika halmashauri mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na fursa zilizopo bado kumekuwa na changamoto kadhaa katika biashara ya kaboni. Kwanza ni uelewa mdogo wa jamii katika utekelezaji wa biashara ya kabon na pili ni uwazi wa biashara ya kaboni katika soko la dunia. Pamoja na changamoto hizo, Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi kwa wadau wote ili kuhamasisha uwekezaji wa miradi ya biashara ya kaboni katika sekta mbalimbali pamoja na biashara ya kaboni kwa wadau mbalimbali ili kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu biashara hii, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Njeza.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali.

Swali la kwanza; sasa kutokana na hizo changamoto alizozisema Mheshimiwa Waziri kuna makubaliano ya Paris na *Article 6,* imewezesha nchi kwa nchi kufanya biashara na nchi nyingi zikiwemo Nchi za Afrika Mashariki zimefaidika kupitia hilo. Wenzetu majirani wameweza kuwekeza kwenye hekta 100 na wamezalisha ajira takriban 200,000. Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia Soko la Mitaji *(Capital Market Authority)* ili iweze kuweka *regulation* na kuweza kuleta wawekezaji kutoka nje ambao wako tayari kuja kuwekeza hapa kwetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa sababu imeonesha kuwa uwekezaji katika biashara ya kaboni umesaidia sana kwenye kilimo kupunguza mbolea. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa maeneo kama ya Nyanda za Juu Kusini

inawekezwa biashara ya kaboni ili tupunguze matumizi ya mbolea na tuongeze uzalishaji wa mazao? Nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Oran, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Oran kwa maono yake mazuri na hasa katika eneo hili jipya la biashara ya kaboni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2022 tulitengeneza kanuni za kwanza, tulikuwa watu wa kwanza katika *East Africa* kuwa na kanuni, lakini kutokana na utekelezaji wa *Article* 6 ya *Paris Agreement* mwaka 2023 tulifanya rejea katika eneo hilo. Hivi sasa, kama nilivyosema juzi hapa kwamba zaidi ya miradi 42 imeshasajiliwa. Sasa hivi tuko katika mchakato na baadhi ya maeneo kampuni nyingine sasa zimeonesha hali ya kutaka kwenda katika eneo hilo. Kwa hiyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumejipanga vizuri kwa upande wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la uwekezaji katika Nyanda za Juu Kusini, naomba niwahakikishie, miongoni mwa kampuni hizi 42 nyingine zime-*identify* miradi katika eneo hilo. Kwa hiyo imani yetu kubwa ni kwamba miradi hii sasa itakayotekelezwa katika maeneo mbalimbali italeta manufaa makubwa sana, hususan katika nyanda za juu kusini. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa wanunuzi wa *carbon* kwa Tanzania asilimia kubwa ni *middleman*, ambao wanatulipa fedha kiduchu kuliko zile ambazo ni stahiki. Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuwapata wanunuzi wa moja kwa moja kuliko walivyo sasa hivi tunaopata hawa ambao ni *middleman*? Tunaomba kufahamu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Tanganyika, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Kakoso, katika watu ambao wamekuwa *aggressive* katika maeneo yao katika biashara ya *carbon* ni Mheshimiwa Kakoso. Tunakumbuka kwamba hivi karibuni Halmashauri ya Tanganyika ilikuwa ikipata fedha kadhaa na gawio la mwisho ilikuwa imepata karibuni *three point something billions,* lakini kutokana na huo uhitaji na nguvu kubwa mwaka huu *expectation* wataweza kupata kati ya shilingi bilioni 10 mpaka shilingi bilioni 14.7, kwa hiyo, Mheshimiwa Kakoso hongera sana katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanya hilo sasa Serikali ndiyo maana imetengeneza kanuni, katika kanuni ya 4(2) inazungumzia *issue* ya *transparency*. Lengo letu ni nini, katika eneo hili watu wanaotoa *credit* zao hapa nchini watakapokwenda katika *stock exchange* lazima ku-*declare* kwamba wametoa ngapi na wameuza ngapi, kwa lengo la kuhakikisha mahitaji halisi hasa ya kifedha yanawafikia watu ambao wanatunza rasilimali za misitu katika nchi yetu, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Halmashauri ya Masasi imekuwa na elimu ndogo kuhusiana na jambo hili. Je, Serikali ina-*commitment* gani kuhakikisha inatupa elimu hii, hususani katika Jimbo langu la Lulindi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungahela, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli nimesema kuna *gap* kidogo, suala la uelewa na ndiyo maana Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, iliamua kutafuta fursa ya kutoka kwa wadau kwa ajili ya kufanya *capacity building* kwa wataalamu wetu. Ndiyo maana sasa hivi Serikali kupitia Shirika la *UNEP* tutaenda kufanya *awareness* na *capacity building* kwa wataalamu wetu wa mazingira katika halmashauri zetu, Lengo kubwa tuwe na uelewa mzuri katika suala zima la uwekezaji katika biashara ya *carbon*. Kwa hiyo, kwenye hilo ni kwamba hata wataalamu wa Lulindi watapata fursa hiyo kupitia uhusiano huu tuliokuwa nao na *UNEP*. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Suleiman Haroub Suleiman.

Na. 123

**Serikali Kuwaenzi na Kuwatunza Waasisi wa Muungano**

**MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaenzi na kuwatunza Waasisi wa Muungano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Haroub Suleiman, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetunga Sheria maalum Na. 18 ya Mwaka 2004 mahususi kwa ajili ya waasisi hao wa Muungano wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja na sheria hiyo imetungwa kanuni ya mwaka 2005 inayoweka utaratibu wa namna ya kuwezesha waasisi wetu, ikiwemo kuhifadhi kumbukumbu zao, kazi zao na kueneza falsafa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara Maalum ya Kuwaenzi Waasisi imeundwa ikiwa chini ya Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka ya Taifa, ikishughulikia na kusimamia ukusanyaji na uhifadhi wa kumbukumbu na vitu vya waasisi wa Taifa kwenye umuhimu wa kihistoria. Aidha, Serikali inaendelea kuhakikisha kuwa kila mwaka kumbukumbu za kifo cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume pamoja na maadhimisho ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar zinafanyika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suleiman Haroub Suleiman.

**MHE. SULEIMAN HAROUB SULEIMAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kuna baadhi ya viongozi ambao walitumikia Serikali ya Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania akiwemo Dkt. Salmini Amour Bin Jumaa, anaishi kwenye hali ngumu sasa hivi kwa maana kwamba nyumba yake inaendelea sasa hivi kupata *erosion,* ipo karibu na bahari. Je, Serikali ama Ofisi hii ipo tayari kushirikiana na Kamati ya Viongozi Wakuu wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar ili kutatua changamoto hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kuna baadhi ya maeneo ambayo yanahitaji kutunzwa, lakini mpaka hivi sasa maeneo hayo yanakuwa kwenye hali hatarishi ikiwemo shule aliyosoma Mzee Karume. Je, Serikali ina mpango gani kutunza maeneo kama hayo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimshukuru Mheshimiwa Haroub. Naomba niseme Mheshimiwa Haroub ni mfuatiliaji sana na watu kule Baraza la Wawakilishi lazima wajue *recognition* yake ya kazi kubwa anayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, tulikuwa na sheria yetu ambayo nimezungumza hapa, lakini hii ilikuwa inagusa maeneo mahususi, kwa sababu mimi ni Waziri wa Muungano haya mambo ambayo amezungumza, mengine tutayachukua kwa ajili ya kuyafanyia kazi kupitia taratibu zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mambo ya kumbukumbu ya maeneo hayo niseme, kwa sababu ofisi yangu inahusika na mambo mbalimbali na kwa sababu ofisi yangu inashirikiana vizuri na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kule Zanzibar, tunalichukua jambo hili, tunali-*discuss* halafu tuone *way forward,* tunafanyaje kuboresha maeneo hayo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Yahya Mhata kwa niaba ya Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate.

Na. 124

**Ajira kwa Vibarua Madereva na Mafundi wa *TANESCO***

**MHE. YAHYA A. MHATA K.n.y. MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaajiri Madereva na Mafundi ambao wamekuwa vibarua wa muda mrefu *TANESCO*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* limekuwa likiajiri watumishi wa kada mbalimbali kwa kuzingatia mahitaji ya kiuendeshaji na uwezo wa kibajeti kwa mwaka husika. Katika ikama na bajeti ya mishahara ya mwaka 2024/2025 pamoja na mambo mengine, shirika limetenga fedha kwa ajili ya nafasi 430 za ajira mpya kwa mchanganuo ufuatao:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wahandisi 67, fundi sanifu 135, fundi mchundo 205 na madereva 23. Aidha, ujazaji wa nafasi hizi utazingatia sheria na taratibu katika utumishi wa umma. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yahya.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali

la kwanza; kule Tunduru Kusini na Jimbo langu la Nanyumbu tunao madereva pamoja na mafundi sanifu ambao sasa hivi wapo katika ajira za muda kati ya miaka mitano na miaka saba. Je, wizara ipo tayari sasa katika ajira zinazokuja kuwafikiria madereva hawa ambao wamekuwa muda mrefu katika shirika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, jukumu la kupeleka umeme vijijini lipo chini ya *REA*. *REA* jukumu lake ni kupeleka umeme vijijini na baadaye kuwaachia *TANESCO* kuwaunganishia wateja. Je, Serikali haioni wakati umefika *REA* baada ya kupeleka umeme vijijini iwaunganishie wateja ndipo iwakabidhi kwa *TANESCO* wateja wote badala ya kuwaachia *TANESCO* kufanya kazi ya kuwaunganishia wateja hao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na ajira kwa ajili ya madereva, kwanza niwapongeze Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mhata na Mheshimiwa Mpakate, kwa kazi nzuri wanazofanya katika majimbo yao. Kuhusiana na ajira za vibarua hawa, kama wizara tunathamini sana mchango wa wafanyakazi wetu vibarua hususani mafundi na madereva. Nataka niwahakikishie kwa kuwa ni wafanyakazi wetu ambao wanafanya kazi kwa jitihada kubwa sana kulitegemeza shirika letu, tutahakikisha ajira zinapotoka wanazingatiwa ipasavyo kulingana na sheria na taratibu za utumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la *REA* kuendelea na kuunganisha wateja pale ambapo miradi inakamilika. Ushauri wa Mheshimiwa Mbunge tumeupokea na tutauchakata kuona kama unatekelezeka na kama unatekelezeka hatutasita kuufanyia kazi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lambert.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanaotumia umeme wa *REA* vijijini wamekuwa wakipata changamoto kubwa sana za huduma za haraka pale inapotokea hitilafu ya umeme na hii ni kwa sababu ya mafundi wengi wanakaa Makao Makuu. Swali langu, je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuajiri mafundi hawa maalum kwa ajili ta kitengo cha dharura na kuwasambaza huko vijijini ili wananchi hawa waweze kupata huduma za haraka? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa mawazo mazuri. Nataka nimhakikishie kuhusiana na suala la huduma kwa wateja tayari tumeshaanza kufanyia kazi kuhakikisha tunakitegemeza kitengo hiki ili kiweze kuwa na huduma nzuri kwa wateja. Kuhusiana na suala la mafundi tayari tumekuwa tukiongeza viunga kwenye maeneo ya mbali ili wananchi waweze kupata huduma za uhakika. Kwenye suala la mafundi, kuongeza mafundi Mheshimiwa Mbunge tumelipokea na tutaendelea kulifanyia kazi kuhakikisha wananchi wanapata huduma nzuri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Ally Juma Makoa.

Na. 125

**Kupeleka Umeme wa *REA* Mitaa yenye Sifa ya Vijijini Kondoa**

**MH. ALLY J. MAKOA** aliuliza:-

Je, lini umeme wa *REA* utapelekwa Mitaa ya Chemchem, Tampori, Kwamtwara, Guluma, Mongoroma, Chandimo, Chang'ombe na Tura?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini imeendelea kutekeleza kazi ya kusambaza umeme katika maeneo ya vijijini na maeneo ya mitaa ambayo ipo katika mamlaka za miji na miji midogo yenye hadhi sawa na vijiji. Kwa kuwa Jimbo la Kondoa Mjini lipo katika mamlaka ya mji, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, *REA* itapeleka umeme katika mitaa 15 ambayo imefikiwa na miundombinu ya msongo wa kati, ikiwemo Mitaa ya Chemchem, Tumbelo na Chang'ombe. Aidha Mitaa ya Tura na Tumbelo imepatiwa umeme kupitia Mradi wa Ujazilizi Mbili (A). Serikali kupitia *REA* itaendelea kuratibu kazi ya kusambaza umeme katika vitongoji na mitaa ambayo haina umeme kulingana na upatikanaji wa fedha. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Makoa.

**MH. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali yenye kutupa matumaini naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; baada ya Serikali kutupatia katika kipindi hiki hiyo mitaa 15, vipi sasa kuhusiana na ile mitaa ambayo haikutajwa hapo ambayo imebaki mfano Chora, Damai, Ngereli pamoja na Hurumbi na yenyewe mpango wao ukoje?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; je, ni lini Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kufuatana na mimi twende Kondoa kwa ajili

ya kuona yale mazingira na namna watu wanavyohitaji huo umeme. Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye jimbo lake. Katika mitaa ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge tutazingatia katika bajeti inayofuata kuona kama mitaa mingine imebakia tunaweza kuiingiza baadhi ili kuweza kuwafikishia wananchi huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na kuambatana na yeye jimboni, tutapanga na Mheshimiwa Mbunge siku za hivi karibuni ili tuweze kwenda kuona utekelezaji wa miradi katika jimbo lake, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, *TANESCO* na Wizara ya Nishati imeweka mabanda ya *REA* na *TANESCO* kwenye viwanja vya Bunge. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge mwende na kero zenu zote ili zipate huduma na wananchi wenu wapate furaha na raha. *(Makofi)*

Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa David Mathayo.

Na. 126

**Kuelimisha Mtoto wa Kiume kuwa Baba wa Familia**

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kumwelimisha mtoto wa kiume kujitegemea, kujiamini na kufahamu majukumu ya baba wa familia pindi anapooa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeandaa Mwongozo wa Wajibu wa Wazazi katika Malezi ya Watoto kwa kuzingatia jinsi ambavyo inajumuika kama Familia Bora, Taifa Imara, wenye lengo la kuimarisha ushiriki wa wazazi na walezi katika malezi ya watoto. Moja ya eneo lililoainishwa katika mwongozo huo ni kumwandaa mtoto wa kiume ili aweze kumudu majukumu ya baba katika nyanja tofauti ikiwa ni pamoja na kutambua wajibu na nafasi katika malezi ya watoto na familia, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mathayo.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali, hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza. swali la kwanza; tumekuwa na kampeni kwa miaka mingi iliyopita, kuelimisha na kuwezesha mtoto wa kike, tukasahau mtoto wa kiume. Sasa je, Serikali ina mikakati gani kuwapa upendeleo maalum watoto wa kiume ili waweze kupata elimu nzuri na kujiamini ili baadaye waweze kuoa wanawake waliosoma?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kumekuwa na kuvunjika kwa ndoa, siku hizi ndoa zinavunjika sana na watu wanaachana sana kiasi ambacho kunakuwa na watoto ambao hawana wazazi wawili wa kuwalea. Je, Serikali ina mikakati gani katika kuelimisha, kutoa elimu kwa Watanzania hasa kuonesha

majukumu ya akina mama na majukumu ya akina baba katika ndoa ili watoto hawa waweze kulelewa na wazazi wawili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, Serikali kupitia Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 inatoa haki sawa kwa watoto wote wa kike na wa kiume wakiwemo wenye ulemavu. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametoa fedha nyingi kujenga madarasa katika kila mkoa kuhakikisha kwamba watoto wote wanapata elimu na waweze kufikia malengo ambayo wamekusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya Mwaka 2023 inatambua umuhimu wa ushiriki wa wanawake na wanaume akiwemo mtoto wa kiume kama wakala muhimu wa kuleta mabadiliko na kuimarisha maendeleo ya familia nchini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Mwaifunga.

Na. 127

**Kukarabati Uwanja wa Mpira wa Ali Hasan Mwinyi – Tabora**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafanya ukarabati mkubwa wa Uwanja wa Mpira wa Ali Hassan Mwinyi - Tabora ili utumike *AFCON 2027*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa ukarabati wa Uwanja wa Mpira wa Ali Hassan Mwinyi uliopo Tabora pamoja na viwanja vingine hapa nchini na imeendelea kusisitiza wadau na wamiliki wa viwanja kujenga na kutunza miundombinu hiyo sawa na maelekezo ya Sera ya Maendeleo ya Michezo ya Mwaka 1995 sehemu ya 7(1)-(6).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hivi sasa Serikali inajenga na kukarabati viwanja vitakavyotumika katika mashindano ya *AFCON* 2027 ambavyo ni Benjamin Mkapa uliopo Dar es Salaam, Amaan Zanzibar na Uwanja mpya wa Dkt. Samia Suluhu Hassan unaojengwa katika Jiji la Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ipo tayari kutoa ushauri wa kitaalam wa namna bora ya kujenga, kukarabati na kuhudumia miundombinu mbalimbali ya michezo kulingana na mahitaji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kumekuwa na taarifa mbalimbali kwamba kuna viwanja ambavyo vitakwenda kufanyiwa ukarabati na Serikali. Je, kiwanja cha Ali Hassan Mwinyi kilichopo Tabora ni moja kati ya viwanja vitakavyofanyiwa ukarabati huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; kutokana na Serikali kutokuwa na viwanja vingi vya michezo nchini, Serikali ina mkakati gani wa kukaa na Chama Cha Mapinduzi, kuzungumza nao na kuona namna bora ya kuchukua viwanja hivi vya michezo ambavyo wanavyo ili viweze kwenda Serikalini na viweze kufanyiwa ukarabati ili tuweze kukuza michezo nchini? Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi, kwa sasa Serikali inaweka mkazo kwenye kumalizia miundombinu ya viwanja vya michezo vitakavyotumika kwa ajili ya *AFCON* 2027. Aidha, kwa kujenga miundombinu mipya kama tunavyofanya kwenye uwanja wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Arusha, ama kukarabati kama ilivyofanyika kwa uwanja wa Amani na uwanja wa Benjamin Mkapa ambapo ukarabati unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo Serikali inaendelea na mpango wa kukarabati kwa awamu viwanja mbalimbali vilivyopo katika majiji, mikoa, halmashauri na manispaa kote nchini na uwanja wa Ali Hassan Mwinyi utakuwepo katika awamu zitakazofuata. Kwa sasa Serikali imeanza na viwanja vitano ambavyo ni Uhuru uliopo Dar es Salaam, Mkwakwani uliopo Tanga, Jamhuri uliopo Morogoro, Maji Maji uliopo Songea na Sheikh Amir Abed uliopo Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la pili, mazungumzo kati ya Serikali na Chama Cha Mapinduzi kuhusiana na kukabidhiwa viwanja vyake ili vifanyiwe ukarabati viweze kutumika katika matukio mbalimbali yanaendelea na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, yanaendelea vizuri na hivi karibuni Serikali itatoa tamko kuhusiana na uwezekano wa Serikali kuvichukua

viwanja ambavyo vipo chini ya Chama Cha Mapinduzi na kuvifanyia ukarabati kwa ajili ya matumizi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Deo Sanga kwa niaba ya Mheshimiwa Justin.

Na. 128

**Malipo ya Fidia Eneo la Idefu kupisha Ujenzi wa *One Stop Centre***

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA K.n.y. MHE. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali italipa fidia eneo la Makaburi Idefu – Makambako ili kupisha ujenzi wa *One Stop Centre*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Sanga, Mbunge wa Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshalipa fidia ya shilingi bilioni 4.6 kwa wananchi waliopisha eneo kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi wa *One Stop Centre*. Aidha, Serikali imeanza taratibu za tathmini ya eneo la makaburi ya Idefu, Makambako na taratibu za malipo zitaanza baada ya kuidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; kabla ya swali Mheshimiwa Deo Sanga anashukuru sana kwamba malipo ya fidia ile yamefanyika na swali lake namba moja ni kwa sababu malipo yameshafanyika na lile eneo la makaburi siyo kubwa, Serikali haioni umuhimu wa kulipa haraka ili ipate uhuru wa kuendelea na ujenzi wa *One Stop Centre* pale Makambako?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; pale Kilolo ambapo Makao Makuu ya Wilaya yamejengwa, kuna madai ya fidia ya muda mrefu na yalikwishawasilishwa Hazina mara kadhaa. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuyaharakisha malipo yale ili wale wananchi pia waweze kupata haki yao? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nyamoga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kuhusu ulipaji wa fidia kule Idefu, Makambako, kwa kuwa tumeshalipa fedha nyingi sana shilingi bilioni 4.6 kilichobakia ni kidogo tu ni shilingi milioni 100. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ndani ya mwaka huu wa fedha tunaenda kulipa fidia iliyobakia. Upande wa Kilolo Serikali ipo tayari kufanya haraka, tunasubiri tu Mthamini Mkuu aweke idhini, akishatoa idhini yake tunaenda kulipa hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa wananchi wa Gona, Sehemu ya Njia Panda pale Himo na Mabungo pale Uchira

ambao nao wamepisha Serikali kujenga *one stop center* ya *customs? (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali ya nyongeza la Mheshimiwa Kimei, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Kimei suala hilo linatambulika Serikalini na tunalifanyia kazi. Awe na subira, fidia hiyo katika eneo alilolitaja italipwa kwa wakati mahususi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Costantino Mwakamo.

Na. 129

**Kuepuka Mzigo Mkubwa wa Kulipia**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuepuka mzigo mkubwa wa ulipaji wa fidia wakati inapoongeza ukubwa wa barabara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Sheria ya Barabara Na. 13 ya Mwaka 2007, iliongeza upana wa hifadhi ya barabara kutoka meta 45 hadi meta 60 kwa barabara kuu na za Mikoa ili kukidhi mahitaji ya uendeshaji wa miundombinu ya barabara kwa

wakati huu na wakati wa baadaye, ili uendane na ongezeko la watu na ukuaji wa shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupunguza ulipaji wa fidia Wizara, kupitia *TANROADS,* imefanya tathmini ya awali ya gharama inayohitajika kwa ajili ya kulipa fidia kwa mali zilizomo ndani ya eneo la hifadhi ya barabara lililoongezeka la meta 7.5 kila upande na kuonesha kuwa, gharama kubwa za fidia ziko katika majiji na miji. Kutokana na hali hiyo, Serikali inaangalia uwezekano wa kuchepusha barabara kwenye maeneo hayo. Aidha, uchambuzi wa kina unafanyika, ili kubaini ni barabara zipi kweli zinahitaji upana wa eneo la hifadhi ya barabara wa meta 60 kwa kuzingatia mahitaji ya sasa na ya hapo baadaye ya kuzipanua kulingana na ongezeko la wingi wa magari. Zoezi hili likikamilika taarifa kamili itatolewa, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Michael.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kule Jimboni Kibaha kuna kipande cha Mlandizi kwenda *Station* ya *SGR,* Ruvu na Kongowe Soga, ambacho kinaunganisha na reli ya mwendokasi ambayo inatarajiwa kuanza kufanya kazi. Je, ni nini mpango wa Serikali wa kujenga barabara hizi kwa haraka ili ziweze kutoa huduma kwenye hizo *station* za abiria?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; wananchi wa Majimbo manne ya Bagamoyo, Kibaha Mjini, Kibaha Vijijini na Kisarawe walikuwa wanapata majibu tofauti kila wanapouliza swali lao linalohusiana na Barabara ya Makofia –Mlandazi – Mzenga hadi Vikumburu. Sasa kwa kuwa, majibu ya Serikali ni tofauti mara kwa mara, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kwenye kipindi hiki cha Bunge kutenga muda kuambatana na Waheshimiwa Wabunge

wa maeneo hayo kwenda kutoa msimamo wa Serikali juu ya utaratibu wa ujenzi wa barabara hiyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kipande cha barabara cha Mlandizi kwenda *Ruvu Junction* ambacho kina kilometa 23, ni kati ya zile barabara ambazo wakati *SGR* inajengwa zinatakiwa ziunganishwe na miji ama vijiji ama *centers* ambazo zipo karibu na reli kwa ajili ya kuunganisha na hii ni barabara mojawapo. Kwa kuwa, barabara hii inahusisha barabara illiyokuwa ya *TANROADS* na *TARURA* kuna maeneo ambayo yalikuwa hayajasanifiwa. Kwa hiyo, ili kuharakisha ujenzi wa barabara hii, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Kibaha kwamba, tumeamua kutumia utaratibu wa *design and build* yaani unasanifu, Mkandarasi atasanifu na kujenga. Hivi tunavyoongea, tayari tuko kwenye hatua za mwisho za kumpata mkandarasi kwa ajili ya kujenga kilometa zote 23 kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Makofia – Mlandizi – Maneromango kwenda Vikumburu, tathmini imeshafanyika ya fidia. Najua Mheshimiwa Mbunge anataka kujua wananchi wanataka kujua italipwaje? Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tukubaliane ni lini tutapata nafasi, ili twende tukaongee na wananchi hao kuwaeleza mpango wa Serikali kuhusu barabara na fidia ambayo wanadai, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea, Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu.

Na. 130

**Ujenzi wa Barabara ya Ikungi Hadi Kilimatinde**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Ikungi – Mang'onyi – Londoni hadi Kilimatinde?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, zabuni ya manunuzi kwa ajili ya kumpata mhandisi mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Barabara ya kutoka Ikungi – Mang'onyi – Londoni hadi Kilimatinde yenye urefu wa kilometa 117.8 iko katika hatua za mwisho. Mkataba wa kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina utakuwa umesainiwa kabla ya mwezi Juni, 2024. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inatarajiwa kuchukua kipindi cha mwaka mmoja na nusu, hivyo zitakamilika mwezi Disemba, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; barabara hii inakatisha katikati ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi pamoja na hospitali ya wilaya, tayari tumejengewa kilometa mbili ambazo hazijafika kwenye ofisi hizo. Je, ni nini mpango wa muda mfupi wa

Serikali kuhakikisha kwamba, Ofisi za Serikali na Hospitali ya Wilaya inafikiwa barabara ya lami? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; nataka tu kueleza kwamba, barabara hii ni barabara ya kiuchumi inakatisha kwenye Kata ya Mang'onyi ambayo imebeba Mgodi mkubwa wa Madini wa *Shanta Gold Mine* na kwa sababu, mgodi huu tayari umeanza kumimina dhahabu, kwa mwaka unatoa *ounce* 30,000 ambazo ni sawasawa na dola bilioni 60 au Shilingi za Kitanzania bilioni 150, maana yake ni mapato mengi ya Serikali. Kwa sababu, mgodi unahitaji pia barabara hii, je, ni nini mpango wa Serikali kwa kushirikiana na mwekezaji huyu ili kuhakikisha Barabara hii ya kutoka Ikungi mpaka Mangonye ambayo ni kilometa 50 tu iweze kuwekwa lami na kumsaidia mwekezaji aweze kuwa na mazingira mazuri? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba, barabara hii inafanyiwa usanifu, lakini tunatambua kwamba, barabara hii ndio inapita kwenye Ofisi ya Halmashauri, Mkuu wa Wilaya na Hospitali ya Wilaya. Tayari tumeanza na pia, tayari tumepata maombi ya Meneja wa Mkoa kutaka kuendelea kujenga kwa awamu hadi kufika katika hospitali ya wilaya. Kwa hiyo, hilo tutaendelea nalo wakati tunaendelea na usanifu kuhakikisha kwamba, tunafika hapo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. La pili, tayari?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, la pili bado.

**NAIBU SPIKA:** Haya, jibu la pili.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili, hata wawekezaji wenyewe wamekuja Ofisi ya Mkoa na Wizarani pia, kuomba barabara hii iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Ushauri wake kama alivyosema, tutaendelea kushauriana kama tulivyofanya *Barrick* ambao wameamua kusaidia kujenga kama *CSR*. Kwa hiyo, taratibu zinafanyika kuona namna ambavyo tunaweza kusaidiana na Serikali na *Shanta Mine* kuweza kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara. Vipi mzee, bado uko Bunda? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi. Tumepata barabara ya kutoka Tarime Mjini mpaka pale Mugumu, Serengeti, hasa maeneo ya Nyamongo, lakini barabara imesimama ujenzi wake kwa muda mrefu sasa kwa sababu, yule mkandarasi anadai shilingi bilioni 6.8 mpaka leo. Je, ni lini mkandarasi huyu atalipwa fedha ili ujenzi ukamilike kwa wakati na watu wetu waendelee kupata huduma? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, taarifa nilizonazo, nitaongea na Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, tuna *lot* mbili, *lot* ya kwanza ni Mugabiri kwenda Serengeti na kipande kile ambacho ni cha pili, nilichoambiwa ni kwamba, yupo

kwenye *mobilization* na anaendelea kuandaa *camp* kwa ajili ya kujenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tumekuwa na changamoto kubwa, barabara nyingi zimesimama kwa sababu ya hali ya hewa ambayo inazuia wakandarasi kuendelea na kazi za ujenzi wa barabara, lakini nitaomba nionane na Mheshimiwa Mbunge, tuone kama kuna changamoto nyingine zaidi ya hii. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Dkt. Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Nyanguge – *Airport* yenye urefu wa kilometa 46, Serikali ilipanga kuijenga kwa kilometa 10 na tayari mkandarasi alipatikana. Je, ni lini mkandarasi huyu atakabidhiwa *site* ili aanze kazi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumetangaza na Mkandarasi amepatikana, lakini kutokana na ukubwa wa barabara imehamishiwa, badala ya kusimamiwa na mkoa sasa itasimamiwa na *TANROADS,* Makao Makuu. Kwa hiyo, ni suala linalosubiri kumkabidhi mkandarasi hiyo *site* ili aanze kazi ya ujenzi. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali ya nyongeza. Barabara ya kutoka Bariadi – Itilima – Kisesa - Meatu mpaka Sibiti – Singida iko kwenye ilani. Je, ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja ni Barabara ya Mkoa ambayo tunavyoongea sasa hivi ipo kwenye utaratibu wa usanifu wa kina. Ikikamilika, Serikali itatafuta fedha ya kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize swali dogo la nyongeza. Barabara inayotokea Tegeta kupita Mabwepande mpaka Mbezi imekuwa ni kero, haipitiki na kumekuwa na msongamano mkubwa katika Barabara ya Bagamoyo. Je, ni lini Serikali itaijenga barabara hii ili kuondoa adha kwa wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Hii barabara ni kati ya barabara ambazo zipo kwenye mpango mkubwa wa kupunguza foleni katika Mkoa wa Dar es Salaam. Tunavyoongea sasa hivi ni kwamba, kuanzia Bunju B – Mabwepande hadi *Station* ya Magufuli ipo kwenye usanifu. Tunategemea mwaka ujao wa fedha tutaanza kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kabati. Mheshimiwa Kabati au tukuite Dkt. ndio utajua?

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itaijenga kwa kiwango cha lami barabara ya mchepuo inayotoka Tumaini kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la magari makubwa yanayopita katikati ya mji na kusababisha

hatari kwa wafanyabiashara pamoja na watumiaji wengine wa barabara? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naamini Barabara ya Mchepuo kutoka Tumaini ni ile inayokwenda *Station* Kuu pale Ipogolo chini, kilometa saba. Barabara hiyo ilikuwa haipo, ndiyo tunaendelea kuifungua na baada ya kuifungua, kwa umuhimu wake na eneo ilipo baada ya kuifungua kinachofuata ni kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo. Mheshimiwa Leah Komanya. *(Makofi)*

Na. 131

**Ujenzi wa Malambo Jimbo la Meatu**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Malambo ya kunyweshea mifugo katika Jimbo la Meatu?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa bwawa/lambo hufanyika kwa hatua tatu ambazo ni kutafuta chanzo cha maji *(water source)*, kufanya usanifu *(design)* na kutekeleza kazi ya ujenzi. Wizara itawasiliana na Halmashauri ya Wilaya Meatu kwa ajili ya kupata mapendekezo ya eneo linalofaa kujenga lambo ambalo halina mgogoro wa umiliki, ili hatua za usanifu ziweze kufanyika na kuingiza gharama zake kwenye Mpango wa Bajeti ya Wizara kadiri ya upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kutoa wito kwa wafugaji na wadau wengine hapa nchini kuwekeza kwenye ujenzi wa miundombinu ya maji ili kusaidia kupunguza changamoto ya maji kwa ajili ya mifugo. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Komaya.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali haioni haja kwenye mabwawa saba yaliyotengwa katika Mradi wa *ASDP II* ukiwemo Mkoa wa Simiyu, likajengwa katika Jimbo la Meatu kwa sababu ndio wilaya yenye mifugo mingi, ndio wilaya yenye ukame mkubwa na maeneo yapo mengi, wafugaji wapo tayari kuyatoa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; je, ni lini Serikali itakipelekea shilingi milioni 6.8 Kikundi cha Mwamalole cha kupanda nyasi kwa kuwa, mvua nazo zinaeleka kwisha? Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na hili la kwanza la mabwawa saba; tumepokea maombi ya Mheshimiwa Mbunge na ushauri wake. Tutatazama tuone namna ambayo inafaa zaidi kwenye Jimbo lake hili la Meatu. Kwa kuongezea katika hilo ni kwamba, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Kilimo pamoja na Wizara ya Maji tumekubaliana yale malambo yanayojengwa kwa ajili ya shughuli za kilimo cha uwagiliaji ambayo yanajengwa na Wizara ya Kilimo pamoja na mabwawa makubwa yanayojengwa na Wizara ya Maji ambayo yanafanya shughuli za kuhifadhi maji, tumekubaliana sasa yawe na mabirika kwa ajili ya wafugaji ili yaweze kutumika kwa shughuli za mifugo katika maeneo yetu.  Kwa hiyo, tutaangalia katika

malambo saba ambayo yanajengwa na pia, tutaangalia katika Wizara ya Kilimo na Wizara ya Maji, kama kuna uwezekano wa kutengeneza mabirika kwa ajili ya wafugaji wetu ili waweze kupata huduma hiyo ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili, la shilingi milioni sita kwenda kwa vikundi vyake. Namwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba, leo nitalifuatilia jambo hili na baada ya hapo nitakupa majibu halisi juu ya namna gani ambayo tunakwenda kusaidia vikundi vyetu hivyo katika maeneo yetu. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Khenani.

Na. 132

**Kuboresha Skimu ya Umwagiliaji ya Rwamfi**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha Skimu ya Umwagiliaji ya Rwamfi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Rwamfi, Katongolo, ni Skimu ya Umwagiliaji ambayo ipo katika Kata ya Kirando na Kipili, Tarafa ya Kirando katika Wilaya ya Nkansi, Mkoani Rukwa. Skimu hii ina eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji lenye ukubwa wa hekta 3,300 na inahudumia jumla ya vijiji sita kikiwemo Kijiji cha Masolo, Katongolo, Kipili, Mtakuja, Kamwanda na Katete.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilikamilisha upembuzi

yakinifu na usanifu wa kina wa skimu hiyo kwa lengo la kuiboresha kwa kufanya ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Katika mwaka wa fedha 2023/2024, Mkandarasi *Halem Construction Company Limited* amepatikana na mkataba unategemewa kusainiwa mwishoni mwa Mwezi Aprili, 2024 kwa ajili ya kuanza ukarabati na ujenzi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea majibu ya Serikali. Sasa kwa kuwa, kusainiwa mkataba ni jambo moja na ile miundombinu imeharibika sana na uchumi wa Nkansi sisi tunategemea kilimo na uvuvi. Tunatamini kusikia, mkataba huo utaanza lini na kukamilika ili wananchi waendelee kupata hudumu kwenye Skimu hiyo ya Rwanfi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumzia hekta 3,300, Wilaya ya Nkansi tuna hekta 6,145. Je, ni lini watamalizia eneo lingine lililobaki kwa sababu ndiyo uchumi wetu wa Wilaya ya Nkansi? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO**: Mheshimiwa Naibu Spika, namthibitishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, mara baada ya mkandarasi kusaini mkataba anatakiwa aanze kazi mara moja. Matarajio yetu ni, kwa sababu kazi ni *process,* ndani ya miezi 24 kazi yote iwe imekamilika na mradi uwe na *full capacity*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuongeza ukubwa kutoka hekta 3,300 mpaka hekta 6,145. Hili ni lengo la Wizara kwamba, katika hatua ya kwanza tuta-*deal* na hizi hekta 3,300 na baada ya hapo tutaongeza miundombinu katika hizi hekta nyingine. Kwa hiyo, ni kazi ambayo ipo katika mipango yetu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Massare.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Halmashauri ya Itigi ina skimu moja tu na haifanyi kazi vizuri. Je, Serikali sasa ipo tayari kutuongezea angalau skimu nyingine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipo tayari kuongeza skimu katika Halmashauri ya Itigi na ipo katika mipango yetu. Ukiangalia katika mpango wa Tume ya Taifa, Itigi kuna *schemes* ambazo zimeongezeka pale, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha.

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika, wageni 18 wa Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Bwana Mululi M. Mahendeka, Katibu Mkuu Ikulu; Bwana Juma Seleman Mkomi, Katibu Mkuu Menejimenti ya Utumishi wa Umma; *CP*. Salum R. Hamduni, Mkurugenzi TAKUKURU; Bwana Xavier Mrope Daudi, Naibu Katibu Mkuu Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Mheshimiwa Jaji Sivangilwa, Kamishna wa Maadili Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi; Bwana Kadari Singo, Mtendaji Mkuu Taasisi ya Uongozi; Bwana Shedrack Mziray, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji *TASAF*; *Engineer* Benedict Ndomba, Mtendaji Mkuu Mamlaka ya Serikali Mtandao; Ndugu Sauda Mguwa, Afisa Mtendaji Mkuu Wakala wa Ndege za Serikali Tanzania; Bwana Mathew Kirama, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma; na Dkt. Mwatima Juma, Mjumbe Sekretarieti ya Baraza la Kumshauri Rais Masuala ya Chakula na Kilimo. *(Makofi)*

Wengine ni Bwana Innocent Bomani, Kaimu Mtendaji Mkuu, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Dkt. Ernest Mabonesho, Kaimu Mkuu wa Chuo cha Utumishi wa Umma; Bwana Firmin Msiangi, Mtendaji Mkuu Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa; Bwana Fred Msemwa, Mtendaji Mkuu Watumishi *Housing Investment*; Dkt. Florens Turuka, Mjumbe Sekretarieti ya Baraza la Kumshauri Rais, Masuala ya Chakula na Kilimo; na Bi. Mariana Nani, Mke wa Mheshimiwa Waziri George Simbachawene. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 39 wa Mheshimiwa Spika, Kikundi Cha Uyole *in Dar es Salaam (UID)*. Karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni 23 wa Mheshimiwa Dkt. Selemani Jafo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ambao ni Wakuu wa Shule kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe, Mkoa wa Pwani. *(Makofi)*

Tunao wageni 24 wa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimbo la Chalinze, Wajumbe wa Baraza la Wazee Taifa kutoka Mkoa wa Pwani na marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, Naibu Waziri wa Afya ambaye ni Katibu wa Baraza la Waislam kutoka Siha, Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Tunao wageni 50 wa Mheshimiwa Judith Kapinga, Naibu Waziri wa Nishati ambao ni Viongozi na Watendaji wa *REA* Mikoa yote ya Tanzania Bara. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ramadhani Ighondo, ambaye ni mpigakura wake kutoka Jimbo la Singida Kaskazini. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi ambaye ni mpigakura wake kutoka Kibondo, Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya ambaye ni Mwalimu kutoka Nyasa, Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, ni Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari Nampungu kutoka Wilaya ya Tunduru, Mkoa wa Ruvuma. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Abdulhafar Juma, ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Sylvia Sigula, Makada wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Nicholaus Ngassa, wanafunzi wa Shahada ya Uzamili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)*. *(Makofi)*

Tunao wageni nane wa Mheshimiwa Justin Nyamoga ambao ni Viongozi wa UVCCM kutoka Kilolo Mkoa wa Iringa. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 13 wa Chuo cha Uongozi *Institute* kutoka Jijini Dar es Salaam na wanafunzi 134 na Walimu 10 wa Shule ya *St. Gasper Primary School* kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30); Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33); Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Fungu 32); Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67); Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94); na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 04) kwa mwaka wa fedha 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana katika kipindi hiki cha Mkutano wa Kumi na Tano wa Bunge la Kumi na Mbili kwa ajili ya kupokea utekelezaji wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na kutafakari mipango ijayo katika kuyafikia malengo ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuliahidi Bunge lako Tukufu na Watanzania wote kuwa nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa uadilifu, bidii na weledi mkubwa ili kuendeleza mafanikio yaliyofikiwa na kuhakikisha kwamba Bajeti hii inasimamiwa vyema na kutekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kwangu na kuendelea kunipa dhamana ya kusimamia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yenye jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa utumishi wa umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora, sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali ya usimamizi wa utumishi wa umma na hatimaye kuwa na utumishi wa umma wenye ufanisi na uwajibikaji kwa ustawi wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende kutumia fursa hii pia kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza kipindi cha miaka mitatu ya kuiongoza nchi yetu kwa mafanikio makubwa yanayojidhihirisha kupitia kazi mbalimbali zinazotekelezwa katika sekta zote hapa nchini. Ni dhahiri kwamba uongozi wake umekuwa ni chachu ya mabadiliko chanya na maendeleo endelevu katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kidiplomasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jinsi anavyochapa kazi na kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake katika kuliletea Taifa letu maendeleo. Hali kadhalika, kwa dhati kabisa nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la

Mapinduzi, kwa jitihada zake kubwa na za dhati za kuimarisha utendaji wenye malengo ya kuleta maendeleo Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kusimamia na kuratibu utendaji kazi na uwajibikaji Serikalini. Vilevile, kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kuteuliwa kumsaidia Waziri Mkuu na kutusimamia sisi Mawaziri katika kutekeleza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikupongeze wewe binafsi na Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa uliodhihirika katika kufikia maamuzi yenye manufaa kwa ustawi wa Taifa letu. Hakika mmesimama imara katika kuongoza mhimili huu muhimu wa kufanya maamuzi yenye tija kwa maendeleo ya Taifa letu. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kuwasaidia Mheshimiwa Spika kuongoza vyema vikao vya Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kuwapongeza Mawaziri wenzangu wote wa Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kupewa dhamana ya kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha nikiwa mmojawapo wa watekelezaji wa Ilani ya CCM nichukue fursa hii kuwapongeza viongozi wote walioteuliwa kushika nafasi mbalimbali za kumsaidia Mwenyekiti wetu wa Chama Cha Mapinduzi kusimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria

ikiongozwa na Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama, Mbunge wa Madaba na Makamu wake Mheshimiwa Florent Kyombo, Mbunge wa Nkenge, pamoja na Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024; na Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Maoni, ushauri na ushirikiano wa Kamati umetuwezesha kuboresha utendaji kazi wa Ofisi yetu na maandalizi ya hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi maalum kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi Maalum, Mheshimiwa George Huruma Mkuchika kwa namna anavyosaidia utekelezaji wa kazi maalum za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika yeye ni hazina na mchango wake umekuwa nguzo muhimu ya maamuzi mengi ya uendeshaji wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Mrisho Kikwete kwa jinsi anavyonisaidia katika kutekeleza majukumu ya Ofisi yetu. Nikuhakikishie kuwa kijana huyu ni makini, hodari na mchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Dkt. Moses M. Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi; Bwana Mululi M. Mahendeka, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu; Bwana Juma S. Mkomi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Bwana Xavier M. Daudi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Makamishna, Watendaji Wakuu wa Taasisi; Wakurugenzi na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais Ikulu na Menejimenti ya Utumishi

wa Umma na Utawala Bora kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi kufikia malengo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuzishukuru nchi wahisani na washirika wa maendeleo ambao wamechangia jitihada zetu za kuleta maendeleo kwa wananchi. Hivyo, nachukua fursa hii kuwashukuru na kuwataja wachache ambao ni: Jamhuri ya Watu wa China, Japan, Uingereza, India, Jamhuri ya Korea, Canada, Marekani, Sweden, Australia, Umoja wa Ulaya, Denmark, Norway, Uholanzi, Finland, Uswisi, Italy, Malaysia, Misri, Singapore, Cuba, Thailand na Ireland. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nayashukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ambayo ni: Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB*), Benki ya Dunia, *OFID-OPEC, Foreign Commonwealth Development Office (FCDO), KOICA, GIZ, USAID, SIDA, UNDP,* Jumuiya ya Madola, *DANIDA, JICA, UNICEF, ILO, WFP, UN Women, Global Fund,* Mfuko wa Fedha wa Kimataifa *(IMF)* na Taasisi ya *Bill and Melinda Gates Foundation*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kibakwe kwa kuendelea kunipa ushirikiano na kwa dua zao kwangu zinazonifanya nipate nguvu ya kuwatumikia Watanzania wote. Nawashukuru sana na tuendelee kushikamana kwa ajili ya maendeleo ya Jimbo letu la Kibakwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, nimshukuru sana mke wangu Mariana kwa ushirikiano anaonipa na kunitia moyo katika kutekeleza majukumu haya mazito ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi yetu ndio yenye dhamana ya kuwahudumia viongozi wakuu wastaafu wa Kitaifa. Kwa masikitiko makubwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha, Taifa letu liliondokewa na waliokuwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa ambao ni Hayati Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili na Hayati Edward Ngoyai Lowassa, Waziri Mkuu Mstaafu. Hivyo, naomba nitumie fursa hii adhimu kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wanafamilia wote, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na viongozi waliokuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa letu. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024, nchi yetu imekumbwa na maafa yaliyosababisha athari mbalimbali zikiwemo vifo, majeruhi, uharibifu wa mali na mazingira. Nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa na mali zao kutokana na maafa yaliyojitokeza. Mwenyezi Mungu awape marehemu pumziko la milele. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Mpango na Bajeti ya Ofisi na kuomba fedha ili kutekeleza majukumu ya Ofisi. Ninayo heshima kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kutoa taarifa ya utekelezaji wa Mpango ulioombewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na kuwasilisha Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango na Bajeti kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 ulitekelezwa kwa kuzingatia

miongozo ya Kitaifa ambayo ni: Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025; Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Hotuba ya Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kuhutubia Bunge la Kumi na Mbili tarehe 22 Aprili, 2021; pamoja na maelekezo yake mbalimbali. Aidha, utekelezaji umezingatia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (2021/2022 - 2025/2026), unaotaka Tanzania iwe ni nchi ya uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Fungu 20 na Ofisi ya Rais, Ikulu iliidhinishiwa shilingi bilioni 32.157 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi, 2024, shilingi bilioni 24.359 sawa na 75.75% zilipokelewa na kutumika. Vilevile Fungu 30 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri iliidhinishiwa shilingi bilioni 860.186. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 678.193 sawa na 78.84% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 181.992 sawa na 21.16% ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2024 shilingi bilioni 645.881 sawa na 75.09% zilipokelewa na kutumika ambapo shilingi bilioni 507.371 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 138.510 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Ofisi ya Rais Ikulu na taasisi zake (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Taasisi ya Uongozi, *TASAF* na Wakala wa Ndege za Serikali) imetekeleza shughuli mbalimbali kama zinavyoonekana katika kitabu chetu cha hotuba ambacho chote tunaomba kiingie kwenye *Hansard* (Taarifa Rasmi za Bunge) na inapatikana katika ukurasa wa tisa hadi ukurasa wa 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma

ilitengewa shilingi bilioni 12.763. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 10.813 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 1.950 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2024, kiasi cha shilingi bilioni 9.357 sawa na 73.32% kilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 8.982 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi milioni 374.717 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitekeleza shughuli zake kama zinavyoonekana katika hotuba yetu rasmi ukurasa wa 31 hadi 33.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedhawa 2023/2024, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Fungu 32 inayojumuisha Mamlaka na Taasisi zilizo chini yake, ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 69.317 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 57.130 sawa na 82.42% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 12.187, sawa na 17.58% ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2024 kiasi cha shilingi bilioni 42.280 sawa na 65.32% ya bajeti iliyotengwa kilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 40.5 zilikuwa ni matumizi ya kawaida na shilingi 4.753 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na taasisi zake, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Mamlaka ya Serikali Mtandao na Watumishi *Housing Investment* ilitekeleza shughuli mbalimbali kama

zinavyoonekana kuanzia ukurasa wa 33 hadi ukurasa wa 59 wa taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Fungu 67 ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 13.7 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 10.139, sawa na asilimia 73.9 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 3.572, sawa na asilimia 26.1 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2024, kiasi cha shilingi bilioni 9.737 sawa na asilimia 71.01 ya bajeti iliyotengwa kilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 7.3 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 2.4 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi imetekeleza shughuli mbalimbali kama zinavyoonekana katika ukurasa wa 60 hadi ukurasa wa 63.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma, Fungu 94 ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 8.6 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 8.3 sawa na 96.5% ni matumizi ya kawaida na shilingi milioni 300 sawa na 3.5% ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2024, shilingi bilioni 5.778 sawa na 67.01% zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 5.478 zilikuwa ni matumizi ya kawaida na shilingi milioni 300 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Tume imetekeleza shughuli kama zinavyoonekana katika taarifa yetu ukurasa wa 64 hadi 66.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 4.347. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 3.897 sawa na 90% ni kwa ajili matumizi ya kawaida na shilingi milioni 450 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya shilingi bilioni 2.4 sawa na 56% zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 2.26 ni matumizi ya kawaida na shilingi milioni 173.88 ni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo. Taarifa ya utekelezaji inaonekana kuanzia ukurasa wa 66 hadi wa 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nielezee Mpango wa Utekelezaji na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na mambo muhimu yatakayozingatiwa. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imepanga kutekeleza vipaumbele vyake kwa kuzingatia misingi ya utawala bora, sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali ya usimamizi wa utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi ya Rais, Ikulu, Fungu Namba 20 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 33.544 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, Fungu Namba 30 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 969.285 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 805.676 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 110.439 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa fedha za ndani na shilingi bilioni 53.169 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia maombi haya ya Ofisi ya Rais, Ikulu na taasisi zake, yaani Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Taasisi ya Uongozi, *TASAF*, Wakala wa Ndege za Serikali, Mamlaka za Serikali Mtandao na Baraza la Kumshauri Rais kuhusu Masuala ya Chakula na Kilimo, imepanga kutekeleza

shughuli mbalimbali kama ambavyo zinaonekana kuanzia ukurasa wa 71 hadi ukurasa wa 85.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Fungu Namba 33 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi 13,142,650,000; kati ya fedha hizo shilingi bilioni 11.6 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 1.5 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kupitia maombi hayo, Ofisi hii imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali kama zinavyoonekana kuanzia ukurasa wa 85 hadi 87.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Fungu Namba 32, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 58.314. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 48.254 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 9.9 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa fedha za ndani na shilingi milioni 127.7 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia maombi hayo ofisi hii imepanga kutekeleza shughuli kama zinavyoonekana katika hotuba yetu kuanzia ukurasa wa 88 hadi 97.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Fungu Namba 67 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 13.179. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 10.8 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 2.3 ni fedha za miradi ya maendeleo. Kupitia maombi haya ofisi imepanga kutekeleza majukumu yake kama yanavyoonekana katika ukurasa wa nane wa hotuba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Fungu Namba 94, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 9.24 ili kutekeleza shughuli zilizopo hapo juu. Kati ya fedha hizo shilingi

bilioni 8.7 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi milioni 500.176 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani. Majukumu yatakayotekelezwa yanaonekana kuanzia ukurasa wa 99 hadi ukurasa wa 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka, Fungu Na.4, inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 4.36. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 4.065 ni matumizi ya kawaida na shilingi milioni 295.7 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani. Majukumu yatakayotekelezwa yanapatikana katika ukurasa wa 101 hadi ukurasa wa 102.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; Bajeti ya Mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imelenga kuwa na Utumishi wa Umma unaotoa huduma bora kwa haraka na staha, ukizingatia Katiba, Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo katika kujenga imani zaidi kwa wananchi na kuendana na kauli ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa tarehe 22 Aprili, 2021 wakati akilihutubia Bunge la 12 aliposema, naomba kunukuu: "Tutawapima viongozi na watumishi kwa namna wanavyotimiza majukumu yao, hatutawaonea aibu viongozi na watumishi wazembe, wezi na wabadhirifu wa mali za umma. Tutaendeleza pia juhudi za kupambana na rushwa kwenye utumishi wa umma. Wajibu wa watumishi wa umma ni lazima uendane na haki zao." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendana na wakati, jitihada zaidi zitawekwa kwenye kujenga uwezo wa mifumo ya kimenejimenti na utoaji huduma, ikiwemo matumizi sahihi na salama ya fursa zinazopatikana katika utoaji huduma kwa TEHAMA ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, itawezesha utekelezaji wa majukumu ya vyombo vinavyosaidia kwenye maamuzi ya nchi, ulinzi na usalama, uimarishaji wa vita dhidi ya rushwa, usimamizi wa maadili ya viongozi wa umma, usimamizi wa rasilimali watu na rasilimali fedha katika utumishi wa umma, kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Hati Idhini, nawajibika kuwasilisha mapitio ya utekelezaji mipango na bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; na Ofisi ya Rais, Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na mpango na bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, sasa naomba kuwasilisha rasmi mapendekezo ya maombi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

(i) Matumizi ya kawaida ni shilingi 33,544,557,000.00 hili ni Fungu Na. 20.

(ii) Fungu Na. 30 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, matumizi ya kawaida ni shilingi 805,676,639,000.00, matumizi ya maendeleo ni shilingi bilioni 163,609,084,000.00.

(iii) Fungu Na. 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, matumizi ya kawaida ni shilingi

11,642,650,000 na miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 1.5.

(iv) Fungu Na. 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, matumizi ya kawaida ni shilingi 48,254,069,000.00, matumizi ya maendeleo ni shilingi 10,600,924,000.00.

(v) Fungu Na. 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Matumizi ya kawaida ni shilingi 10,831,831,000.00 na matumizi ya miradi ya maendeleo ni shilingi 2,348,047,000.00.

(vi) Fungu Na. 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma. Matumizi ya kawaida ni shilingi 8,740,713,000.00 na matumizi ya maendeleo ni shilingi 500,176,000.00.

(vii) Fungu Namba 04 Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa. Matumizi ya kawaida ni shilingi 4,065,013,000.00 na matumizi ya maendeleo ni shilingi 295,764,000.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla kuu ya bajeti ninayoomba kwa Mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2024/2025, ni kama ifuatavyo: Matumizi ya kawaida, jumla kuu ni shilingi 922,755,472,000.00. Matumizi ya miradi ya maendeleo ni shilingi 178,313,995,000.00. Jumla kuu kwa Mafungu yote ni shilingi 1,101,690,467,000.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba kuwasilisha maombi haya ili Bunge lako Tukufu liweze kuyajadili na kuyaidhinisha. Nashukuru sana kwa kunisikiliza na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**19 APRILI, 2024**

## HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA - MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/2025 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka 2023/24 na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30); Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33); Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Fungu 32); Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67); Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94); na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 04) kwa Mwaka 2024/25.

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema na huruma kwa kutujalia uzima, afya njema, amani na utulivu vinavyotuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu yanayochangia kuleta maendeleo na kujenga ustawi wa Taifa. Pia, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana katika kipindi hiki cha Mkutano wa 15 wa Bunge la 12 kwa ajili ya kupokea utekelezaji wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na kutafakari mipango ijayo katika kuyafikia malengo ya Nchi.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa imani yake kwangu na kuendelea

kunipa dhamana ya kusimamia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, yenye jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora, Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma na hatimaye kuwa na utumishi wa umma wenye ufanisi na uwajibikaji kwa ustawi wa Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kuliahidi Bunge lako Tukufu na Watanzania wote kuwa nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa uadilifu, bidii na weledi mkubwa ili kuendeleza mafanikio yaliyofikiwa na kuhakikisha kwamba Bajeti hii inasimamiwa vema na kutekelezwa ipasavyo. Ni dhahiri kwamba mafanikio makubwa yaliyofikiwa katika Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yametokana na maono makubwa ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan katika kuwaletea Watanzania maendeleo. Tunajivunia na kumshukuru Mungu kwa kuwa na kiongozi mwenye maono chanya kwa mustakabali wa Taifa letu. Naomba tuendelee kumuombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia afya thabiti, hekima, busara na ustahimilivu katika kuliongoza Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** nipende kutumia fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza kipindi cha miaka mitatu ya kuiongoza Nchi yetu kwa mafanikio makubwa yanayojidhihirisha kupitia kazi mbalimbali zinazotekelezwa katika sekta zote. Ni dhahiri kwamba uongozi wake umekuwa ni chachu ya mabadiliko chanya na maendeleo endelevu katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kidiplomasia.

**Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jinsi anavyochapa kazi

na kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake katika kuliletea Taifa letu maendeleo. Halikadhalika, kwa dhati kabisa nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa jitihada zake kubwa na za dhati za kuimarisha utendaji wenye malengo ya kuleta maendeleo Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kusimamia na kuratibu utendaji kazi na uwajibikaji Serikalini ambapo usimamizi, uratibu na ufuatiliaji wake umetoa mwangwi wa uwajibikaji katika Utumishi wa Umma. Vilevile, kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb) Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kuteuliwa kumsaidia Waziri Mkuu na kutusimamia sisi mawaziri katika kutekeleza majukumu yetu. Naahidi kuendelea kutoa ushirikiano wa dhati katika kusimamia Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**Mheshimiwa Spika,** naomba nikupongeze wewe binafsi pamoja na Naibu Spika kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa uliodhihirika katika kufikia maamuzi yenye manufaa kwa ustawi wa Taifa letu, hakika mmesimama imara katika kuongoza Muhimili huu muhimu kufanya maamuzi yenye tija kwa maendeleo ya Taifa na Mwenyezi Mungu aendelee kuwatia nguvu zaidi. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia Mheshimiwa Spika kuongoza vyema vikao vya Bunge letu, ni dhahiri kuwa muhimili huu wa Bunge umetoa mchango mkubwa kwenye maamuzi ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba nichukue nafasi hii pia kuwapongeza Mawaziri wenzangu wote wa Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kupewa dhamana ya kuwatumikia Watanzania na kwa kusimamia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya

2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Ilani ya CCM. Aidha nikiwa mmojawapo wa watekelezaji wa ilani ya CCM nichukue fursa hii kuwapongeza viongozi wote walioteuliwa kushika nafasi mbalimbali za kumsaidia mwenyekiti kusimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM. Tuendelee kushirikiana kutekeleza Ilani na miongozo mingine ya kitaifa ili kujenga Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala Katiba na Sheria ikiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Joseph K. Mhagama, Mbunge wa Madaba na Makamu wake Mheshimiwa Florent L. Kyondo, Mbunge wa Nkenge, pamoja na Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/24 na Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/25. Maoni, ushauri na ushirikiano wa Kamati umetuwezesha kuboresha utendaji kazi wa Ofisi yetu na maandalizi ya hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi maalum kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi Maalum, Mheshimiwa George Huruma Mkuchika kwa namna anavyosaidia Utekelezaji wa kazi maalum za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika yeye ni hazina na mchango wake umekuwa nguzo muhimu ya maamuzi mengi ya uendeshaji wa shughuli za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete kwa jinsi anavyonisaidia katika kutekeleza majukumu ya Ofisi yetu. Nikuhakikishie kuwa kijana huyu ni hodari, makini na mchapa kazi.

**Mheshimiwa Spika,** nawashukuru Dkt. Moses M. Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi; Bw. Mululi M. Mahendeka, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu; Bw. Juma S. Mkomi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Bw. Xavier M. Daudi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Makamishna, Watendaji Wakuu wa Taasisi; Wakurugenzi na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kazi nzuri wanazofanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi kufikia malengo yake, ikiwa ni pamoja na kukamilisha Hotuba hii kwa wakati. Aidha, napenda kuwashukuru waajiri na watumishi wote wa Umma kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi, uzalendo pamoja na imani yao kwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita ambao umeiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee napenda kuzishukuru Nchi Wahisani na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia jitihada zetu za kuleta maendeleo kwa wananchi. Hivyo, nachukua fursa hii kuwashukuru na kuwataja wachache ambao ni: Jamhuri ya Watu wa China, Japan, Uingereza, India, Jamhuri ya Korea, Canada, Marekani, Sweden, Australia, Umoja wa Ulaya, Denmark, Norway, Uholanzi, Finland, Uswisi, Italia, Malaysia, Misri, Singapore, Cuba, Thailand na Ireland. Vile vile, nayashukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ambayo ni: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), OFID-OPEC Fund for International Development, Foreign Commonwealth Development Office (FCDO), KOICA, GIZ, USAID, SIDA, UNDP, Jumuiya ya Madola, DANIDA, JICA, UNICEF, ILO, WFP, UN Women, Global Fund, Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) na Taasisi ya Bill and Melinda Gates Foundation.

**Mheshimiwa Spika,** natumia fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kibakwe kwa kuendelea kunipa ushirikiano na kwa dua zao wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi yetu ndio yenye dhamana ya kuwahudumia viongozi wakuu wa kitaifa wastaafu. Kwa masikitiko makubwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha Taifa liliondokewa na waliokuwa viongozi wakuu wa kitaifa ambao ni Hayati Ali Hassan Mwinyi, Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili na Hayati Edward Ngoyai Lowassa, Waziri Mkuu Mstaafu. Hivyo, ninaomba nitumie fursa hii adhimu kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, wanafamilia wote, Bunge lako Tukufu, ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na viongozi waliokuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/24 nchi yetu imekumbwa na maafa yaliyosababisha athari mbalimbali zikiwemo vifo, majeruhi, uharibifu wa mali na mazingira. Nitumie fursa hii kuwapa pole Watanzania wote waliopoteza ndugu, jamaa na mali zao kutokana na maafa hayo. Mwenyezi Mungu awape marehemu pumziko la milele. Amina!


**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/24 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Mpango na Bajeti ya Ofisi na kuomba fedha ili kutekeleza majukumu ya Ofisi. Ninayo heshima kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kutoa taarifa ya utekelezaji wa Mpango ulioombewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 na kuwasilisha Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/25.

19 APRILI, 2024

1925 - 2024

# HAYATI ALI HASSAN MWINYI

RAIS MSTAAFU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



**“Pamoja na umuhimu wa uvumilivu, ni vyema viongozi wakawa wapenda na watenda haki kwa dhati, wanaojua na kuheshimu kwa vitendo haki za raia, na kujali usawa wa binadamu.”**

*Hayati Ali Hassan Mwinyi*

**19 APRILI, 2024**


**1953 - 2024**

# HAYATI EDWARD NGOYAI LOWASSA

WAZIRI MKUU MSTAAFU WA JAMHURI
YA MUUNGANO WA TANZANIA

**“Mabadiliko ni fıkra.
Ni kufikiri na kutenda tofauti.”**

*Hayati Lowassa*



## MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA WA FEDHA 2023/24

**Mheshimiwa Spika,** Mpango na Bajeti kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/24 ulitekelezwa kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa ambayo ni Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Hotuba ya Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kuhutubia Bunge la 12 tarehe 22 Aprili, 2021 pamoja na maelekezo yake mbalimbali. Aidha, utekelezaji umezingatia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (2021/22 2025/26), unaotaka Tanzania iwe na Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

## OFISI YA RAIS - IKULU NA TAASISI ZAKE

### A. Ofisi ya Rais – Ikulu

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24, Fungu: 20 Ofisi ya Rais, Ikulu iliidhinishiwa **shilingi 32,157,384,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2024 **shilingi 24,359,080,531.40** sawa na **asilimia 75.75** zilipokelewa na kutumika.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake mwaka 2023/24, Fungu 30 Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inayojumuisha taasisi zilizo chini ya Ikulu, **iliidhinishiwa shilingi 860,186,476,000.00** Kati ya fedha hizo, **shilingi 678,193,941,000.00** sawa na asilimia 78.84 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 181,992,535,000.00** sawa na **asilimia 21.16** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2024 **shilingi 645,881,733,209.54** sawa na **asilimia 75.09** zilipokelewa na

kutumika ambapo **shilingi 507,371,469,218.81** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 138,510,263,990.73** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Yafuatayo ni maelezo ya matumizi kwa kila taasisi:

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais, Ikulu imeendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali na nchi nzima. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, kazi zifuatazo zilitekelezwa:

(i) Ushauri umetolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia, Mawasiliano na Habari, Uhusiano wa Kikanda, Kimataifa na masuala mengine muhimu kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi;

(ii) Ofisi imewezesha utekelezaji wa ratiba ya kila siku ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutekeleza shughuli zake kama zilivyopangwa;

(iii) Huduma zimeendelea kutolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na familia yake;

(iv) Mikutano (10) ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo nyaraka 31 zilijadiliwa na kutolewa uamuzi. Vikao vitano (5) vya Kamati ya Katiba na Sheria ya Baraza la Mawaziri vilifanyika ambapo miswada 15 ilijadiliwa. Aidha, mikutano 12 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) ilifanyika ambapo nyaraka 32 zilijadiliwa na kutolewa maoni na ushauri. Vilevile, mikutano ya kazi sita (6) ya Makatibu Wakuu ilifanyika ambapo taarifa 15 zilijadiliwa na kutolewa ushauri wa namna ya kuboresha utekelezaji wake na kujenga uelewa wa pamoja;

(v) Mikutano 18 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo nyaraka 37 zilijadiliwa na kutolewa maoni na ushauri. Aidha, mikutano ya kazi miwili (2) ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo taarifa mbili (2) zilijadiliwa na kutolewa maoni na ushauri;

(vi) Kumbukumbu za Mikutano ya Baraza la Mawaziri, Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ziliandaliwa na kusambazwa kwa wahusika kwa rejea na hatua za utekelezaji. Aidha, ufuatiliaji na tathmini ya Maamuzi ya Baraza la Mawaziri ulifanyika na taarifa iliandaliwa. Vilevile, Taarifa ya Utekelezaji wa Uamuzi na Shughuli za Baraza la Mawaziri kwa kipindi cha kuanzia Januari, 2021 hadi Desemba, 2023 imeandaliwa na kuchapishwa;

(vii) Mafunzo ya kujenga uwezo kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne (NACSAP IV) kwa Wajumbe 1,050 wa Kamati za Uadilifu za Mikoa 26 na Halmashauri 184, wajumbe 199 wa Taasisi nyingine za Umma na wajumbe 112 wa Taasisi zisizo za Serikali yamefanyika Mkoani Arusha;

(viii) Uratibu wa kikao kimoja cha Makatibu Wakuu wanaosimamia utekelezaji wa Programu za Maboresho nchini na kikao cha Waratibu wa Programu za Maboresho umefanyika ili kuimarisha usimamizi, uongozi na umiliki wa mchakato wa maboresho katika sekta ya umma nchini;

(ix) Uratibu wa Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu Kitaifa umefanyika tarehe 10 Desemba 2023 yakijumuisha Taasisi za Umma na AZAKI;

(x) Jukwaa la Kitaifa la Juhudi Dhidi ya Rushwa limefanyika;

(xi) Ziara za ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa zimefanyika katika Wizara zote na katika Mikoa ya Manyara, Arusha na Kilimanjaro;

(xii) Rufaa 749 zilipokelewa na kati ya rufaa hizo rufaa 144, zimechambuliwa na kutolewa uamuzi. Aidha, malalamiko 466 yamepokelewa, yamechambuliwa na kutolewa uamuzi;

(xiii) Maafisa wa Serikali 490 wamepatiwa mafunzo kuhusu ushughulikiaji wa rufaa na malalamiko;

(xiv) Ujenzi wa uzio kuzunguka jengo la Ofisi Chamwino umefikia asilimia 50 ya utekelezaji. Aidha, ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la Mapokezi Chamwino unaendelea na umefikia asilimia 90; na

(xv) Ukarabati wa uzio wa majengo saidizi katika Ikulu Ndogo Arusha unaendelea na ujenzi umefikia asilimia 98. Aidha, ujenzi wa jengo jipya la Ikulu Ndogo Arusha umefikia asilimia 70.

**B. Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)**

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329. Majukumu hayo ni pamoja na kuchukua hatua stahiki za kuzuia na kupambana na rushwa kwenye sekta ya umma, mashirika na sekta binafsi kwa kuchambua mifumo ya utendaji kazi na utoaji huduma, kuishauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu rushwa, kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa, kuwafikisha watuhumiwa wa tuhuma za rushwa na ufisadi mahakamani pamoja na kuelimisha umma kuhusu madhara ya rushwa, wajibu

wao wa kushiriki kwenye kuzuia na kupambana na rushwa na juhudi za Serikali katika kukabiliana na rushwa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza dhamira ya Serikali ya kutokomeza rushwa nchini jitihada zimeongezwa kwenye kuzuia vitendo vya rushwa katika maeneo yote ambapo katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024 kazi zifuatazo zilitekelezwa:

**Uzuiaji Rushwa**

(i) Miradi ya maendeleo 1,086 yenye thamani ya Shilingi bilioni 743.90 ilifuatiliwa ambapo miradi 179 yenye thamani ya Shilingi bilioni 61.01 ilibainika kuwa na kasoro mbalimbali na kupelekea kuanzishiwa uchunguzi ili hatua stahiki zichukuliwe. Aidha, elimu imetolewa kwa watekelezaji wa miradi 482 kuhusu usimamizi wa miradi na miradi 316 imefanyiwa udhibiti ili ikamilishwe kama ilivyopangwa kwa mujibu wa mikataba ya kazi hizo;

(ii) Uchambuzi wa mifumo 446 umefanyika kwa lengo la kubaini mianya ya rushwa katika maeneo ya Huduma za Jamii, Fedha, Majengo, Utawala, Usafirishaji, Biashara, Umeme, Kilimo na Misitu. Kutokana na chambuzi hizi mapendekezo ya kuziba mianya ya rushwa yalitolewa;

(iii) Vikao kazi 252 vya wadau vilifanyika na kazi 79 za ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikakati ya kuziba mianya ya rushwa iliyobainishwa katika matokeo ya kazi za utafiti, uchambuzi wa mifumo na ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma katika miradi ya maendeleo zilifanyika; na

(iv) Kupitia Mpango wa TAKUKURU RAFIKI, mikutano 1,039 imefanyika na jumla ya kero 8,708 ziliibuliwa ambapo kati ya kero hizo, kero 5,061 zimepatiwa ufumbuzi katika sekta za

Afya, Elimu, Maji, Nishati, Ujenzi, Utawala, Ardhi, Kilimo, Polisi, Usafirishaji na Ufugaji.

**Uelimishaji Umma**

(i) Kushiriki katika Siku ya Mapambano Dhidi ya Rushwa Barani Afrika, sambamba na maadhimisho ya miaka 20 ya utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa (AUCPCC) tarehe 11 Julai, 2023 Mkoani Arusha. Maadhimisho haya yaliandaliwa kwa kushirikisha Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi (ZAECA) na Bodi ya Ushauri wa Mapambano dhidi ya Rushwa Afrika (AUABC);

(ii) Klabu za wapinga rushwa 128 zilifunguliwa katika shule za msingi na sekondari, Klabu za wapinga rushwa 4,797 ziliimarishwa na taasisi imeendelea kuelimisha vijana wa SKAUTI ili kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa kupitia kazi. Vilevile, TAKUKURU imeendelea kushirikiana na asasi zisizokuwa za kiserikali zinazoshiriki kupambana na rushwa katika kuelimisha umma. Mfano wa asasi hizo ni Anti-Corruption Voices Foundation (ACVF) iliyoshiriki katika maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu 2023 kupitia kampeni yao ya Badili Tabia Sepesha Rushwa inayohamasisha na kuwashirikisha vijana wengi kushiriki mapambano dhidi ya rushwa;







1. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akipokea Taarifa ya Utendaji Kazi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kwa mwaka 2022/2023 kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo CP. Salum Hamduni Ikulu Chamwino jijini Dodoma tarehe 28 Machi,2024.
2. Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Ridhiwani Kikwete akiwaonyesha Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ramani ya jengo linaloendelea kujengwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kabla ya kukagua jengo hilo mkoani Iringa.

(iii) Mafunzo yalitolewa kwa Maafisa wa uelimishaji Umma wa TAKUKURU Makao Makuu na Mikoa na Maafisa wa DCEA kwa lengo la kuwajengea uwezo katika kuzuia na kupambana na rushwa, biashara haramu na matumizi ya dawa za kulevya. Mafunzo hayo yaliambatana na uzinduzi wa kampeni ya "Tokomeza Rushwa na Dawa za Kulevya Shuleni na Vyuoni" yenye lengo la kupinga rushwa na dawa za kulevya hususani kwa vijana, yenye kauli mbiu isemayo "Kataa Rushwa, Kudhibiti Dawa za Kulevya";

(iv) TAKUKURU imeendelea kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) kwenye uboreshaji wa mitaala ya Elimu nchini, itakayohusisha ufundishwaji wa masuala ya rushwa kuanzia ngazi ya Elimu ya awali hadi Chuo Kikuu. Aidha, maudhui ya rushwa yameingizwa katika kitabu cha darasa la tatu "Historia ya Tanzania na Maadili" na kidato cha kwanza, mchakato wa kuingiza maudhui ya rushwa kwa darasa la 4 hadi 6, na kidato cha 2 hadi 6 unaendelea;

(v) Elimu ya utambuzi wa haki na wajibu wa namna ya kutoa taarifa za vitendo vya rushwa imefanyika kwa kuendesha semina 2,873, mikutano ya hadhara na mijadala ya wazi 2,680 kwa wadau mbalimbali wa kupambana na rushwa wakiwemo viongozi na watumishi wa Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, sekta binafsi, wanachama wa vyama vya ushirika, wanafunzi wa shule, vyuo vya kati na vyuo vikuu, viongozi wa taasisi za kidini, viongozi na wanachama wa vyama vya siasa, wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla;

(vi) Kushiriki maonesho 296 ya kitaifa na kimataifa kama vile maonesho ya Wiki ya Sheria, Wiki ya Maadili na Haki za Binadamu, Sabasaba, Nanenane, Madini, na Mbio za Mwenge wa Uhuru. Maonesho hayo yalitoa fursa kwa

wananchi kuuliza maswali, kutoa maoni, ushauri na taarifa za vitendo vya rushwa;

(vii) TAKUKURU imeendelea Kushirikiana na vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kwa kutoa elimu kuhusu mapambano dhidi ya rushwa ambapo vipindi 370 vya redio na televisheni vimerushwa kupitia redio na televisheni mbalimbali, vipindi/ Makala za video 45 vimeandaliwa na kurushwa kupitia televisheni mtandao ya TAKUKURU TV na matangazo (graphic adverts) 41 yameandaliwa na kusambazwa katika mitandao ya kijamii; na

(viii) Elimu kwa njia ya runinga imetolewa kwa kufanya maonesho matatu (3), makala za picha zinazohamasisha wananchi kushiriki kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo zilirushwa wakati wa Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2023, ambapo wananchi 1,850 walifikiwa na elimu hiyo.

**Uchunguzi na Mashtaka**

(i) Kesi 767 ziliendeshwa mahakamani zikiwemo kesi mpya 314. Kati ya kesi mpya zilizofunguliwa mahakamani tatu (3) ni kesi ambazo kila moja thamani yake inaanzia shilingi bilioni 1 na kuendelea, ambazo zilifunguliwa katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi. Kesi 259 ziliamuliwa mahakamani ambapo Jamhuri ilishinda kesi 175 kwa watuhumiwa kuhukumiwa kifungo au/na kulipa faini. Hadi kufikia Machi, 2024 kesi 453 zilikuwa zinaendelea mahakamani. Aidha, kiasi cha Shilingi bilioni 15.40 zimeokolewa kutokana na operesheni mbalimbali za uchunguzi uliofanyika kote nchini ambapo Shilingi bilioni 14.46 ni fedha taslimu zilizorejeshwa Serikalini na Shilingi bilioni 1.04 zilidhibitiwa; na

(ii) Mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 unaendelea na maoni kutoka kwa wadau yamekusanywa. Aidha, rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri imeandaliwa tayari kwa kuwasilishwa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

**Uwezeshaji**

(i) Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya TAKUKURU Makao Makuu umefikia asimilia 92 ya awamu kwanza. Majengo mengine yanayojengwa ni pamoja na Ofisi ya Mkoa wa Iringa (39%), Ofisi ya Wilaya ya Nzega (42%), Ofisi ya Wilaya ya Kishapu (60%), Ofisi ya Wilaya ya Monduli (54%), Ofisi ya Wilaya ya Rombo (45%). Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkoa wa Shinyanga, Wilaya ya Nkasi na ukarabati wa Ofisi ya Bagamoyo na Majengo ya makazi ya Watumishi Mtwara upo katika hatua za awali za manunuzi. Ukarabati wa jengo la Wilaya ya Kahama umekamilika kwa asilimia 100. Ukarabati wa majengo ya Wilaya ya Newala umefikia asilimia 90. Aidha, kazi ya ukarabati wa majengo ya Ofisi na makazi ya watumishi Makao Makuu inaendelea;

(ii) Mifumo ya TEHAMA imeimarishwa kwa kukamilisha usimikaji wa mtandao kiambo katika Ofisi za mikoa ya Simiyu na Morogoro pamoja Ofisi za Wilaya za Nyasa, Momba, Ngorongoro, Manyoni, Chamwino, Mpwapwa, Liwale, Masasi, Namtumbo, na Mvomero. Aidha, ukarabati wa Mtandao Kiambo katika Ofisi ya Mkoa wa Temeke na matengenezo kinga ya vifaa vya TEHAMA yamefanyika; na

(iii) Watumishi 805 wamejengewa uwezo ili kuongeza weledi wa kutekeleza majukumu kwa ufanisi.

B. Taasisi ya UONGOZI

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya UONGOZI imeendelea kusimamia malengo yake ya kuwa Kituo cha utaalam wa hali ya juu cha kuendeleza Viongozi Barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania, Ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika kwa ujumla. Walengwa ni Viongozi Waandamizi waliopo na wanaojitokeza wakiwemo wanasiasa, watumishi wa Serikali na Mahakama. Katika kipindi cha mwezi Julai, 2023 hadi Machi, 2024 kazi zifuatazo zilitekelezwa:

(i) Mafunzo ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi yametolewa kwa Maafisa Waandamizi 37 kutoka Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma, Taasisi za Kiraia na Taasisi Binafsi ambapo Moduli tisa (9) zilitolewa kama ilivyopangwa. Moduli hizo zilihusu Uongozi Binafsi na wa Shirika, Kutunga na Kutekeleza Mikakati, Ujuzi wa Fedha kwa Wasimamizi, Kuongoza kwa Matokeo, Mbinu za Ubunifu kwa Maendeleo ya Shirika, Maendeleo Endelevu, Mawasiliano ya Kimkakati pamoja na Usimamizi wa Kimkakati wa Rasilimali watu;

(ii) Mafunzo katika ngazi ya cheti yametolewa kwa viongozi 90 kutoka Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma, Taasisi za kiraia na Taasisi Binafsi. Jumla ya moduli kumi zilitolewa kwa washiriki juu ya Misingi ya Ufahamu wa Kihisia, Misingi ya Kuongoza Mabadiliko, Misingi ya Takwimu na Uchanganuzi pamoja na Usimamizi wa Rasilimali Fedha. Idadi ya washiriki imeongezeka kutoka 65 waliopangwa awali kutokana na uhitaji mkubwa wa mafunzo kutoka benki ya NBC. Hii imesababisha pia kuongezeka kwa moduli zilizopangwa kutolewa kutoka 3 mpaka 10;

(iii) Programu mahususi kwa viongozi wanawake ilitekelezwa ambapo wanawake viongozi 100 kutoka Taasisi za Umma,

Taasisi Binafsi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali walishiriki. Aidha, baadhi ya washiriki walitoka nje ya nchi zikiwemo Nigeria, Malawi, Kenya, Eswatini na Jamhuri ya Demokrasia Congo (DRC). Programu hii inalenga kuchangia jitihada za kitaifa katika kushughulikia suala la uwakilishi mdogo wa wanawake katika nafasi za juu za maamuzi katika Serikali, siasa, biashara na taasisi za kiraia. Lengo la kutoa mafunzo kwa viongozi wanawake 50 limevukwa kutokana na wadau wa Maendeleo ambao ni Umoja wa Ulaya, kupitia shirika la UN Women kuvutiwa na Programu na kutoa ufadhili;

(iv) Kutoa mafunzo ya kozi fupi ambapo Jumla ya kozi 50 zimetolewa kwa viongozi 3,611. Mafunzo haya yalilenga kuimarisha uwezo wa viongozi kufanya maamuzi ya kimkakati, kuongoza rasilimaliwatu na matumizi ya rasilimali nyingine, na uongozi binafsi. Taasisi imeweza kuvuka lengo la kutoa kozi 40 kwa kipindi hiki kutokana na mahitaji makubwa kutoka kwa wadau;

(v) Bodi za Wakurugenzi wa Taasisi na Mashirika ya Umma 23 zimepatiwa mafunzo ya kujenga uwezo kuhusu uongozi wa kimkakati, usimamizi wa rasilimali za umma, usimamizi wa rasilimaliwatu na usimamizi wa viashiria hatarishi kwa ajili ya kuongeza ufanisi, uwajibikaji na uzalendo wa utendaji wa kazi katika mashirika;

## 19 APRILI, 2024







1. Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan akifunga semina ya mafunzo ya uongozi kwa Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala Tanzania Bara - Agosti 2023.

2. Sherehe ya utoaji vyeti kwa wahitimu wa Programu ya Uongozi ngazi ya Cheti kutoka Benki ya NBC, iliyokuwa na uwepo wa Dkt. Laurean Ndumbaro, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Taasisi ya Uongozi, kama Mgeni Rasmi. Wageni muhimu wengine waliohudhuria tukio hilo ni wakufunzi wa programu kutoka Chuo Kikuu cha Aalto (Finland).




3.Mheshimiwa George B. Simbachawene (kushoto) na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete (Katikati) wakifuatilia wasilisho la utekelezaji wa shughuli na programu za Taasisi ya UONGOZI wakati wa ziara yao kwenye Taasisi hiyo Julai 2023. Kulia ni Bw. Kadari Singo, Afisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya UONGOZI.

(vi) Tafiti mbili (2) zimeendelea kutekelezwa kuhusu "Uandaaji na Uendelezaji wa Viongozi Nchini Tanzania" na "Mchango wa Viongozi Wanawake kwenye Maendeleo ya Taifa". Aidha, Tafiti tatu (3) kuhusu utekelezaji wa Sera ya Uwekezaji, Usimamizi mathubuti wa Maliasili, na madini ya kimkakati zimeanza kutekelezwa;

(vii) Uandishi wa Tawasifu ya Hayati Rashid Mfaume Kawawa, Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uko katika hatua za awali ambapo mwandishi ameainishwa na kazi imeanza mwezi Februari 2024;

(viii) Kwa kushirikiana na taasisi za ndani na nje ya nchi, jumla ya makongamano manne (4) yaliyokuwa na ushiriki wa viongozi 1,222 yalifanyika. Lengo la makongamano haya ni kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu na kuwaongezea uelewa wa masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu. Taasisi iliweza kuvuka malengo iliyojiwekea ya kufanya makongamano matatu (3) kwa kipindi cha nusu mwaka kutokana na ongezeko la Taasisi kuomba kushirikiana katika kuandaa makongamano ya kisera nchini;

(ix) Vipindi viwili (2) vya mahojiano na viongozi waandamizi na wataalam wa masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu viliandaliwa na kufanyika kama ilivyopangwa. Viongozi waliohojiwa ni pamoja na Mheshimiwa Joaquim Alberto Chissano, Rais Mstaafu wa Msumbiji; na Dkt. Agness Kalibata, Rais wa "Alliance for a Green Revolution in Africa" (AGRA);

(x) Ushauri wa kitaalam kuhusu kutengeneza mitaala, kuboresha mifumo, kuratibu michakato ya kupata maoni kwa wadau na kuendesha mikutano, umetolewa kwa Taasisi Tano (5) za Serikali ambazo ni Ofisi ya Waziri Mkuu, Tume ya Mipango, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Sekretarieti ya Maadili; na

(xi) Habari na machapisho mbalimbali kuhusu shughuli zinazofanywa na Taasisi na Masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu zilitolewa kwa njia mbalimbali za mawasiliano ikiwemo vipeperushi vinne (4) na ripoti mbili (2). Aidha, taarifa 62 kwa vyombo vya habari, picha 2,750 za matukio, makala 12 za magazeti na video zilisambazwa kwa wadau wa Taasisi ya UONGOZI kupitia mitandao ya kijamii X (twitter), YouTube, LinkedIn, Instagram, Facebook na WhatsApp).

## C. Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) umeendelea kutekeleza Awamu ya Tatu ya TASAF kwa kuweka kipaumbele kwenye maeneo ya Ukuzaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; Kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii; na Utawala bora na uwajibikaji. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi, 2024, Mfuko wa Maendeleo Jamii (TASAF) umetekeleza kazi zifuatazo:

(i) Uhakiki wa kaya katika Mamlaka 135 za utekelezaji ili kutambua hali za ustawi wa maisha ya kaya za walengwa wa Mpango umefanyika ambapo jumla ya kaya 607,995 zilihakikiwa. Aidha, uchakataji wa takwimu unaendelea ili kubaini kaya ambazo zitaendelea kuwepo katika Mpango na kaya ambazo zimeboreka kiuchumi;

(ii) Ruzuku ya shilingi bilioni 169 ilihawilishwa kwa kaya za walengwa 1,336,600 zenye jumla ya wanakaya 5,164,333 kutoka katika maeneo 186 ya utekelezaji kwa Tanzania Bara, Unguja na Pemba kwa Zanzibar ili waweze kujikimu na mahitaji ya msingi;

(iii) Jumla ya miradi 10,442 ya ajira za muda iliibuliwa na jamii na kuanza kutekelezwa katika maeneo ya utekelezaji 123 ambapo kaya za Walengwa 609,114 zinashiriki kutekeleza miradi hiyo yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 105.7. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 11.6 kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi na shilingi bilioni 94.1 kwa ajili ya ujira wa kaya za walengwa wanaofanya kazi katika miradi hiyo;

(iv) Miradi 1,037 ya kuendeleza miundombinu iliibuliwa na utekelezaji wake upo katika hatua mbalimbali ambapo Miradi 252 katika sekta ya elimu, afya, maji, mazingira,

barabara za vijijini na ujasiriamali imekamilika na kuanza kutoa huduma. Jumla ya shilingi bilioni 65.01 zimetumika katika utekelezaji wa miradi hiyo na jumla ya Wataalam 120 kutoka Mamlaka za utekelezaji wa Mpango 25 walipatiwa mafunzo ya uwezeshaji na usimamizi wa miradi hiyo;

(v) Jumla ya vikundi 6,527 vyenye wanachama 87,913 katika Mamlaka 35 za Utekelezaji Tanzania Bara vimeundwa. Walengwa 17,931 kutoka kwenye maeneo ya utekelezaji 35 wamepewa ruzuku ya uzalishaji yenye thamani ya shilingi bilioni 1.7 ili waweze kuanzisha shughuli za kiuchumi. Aidha, mafunzo kwa wawezeshaji 808 kuhusu uhamasishaji na uundaji wa vikundi, uwekaji kumbukumbu za taarifa za fedha, usimamizi wa mikopo na utatuzi wa migogoro yamefanyika;

(vi) Walengwa 503,618 sawa na asilimia 38 ya walengwa wote walilipwa kwa njia ya kielektroniki kwa malipo ya kipindi cha Septemba – Oktoba, 2023 ambapo asilimia 49 walilipwa kupitia Benki na asilimia 51 walilipwa kwa mitandao ya simu. Zaidi ya shilingi bilioni 18 zililipwa kwa walengwa hao. Uhamasishaji unaendelea ili kuandikisha walengwa zaidi katika mfumo huu. Aidha, Katika kuongeza uwazi na uwajibikaji mfumo umewezeshwa kutuma muhtasari wa taarifa za malipo kwa njia ya simu kwa viongozi wa Vijiji/Mitaa/Shehia kabla ya siku ya malipo;

(vii) Taarifa ya Tathmini ya awali ya Kipindi cha Pili cha Mpango imeandaliwa na kuzinduliwa Mwezi Novemba, 2023; na

**19 APRILI, 2024**



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama na wajumbe wa kamati hiyo wakitoka kukagua ujenzi wa stendi ya mabasi Peramiho-Lundusi wakati kamati hiyo ilipofanya ziara ya kikazi kwa lengo la kukagua mradi huo kupitia TASAF. Wengine ni Viongozi na Watendaji wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na wananchi wa eneo hilo.

## 19 APRILI, 2024







1. Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, akiungana na wanafunzi wa Skuli ya Msingi Kiwani katika kuimba wimbo wa Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar mara baada ya ufunguzi wa Kituo cha Afya Daraja la Pili cha Kendwa, Pemba.

2. Mwonekano wa kabla na baada ya ujenzi wa Kituo cha Afya Daraja la Pili cha Kendwa, Pemba.

## 19 APRILI, 2024





(viii) Mapitio ya pamoja baina ya Serikali na Wadau wa Maendeleo kuhusu utekelezaji wa Mpango yamefanyika katika kipindi cha Julai, 2023. Aidha, Wadau wa Maendeleo na walengwa walionesha kuridhishwa na namna Serikali inavyotekeleza shughuli za mpango.

## D. Wakala wa Ndege za Serikali

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Ndege za Serikali ina jukumu la kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa. Wakala ilianzishwa ili kuboresha huduma na kuimarisha usalama wa usafiri wa ndege kwa Viongozi wanaotumia huduma hizo. Aidha, Wakala imeongezewa jukumu lingine la kuratibu kwa niaba ya Serikali, ununuzi wa ndege, kuzikodisha kwa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) na kusimamia mikataba ya ukodishwaji wa ndege hizo. Katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024 kazi zifuatazo zimetekelezwa:

(i) Huduma ya usafiri wa anga imeendelea kutolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa;

(ii) Matengenezo makubwa ya ndege aina ya Gulfstream G550 yamefanyika kwa mujibu wa Kalenda ya matengenezo;

(iii) Hatua ya awali ya ukarabati na upanuzi wa Karakana ya Ndege za Serikali katika Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere iliyohusisha ubomoaji wa karakana iliyokuwa ikitumika umekamilika. Aidha, kazi ya ujenzi na upanuzi wa Karakana hiyo inaendelea;

(iv) Wanaanga 53 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi ili kuhuisha leseni zao pamoja na mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi wengine 23;

(v) Gharama za bima za ndege pamoja na bima za Wanaanga zimelipwa; na

(vi) Ununuzi wa ndege mpya tatu (3) kwa niaba ya Serikali umeratibiwa na mikataba ya ukodishwaji wa ndege za Serikali kwa Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL) imesimamiwa.




Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwa kwenye picha ya pamoja na viongozi wengine wakati wa mapokezi ya ndege mpya aina ya Boeing 737-9MAX

## OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2023/24, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitengewa **shilingi 12,763,016,000.00.** Kati ya fedha hizo **shilingi 10,813,016,000.00ni** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 1,950,000,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2024 fedha zilizopokelewa na kutumika ni **shilingi 9,357,430,675.20** sawa na **asilimia 73.32.** Kati ya fedha hizo **shilingi 8,982,713,424.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 374,717,251.20** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitekeleza kazi zifuatazo:

(i) Matamko ya viongozi wa Umma kuhusu rasilimali na madeni yapatayo 15,756 kati ya 15,893 yamepokelewa ikiwa ni sawa na asimilia 99 ya matarajio hadi kufikia Desemba, 2023. Aidha, elimu kwa viongozi wa Umma imeendelea kutolewa;

(ii) Malalamiko 164 ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma yalipokelewa na kuchambuliwa. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 113 yalihusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na malalamiko 51 hayakuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma hivyo yalipelekwa kwa taasisi husika. Aidha, uchunguzi wa malalamiko unaendelea ambapo ushauri na maridhiano baina ya mlalamikiwa na mlalamikaji unaendelea kufanyika;

(iii) Uchunguzi wa malalamiko 17 yaliyopokelewa dhidi ya Viongozi wa Umma kuhusu tuhuma za ukiukwaji wa Sheria ya Maadili umefanyika ambapo taarifa zimewasilishwa kwa Mamlaka za Nidhamu za Viongozi husika kwa ajili ya kufanya

maamuzi. Aidha, uchunguzi kwa tuhuma 96 bado unaendelea;

(iv) Uhakiki wa matamko ya Rasilimali na Madeni ya viongozi wa umma pamoja na utambuzi wa Mgongano wa Maslahi kwa viongozi wa Umma ulifanyika kwa viongozi 470. Matokeo ya uhakiki yanaonesha kuwa asilimia 87 ya waliohakikiwa, hawakukutwa na kasoro katika matamko yao na asilimia 13 wamebainika kuwa na kasoro katika Matamko yao ambapo wanaume ni asilimia 76 na wanawake ni asilimia 24. Viongozi wenye kasoro watafanyiwa uchunguzi wa kina na ambao tuhuma zitathibitika watafikishwa kwenye Baraza la Maadili;

(v) Malalamiko mawili (2) yalifikishwa mbele ya Baraza la Maadili kwa ajili ya uchunguzi wa kina. Idadi ya malalamiko imepungua kutoka malalamiko tisa (9) hadi mawili (2) kutokana na kukosekana kwa malalamiko yaliyokidhi vigezo vya kufikishwa kwenye Baraza la Maadili;

(vi) Elimu kwa Viongozi wa Umma, watumishi wa umma, wananchi na wadau 13,468 kuhusu maadili na dhana ya Mgongano wa Maslahi ilitolewa, Aidha, wadau 1,033 kutoka katika taasisi tano (5) na halmashauri 15 walifikiwa kupitia programu ya uwajibikaji wa pamoja kwa viongozi wa umma; na

(vii) Klabu 263 za Maadili katika shule za msingi 189, sekondari 72 na vyuo viwili 2 zilianzishwa zikiwa na wanachama 2,784. Klabu husika zilianzishwa katika Kanda za Kaskazini, Maalum, Magharibi na Mashariki. Aidha, klabu za maadili 41 zilitembelewa kwa lengo la kuwajengea uwezo wanafunzi katika misingi ya uadilifu na kusisitiza katika uzingatiaji wa maadili kwa maendeleo ya taaluma pamoja na kufanya

ufuatiliaji kuhusu utendaji wa klabu husika ikiwa ni kuwaandaa kuwa viongozi waadilifu wa kesho;

**OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA NA TAASISI ZAKE**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2023/24, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Fungu 32 inayojumuisha Mamlaka na Taasisi zilizo chini yake ilitengewa jumla ya **shilingi 69,317,460,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **shilingi 57,130,005,000.04** sawa na asilimia 82.42 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 12,187,455,000.00** sawa na **asilimia 17.58** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2024 kiasi cha **shilingi 45,280,059,705.77** sawa na **asilimia 65.32** ya bajeti iliyotengwa kilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **shilingi 40,526,557,802.56** zilikuwa ni matumizi ya kawaida na **shilingi 4,753,501,903.21** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**A. Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Machi, 2024 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na taasisi zake, ilitekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Taasisi za Umma 570 zimejengewa uwezo na kuwezeshwa kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma (PEPMIS & PIPMIS) ambapo yalihusisha hatua za utekelezaji wa mfumo zikiwemo kupanga, kufuatilia utekelezaji, kuhuisha mpango, kufanya tathmini ya utendaji kazi wa watumishi na taasisi.

(ii) Watumishi wa Umma 589,076 kati ya 603,699 ambao ni sawa na asilimia 97.6 wamesajiliwa katika mfumo wa Employee Self Services (ess) kwa ajili ya kuwawezesha kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma (PEPMIS na PIPMIS). Aidha, jumla ya watumishi wa umma 571,586 kati ya 603,699 ambao ni sawa na asilimia 94.7 wameweka Mipango ya Utendaji Kazi katika mfumo wa PEPMIS/PIPMIS inayojumuisha majukumu yanayotekelezwa na watumishi katika taasisi husika;

(iii) Programu ya simu (Mobile App) ya mfumo wa PEPMIS /PIPMIS imeandaliwa na kwa sasa iko kwenye hatua ya majaribio (System Testing);

(iv) Usimamizi wa utekelezaji wa Ikama na Bajeti ya Mishahara kwa Waajiri 433 wanaotumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara umefanyika ambapo kiasi cha Shilingi 5,519,691,369,695.58 kimetumika kulipa mishahara na posho mbalimbali za kimshahara kwa Watumishi wa Umma wa kada mbalimbali;

(v) Taarifa 145,472 za kiutumishi na mishahara katika Orodha ya Malipo ya Mishahara (Payroll) zilifanyiwa uchambuzi na kuidhinishwa kupitia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS). Uidhinishaji huu unajumuisha taarifa za Ajira Mpya/Mbadala 26,514 (Ajira hizi ni za mwaka wa Fedha 2022/2023 ambazo utekelezaji wake umefanyika Mwaka wa Fedha 2023/2024); Mabadiliko ya Hali ya Kiutumishi 2,848; Usafishaji wa Taarifa (Data Cleaning) 51,625; Mabadiliko ya Mishahara 1,957; Mshahara Binafsi 824; Uidhinishaji wa Posho 54,223; Kuajiriwa Upya katika Utumishi wa Umma 369; Ubadilishwaji Kada 3,043 (Ubadilishwaji kada huu ni wa nafasi zilizokasimiwa katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 ambazo utekelezaji wake umefanyika Mwaka wa Fedha 2023/2024); na Upandishwaji vyeo 12,342 (Upandishwaji Vyeo huu ni wa nafasi

zilizokasimiwa katika Ikama na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/2023 ambazo utekelezaji wake umefanyika Mwaka wa Fedha 2023/2024);

(vi) Uhakiki wa watumishi na usafishaji wa taarifa za kiutumishi na mishahara kwa watumishi waliopo kwa waajiri 400 kati ya 433 umefanyika kupitia Mfumo wa HCMIS;







1. Mkurugenzi wa Mipango, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Bw. Cosmas Ngangaji akifafanua jambo wakati wa mafunzo ya namna ya kutumia mfumo wa PEPMIS kwa watumishi wa umma wa Mkoa wa Kilimanjaro.

2. Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Utawala, Ofisi ya Rais UTUMISHI Bi. Nyasinde Mukono (Aliyesimama) akifafanua jambo kwa Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, CPA. Habibu Suluo (Wa kwanza kulia) wakati wa Mafunzo ya Mfumo wa Upimaji wa Utendaji kazi wa wa Watumishi Serikalini (PEPMIS) kwa Menejimenti ya LATRA yaliyofanyika katika ukumbi mdogo wa Bunge Jijini Dodoma.

(vii) Vibali vya ajira mpya 4,419 vimetolewa vikijumuisha ajira mpya 3,323 kati ya nafasi 47,404 zilizoidhinishwa kwa Taasisi ambazo watumishi wao hulipwa mishahara na wizara ya Fedha kupitia Mfumo wa HCMIS pamoja na nafasi za ajira mpya 1,096 zilizotolewa kwa Taasisi zilizoanza kutumia Mfumo wa HCMIS na kulipa mishahara ya watumishi wao kwa mapato ya ndani ya taasisi husika. Aidha, vibali vya ajira mbadala 3,992 vimetolewa kwa Waajiri mbalimbali na maandalizi ya utekelezaji wa Ajira Mpya 44,081 zilizosalia yanaendelea na yatafanyika kabla ya kukamilika kwa mwaka huu wa fedha;

(viii) Madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma 26,331 yenye jumla ya Shilingi 39,055,480,683.58 kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Umma yamehakikiwa na kulipwa kwa watumishi stahiki;

(ix) Madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma waliokoma utumishi wao kwa sababu mbalimbali kutoka katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Taasisi mbalimbali za umma yamehakikiwa na kuidhinishwa, ambapo jumla ya madai ya watumishi 1,863 yenye jumla ya Shilingi 7,026,231,778.48 yamelipwa;

(x) Mafunzo ya matumizi ya Mfumo mpya (New HCMIS) yametolewa kwa Maafisa Utumishi 223, Wakuu wa Idara za Utumishi na Utawala 11, Wakaguzi wa Ndani 28 na Wahasibu 35 wa Taasisi za Umma;

(xi) Taarifa za Watumishi 9,398 kutoka Taasisi 25 kati ya 89 zimeingizwa kwenye Mfumo Mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (New HCMIS) na taasisi hizo zimeanza kutumia Mfumo huo katika kusimamia masuala ya kiutumishi na mishahara;

(xii) Miundo na Mgawanyo wa Majukumu wa Taasisi za Umma 80 kati ya 120 imepitiwa na kuhuishwa ili kuziwezesha taasisi hizo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

(xiii) Mfumo wa Tathmini ya Watumishi wa Umma (HR Assessment Sytem) umejengwa ili kufanya uchambuzi wa Mahitaji ya watumishi, ambapo kuanzia Novemba 2023 hadi Februari 2024, mfumo huo umetumika kufanya uchambuzi wa mahitaji ya watumishi kwa Taasisi za Umma 571;

(xiv) Ofisi imebuni Daftari la kieletroniki la Huduma za Serikali (Government Service Directory) litakalowezesha wananchi kupata taarifa za huduma zote za Serikali katika sehemu moja (single gateway) kwa wakati ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha, taarifa za Huduma katika Taasisi za Umma 56 zimekusanywa kwa ajili ya kuandaa Daftari la Huduma za Serikali. Rasimu ya Kieletroniki ya Mfumo wa Daftari la Huduma za Taasisi imeandaliwa (e-Government Services Directory Platform) ambapo majaribio ya utekelezaji wa mfumo huo yanaendelea;

(xv) Michakato ya kuboresha huduma (BPI) za Ofisi za Masijala kwa Taasisi 4 (Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, TEMESA, DUWASA na Dodoma Jiji) imefanyika;

(xvi) Matumizi ya mifumo miwili ya Serikali Mtandao (e-Helpdesk na Fleet) yameanza ambapo madereva wamesajiliwa kwenye mfumo wa FLEET ili kuwawezesha kuomba vibali vya mafuta na matengenezo ya magari;

(xvii) Ujenzi wa moduli ya Likizo Mtandao ( e-Leave) ambayo ni huduma mojawapo katika dirisha la watumishi portal umekamilika kwa sasa ipo katika hatua ya majaribio;

(xviii) Sera ya Motisha na Malipo ya mwaka 2010 imeanza kufanyiwa mapitio kwa lengo la kuhakikisha masilahi katika Utumishi wa Umma yanaoanishwa na kuwianishwa;

(xix) Rasimu ya Sera ya TEHAMA Serikalini imeandaliwa na kuanza kujumuisha maoni ya wadau kutoka katika Taasisi za Umma;

(xx) Miundo ya Maendeleo ya Utumishi ya Taasisi na Mashirika ya Umma 26 imefanyiwa mapitio na imependekezwa kwa ajili ya kupata idhini ya kutumika;

(xxi) Mipango ya Motisha/Mikataba ya Halibora kwa Taasisi na Mashirika ya Umma 24 imefanyiwa mapitio na imependekezwa kwa ajili ya kupata idhini ya kutumika;

(xxii) Jumla ya wageni 2,213 walipatiwa ushauri kuhusu masuala mbalimbali ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu na Utawala, na pia malalamiko 2,204 yatokanayo na ukiukwaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia Utumishi wa Umma yalipokelewa na kushughulikiwa. Vilevile, vibali vya uhamisho kwa watumishi wapatao 6,268 na vibali vya likizo bila malipo 286 vimetolewa;

(xxiii) Katika kusimamia utawala wa utumishi wa umma ili kupata viongozi wenye sifa stahiki, weledi na maono ya utumishi wa umma wenye kuzingatia Dira ya Maendeleo na mikakati mbalimbali ya kitaifa, vibali vya uteuzi 836 vimetolewa ili kujaza nafasi wazi za uongozi kwenye taasisi za umma. Aidha, Maafisa Waandamizi 241 waliomaliza vipindi vyao vya majaribio walithibitishwa katika nafasi za uongozi na vibali 738 vya kukaimu vilitolewa. Vilevile, taratibu za upekuzi wa maafisa 1,528 waliopendekezwa na taasisi za umma kujaza nafasi mbalimbali za uongozi zilifanyika;

(xxiv) Marekebisho ya Sheria ya Mafao ya kustaafu katika Utumishi wa Kisiasa, Sura ya 255 yamekamilika;

(xxv) Taarifa ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai iliandaliwa na kuwasilishwa;

(xxvi) Waraka wa Mkuu wa Utumishi wa Umma Na. 1 wa Mwaka 2023, Kuhusu Matumizi ya Madaraka ya Ukamataji wa Watuhumiwa yaliyokasimiwa kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Viongozi wengine katika Mamlaka za Serikali za Mitaa umeandaliwa;

(xxvii) Toleo la kwanza la Mwongozo wa Ujumuishaji wa Jinsia katika Utumishi wa Umma wa mwaka 2023 limeandaliwa na kusambazwa kwa Wizara 26, Idara Zinazojitegemea 31, Wakala za Serikali 27, Mashirika na Taasisi za Umma 267, Sekretarieti za Mikoa 26 na Mamlaka za Serikali za Mtaa 184;

(xxviii) Taasisi za Umma 208 zimepatiwa mafunzo kuhusu mbinu za Kudhibiti VVU/UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza mahali pa kazi;

(xxix) Kanuni za Utumishi na Kanuni za Fedha za Taasisi za Umma 17 zimeandaliwa;

(xxx) Kampeni ya Uhamasishaji na upimaji wa VVU na Magonjwa Yasiyoambukizwa mahali pa kazi imeratibiwa na kuendeshwa kwa kushirikiana na Wizara ya Afya ambapo Watumishi wa Umma 1,107 kutoka katika Wizara 14 na Halmashauri ya Wilaya Bahi walishiriki;

(xxxi) Takwimu za Watumishi wa Umma wanaoishi na VVU na Magonjwa yasiyoambukiza katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Mashirika ya Umma, Tawala za

Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zimehuishwa, ambapo hadi sasa jumla ya Watumishi 2,238 wameweka wazi hali zao za maambukizi na wanapatiwa huduma toka kwa Waajiri wao;

(xxxii) Takwimu za Watumishi wa Umma wenye Ulemavu zimehuishwa, ambapo kupitia HCMIS jumla ya Watumishi 1,533 (ME 966; KE 567) wamesajiliwa, wakati 116 wametambuliwa kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina;

(xxxiii) Mkutano wa Baraza Kuu la Tano la Wafanyakazi katika Utumishi wa Umma - Tanzania Bara umefanyika mwezi Februari, 2024;

(xxxiv) Mapitio ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma Toleo la 3 la mwaka 2009 yamefanyika;

(xxxv) Hadidu za rejea za maandalizi ya Kiunzi cha Uendelezaji Ubora/umahiri wa Uongozi zimeandaliwa na Zabuni imetangazwa kwa ajili ya kuzialika Taasisi za Umma zenye sifa na uwezo wa kuandaa Kiunzi husika;

(xxxvi) Jumla ya Watumishi wa Umma 722 wamewezeshwa kupata ufadhili wa mafunzo mbalimbali ambapo, watumishi 165 walipata mafunzo ya muda mrefu na watumishi 557 walipata mafunzo ya muda mfupi kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Korea, Japan na India. Ufadhili wa mafunzo hayo umeendelea kutolewa kwa kuzingatia ujuzi unaohitajika ili kufikia malengo ya Dira Taifa ya mwaka 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa (FYDP III);


THE UNITED REPUBLIC
OF TANZANIA
UONGOZI
Institute
1


2

## 19 APRILI, 2024






1. Mheshimiwa George B. Simbachawene akizindua Mwongozo wa Ujumuishaji wa Jinsia katika Utumishi wa Umma wa mwaka 2023 makati wa Kongamano la Tatu la Wanawake katika Uongozi - Oktoba 2023.
2. Mwongozo wa Ujumuishwaji wa Jinsia ukisambazwa kwa mmoja wa Wakurugenzi wa Wizara - Oktoba 2023.

(xxxvii) Mafunzo Maalum yalitolewa kwa Maafisa Tarafa 547 kutoka katika mikoa yote ya Tanzania Bara kwa lengo la kuwakumbusha masuala muhimu ya kiutendaji na kuwajengea uwezo ili kuboresha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya msingi kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Utumishi wa Umma;

(xxxviii) Jumla ya vibali 854 vya wataalam wa kigeni vyenye msamaha wa ada vimetolewa kwa wataalam wanaokuja katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati na shughuli za sekta na mashirika mbalimbali ya Umma;

(xxxix) Nafasi za ajira 115 kutoka katika Taasisi za Kikanda na Kimataifa ziliratibiwa kwa lengo la kuwawezesha Watanzania wenye sifa kuomba nafasi hizo. Mashirika yaliyotoa nafasi za ajira kwa ajili ya wataalam wazawa ni pamoja na ADC, UNWTO, UNDP, UNESCO, WHO, AfDB, AU, WIPO, FAO, UNFPA, OACPS na UN – HABITAT;

(xl) Jumla ya Taasisi za Umma 14 zimewezeshwa kuandaa Mipango ya Rasilimaliwatu na Urithishanaji Madaraka. Taasisi zilizowezeshwa kuandaa Mpango wa Rasilimaliwatu ni Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Viautilifu na Afya ya Mimea Tanzania (TPHPA), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA) na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT). Aidha, Taasisi zilizowezeshwa kuandaa Mpango wa Urithishanaji Madaraka ni Mamlaka ya Maabara yaa Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), Baraza la Rufani ya Kodi (TRAT), DAWASA na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET). Aidha, Taasisi zilizowezeshwa kuandaa Mpango wa Mafunzo ni Hospitali ya Benjamini Mkapa (BMH), Kampuni ya Uvuvi (TAFICO), Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bodi ya Rufani ya

Kodi (TRAB), Wakala wa Umeme Vijijini (REA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA);

(xli) Taarifa 94, picha 684 na mabango 43 yenye ujumbe mbalimbali kuhusu masuala ya kiutumishi na utawala bora yametolewa na kurushwa kwenye vyombo mbalimbali vya habari ambavyo ni magazeti, televisheni, redio, tovuti ya Ofisi, mitandao ya kijamii ya Ofisi na ya watu binafsi ili kuhabarisha umma masuala yanayohusu Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;

(xlii) Makala fupi za mwendo (video clips) 146 za utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ziliandaliwa na kuchapishwa kwenye mitandao ya kijamii ya Ofisi na binafsi kwa ajili ya kuuhabarisha umma;

(xliii) Uratibu na uhariri wa matangazo toka taasisi za umma na watu binafsi kwa ajili ya kuchapishwa katika Gazeti la Serikali umefanyika na kuwezesha magazeti 39 kuchapishwa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali;

(xliv) Malalamiko 899 yaliyohusu masuala ya Kiutumishi na Rasilimaliwatu kutokana na uvunjwaji wa Sheria, Taratibu, Kanuni na Miongozo mbalimbali katika Utumishi wa Umma yalipokelewa kupitia Mfumo wa Sema na Waziri wa Utumishi/e-Mrejesho. Kati ya malalamiko yaliyopokelewa, malalamiko 888, sawa na asilimia 98.8 yamefanyiwa kazi na kufungwa, na malamiko 11, sawa na asilimia 1.2 yanaendelea kuchambuliwa. Aidha, kupitia kituo cha huduma kwa Mteja, jumla ya hoja 4,124 zilipokelewa ambapo hoja 4,075 sawa na asilimia 98.8 zilishughulikiwa na kuhitimishwa na hoja 49 sawa na asilimia 1.2 zinaendelea kushughulikiwa;

(xlv) Kampeni za kimaadili zimefanyika kupitia vyombo vya habari katika vipindi vya runinga (ITV) na redio (TBC FM na E-FM) ambapo vipindi 11 vilirushwa kupitia vyombo hivyo pamoja na kushiriki katika Maadhimisho ya Wiki ya maadili na haki za binadamu Kitaifa yaliyofanyika kuanzia tarehe 04 hadi 10 Disemba, 2023 katika Viwanja vya ‘‘Nyerere Square”;

(xlvi) Mafunzo ya Mfumo wa kielekroniki wa e-Mrejesho yametolewa kwa Watumishi wa Umma 39 kutoka katika Taasisi za Umma 19;

(xlvii) Mafunzo ya kujenga Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma yametolewa kwa Watumishi 4,210 kutoka Taasisi za Umma 35. Aidha Kampeni za Kimaadili zimefanyika katika Mkoa wa Arusha ikiwemo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa pamoja na Halmashauri zake ambapo jumla ya watumishi 822 kutoka Taasisi za Umma 12 walishiriki mafunzo hayo. Aidha, Ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma umefanyika katika Mkoa wa Tabora ikiwemo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Halmashauri zake pamoja na Taasisi za Umma 3;

(xlviii) Kikao kazi cha kubadilishana uzoefu baina ya OR-MUUUB, Taasisi Simamizi za Maadili 8 na Taasisi Simamizi za Maadili ya Kitaaluma 7 kilifanyika tarehe 21 – 22 Septemba, 2023. Lengo la kikao ni kukuza uadilifu na kuimarisha ushirikiano endelevu wa Usimamizi wa Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma na Maadili ya Kitaaluma;

(xlix) Ujenzi wa jengo la ghorofa tano (5) la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika eneo la Mtumba umeendelea na hadi sasa ujenzi huo umefikia asilimia 98;





1. Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Bw. Xavier Daudi akimkabidhi cheti cha ushiriki mmoja wa washiriki wa mafunzo ya mfumo wa eMrejesho kwa watumishi wa umma kutoka taasisi mbalimbali za Serikali - Desemba 2023, Jijini Dodoma.
2. Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora Bw. Xavier Daudi akifunga mafunzo ya mfumo wa eMrejesho kwa watumishi wa umma kutoka taasisi mbalimbali za Serikali - Desemba 2023, Jijini Dodoma.

(l) Huduma zimeendelea kutolewa kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa Wastaafu (Viongozi tisa (9) na wajane kumi (10) kwa mujibu wa sheria; na

(li) Ujenzi wa Klabu ya Viongozi - Makao Makuu eneo la Nzuguni karibu na Stendi ya Mabasi ya Nanenane, Dodoma umeendelezwa kwa kujenga uzio ambao umefikia asilimia 68.

**B. Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC)**

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Machi 2024, shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

(i) Mafunzo ya awali yametolewa kwa watumishi wa umma wapya 1,763 ili kuwajengea uwezo wa kutenda kazi za Serikali kwa usahihi na kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya utumishi wa umma;

(ii) Watumishi wa umma 3,627 wamepatiwa mafunzo ya Uongozi na Maendeleo, Menejimenti na Usimamizi wa Ofisi katika kuimarisha taswira nzuri ya Utumishi wa Umma;

(iii) Watumishi 1,389 wamepatiwa mafunzo ya kujiandaa kufanya Mitihani ya Utumishi wa Umma ili kuimarisha utendaji kazi wao na kutoa huduma bora kwa wananchi;

(iv) Ushauri wa kitaalam katika maeneo matano (5) ulitolewa ili kuwawezesha watumishi wa umma kuboresha mifumo na mbinu za utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa mahitaji halisi ya utumishi wa umma na wadau mbalimbali kwa lengo la kutatua changamoto za utendaji na kuendeleza mchango wa utumishi wa umma katika ustawi wa Taifa;

(v) Washiriki 364 walijengewa uwezo wa utaalam wa Kitaifa na Kimataifa katika fani mbalimbali ikiwemo Menejimenti ya Utumishi wa Umma kupitia midahalo iliyosaidia kubadilishana uzoefu kwa njia ya mtandao;

(vi) Wanachuo 10,762 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika fani za Utunzaji wa Kumbukumbu, Uhazili, Kompyuta, Utunzaji wa Fedha za Umma, na Menejimenti ya Rasilimaliwatu, Usimamizi wa Ununuzi wa Umma, Uongozi na Utawala Bora ili kuwapatia stadi, weledi na ujuzi wa kazi za Serikali;

(vii) Watumishi wa Umma 379 waliwezeshwa kushiriki mafunzo ya muda mfupi katika fani za uongozi na utawala yaliyofanyika kwa njia ya mtandao. Njia hii imesaidia Serikali kupunguza gharama, kuwa na mazingira rafiki katika kujifunza, kuepuka muingiliano wa mafunzo na majukumu ya kazi na kupunguza safari nje ya vituo vya kazi;

(viii) Watumishi watano (5) wa chuo waliwezeshwa kuendelea na masomo katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu na Shahada ya Uzamili ili kujenga hazina ya wakufunzi na watumishi wengine wenye weledi;

(ix) Ujenzi wa majengo ya kampasi ya Singida (awamu ya pili) katika eneo la Mungumaji mkoani Singida unaojumuisha madarasa ya kufundishia, ofisi, kumbi za mikutano/mafunzo na vyoo umeendelea na kwa sasa upo katika hatua ya kupaua ambapo jumla ya Shilingi 439,562,547.29 za mapato ya ndani zimetumika; na

(x) Ufuatiliaji wa kupata eneo la ujenzi wa kampasi ya Tanga umekamilika.

## C. Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Machi 2024, shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

(i) Ujenzi wa Mfumo maalum wa kuwezesha Mifumo ya Serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa (Government Enterprise Service Bus - GovESB) umeendelezwa ambapo mifumo 132 ya Taasisi za Umma 122 imewezeshwa kuwasiliana na kubadilishana taarifa kidigitali. Lengo ni kuongeza ufanisi wa utendaji kazi, kupunguza gharama za uendeshaji wa Ofisi na kuokoa muda kwa kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati;

(ii) Miundombinu ya Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato Serikalini (Government ePayment Gateway – GePG) imeboreshwa ambapo vituo vya kutolea huduma na taasisi mpya 24 zimeunganishwa kwenye mfumo huo na kufanya jumla ya taasisi na vituo vya kutolea huduma vilivyounganishwa kufikia 1007;

(iii) Mifumo mbalimbali ya TEHAMA imeboreshwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Ikulu ili kuboresha utendaji kazi katika Ofisi hiyo;

(iv) Ujenzi wa awamu ya kwanza ya mfumo wa uondoshaji wa shehena maeneo ya forodha (Tanzania electronic Single Window System - TeSWS) umekamilishwa kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali. Kwa sasa Mfumo huu unatumika katika uondoshaji wa shehena zinazopita katika Bandari ya Dar es Salaam na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere ambapo kampuni za wakala wa forodha (CFA) 1,496 pamoja na kampuni za kuhifadhi mizigo (Cargo Keepers) 253 zinatumia mfumo. Mfumo umewezeshwa kubadilishana taarifa na mifumo ya TRA (TANCIS), TPA (TOS), TBS, TMDA, GCLA, TAEC,

TASAC, TCAA, Bodi ya Nyama (TMB), Bodi ya Maziwa (TDB), Wizara ya Mifugo na Wizara ya Uvuvi. Mfumo umewezesha Taasisi wadau katika uondoshaji wa shehena kufanya ukaguzi wa pamoja wa shehena (joint inspection).

(v) Ujenzi wa awamu ya pili ya mfumo wa TeSWS umekamilishwa kwa kushirikiana na wadau wengine. Mfumo huu umeanza kutumika na umeunganishwa na kuwezesha unabadilishanaji wa taarifa kati ya mfumo wa TPA – TOS na mfumo wa TRA - TANCIS kwenye maeneo yanayohusu usimamizi wa meli, uondoshaji wa shehena zinazoingia nchini pamoja na malipo. Jumla ya Mawakala wa Meli (Shipping Agents) 27, mawakala wa meli wasio na meli (Consolidators) 21 wanatumia mfumo na jumla ya meli 414 zimesajiliwa kupitia mfumo wa TeSWS tangu Oktoba 2023. Vile vile, Mamlaka kwa kushirikiana na Taasisi wadau imekamilisha ujenzi wa awamu ya tatu ya mfumo wa TeSWS ambapo kwa sasa jitihada za majaribio zinaendelea kwa ajili ya kuanza matumizi;

(vi) Tathmini ya usalama wa mifumo ya TEHAMA imefanyika kwa taasisi za umma 429 kwa mifumo inayopatikana mtandaoni;

(vii) Tathmini ya kina ya uzingatiwaji wa viwango na miongozo ya usalama wa Serikali mtandao katika mifumo na Miundombinu ya TEHAMA (Compliance and Security Assessment) imefanyika katika taasisi za umma 57;

(viii) Tathmini ya usalama wa mifumo ya TEHAMA 113 (protective security assessment) imefanyika ili kujiridhisha juu ya hali ya usalama wa mifumo hiyo kabla ya kuhifadhiwa katika Vituo vya Kuhifadhi Taarifa vya Serikali (Government Data Centers);







1. Mheshimiwa George B. Simbachawene akiwa katika picha ya pamoja na meza kuu na baadhi ya washiriki wa Kikao Kazi Cha 4 cha Serikali Mtandao - Februari 2024.

2. Mafunzo ya siku sita kwa Maafisa TEHAMA Wachambuzi wa Mifumo (Business Analysts) kutoka katika taasisi za umma - Novemba 2023.



3.Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishiwa Umma Bw. Juma Mkomi akitoa maelezo ya awaliwakati wa ufunguzi wa Kikao Kazi cha 4 cha Serikali Mtandao - Februari 2024, Arusha.

(ix) Doria za kimtandao kwa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA ya Serikali "Monitoring of Government ICT Systems and Infrastructure" zimefanyika kwenye mifumo yote iliyohifadhiwa katika Vituo vya Kuhifadhi Taarifa vya Serikali;

(x) Msaada wa kiufundi katika majanga mbalimbali ya kimtandao "Cyber security incidents" umetolewa kwa Taasisi za Umma 17;

(xi) Mafunzo kuhusu Usalama wa Mtandao, Sheria, Kanuni, Viwango, na Miongozo ya Serikali Mtandao yametolewa kwa Taasisi za Umma 291;

(xii) Ukaguzi wa uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Viwango, na Miongozo ya Serikali Mtandao umefanyika katika Taasisi za Umma 54 kwa lengo la kuhakiki ubora na ufanisi wa mifumo hiyo. Aidha, ukaguzi wa kina ulifanyika kwa baadhi ya Mifumo ya TEHAMA ya Taasisi za Umma, ikiwemo Mfumo wa Malipo wa Serikali Kielektroni (GePG) wa Wizara ya Fedha, Mfumo wa Vibali Maalum vya

Barabarani (Special Road Permit System) wa Wizara ya Ujenzi, Mfumo Jumuishi wa Kukusanya Nauli (IFCS) wa Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Mfumo wa Kuchakata Taarifa za Hali ya Hewa (HPC System) wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), na Mfumo wa Vibali vya Kazi (OWAIS) wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira, na wenye Ulemavu);

(xiii) Mafunzo kuhusu sheria, kanuni, viwango na miongozo ya Serikali Pamoja na kujenga uwezo na ujuzi wa kukagua eneo la TEHAMA yametolewa kwa wakaguzi wa ndani kutoka taasisi za Umma 70. Aidha, mafunzo ya uelewa wa usalama wa TEHAMA yametolewa kwa Taasisi 291;

(xiv) Matumizi ya Mifumo ya kutolea huduma kwa wananchi yamewezeshwa kwa kushirikiana na sekta binafsi. Mifumo hiyo ni pamoja na Mfumo wa Kutolea Ruzuku za Mbolea kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, TFRA, Vodacom PLC na CRDB Bank. Aidha, kwa kushirikiana na Vodacom Foundation, Pathfinder, Wizara ya Afya,OR-TAMISEMI na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imewezesha matumizi ya Mfumo wa kusaidia kutoa huduma ya usafiri wa dharura kwa kinamama na watoto (M-MAMA);

(xv) Mfumo wa Kusimamia Rasilimali za Taasisi (ERMS) umeboreshwa ambapo jumla ya Taasisi zilizounganishwa zimefika 63;


(xvi) Programu za mafunzo 34 zimetolewa kwa taasisi za umma 146, ambapo zaidi ya watumishi 763 wamepatiwa mafunzo kuhusu usimamizi na uendeshaji wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA;

(xvii) Utafiti na ubunifu wa matumizi ya teknolojia mpya za TEHAMA katika utoaji huduma kwa umma na utendaji kazi wa Serikali umeendelea kufanyika na kuboreshwa katika maeneo ya BlockChain na Digital Currency, Internet of Things (IoT), Artificial Intelligence (AI), na Machine Learning (ML); na


(xviii) Ushauri wa kitaalam kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya TEHAMA, Usalama wa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA, na uzingatiaji

wa Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao umetolewa kwa Taasisi za Umma 57.

**Hali ilivyokuwa (*Point to point integration)***



**Hali ilivyo sasa (Muunganisho kupitia mfumo wa GOVESB)**




**E. Watumishi Housing Investment (WHI)**

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Machi 2024, shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

(i) Katika mradi wa ujenzi wa nyumba 1,000 jijini Dodoma pamoja na mikoa mingine zikiwemo Wilaya mpya, ujenzi wa nyumba 42 umekamilika na ujenzi wa nyumba 30 unaendelea katika eneo la Njedengwa Dodoma. Vile vile, katika eneo la Chamwino Buigiri Vitalu Na. 383, 384, 385, 549 na Mtumba Kitalu Na. 695 yamenunuliwa kwa ajili ya ujenzi;

(ii) Katika kutekeleza mradi wa Ujenzi wa nyumba 80 za Makazi kwa Watumishi wa Umma katika Halmashauri Mpya, maeneo ya ujenzi yameainishwa na michoro ya ujenzi wa nyumba hizo imekamilika;

(iii) Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja wa Faida Fund umeendelea kukuzwa ambapo vipande vyenye thamani ya Shilingi bilioni 21.12 vimenunuliwa na wawekezaji wapatao 4,160;

(iv) Viwanja 222 kati ya viwanja 326 vilivyopimwa katika eneo la USA RIVER jijini Arusha vimeendelea kuuzwa kwa njia ya malipo ya awamu ambapo hadi sasa kiasi cha shilingi bilioni 1.6 kimekusanywa; na

(v) Ofisi imeendelea kutoa huduma za ujenzi na ushauri kwa Taasisi za Serikali ikiwemo Usimamizi wa ujenzi wa jengo la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika Utumishi Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma.

**OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2023/24, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Fungu 67 ilitengewa jumla ya **shilingi 13,711,815,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **shilingi 10,139,298,000.00** sawa na **asilimia 73.9** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 3,572,517,000.00** sawa na **asilimia 26.10** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2024, kiasi cha **shilingi 9,737,114,818.94** sawa na **asilimia 71.01** ya bajeti iliyotengwa kilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **shilingi 7,320,059,748.30** zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 2,417,055,070.64** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 Hadi kufikia Machi, 2024, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ilitekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Mchakato wa Ajira katika Taasisi mbalimbali za Umma umekamilishwa baada ya kupokea vibali vyenye jumla ya nafasi 7,741 ambapo kati ya vibali hivyo, nafasi zilizojazwa ni 6,582 na kati ya hizo wanaume ni 4,268 na wanawake ni 2,314 na taratibu za kujaza nafasi 1,159 zinaendelea;

(ii) Taarifa za wasailiwa 6,326 waliofaulu katika usaili wa mahojiano zimehifadhiwa kwenye kanzidata. Wasailiwa hawa watapangiwa kazi kulingana na uhitaji wa Waajiri mbalimbali serikalini;

(iii) Jumla ya Vyeti 13,998 vimehakikiwa kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali (NECTA - 10,244; TRA – 257; VETA – 223; RITA - 1,485; JKT, PASIANSI na MWEKA - 1,299; Vyuo vya mafunzo ya udereva – 241; NIT – 249; ERB – 24). Kati ya vyeti hivyo, vyeti 25 sawa na asimilia 0.1 viligundulika kuwa ni vya kughushi na hatua stahiki zilichukuliwa;

(iv) Mitihani ya usaili 1087 imeandaliwa, ambapo kati ya hiyo, Mitihani ya usaili wa kuandika ni 289, Mitihani ya usaili wa Mahojiano ni 646 na Mitihani ya usaili wa Vitendo ni 152 kwa jumla ya Waajiri 226;

(v) Vipindi saba (7) vya kutoa hamasa na elimu kwa Umma kuhusu mchakato wa Ajira vilirushwa kupitia runinga za TBC I, ITV, Clouds TV, Azam TV, Channel Ten, Star TV na redio za UFM, TBC FM, AFM na CFM;

(vi) Chaneli ya kimtandao ya Ajira imefanyiwa maboresho, ambapo, hadi mwezi Machi, 2024 chaneli hiyo inapatikana katika mtandao wa 'Youtube" na imepakuliwa na watazamaji zaidi ya 16,888 na inawatumiaji wapya (new subscribers) zaidi ya 2,507;

(vii) Umma umehabarishwa kuhusu shughuli za Sekretarieti ya Ajira kupitia mitandao ya kijamii ambapo hadi mwezi Machi, 2024 mtandao wa "facebook" umetembelewa na watumiaji wapya zaidi ya 60,000 mtandao wa X (twitter) umetembelewa na watumiaji wapya 827 na mtandao wa "instagram" umefuatiliwa na zaidi ya watumiaji 16,200;

(viii) Semina kuhusu kanuni za uendeshaji wa shughuli za Ajira zimefanyika kwa Vyuo vya Elimu ya Juu vya Umma 14, Vyuo viwili (2) vya kati, Mamlaka za udhibiti wa Elimu ya juu na Elimu ya ufundi na Halmashauri 135 zilizopo Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kati na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini;

(ix) Huduma ya dawati la msaada na utatuzi kwa watumiaji wa mfumo wa 'Ajira Portal' imetolewa ambapo, jumla ya wadau 15,906 walihudumiwa na kati ya hao wadau 9,645 walihudumiwa kwa njia ya simu, na wadau 6,261 walihudumiwa kwa njia ya barua pepe;

(x) Maboresho ya programu rununu (App) ya Ajira yamefanyika, ambapo hadi kufikia Machi, 2024, 'Ajira Portal App' ilikuwa imepakuliwa na zaidi ya watumiaji 172,000 na kushika nafasi ya kwanza miongoni mwa 'Mobile App' zinazotumiwa zaidi nchini katika kundi la Magazeti na Majarida;

(xi) Takwimu za Ajira zimekusanywa kutoka Sekretarieti za Mikoa 26 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 184;

(xii) Ujenzi wa mfumo wa kupima uelewa na ufahamu wa wasailiwa (Online Aptitude Test System) umefanyika ambapo mfumo huu utawezesha wasailiwa kufanya usaili mahali walipo na hivyo kupunguza gharama kwa wasailiwa, wazazi/walezi na Serikali. Hadi sasa ujenzi wa mfumo umekamilika kwa asilimia 95, mfumo utaanza utekelezaji wa majaribio kwa kuanza na kada tano (5) kuanzia mwezi Machi 2024 na baada ya majaribio hayo kada 30 zitafuatia;

(xiii) Vituo 30 vya Mamlaka ya Mafunzo na Ufundi Stadi (VETA), Vyuo vikuu na matawi ya vyuo vikuu 58 katika Mikoa 27 ya Tanzania Bara pamoja na Zanzibar vimetathminiwa kwa ajili ya kubaini miundombinu inayoweza kutumika na mfumo wa kielektroniki wa usaili wa mchujo (Online Aptitude Test System);

(xiv) Kanzidata ya maswali imeendelea kuboreshwa kwa kufanya uchambuzi wa maswali 56,000 yaliyokusanywa kutoka kwa wadau mbalimbali. Aidha, maswali 7,782 yamechambuliwa na yapo katika hatua ya kuingizwa kwenye kanzidata hiyo;

(xv) Mafunzo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa "Ajira Portal" yamefanyika, ambapo jumla ya washiriki 526 walipatiwa mafunzo kutoka Halmashauri 175 na Sekretarieti za Mikoa 22 ya Tanzania Bara. Waliopatiwa mafunzo ni Wakuu wa Idara za Utawala na Rasilimaliwatu,

maafisa TEHAMA na Maafisa Utumishi wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaoshughulikia ajira;

(xvi) Mafunzo kwa Wajumbe wa Sekretarieti ya Ajira watano (5) kuhusu mfumo wa usaili kwa njia ya mtandao (OATS) pamoja na mfumo wa kanzidata ya maswali yametolewa;

(xvii) Ziara za mafunzo kwa Watumishi watano (5) zimefanyika nchini Estonia ili kujenga uwezo wa mifumo kuhusu masuala ya Ajira kimtandao; na

(xviii) Kikao kazi kuhusu uendeshaji usaili wa kuandika kidigitali kupitia maabara za kompyuta kimefanyika mwezi Machi, 2024. Kikao hicho kilihusisha Makatibu Tawala Wasaidizi wanashughulikia Rasilimaliwatu katika Mikoa yote ya Tanzania Bara pamoja na Maafisa TEHAMA kutoka vyuo vikuu, vyuo vya kati, vyuo vya Mamlaka ya Ufundi stadi na Vyuo vya Amali.

**OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2023/24, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma, Fungu 94 ilitengewa jumla ya **shilingi 8,624,091,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **shilingi 8,324,091,000.00** sawa na **asilimia 96.5** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 300,000,000.00** sawa na **asilimia 3.5** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2024 **shilingi 5,778,754,899.86** sawa na **asilimia 67.01** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **shilingi 5,478,754,899.86** zilikuwa ni matumizi ya kawaida na **shilingi 300,000,000.00** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Machi, 2024, Tume imetekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Rufaa 482 sawa na asilimia 83.1 ya rufaa 580 zilizokuwepo zilitolewa maamuzi, rufaa 41 zinaendelea kuchambuliwa na vielelezo vya rufaa 57 vinafuatiliwa kutoka mamlaka husika;

(ii) Malalamiko 236 sawa na asilimia 77.9 ya malalamiko 303 yaliyokuwepo yalitolewa maamuzi, uchambuzi wa malalamiko 14 unaendelea na vielelezo vya malalamiko 53 vinafuatiliwa kutoka mamlaka husika;

(iii) Warufani na Warufaniwa wote walioomba kufika na kujitetea mbele ya Tume kwa mujibu wa Kanuni ya 62(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022 walipewa nafasi. Hadi kufikia Machi, 2024 Warufani 45 na Warufaniwa wawili (2) walisikilizwa katika Mikutano mitatu (3) ya Tume kwa mwaka 2023/24;

(iv) Ukaguzi wa Uzingatiaji wa Sheria umefanyika katika katika Taasisi 180, na kati ya hizo Taasisi za Serikali Kuu zilikuwa 51, Mamlaka za Serikali za Mitaa ni 51 na Taasisi za Umma ni 78. Taarifa ya ukaguzi imekamilika na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika;

(v) Elimu kwa wadau kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu, na Miongozo inayosimamia Utumishi wa Umma imetolewa kwenye vyama viwili (2) vya wafanyakazi na Taasisi sita (6) ambazo zilihusisha jumla ya Washiriki 1,032. Taasisi hizo ni Wizara ya Afya, Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira TURIANI, Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC), Bodi ya Stakabadhi za Ghala (WRRB), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Taasisi ya Uhasibu Tanzania (TIA) na Vyama vya Wafanyakazi ambavyo ni Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa (TALGWU) na Chama cha Wafanyakazi wa Serikali Kuu na Afya (TUGHE). Aidha, Tume ilitoa elimu kupitia vyombo vya habari vinne (4) ambavyo ni TBC 1, ITV, Abood FM na Gazeti la Mwananchi. Vilevile, mitandao ya kijamii na tovuti ilitumika kutoa elimu kwa wadau;

(vi) Maandalizi ya Taarifa ya Hali ya Utumishi wa Umma na Utekelezaji wa Majukumu ya Tume katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/23 imeandaliwa na kuwasilishwa kwenya mamlaka husika;

(vii) Maafisa 75 wa Tume walijengewa uwezo kuhusu ukaguzi wa uzingatiaji Sheria, Kanuni, Taratibu, na Miongozo ya masuala ya kiutumishi kwa lengo la kuwawezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo;

(viii) Kukamilika na kuanza kutumika kwa Moduli ya Ukaguzi wa Uzingatiaji wa Sheria katika Mfumo wa Kielektroniki wa Kushughulikia Rufaa na Ukaguzi wa Uzingatiaji wa Sheria katika Utumishi wa Umma. Moduli ya Rufaa na Malalamiko inaendelea kukamilishwa; na

(ix) Ujenzi wa jengo la Ofisi za Tume katika Mji wa Serikali Mtumba umeendelezwa na hadi sasa umekamilika kwa asilimia 72.

**OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha wa 2023/24, Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 4,347,811,000.00** Kati ya fedha hizo, **shilingi 3,897,811,000.00** sawa na **asilimia 90** ni kwa ajili matumizi ya kawaida na **shilingi 450,000,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya **shilingi 2,434,658,276.62** sawa na **asilimia 56** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **shilingi 2,260,774,840.00** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 173,883,436.00** ni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Julai 2023 hadi Machi, 2024, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa imetekeleza majukumu yafuatayo:

(i) Majalada 11,514 yaliyofungwa yamekusanywa na kuhifadhiwa katika Kituo cha Kanda ya Ziwa – Mwanza na Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu Dodoma. Kati ya majalada hayo kutoka Wizara ya Fedha ni 2,750; Mamlaka ya Viwanja vya Ndege 2,200; Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi 1,720; na katika Mahakama Kuu Kanda ya Arusha 1,113, Kanda ya Moshi 1,127, Kanda ya Manyara 540, Kanda ya Dodoma 848 na Kanda ya Singida 1,216;

(ii) Uchambuzi, upangaji na uhifadhi wa kumbukumbu, nyaraka na taarifa 8,488 za Mwl. Julius K. Nyerere umefanyika katika Maktaba ya nyumba yake Butiama, Mkoa wa Mara;

(iii) Kumbukumbu na nyaraka 640 za Marais wengine wastaafu zimetambuliwa na kukusanywa;

(iv) Ukaguzi wa hali ya utunzaji wa kumbukumbu umefanyika katika Taasisi za Umma 42 kati ya 60 kwa lengo la kujua hali halisi ya utunzaji ili kubaini changamoto na kuzipatia ufumbuzi;

(v) Mfumo wa Utunzaji wa Kumbukumbu za Kiutendaji (Keyword Filing System) katika Taasisi za Umma 44 kati ya 40 zilizopangwa kuwekewa Mfumo;

(vi) Taasisi za Umma 24 kati ya 40 zimewekewa mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office);

(vii) Mwongozo wa utunzaji na uteketezaji kumbukumbu katika Taasisi za Umma tano (5) kati ya 15 kwa mwaka kwa mujibu wa Sheria umeandaliwa. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Chuo cha Nelson Mandela (NM – AIST) na Jeshi la Magereza Tanzania. Aidha, Idara imeanza kuratibu utekelezaji wa miongozo ya uteketezaji katika Shirikala Viwango Tanzania (TBS), Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT) na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF);

(viii) Taasisi za Umma 26 kati ya 30 zimejengewa uwezo wa utunzaji wa kumbukumbu;

(ix) Utaalam wa uhifadhi wa nyaraka kidigitali ulitolewa kwa makavazi ya Dkt. Salim Ahmed Salim (Dr. Salim Ahmed Salim Digital archives), Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katibu Mkuu Mstaafu wa O.A.U. Aidha, uzinduzi wa tovuti ya makavazi ya Dkt. Salim Ahmed Salim ulifanyika tarehe 30/09/2023 ambapo mgeni rasmi alikuwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(x) Tanzania imewakilishwa katika Mkutano wa Baraza la Nyaraka la Kimataifa Tawi la Mashariki na Kusini mwa Afrika (Eastern and Southern Africa Regional Branch of International Council on Archives - ESARBICA) pamoja na Baraza la Nyaraka la Kimataifa (Internatinal Council on Archives – ICA) iliyofanyika nchini Afrika Kusini (Johannesburg) na Falme za Kiarabu - UAE (Abu Dhabi);

(xi) Watafiti 25 waliwezeshwa kupata taarifa katika Ofisi za Idara, Kanda ya Mashariki - Dar es salaam ambapo watafiti 18 walitoka ndani ya nchi na saba (7) nje ya nchi. Aidha, wanafunzi 210 wa vyuo vya elimu walielimishwa kuhusu uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka;

(xii) Kukamilika kwa uingizwaji wa majalada 697 yenye kurasa 84,412 kwenye mfumo wa nyaraka kidigitali (Digital Records Management and Preservation System);

(xiii) Kukamilika kwa matengenezo ya Scanner nne (4) za kurudufu nyaraka; na

(xiv) Ujenzi wa jengo la Utawala la Kumbukumbu na Nyaraka la Makao Makuu Jijini Dodoma umefanyika na umefikia hatua ya msingi.



Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan akizindua Tovuti ya Makavazi ya Dkt. Salim Ahmed Salim, Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katibu Mkuu Mstaafu wa Umoja wa Afrika (O.A.U) – Septemba, 2023

**19 APRILI, 2024**

**MPANGO WA UTEKELEZAJI NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25 NA MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA**

**Mheshimiwa Spika,** Mpango na Bajeti kwa mwaka 2024/25 umeandaliwa kwa kuzingatia: Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025; Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26); na hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akihutubia Bunge tarehe 22 Aprili 2021. Shughuli zitakazotekelezwa na kila taasisi ni kama ifuatavyo:

**OFISI YA RAIS - IKULU NA TAASISI ZAKE**

**A. Ofisi ya Rais – Ikulu**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kutoa ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia, Mawasiliano na Habari, Uhusiano wa Kikanda, Kimataifa na ushauri mwingine kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi;

(ii) Kuwezesha ratiba ya kila siku ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(iii) Kutoa huduma kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na familia yake;

(iv) Kuratibu, kuandaa na kushiriki mikutano 45 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, mikutano 30 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) na mikutano 15 ya Baraza la Mawaziri;

(v) Kuandaa mikutano miwili (2) ya tathmini kati ya Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na wadau wengine;

(vi) Kutoa mafunzo kuhusu utayarishaji na uwasilishaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na uchambuzi wa sera kwa maofisa wa

Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na waratibu wa shughuli za Baraza la Mawaziri;

(vii) Kuchambua na kutoa ushauri kwa Katibu Mkuu Kiongozi katika masuala ya kiuchumi, kijamii, kisheria, kiulinzi na kiusalama, kimataifa na masuala mengine yote yanayowasilishwa;

(viii) Kufanya mafunzo na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Programu za Maboresho katika ngazi za Wizara, Mikoa na Serikali za Mitaa;

(ix) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa kwa kushirikisha wadau wa Sekta ya Umma na Binafsi;

(x) Kupokea na kuchambua taarifa za robo mwaka za utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Programu nyingine za maboresho;

(xi) Kujenga uwezo wa Taasisi za Umma kuhusu uzingatiaji wa utawala bora katika kutoa huduma kwa umma;

(xii) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu za maboresho katika ngazi za utekelezaji;

(xiii) Kupokea, kupitia na kuchambua rufaa 400 na malalamiko 500 ya watumishi wa umma na wananchi;

(xiv) Kuendesha mikutano mitatu (3) ya watendaji na maafisa wa Serikali kuhusu utaratibu wa kushughulikia malalamiko na rufaa pamoja na kufuatilia utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya Katibu Mkuu Kiongozi;

(xv) Kufanya ziara ya ufuatiliaji wa uzingatiaji wa sheria na maelekezo yanayotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi na Mkuu wa Utumishi wa Umma yanayohusu masuala ya usimamizi wa utawala wa Utumishi kwenye Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

(xvi) Kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Programu ya Kujenga Uwezo wa Taasisi za Serikali Kupambana na Rushwa (BSAAT).

**B. Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25, TAKUKURU imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kufanya utafiti na uchambuzi wa mifumo ya kiutendaji na utoaji huduma katika ajira, elimu, afya, na mifumo ya ukusanyaji mapato ili kubaini maeneo yenye mianya ya rushwa na kushauri namna ya kuziba mianya hiyo;

(ii) Kufuatilia matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha utekelezaji wake unazingatia thamani halisi ya fedha;

(iii) Kutekeleza mpango wa TAKUKURU RAFIKI ili kuwashirikisha wadau wengi zaidi kwenye kuzuia na kupambana na rushwa;

(iv) Kufanya warsha/vikao vya kuwashirikisha wadau kuweka mikakati ya kudhibiti mianya ya rushwa na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikakati hiyo;

(v) Kufuatilia matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha upatikanaji wa thamani halisi ya fedha;

(vi) Kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano wa TAKUKURU ili kujenga uwezo na uelewa kuhusu rushwa, ufisadi na juhudi za Serikali katika kupambana na rushwa kwa makundi mbalimbali katika jamii kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano kuyashawishi makundi haya kuunga mkono na kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa nchini;

(vii) Kutumia njia za mawasiliano za kimkakati kulifikia kundi la vijana ili washiriki katika shughuli zinazowajenga kimaadili na kupambana na rushwa;

(viii) Kutekeleza kazi za uelimishaji katika kutekeleza Awamu ya Nne ya Mpango Kazi wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa;

(ix) Kushirikisha umma katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kuandaa ajenda zenye maudhui ya mapambano hayo kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii;

(x) Kukamilisha uchunguzi wa majalada ya tuhuma za rushwa unaoendelea pamoja na tuhuma mpya zitakazojitokeza;

(xi) Kuhuisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura 329;

(xii) Kuendesha Mashauri ya rushwa mahakamani kwa kibali cha Mkurugenzi wa Mashataka;

(xiii) Kuimarisha mfumo wa TEHAMA katika taasisi ili kurahisisha na kuwezesha mtiririko mzuri wa majalada, takwimu na mawasiliano kutoka ngazi za Wilaya, mkoa na makao makuu; na

(xiv) Kutoa mafunzo ya weledi kwa watumishi ili kuwajengea umahili wa utendaji kazi na kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Taasisi.

**C. Taasisi ya UONGOZI**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25, Taasisi ya UONGOZI imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi 35 katika maeneo ya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimaliwatu na rasilimali nyingine ili kuongeza tija;

(ii) Kutoa mafunzo ya Cheti cha Uongozi kwa njia ya mtandao kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi 65 katika maeneo ya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimaliwatu na rasilimali nyingine, matumizi ya takwimu (data analytics);

(iii) Kutekeleza programu maalum ya mafunzo ya Uongozi kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi wanaochipukia 35 katika

maeneo ya maamuzi ya kimkakati, mawasiliano ya kimkakati, Uchambuzi wa Sera, na matumizi ya takwimu (data analytics);

(iv) Kutekeleza programu maalum ya mafunzo ya uongozi kwa wanawake viongozi waandamizi na viongozi wanaochipukia 150 kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kufanya maamuzi ya kimkakati, usimamizi wa rasilimali za Serikali na rasilimaliwatu. Vilevile, mafunzo haya yana lengo la kukuza vipaji vya uongozi kwa viongozi wanawake wanaochipukia. Mada zitakazotolewa zinajumuisha akili hisia, sanaa ya uongozi, itifaki, utaalamu na taswira ya kiongozi mwanamke, kuoanisha majukumu ya nyumbani na kazi, muundo wa Serikali na mawasiliano. Mada nyingine ni maadili ya ya uongozi, masuala ya jinsia, mawasiliano na mbinu za majadiliano, uchambuzi wa kimkakati na jinsi ya kufanya maamuzi, viashiria hatarishi na udhibiti wa mifumo ya ndani, uchambuzi wa kifedha, uandishi wa taarifa, na matumizi bora ya muda;

(v) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kupitia kozi 40 kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi 1,400 katika maeneo ya uongozi na maendeleo endelevu kwa ajili ya kuimarisha utendaji wao kwa kuzingatia mahitaji na maombi ya walengwa;

(vi) Kutekeleza programu maalum ya mafunzo ya uongozi kwa bodi 100 za Mashirika ya Umma, taasisi za umma na Wakala za Serikali kwa lengo la kuimarisha usimamizi na utendaji. Mafunzo haya yatahusu uongozi wa kimkakati, usimamizi wa Mashirika ya Umma, usimamizi wa rasilimali za umma na rasilimaliwatu na usimamizi wa viashiria hatarishi;

(vii) Kufanya tafiti tumizi sita (6) kuhusu masuala ya uongozi na maendeleo endelevu ili kutoa ushauri wa kisera kwenye masuala muhimu yanayohusu maendeleo ya nchi ikiwemo maendeleo ya Nne ya Viwanda, Uchumi wa Buluu, na mabadiliko ya Tabia Nchi;

(viii) Kukamilisha tawasifu inayoelezea maisha ya Hayati Rashid Mfaume Kawawa, aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuweka kumbukumbu za viongozi mashuhuri wa Taifa letu katika maandishi;

(ix) Kuandaa mikutano minne (4) ya kitaifa na miwili (2) ya kimataifa katika masuala ya uongozi kwa viongozi 590 kwa lengo la kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu na kuwaongezea uelewa wa masuala ya uongozi na maendeleo endelevu;

(x) Kuandaa vipindi sita (6) vya runinga vitakavyoshirikisha viongozi waandamizi na wataalam mbalimbali wa ndani na nje ya nchi, juu ya uongozi na maendeleo endelevu. Vipindi hivi vitarushwa kwenye runinga, tovuti na mitandao ya kijamii na kuonekana katika bara zima la Afrika;

(xi) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa taasisi tano (5) za Serikali katika maeneo yanayohusu masuala ya uongozi na maendeleo endelevu; na

(xii) Kutoa machapisho 12 juu ya masuala ya uongozi na maendeleo endelevu ikiwemo Tawasifu ya Hayati Rashidi Mfaume Kawawa.

**D. Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25, TASAF imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuhawilisha ruzuku kwa kaya maskini 1,266,567 zinazokidhi vigezo vya Mpango;

(ii) Kuwezesha utekelezaji wa Miradi ya Jamii ya Kutoa Ajira ya Muda kwa Kaya za walengwa katika mamlaka za utekelezaji 72. Jumla ya miradi 6,112 ya Jamii na ya Kutoa Ajira za Muda itatekelezwa katika ngazi ya Vijiji/Mitaa/Shehia na inategemewa kutoa ajira za muda kwa Walengwa 386,340;

(iii) Kuwezesha Jamii kutekeleza miradi ya kuendeleza miundombinu ya huduma za jamii katika sekta mbalimbali. Jumla ya miradi 271 itatekelezwa katika Vijiji/Mitaa/shehia katika sekta za afya, elimu, maji, mazingira na ujasiriamali. Aidha, Wafanyakazi 120 wa Halmashauri watapewa mafunzo juu ya namna ya kutekeleza na kusimamia miradi hii;

(iv) Kuwezesha uundaji wa Vikundi vya Kuweka Akiba na Kuwekeza katika mamlaka za utekelezaji 62. Jumla ya Vikundi 6,820 vya jamii vya Kuweka Akiba na Kuwekeza vinatarajiwa kuundwa na kuwawezesha walengwa kuanzisha shughuli za kiuchumi na kaya zilizofikia hatua hiyo kupatiwa ruzuku ya kuboresha biashara zao. Aidha, mafunzo kwa wawezeshaji 1,860 yatatolewa katika Maeneo ya Utekelezaji 62 kuhusu uundaji wa Vikundi vya Kuweka Akiba na Kuwekeza;

(v) Kuongeza idadi ya walengwa wanaolipwa kwa njia za kielekitroniki kufikia 50% ya walengwa wote;

(vi) Kuimarisha miundombinu ya mifumo ili kulinda usalama wa taarifa za walengwa na kuungamanisha mfumo wa walengwa na mifumo mingine ya Serikali ili kuweza kubadilishana taarifa kwa urahisi. Aidha, mfumo wa sasa utafanyiwa mapitio kwa ajili ya maboresho makubwa yanayoendana na mabadiliko ya teknolojia na mahitaji ya taarifa za walengwa kwa Taasisi na wadau wangine;

(vii) Kufanya tathmini na ufuatiliaji wa shughuli za Mpango ili kuona ni kwa kiwango gani malengo ya Mpango yanafikiwa, kubainisha changamoto na kuzishughulikia ili kuboresha utendaji kazi na matokeo ya Mpango yanayotarajiwa; na

(viii) Kufanya Mapitio ya pamoja baina ya Timu ya Serikali na Wadau wa Maendeleo kuhusu utekelezaji wa shughuli za Mpango.

**E. Wakala wa Ndege za Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25, Wakala wa Ndege za Serikali imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa;

(ii) Kuratibu ununuzi pamoja na kusimamia mikataba ya ukodishaji wa ndege kwa Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL);

(iii) Kulipia gharama za bima za ndege pamoja na wanaanga;

(iv) Kugharamia uendeshaji wa Ofisi na kulipia gharama za mafuta ya ndege; na

(v) Kutoa mafunzo ya kisheria kwa wanaanga kwa ajili ya kuhuisha leseni zao.

**F. Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) imeanzishwa kwa Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019 ikiwa na jukumu la Kuratibu, Kusimamia na Kukuza jitihada za Serikali Mtandao pamoja na kusimamia uzingatiwaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo ya Serikali Mtandao kwa Taasisi za Umma. Mamlaka ya Serikali Mtandao ni taasisi iliyoirithi Wakala ya Serikali Mtandao ambayo iliundwa kwa kwa Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 Sura ya 245 ya Mwaka 1997 Mamlaka ikiwa na nguvu zaidi za usimamizi. Kwa kipindi chote hicho Mamlaka imekuwa chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mnamo tarehe 14 Februari, 2024, Katibu Mkuu Kiongozi alitoa maelekezo ya kuihamisha Mamlaka ya Serikali Mtandao kutoka Ofisi ya Rais – Utumishi kwenda Ofisi ya Rais – Ikulu ili kuiongezea ufanisi katika kutekeleza Majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25, Mamlaka ya Serikali Mtandao imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kusimamia na kutathmini hali ya usalama wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA, hatimaye kushauri maeneo ya kuboresha na kufuatilia utekelezaji wake ili kuhakikisha kuwa Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA Serikalini inafanya kazi na kutoa huduma kwa Taasisi za Umma na wananchi wakati wote kwa ufanisi na usalama;

(ii) Kuboresha utoaji wa huduma katika Utumishi wa Umma, kwa kuendelea kufanya maboresho na kuhuisha Mifumo ya TEHAMA jumuishi, Mifumo ya Kisekta na Mifumo ya Kitaasisi inayotumika;

(iii) Kufanya uchambuzi, kusanifu na kujenga Mifumo mipya ya Kisekta kwa Taasisi zenye taratibu za utendaji kazi zinazoendana kwa lengo la kupunguza wingi wa Mifumo ya TEHAMA Serikalini;

(iv) Kuiunganisha Mifumo ya Taasisi za Serikali kwenye Mfumo wa kuwezesha Mifumo ya Serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa (Government Enterprise Service Bus (GovESB)) kwa kufuata mpango kazi;

(v) Kuendeleza Utafiti na Ubunifu katika matumizi ya teknolojia mpya za TEHAMA ili kuibua huduma mpya kwa umma kupitia TEHAMA na kuwezesha matumizi sahihi ya teknolojia mpya zinazoibuka;

(vi) Kupanua miundombinu ya Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (Government Network) ili kuifikisha katika Halmashauri zote nchini na kuziwezesha Taasisi nyingi zaidi kutumia Mifumo ya Serikali ya kutolea huduma na uendeshaji kazi;

(vii) Kukagua Mifumo ya Kimkakati, Kisekta na Kitaasisi ili kuhakikisha kuwa imetengenezwa na inatumika kwa kufuata Sheria, Kanuni, Viwango na Miongozo iliyopo na kushauri maeneo ya kuboresha na kufuatilia utekelezaji wake;

(viii) Kusimamia, kuendesha na kuendeleza Mifumo na Miundombinu Shirikishi ya TEHAMA ya Serikali na Taasisi zake, ikiwa ni pamoja na mtandao wa mawasiliano katika Mji wa Serikali na kusimamia na kuboresha vituo vya kuhifadhi Mifumo na Taarifa za Serikali pamoja na vituo vya kujikinga na majanga;

(ix) Kuwajengea uwezo Watumishi katika kusimamia Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA katika Taasisi za Umma, pamoja na kutoa mafunzo kwa watumiaji kuhusu matumizi sahihi na salama ya Mifumo na Miundombinu ya TEHAMA; na

(x) Kutoa ushauri wa kitaalamu na msaada wa kiufundi kwenye maeneo ya TEHAMA kwa Taasisi za Serikali ili kuhakikisha kuwa Viwango na Miongozo inafuatwa na kuwa na matumizi ya TEHAMA yenye tija na kupunguza gharama.

### *F.* **Baraza la Kumshauri Rais Kuhusu Masuala ya Chakula na Kilimo *(Presidential Food and Agriculture Delivery Council)***

**Mheshimiwa Spika,** Baraza la Kumshauri Rais kuhusu Masuala ya Chakula na Kilimo *(Presidential Food and Agriculture Delivery Council)* lilianzishwa tarehe 14 Machi, 2023 na Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania. Lengo la kuanzishwa kwa Baraza hili ni kumshauri Rais kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu chakula na kilimo, kufuatia maazimio yaliyofanywa na Viongozi Wakuu wa Nchi na Serikali katika Mkutano wa *Dakar 2 Summit on Feed Africa: Food Sovereignty and Resilience* uliofanyika nchini Senegal. Tanzania imeainisha mazao ya kipaumbele katika kuongeza uzalishaji na tija ambayo ni ngano, alizeti, parachichi, nyama ya ng'ombe na maziwa.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25, Baraza la Kumshauri Rais kuhusu Masuala ya Chakula na Kilimo limepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kupitia nyaraka mbalimbali za kisekta, kitaifa, kikanda na kimataifa ili kuwianisha malengo yaliyomo katika Mkakati wa Kufanya Mageuzi katika Kilimo na Kuongeza Upatikanaji wa Chakula Tanzania;

(ii) Kuandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utakaoliwezesha Baraza kubaini mwelekeo katika kutekeleza Mkakati wa Kufanya Mageuzi katika Kilimo na Kuongeza Upatikanaji wa Chakula Tanzania;

(iii) Kujenga uwezo wa Baraza katika kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na mafunzo, ajira za wataalam, ununuzi wa vitendea kazi, utoaji wa huduma na ukarabati kwa ajili ya Ofisi ya Baraza;

(iv) Kufanya mikutano na wadau wa Kanda za Nane Nane zilizobakia ili kujifunza kilichopo katika maeneo hayo kwa kuzingatia malengo ambayo Tanzania imejiwekea katika kutekeleza Mkakati wa Kufanya Mageuzi katika Kilimo na Kuongeza Upatikanaji wa Chakula Tanzania;

(v) Kushauriana na wadau katika sekta ya umma ili kuwa na uelewa wa pamoja katika utekelezaji wa mikakati ya kisekta ambayo inawiana na malengo yaliyomo katika Mkakati wa Kufanya Mageuzi katika Kilimo na Kuongeza Upatikanaji wa Chakula Tanzania;

(vi) Kushauriana wadau wa sekta binafsi, wadau wa maendeleo, makundi maalum na taasisi zisizo za kiserikali ili kufahamu zaidi shughuli zao na namna zinavyoendana na malengo yaliyomo katika Mkakati wa Kufanya Mageuzi katika Kilimo na Kuongeza Upatikanaji wa Chakula Tanzania na pia kuimarisha uhusiano na ushirikiano;

(vii) Kuandaa mapendekezo ya kuongeza upatikanaji wa huduma za kifedha katika maeneo ya vijijini;

(viii) Kuandaa mapendekezo ya namna bora ya kuimarisha ushirikiano baina ya sekta ya Umma na sekta binafsi;

(ix) Kuandaa mikakati ya kushirikisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya kilimo ikiwa ni pamoja na kutambua maeneo ya uwekezaji;

(x) Kuandaa maandiko ya kutafuta fedha kwa ajili ya shughuli za kilimo kwa kushirikiana na Wizara na Taasisi za Serikali zinazohusika ili kutekeleza na kufikia malengo ya Mkakati wa Kufanya Mageuzi katika Kilimo na Kuongeza Upatikanaji wa Chakula kwa ufanisi nchini;

(xi) Kuchambua, kupendekeza na kuwezesha matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya kilimo na ufugaji wa ng'ombe; na

(xii) Kuchambua na kupendekeza mifumo bora na endelevu ya masoko ya mazao na bidhaa za kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais, Ikulu: Fungu 20 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 33,544,557,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri: Fungu 30 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 969,285,723,000.00** kati ya fedha hizo, **shilingi 805,676,639,000.00** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 110,439,177,000.00** kwa ajili ya miradi

ya maendeleo kwa fedha za ndani na **shilingi 53,169,907,000.00** fedha za nje.

**OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma itaendelea na vipaumbele vikuu viwili (2) ambavyo ni kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa taasisi na wananchi ili kuweza kuwafikia kwa urahisi; na kuimarisha uwajibikaji wa pamoja miongoni mwa viongozi wa umma hasa katika suala la viongozi kukinzana kunakosababisha shughuli za maendeleo kutotekelezeka kwa wakati. Kada za viongozi zitakazojumuishwa katika eneo hili ni pamoja na Wakuu wa Idara na Madiwani kutoka katika halmashauri ambazo hazijafikiwa na kupatiwa mafunzo husika. Kupitia vipaumbele hivyo shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:

(i) Kupokea Tamko la Viongozi wa Umma kuhusu Rasìlìmalì na Madeni Ììnalopaswa kutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(ii) Kupokea malalamiko na taarifa za ukiukwaji wa Maadili kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kutoka kwa wananchi;

(iii) Kuchunguza tuhuma yoyote ya kuvunjwa kwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma dhidi ya Viongozi wa Umma;

(iv) Kufanya uhakiki wa matamko ya Rasilimali na Madeni kwa Viongozi wa Umma 650;

(v) Kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Maadili ya Viongozi wa Umma;

(vi) Kuelimisha Viongozi wa Umma na Wananchi kwa ujumla kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Hati ya Ahadi ya Uadilifu na Uwajibikaji wa pamoja;

(vii) Kuandaa taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa shughuli za Sekretarieti na kuiwasilisha kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(viii) Kuendeleza na kuanzisha Klabu za Maadili katika shule na vyuo nchini; na;

(ix) Kuendeleza ujenzi wa Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Ziwa.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma: Fungu 33 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 13,142,650,000.00** Kati ya fedha hizo, **shilingi 11,642,650,000** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 1,500,000,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE**

**A. Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kufanya ufuatiliaji endelevu wa Utekelezaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi wa Mtumishi na Taasisi katika Utumishi wa Umma (PEPMIS & PIPMIS) katika Taasisi za Umma;

(ii) Kujenga uwezo na uelewa kuhusu matumizi ya Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma kwa watumishi na Taasisi za Umma;

(iii) Kutoa msaada wa kitaalamu kwa watumiaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma;

(iv) Kufanya mapitio ya Sera ya Motisha na Malipo ya mwaka 2010;

(v) Kukamilisha Sera ya TEHAMA Serikalini na kuanzisha mchakato wa uidhinishaji katika mamlaka za maamuzi;

(vi) Kuwezesha, kupitia na kupendekeza kuidhinishwa kwa Miundo ya Maendeleo ya Utumishi ya Taasisi na Mashirika ya Umma;

(vii) Kuwezesha, kupitia na kupendekeza kuidhinishwa kwa Miundo ya Motisha/Mikataba ya Halibora kwa Taasisi na Mashirika ya Umma;

(viii) Kufanya utafiti kuhusu hali ya masilahi kwa watumishi wa umma;

(ix) Kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali yanayohusu masilahi kwa watumishi wa Umma;

(x) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Kuangalia Jinsi ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai nchini;

(xi) Kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu Sera za Utawala na Rasilimaliwatu;

(xii) Kufanya ufuatiliaji wa malalamiko yanayohusiana na Utumishi yanayotokana na ukiukwaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na maagizo mengine yanayoongoza Utumishi wa Umma katika eneo la uhamisho, upandishwaji vyeo na uteuzi;

(xiii) Kutoa elimu ya uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia Utumishi wa Umma katika Taasisi kumi (10);

(xiv) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa ujumuishwaji wa anuai za jamii mahali pa kazi katika Utumishi wa umma;

(xv) Kuzindua na kusambaza Toleo la III la Mwongozo wa Kudhibiti VVU, UKIMWI, MYA na changamoto za afya ya AKILI mahali pa kazi;

(xvi) Kushiriki katika vikao vya Jumuiya za kikanda na kimataifa vinavyohusu masuala ya Rasilimaliwatu na utawala;

(xvii) Kuhuisha nyaraka na miongozo inayokinzana katika Utumishi wa Umma;

(xviii) Kukamilisha na kuchapisha Mwongozo wa Kiunzi cha Mpango wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma, na Mwongozo wa Mpango wa Mafunzo katika Utumishi wa Umma;

(xix) Kuzijengea uwezo Taasisi za Umma kuandaa na kutekeleza Mpango wa Rasilimaliwatu, Mpango wa Mafunzo na Mpango wa Urithishanaji Madaraka;

(xx) Kuratibu utoaji wa Vibali vya Kazi na Ukaazi kwa Wataalam wa Kigeni wanaokuja kufanya kazi katika Sekta ya Umma nchini;

(xxi) Kuratibu fursa za mafunzo zinazotolewa na Wadau wa Maendeleo katika Utumishi wa Umma;

(xxii) Kufanya maandalizi ya awali kwa ajili ya kufanya mapitio ya Sera ya Mafunzo katika Utumishi wa Umma ya mwaka 2013;

(xxiii) Kuratibu Ajira za Wataalam Wazawa katika Taasisi za Kikanda na Kimataifa;

(xxiv) Kuendeleza ujenzi wa mfumo wa Kielektroniki wa Mpango wa Rasilimaliwatu (e-HRP);

(xxv) Kuanza usanifu wa mfumo wa Kielektroniki wa fursa za ufadhili wa masomo zinazotolewa na Washirika wa Maendeleo (scholarship portal);

(xxvi) Kutumia mikakati mbalimbali ya mawasiliano ili kuuhabarisha umma juu ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;

(xxvii) Kutumia vyombo vya Habari na mitandao ya kijamii kuelimisha Umma kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;

(xxviii) Kutumia fursa ya maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma kupata mrejesho kutoka kwa wadau kuhusu ufanisi wa utumishi wa umma na kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika utumishi wa umma;

(xxix) Kuboresha huduma za Maktaba ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili watumishi na wadau wengine waweze kupata na kurejea machapisho na nyaraka mbalimbali kwa urahisi;

(xxx) Kuandaa Mwongozo wa Bajeti ya Mishahara kwa kuzingatia vipaumbele vya Taifa na kuratibu maandalizi ya Ikama na Bajeti ya Mishahara ya mwaka 2024/25;

(xxix) Kushughulikia vibali vya ajira ili kujaza nafasi zilizoidhinishwa katika Ikama;

(xxx) Kuhakiki na kuidhinisha madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi kwa taasisi 433;

(xxxi) Kusafisha taarifa za kiutumishi na mishahara (Data Cleaning) kwa watumishi waliopo katika Taasisi 433 zinazotumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara;

(xxxii) Kuhakiki na kuidhinisha mabadiliko ya taarifa za kiutumishi na zinazohusiana na mishahara katika Mfumo wa HCMIS kwa taasisi 433;

(xxxiii) Kutoa mafunzo ya matumizi ya Mfumo Mpya wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara kwa watumishi 640 kwa ngazi tofauti;

(xxxiv) Kuwezesha taasisi 54 kati 89 ambazo kwa sasa hazitumii Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) kuanza kutumia Mfumo huo katika kusimamia masuala ya kikutumishi na mishahara;

(xxxv) Kufanya ufuatiliaji na tathimini kwa Taasisi zilizoingizwa katika Mfumo mpya wa HCMIS;

(xxxvi) Kufanya Mapitio ya Miundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Taasisi mbalimbali za Umma;

(xxxviii) Kuendeleza uchambuzi na usanifu wa Mfumo wa Tathmini ya Mahitaji ya Rasilimaliwatu ili uweze kuwa nyenzo muhimu katika kubaini mahitaji halisi ya watumishi katika Taasisi za Umma;

(xxxix) Kuimarisha na kufanya ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mifumo na Viwango vya Utendaji Kazi na kutoa ushauri wa kitaalam katika taasisi mbalimbali za Serikali;

(xl) Kukusanya taarifa za huduma za Taasisi kwa ajili ya kuziingiza katika Daftari la Huduma za Serikali;

(xlii) Kuwezesha Mifumo ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu kubadilishana taarifa. Hii itahusisha kuiwezesha mifumo ya HCMIS, e-Office, PEPMIS/PIPMIS, HRA, MUSE, Mifumo ya Tume ya Utumishi wa Umma, Tume ya Utumishi wa Waalimu, e-Mrejesho and Ajira Portal kubadilishana taarifa;

(xliii) Kufanya maboresho ya Mfumo wa Taarifa za Usimamizi wa Rasilimaliwatu (HCMIS) kulingana na Teknologia iliyotumika (Java, Angular, Spring Boot);

(xliv) Kuratibu matumizi ya Mifumo jumuishi ya TEHAMA, ikiwemo mifumo ya eOffice, e-Board, ERMS (fuel, maintenance) ili kuondoka kwenye matumizi ya makaratasi na kuendesha shughuli za Serikali kidijitali;

(xlv) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya Utekelezaji wa Sera za Menejimenti ya Utumishi wa Umma;

(xlvi) Kufanya Kampeni za kimaadili kwa Taasisi za Umma katika Sekta ya Afya (Supply Led), pamoja na kufanya Uhamasishaji wa Maadili ya Utendaji katika Taasisi za Umma (Demand lead);

(xlvii) Kufanya kampeni za Kimaadili kupitia vyombo vya habari na kusimamia maadili katika mambo Mtambuka;

(xlviii) Kufanya mapitio ya Kiapo cha Ahadi ya Uadilifu kwa watumishi wa Umma;

(xlix) Kufanya mapitio ya Mwongozo wa Ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma;

(l) Kufanya Ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Maadili ya Utendaji katika Utumishi wa Umma;

(lii) Kukamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi la ghorofa tano (5) la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika eneo la Mtumba – Dodoma;

(liii) Kuendeleza ujenzi wa Klabu ya Viongozi - Makao Makuu eneo la Nzuguni karibu na Stendi ya Mabasi ya Nanenane Dodoma;

(liiii) Kukamilisha usanifu kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Rais wa Awamu ya Sita Mhe. Samia Suluhu Hassan; na

(liv) Kutoa huduma kwa Viongozi wa Kitaifa Wastaafu (Viongozi tisa na wajane tisa) kwa mujibu wa sheria.

**B. Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC)**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25, Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) kimepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kutoa mafunzo ya kujiandaa kufanya mitihani ya Utumishi wa Umma kwa watumishi 1,385 ili kuwajengea uwezo wa utendaji kazi na kutoa huduma bora kwa wananchi;

(ii) Kutoa mafunzo ya Uongozi na Maendeleo, Menejimenti na Usimamizi wa Ofisi kwa watumishi wa umma 7,665 ili kuendeleza stadi, weledi na ujuzi katika maeneo hayo. Aidha, watumishi wa umma 400 watapatiwa mafunzo hayo kwa njia ya mtandao;

(iii) Kutoa Mafunzo ya Awali katika Utumishi wa Umma kwa watumishi wapya wa umma 4,258 ili kuwajengea uelewa wa kitendaji wa serikalini na misingi ya utumishi wa umma;

(iv) Kuwezesha midahalo ya kubadilishana uzoefu wa kitaalam kwa washiriki wa ndani na nje ya nchi wapatao 250 ili kupunguza gharama za Serikali kupeleka watumishi nje ya nchi;

(v) Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa washiriki 12,234 katika fani za Utunzaji wa Kumbukumbu, Uhazili, Kompyuta, Utunzaji wa Fedha za Umma, na Menejimenti ya Rasilimaliwatu, Usimamizi na Manunuzi ya Umma, Uongozi na Utawala Bora;

(vi) Kutoa shauri za kitaalamu katika maeneo mbali mbali kwa Taasisi za Umma 18 kwa ajili ya kutambua changamoto halisi za utendaji na kuchangia katika utoaji wa maamuzi yanayozingatia matokeo ya utafiti;

(vii) Kufanya tafiti tumizi sita (6) katika maeneo ya Utumishi wa Umma yanayolenga kuboresha utoaji huduma kwa wananchi;

(viii) Kuratibu midahalo kwa njia ya mtandao katika maeneo 5 kwa watumishi wa umma na wa sekta binafsi;

(ix) Kuwezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 8 wa Chuo cha Utumishi wa Umma katika ngazi za Shahada ya Uzamivu na Shahada ya Uzamili;

(x) Kutoa mafunzo ya mahali pa kazi kwa watumishi wote 279 ili kuwajengea uelewa kuhusu Mkakati wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa, maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na UKIMWI pamoja na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa;

(xi) Kuwezesha ununuaji wa vitendea kazi kwa ajili ya kuhamia majengo mapya yanayomilikiwa na Chuo;

(xii) Kukarabati majengo katika kampasi ya Tabora kwa ajili ya kuhamishia kada ya Uhazili na Utunzaji Kumbukumbu kwa ngazi ya shahada;

(xiii) Kuandaa mchoro kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya kampasi ya Tanga; na

(xiv) Kufuatilia upatikanaji wa eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi ya Mbeya.

**C. Watumishi Housing Investment (WHI)**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25, Watumishi Housing Investment imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kutekeleza ujenzi wa nyumba 60 katika Mradi wa Magorofa Kisasa Relini, Njedegwa Dodoma (Kisasa Relini Apartments);

(ii) Kutekeleza ujenzi wa nyumba 42 za Mradi wa Makazi kwa Watumishi wa Umma Wilayani hasa Wilaya mpya;

(iii) Kutekeleza ujenzi wa nyumba 15 za magorofa Mradi wa Makazi kwa Watumishi wa Umma Wilayani/Halmashauri zilizopo mijini;

(iv) Kutekeleza ujenzi wa nyumba 90 katika Mradi wa Maghorofa Mikocheni Dar es Salaam (110 Mikocheni Apartments);

(v) Kukuza Mfuko wa Faida ili ufikie thamani ya Shilingi bilioni 35 ifikapo tarehe 30 Juni 2025;

(vi) Kufanya mauzo ya viwanja 223 vilivyopimwa USA River jijini Arusha na kukamilisha miundombinu ya maji na umeme; na

(vii) Kutoa huduma za ujenzi na ushauri kwa Taasisi za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/2025, Fungu 32 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 58,314,993,000.00** Kati ya fedha hizo, **shilingi 48,254,069,000.00** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 9,933,174,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa fedha za ndani na **shilingi 127,750,000.00** fedha za nje.

**OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25 Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Ummaitaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuwezesha kupatikana wataalam katika Utumishi wa Umma katika maeneo ya vipaumbele kama ifuatavyo:

(i) Kusimamia na kuendesha michakato ya Ajira ili kuwezesha waajiri kupata Watumishi wenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa Miundo ya Utumishi husika;

(ii) Kuimarisha Ofisi za Sekretarieti ya Ajira kwa kuwapatia Watumishi vitendea kazi,kuboresha maslahi na mafunzo ili kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Taasisi;

(iii) Kutoa taarifa na elimu kwa umma ili kukuza uelewa kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

(iv) Kuimarisha utendaji kazi wa Taasisi kwa kutumia TEHAMA;

(v) Kuimarisha upatikanaji wa Takwimu za Ajira; na

(vi) Kuimarisha uwajibikaji na udhibiti wa matumizi ya fedha na shughuli nyingine za Sekretarieti ya Ajira kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Fungu 67 inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 13,179,878,000.00**. Kati ya fedha hizo **shilingi 10,831,831,000.00** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 2,348,047,000.00** ni fedha zamiradi ya maendeleo.

**OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA (PSC)**

**Mheshimiwa Spika,** majukumu yaliyopangwa kutekelezwa na Tume kwa mwaka 2024/25 ni kama ifuatavyo:

(i) Kufanya ukaguzi wa kawaida katika Taasisi za Umma 180 na Ukaguzi Maalum katika Taasisi za Umma 10 kwa lengo la kuangalia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;

(ii) Kufanya mikutano minne (4) ya kisheria ya Tume kujadili na kutolea uamuzi rufaa, malalamiko, taarifa za masuala ya Kiutumishi na masuala mengine ya kiutumishi kadri yatakavyopokelewa;

(iii) Kuhuisha Miongozo ya Tume ya Uzingatiaji wa masuala ya Kiutumishi;

(iv) Kuelimisha wadau 1,500 katika Taasisi za Umma na Serikali za Mitaa kuhusu majukumuya Tume na uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma;

(v) Kuwajengea uwezo watumiaji 1,300 wa Mfumo mpya wa Kielektroniki wa Kushughulikia Rufaa, Malalamiko na Ukaguzi wa Uzingatiaji wa Sheria.

(vi) Kuandaa Taarifa ya Hali ya Utumishi wa Umma na Utekelezaji wa Majukumu ya Tume kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2023/24 na kuiwasilisha kwa Rais wa Jamhuri yaMuungano wa Tanzania;

(vii) Kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kutoa ufafanuzi na kujibu hoja za mashauri ya warufani yanayofikishwa Mahakamani;

(viii) Kukamilisha Ujenzi wa Jengo la Ofisi za Tume katika Mji wa Serikali Mtumba; na

(ix) Kufanya maboresho ya Mfumo wa Kielektroniki wa Kushughulikia Rufaa na Ukaguziwa Uzingatiaji kwa ajili ya kuongeza ufanisi kwenye ushughulikiaji wa Rufaa na Ukaguzi wa Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25, Fungu 94, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 9,240,889,000.00** ili kutekeleza shughuli zilizotajwa hapo juu. Kati ya fedha hizo **shilingi 8,740,713,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 500,176,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani.

**OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25 Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kukusanya taarifa, kumbukumbu, nyaraka na machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya nchi yetu kutoka katika Taasisi za Umma na watu binafsi;

(ii) Kutambua, kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa;

(iii) Kuweka na kuhuisha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu (Keyword filing system and e-file management system) katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma Serikalini;

(iv) Kuimarisha mifumo ya kielektroniki katika usimamizi wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka katika teknolojia ya kisasa kwa kuingiza nyaraka katika mfumo wa kidijitali (Digital Records Management and Preservation System) wa kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka ili kurahisisha upatikanaji wake na kulinda nakala halisi;

(v) Kuwezesha Taasisi za Umma kuandaa miongozo ya kuhifadhi na kuteketeza kumbukumbu pamoja na kufanya tathmini (appraisal) ya kumbukumbu tuli za Taasisi za Umma zilizohifadhiwa katika Vituo vya Idara vya kuhifadhia kumbukumbu;

(vi) Kuweka na kusimamia viwango vya utumiaji na utunzaji kumbukumbu na nyaraka katika Taasisi za Umma;

(vii) Kuzijengea uwezo Taasisi za Umma katika usimamizi wa kumbukumbu na nyaraka za Serikali kwa kuandaa mikutano kazi kwa Menejimenti za Taasisi za Umma na mafunzo kazi kwa watumishi, waratibu na watunza kumbukumbu kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya utunzaji wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za Serikali; na

(viii) Kutoa elimu kwa Watumishi wa umma na wananchi kuhusu umuhimu wa utunzaji na uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka pamoja na kukuza uelewa kuhusu shughuli za Idara.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2024/25, Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Fungu 4, inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 4,360,777,000.00**. Kati ya fedha hizo, **shilingi 4,065,013,000.00** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 295,764,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani.

**MAJUMUISHO**

**Mheshimiwa Spika,** kimsingi, Ofisi ya Rais ikiongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, ina dhamana ya kufanya maamuzi muhimu kuhusu nchi, na kwa umuhimu wake inahusika pia na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambavyo, kwa pamoja vinakuwa ndio nguzo kuu katika uendeshaji wa nchi. Ifahamike kuwa Utumishi wa Umma na Utawala Bora una mchango mkubwa katika maendeleo ya Taifa, na ni dhahiri kuwa mchango endelevu wa watumishi wa umma na uwepo wa Utawala Bora utaliendeleza Taifa na kuleta ustawi kwa Watanzania. Aidha, maendeleo haya yanatarajiwa kuongezeka kwa kuimarisha uchumi shindani na viwanda kwa manufaa ya watu kama inavyosisitizwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP III).

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imelenga kuwa na Utumishi wa Umma unaotoa huduma bora kwa haraka na staha, ukizingatia Katiba, Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo katika kujenga imani zaidi kwa wananchi na kuendana na kauli ya, **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa tarehe 22 Aprili, 2021 wakati akilihutubia Bunge la 12 aliposema:

> ***"Tutawapima viongozi na watumishi kwa namna wanavyotimiza majukumu yao, hatutawaonea aibu viongozi na watumishi wazembe, wezi na wabadhirifu wa mali za umma. Tutaendeleza pia juhudi za kupambana na rushwa kwenye Utumishi wa Umma.Wajibu wa watumishi wa umma ni lazima uendane na haki zao."***

Katika kuendana na wakati, jitihada zaidi zitawekwa kwenye kujenga uwezo na mifumo ya kimenejimenti na utoaji huduma ikiwemo matumizi sahihi na salama ya fursa zinazopatikana katika utoaji huduma kwa TEHAMA ndani ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Bajeti ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora itawezesha utekelezaji wa majukumu ya vyombo vinavyosaidia kwenye maamuzi ya nchi, usalama, uimarishaji vita dhidi ya rushwa, usimamizi wa maadili ya viongozi wa umma,

usimamizi wa rasilimaliwatu na rasilimali fedha kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma kwa wananchi kwa ufanisi. Aidha, Ofisi itahakikisha kuwa kunakuwepo na utawala bora ulio imara katika ngazi zote za uongozi ambapo msisitizo zaidi utawekwa kwenye kuimarisha misingi ya utawala bora, ushirikishwaji, uwazi na uwajibikaji. Ofisi ya Rais itahakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa sahihi kuhusu maamuzi ya Serikali na kuimarisha mifumo ya uwajibikaji wa Serikali kwa umma.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Hati Idhini, nawajibika kuwasilisha mapitio ya utekelezaji mipango na bajeti ya Ofisi ya Rais Ikulu; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; na Ofisi ya Rais, Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2023/24 na Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora sasa naomba kuwasilisha rasmi mapendekezo ya maombi ya fedha kwa mwaka 2024/25 kwa muhtasari kama ifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | **Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 33,544,557,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **Sh.** | **33,544,557,000.00** |
| 2. | **Fungu 30: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 805,676,639,000 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 163,609,084,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **Sh.** | **969,285,723,000.00** |
| 3. | **Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 11,642,650,000.00 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 1,500,000,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **Sh.** | **13,142,650,000.00** |
| 4. | **Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 48,254,069,000.00 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 10,060,924,000.00 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | **Jumla Ndogo** | **Sh.** | **58,314,993,000.00** |
| 5. | **Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 10,831,831,000.00 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 2,348,047,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **Sh.** | **13,179,878,000.00** |
| 6. | **Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 8,740,713,000.00 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 500,176,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **Sh.** | **9,240,889,000.00** |
| 7. | **Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 4,065,013,000.00 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 295,764,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **Sh.** | **4,360,777,000.00** |

**Mheshimiwa Spika,** jumla kuu ya Bajeti ninayoomba kwa mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) kwa mwaka 2024/25, ni kama ifuatavyo:

| **MATUMIZI** | **KIASI (SH.)** |
|---|---|
| Matumizi ya Kawaida | 922,755,472,000.00 |
| Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | 178,313,995,000.00 |
| **Jumla Kuu kwa Mafungu Yote** | **1,101,069,467,000.00** |

**Mheshimiwa Spika,** mwisho naomba kuwasilisha maombi haya ili Bunge lako Tukufu liweze kuyajadili na kuyaidhinisha.
**Asanteni kwa kunisikiliza, naomba kutoa hoja.**

**George B. Simbachawene (Mb)**
WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA)

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria. *(Makofi)*

**MHE. FLORENT L. KYOMBO – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuliwezesha Bunge kufuatilia taarifa hii ipasavyo, naomba kutambulisha sehemu nne za taarifa hii ambazo ni: -

(a) Sehemu ya Kwanza inahusu maelezo ya jumla na inabainisha msingi na muundo wa Taarifa hii;

(b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia mwenendo wa upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa ushauri wa Kamati;

(c) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na maoni na ushauri wa Kamati;

(d) Sehemu ya Nne ni Hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa Kamati kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kifungu cha 6(2)(a) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii ni kufanya uchambuzi. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, imeweka masharti yanayotaja taarifa ya utekelezaji na makadirio ya ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mawanda ya uchambuzi. Katika uchambuzi huo Kamati ilipitia jumla ya mafungu saba ambayo ni: -

(a) Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu;

(b) Fungu 30: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;

(c) Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;

(d) Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(e) Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

(f) Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; na

(g) Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matokeo ya uchambuzi wa tathmini. Matokeo ya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa

Umma na Utawala Bora. Kwa msingi huo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, Taarifa hii imejielekeza kwenye maeneo yafuatayo:-

(a) Matokeo ya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(b) Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(c) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge; na

(d) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matokeo ya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Kamati ilizingatia Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kazi iliyofanyika tarehe 22 na 23 Machi, 2024. Uchambuzi huo umejikita kwenye kulinganisha uwiano wa fedha zilizoidhinishwa, fedha zilizopokelewa pamoja na Utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Fungu Na. 20 na Fungu Na. 30 – Ofisi ya Rais, Ikulu na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Fungu Na. 20 - Ofisi ya Rais, Ikulu iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 32.157 kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi bilioni 9.318 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 22.838 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari 2024, Fungu Na. 20 lilipokea jumla ya shilingi bilioni 21.502 kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na 58.47% ya kiasi kilichoidhinishwa na shilingi bilioni 5.715, sawa na 61.34% ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 15.787 sawa na 69.13% ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, fedha zilizopokelewa zimetumika kwa 100%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Fungu Na. 30 – Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 860.186. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 678.193 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 674.342 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 3.851 zilitengwa kwa ajili ya mishahara. Aidha, shilingi bilioni 181.992 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo shilingi bilioni 80.598 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 101.394 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2024, Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 608.297 sawa na 70% ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 490.375 sawa na 72.12% zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 117.922 sawa na 60.48% zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo shilingi bilioni 47.15 sawa na 58.5% ni fedha za ndani na shilingi bilioni 70.766 sawa na 69.8% ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Fungu Na. 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 81.504. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 69.517 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi bilioni 25.141 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 31.988 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha kwenye miradi ya maendeleo jumla ya shilingi bilioni 12.070 ni fedha za ndani na jumla ya shilingi milioni 117.25 ni fedha za nje. Ambapo jumla ya fedha zilizoidhinishwa ni shilingi bilioni 12.17.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2024, Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 42.553 sawa na 52.2% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 38.460 sawa na 67.32% zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi bilioni 22.257 zilipokelewa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 16.203 zilipokelewa kwa ajili ya mishahara. Aidha, shilingi bilioni 4.092 sawa na 33.58% fedha za ndani zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Fungu Na. 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 12.763. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 10.813 zilitengwa kwa ajili ya matumizi

ya kawaida, ambapo shilingi bilioni 7.869 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 2.943 zilitengwa kwa ajili ya mishahara. Aidha, shilingi bilioni 1.950 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo shilingi bilioni 1.5 zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi milioni 450 ni fedha za nje. Hadi kufikia Februari, 2024, Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 6.883 sawa na 54% ya fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Fungu Na. 67 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; katika Mwaka huu wa Fedha 2023/2024, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 13.71. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 10.139 sawa na 74% zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi bilioni 8.393 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 1.746 zilitengwa kwa ajili ya mishahara. Aidha, shilingi bilioni 3.572 sawa na 26% zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2024, Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 7.528 sawa na 55% ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 6.11 sawa na 60.28% zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi bilioni 1.326 sawa na 21.71% ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 4.784 sawa na 78.29% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, shilingi bilioni 1.417 sawa na 39.67% zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Fungu Na. 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 8.624. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 8.324 sawa na 97% zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi bilioni 5.751 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 2.572 zilitengwa kwa ajili ya mishahara. Aidha, shilingi milioni 300 sawa na asilimia tatu zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2024, Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 5.366 sawa na 62.23%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Fungu Na. 04 – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 4.347. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 3.87 sawa na 90% zilitengwa kwa ajili ya

matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 2.575 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 1.322 zilitengwa kwa ajili ya mishahara. Aidha, shilingi milioni 450 sawa na 10% zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2024, Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 2.209 sawa na 50.8% ya fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo haya fedha ziliongezwa katika Fungu hili ambapo ilifikia jumla ya 112% na hizi ziliongezwa kwa ajili ya kugharamia Jengo la Utawala la Makao Makuu ya Idara ya Dodoma, kwa sababu, fungu hilo ndilo lilipokea jumla ya shilingi bilioni 4.851.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa sababu zilizopelekea Fungu hili kupata bajeti pungufu ya matarajio kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni matarajio ya ofisi hii kuwa na ajira mpya na upandishaji vyeo ambao hadi Februari, 2024 hawakupokea watumishi wapya wala watumishi waliopandishiwa vyeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba kwa ujumla, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 1.013 kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Hadi kufikia Februari, 2024, ofisi hii ilipokea jumla ya shilingi bilioni 696.984 sawa na 68.78% ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Taasisi mbili kati ya saba za ofisi hii ndiyo iliyofanikiwa kupata kiasi cha fedha ambacho kinaendana na uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa 66.6% hadi kufikia Februari, 2024. Ofisi hii ingeweza kukusanya maduhuli kupitia taasisi zinazofanya biashara kama vile Wakala wa Ndege za Serikali anayekodisha ndege zake kwa Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Kamati ilielezwa kuwa sababu zilizopelekea taasisi chini ya ofisi hii kuonekana kuwa zimepokea bajeti pungufu ya matarajio kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni Watumishi walipaswa kuajiriwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kutoajiriwa wote na Watumishi kuhamia kwenye taasisi zingine. Aidha, upungufu wa bajeti kwenye miradi ya maendeleo umesababishwa na ucheleweshaji wa kuanza kwa miradi hususani miradi inayotekelezwa kwa fedha za ndani, hivyo kupelekea ucheleweshaji wa kupata hati za malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ujumla si wa kuridhisha. Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kwamba fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya ofisi hii zinapatikana kabla ya kwisha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kama inavyooneshwa katika jedwali Na. 1 na jedwali Na. 2 katika taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa mipango na majukumu ya Ofisi ya Rais. Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, ililenga kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na taasisi zilizopo chini ya Ofisi hiyo. Ili kuliwezesha Bunge kujiridhisha na mwenendo wa matumizi yanayoakisi madhumuni ya kuidhinishwa kwa bajeti hiyo, Kamati ilichambua utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara hii. Uchambuzi huo umebaini mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Fungu Na. 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, hadi kufikia Februari, 2024, bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Fungu hili pamoja na mambo mengine imewezesha utekelezaji wa mambo yafuatayo:-

(a) Usimamizi wa utekelezaji wa ikama na bajeti ya mishahara kwa waajiri 433 wanaotumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara umefanyika ambapo kiasi cha shilingi trilioni 4.534 kimetumika kulipa mishahara na posho mbalimbali za kimshahara kwa watumishi wa umma wa kada mbalimbali;

(b) Madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma 26,331 yenye jumla ya shilingi bilioni 39.055 kutoka wizara, idara zinazojitegemea, wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, mashirika na taasisi za umma yamehakikiwa na kulipwa kwa watumishi stahiki;

(c) Madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma waliokoma utumishi wao kwa sababu mbalimbali kutoka katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Taasisi mbalimbali za Umma yamehakikiwa na kuidhinishwa, ambapo jumla ya madai ya watumishi 1,664 yenye jumla ya shilingi bilioni 6.074 yamelipwa;

(d) Miundo na mgawanyo wa majukumu wa taasisi za umma 80 kati ya 120 imepitiwa na kuhuishwa ili kuziwezesha taasisi hizo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

(e) Mfumo wa Tathmini ya Watumishi wa Umma *(HR Assessment Sytem)* umejengwa ili kufanya uchambuzi wa mahitaji ya watumishi, ambapo kuanzia Novemba 2023 hadi Februari, 2024, mfumo huo umetumika kufanya uchambuzi wa mahitaji ya watumishi kwa taasisi za umma 571; na

(f) Taasisi za umma 570 zimejengewa uwezo na kuwezeshwa kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma *(PEPMIS & PIPMIS)* ambapo watumishi wa umma 587,656 kati ya 603,699 ambao ni sawa na 97.3% wamesajiliwa katika mfumo wa Huduma Binafsi kwa Mtumishi *(Employment Self Service)* kwa ajili ya kuwawezesha kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma *(PEPMIS na PIPMIS)*. Aidha, jumla ya watumishi wa umma 560,652 kati ya 603,699 ambao ni sawa na 92.9% wameweka mipango ya utendaji kazi katika mfumo wa *PEPMIS* na *PIPMIS* inayojumuisha majukumu yanayotekelezwa na watumishi katika taasisi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Fungu Na. 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, hadi kufikia Februari, 2024 bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Fungu hili pamoja na mambo mengine imewezesha usikilizwaji wa malalamiko 164 ya maadili kutoka kwenye kanda tisa. Kati ya malalamiko yaliyopokelewa, malalamiko 113 yalihusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili na malalamiko 51 hayakuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Aidha, malalamiko 17 uchunguzi umekamilika na malalamiko 96 uchunguzi

wake unaendelea. Malalamiko yaliyosalia yalitolewa ushauri. Malalamiko 51 yasiyohusu Sheria za Maadili yamepelekwa katika mamlaka au taasisi husika zikijumuisha; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Polisi, Halmashauri, Mabaraza ya Ardhi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Fungu Na. 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; hadi kufikia Februari, 2024 bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa fungu hili pamoja na mambo mengine imewezesha utekelezaji wa mambo yafuatayo:-

(a) Usikilizaji wa rufaa za migogoro ya kiutumishi 482 kati ya rufaa 580 zilizopokelewa sawa na 83.1% ziliamuliwa na Tume. Rufaa 41 zinaendelea kuchambuliwa na rufaa 57 vielelezo vyake vinafuatiliwa kutoka mamlaka husika;

(b) Malalamiko 236 sawa na 77.9% ya malalamiko 303 yaliyokuwepo yaliamuliwa na Tume. Uchambuzi wa malalamiko 14 unaendelea na malalamiko 53 vielelezo vyake bado vinafuatiliwa kutoka mamlaka husika; na

(c) Kukamilika kwa ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria katika taasisi 180 kwenye utumishi wa umma ambao ulihusisha taasisi za Serikali Kuu 51, Mamlaka za Serikali za Mitaa 51 na taasisi za umma 78.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa bajeti umezingatia mipango na majukumu yaliyoombewa fedha. Aidha, ofisi hii ilitumia fedha zinazopatikana kusimamia na kuimarisha misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, Kamati inampongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa usimamizi madhubuti wa utawala bora. Ni maoni ya Kamati kuwa usimamizi na uratibu wa shughuli za utumishi wa umma umeimarika sana katika misingi ya haki, uwajibikaji na utawala bora, hali ambayo imeendelea kuipandisha nchi yetu katika medani za utawala bora Afrika na duniani kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Ofisi hii imetengewa jumla ya shilingi bilioni 200.452 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 181.992 ziliidhinishwa kwa Fungu Na. 30 - Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri; shilingi bilioni 12.187 ziliidhinishwa kwa Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; shilingi bilioni 1.950 ziliidhinishwa kwa Fungu Na. 33 - Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; shilingi bilioni 3.572 ziliidhinishwa kwa Fungu Na. 67 - Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; shilingi milioni 300 ziliidhinishwa kwa Fungu 94 - Tume ya Utumishi wa Umma; na shilingi bilioni 450 ziliidhinishwa kwa Fungu Na. 04 - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitembelea miradi tisa inayosimamiwa na Wizara na kuchambua utekelezaji wa miradi hiyo kama inavyoonekana kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzingatiaji wa ushauri wa Kamati. Wakati wa kupitia na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati ilitoa maoni na ushauri katika maeneo 15. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; Kanuni za Kudumu za Bunge zimetambua umuhimu wa uzoefu unaopatikana katika mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge. Kamati imezingatia umuhimu huo na masharti ya Kanuni za Bunge kwa kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa matumizi ya kawaida; katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 922.755 ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 42.597

ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 880.162 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya matumizi ya kawaida katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, imeongezeka kwa 13.52% ikilinganishwa na mwaka wa fedha unaoisha ambapo bajeti ya matumizi ya kawaida ilikuwa shilingi bilioni 812.843. Kamati imebaini kwamba moja kati ya sababu za ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri; na ili kuhakikisha zinatumika ipasavyo Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya Kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa sheria. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali Na. 3 katika taarifa yetu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa miradi ya maendeleo; katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 178.313 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 125.016 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 53.297 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepungua kwa shilingi 22,138,512,000/= sawa na 11% ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana katika jedwali namba nne. Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na ushauri wa Kamati, baada ya maelezo hayo, naomba kukamilisha uchambuzi kwa kubainisha Maoni ya Kamati yanayojenga mtazamo ambao ni msingi wa Ushauri wa Kamati, maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ihakikishe upatikanaji wa kiasi chote cha fedha ya bajeti kama iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii ili kutekeleza mipango iliyokusudiwa kwa mwaka wa fedha unaoisha; na

(b) Kamati inaendelea kuishauri Serikali iharakishe mchakato wa uhamishaji wa ndege zilizokodishwa kwa Shirika la Ndege *(ATCL)* kutoka kwa Wakala wa Ndege za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wa Kamati. kwa Maoni niliyobainisha kutokana na uchambuzi, naomba kutoa ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

(a) Serikali kupitia mfumo wa kielektroniki *(Human Resource Assessment)* ihakikishe inafanya tathmini mahitaji ya Watumishi kwenye Taasisi za Umma ili kubaini taasisi zenye ziada ya Watumishi na zile zenye Upungufu wa Watumishi ili kuweka uwiano wa Watumishi;

(b) Serikali iboreshe mfumo wa mtandao ikiwa ni pamoja na ugawaji wa vitendea kazi kama vile kompyuta ama vishkwambi kwa watumishi hususani kwenye maeneo ya vijijini ili kuwezesha utekelezaji fanisi wa ujazaji wa taarifa za kazi kwenye mfumo wa usimamizi wa utendaji kazi katika utumishi wa umma *(PEPMIS & PIPMIS);*

(c) Serikali ihamishe umiliki wa ndege zilizokodishwa kwa Kampuni ya Ndege Tanzania, kutoka kwa Wakala wa Ndege za Serikali kwenda kwa Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL);*

(d) Serikali ihakikishe kuwa fedha inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya ofisi hii na taasisi zake inapatikana ipasavyo ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa;

(e) Serikali iendelee kuimarisha misingi ya Utawala Bora pamoja na kuboresha mifumo ya utendaji kazi katika Utumishi wa Umma sambamba na kuboresha mishahara na maslahi ya Watumishi;

(f) Serikali iendelee kusimamia na kutoa mafunzo maalum ya mara kwa mara kwa Watumishi wa Umma ili kuwezesha utendaji kazi unaozingatia weledi na ustadi mkubwa; na

(g) Tume ya Utumishi wa Umma iweke muda maalum *(Speed truck)* ya usikilizaji na utatuzi wa Rufaa za Watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika, wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Mahususi naomba nimpongeze Dkt. Joseph Kizito Muhagama, Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Utawala, Katiba na Sheria na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika kwa kuchaguliwa kuwa Wenyeviti wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; na Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa jinsi wanavyoendelea kutoa ushirikiano mkubwa na ambao umesababisha Kamati kufanikisha utendaji kazi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi, Dkt. Moses Kusiluka; Makatibu Wakuu wa Ofisi hizo Ndugu Juma Selemani Mkomi, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ndugu Majula Mahendeka, Katibu Mkuu Ikulu; na Ndugu Exavery Daud, Naibu Katibu Mkuu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Wakuu Wote wa Taasisi ndani ya Wizara hii kama walivyotambulishwa na Kiti chako.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, kipekee nawashukuru sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kuhusu Utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja

na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kufuatilia taarifa hii ipasavyo, naomba kutambulisha sehemu nne za Taarifa hii ambazo ni:-

(a) Sehemu ya **Kwanza** inahusu maelezo ya jumla, inabainisha msingi na muundo wa Taarifa hii;

(b) Sehemu ya **Pili** inahusu uchambuzi wa Utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia mwenendo wa upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati;

(c) Sehemu ya **Tatu** inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati;

(d) Sehemu ya **Nne** ni Hitimisho.

### 1.2 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge. Kifungu cha 6 (2) (a) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu saba (7) ambayo ni:-

(a) **Fungu 20**: Ofisi ya Rais, Ikulu;

(b) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;

(c) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;

(d) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(e) **Fungu 67:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

(f) **Fungu 94:** Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; na

(g) **Fungu 04:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwa msingi huo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, Taarifa hii imejielekeza kwenye maeneo yafuatayo:-

(a) Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(b) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(c) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge; na

(d) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

## 2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ilizingatia Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kazi hiyo ilifanyika tarehe 22 na 23 Machi, 2024. Uchambuzi huo umejikita kwenye kulinganisha uwiano wa fedha zilizoidhinishwa, fedha zilizopokelewa pamoja na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo: -

### 2.2.1 Fungu Na. 20 na Fungu Na. 30 – OFISI YA RAIS (IKULU) NA SEKRETARIETI YA BARAZA LA MAWAZIRI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 **Fungu Na. 20** - Ofisi ya Rais (Ikulu) iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 32,157,384,000/=** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2023/24. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Sh. 9,318,876,000/=** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) ya Watumishi na **Sh. 22,838,508,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Februari 2024, Fungu 20 lilipokea jumla ya **Sh. 21,502,957,031.4/=** kwa ajili ya **matumizi ya kawaida sawa na asilimia 58.47 ya kiasi** kilichoidhinishwa ambapo **Sh. 5,715,798,500/=** sawa na asilimia **61.34** ni kwa ajili ya mishahara na **Sh. 15,787,158,531.4/=** sawa na asilimia **69.13** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, fedha zilizopokelewa zimetuumika kwa asilimia **100**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Fungu 30 - Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 860,186,476,000/=**. Kati ya fedha hizo **Sh. 678,193,941,000/=** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 674,342,692,500/= zilitengwa** kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **Sh. 3,851,248,500/=** zilitengwa kwa ajili ya mishahara (PE). Aidha, **Sh. 181,992,535,000/=** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo **Sh. 80,598,000,000/=** ni fedha za ndani na **Sh. 101,394,535,000/=** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2024 Fungu hili lilipokea Jumla ya **Sh. 608,297,732,792.14/=** sawa na **asilimia 70.7** ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **Sh. 490,375,635,583.92/=** sawa na **asilimia 72.12** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. 117,922,097,208.22/=** sawa na **asilimia 64.80** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo Sh. **47,156,037,955.35/=** sawa na **asilimia 58.5** ni fedha za ndani na **Sh. 70,766,059,252.87/=** sawa na **asilimia 69.8** ni fedha za nje.

**2.2.2 Fungu Na. 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 81,504,915,000/=**. Kati ya fedha hizo **Sh. 69,317,460,000/=** zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo **Sh. 25,141,968,000/=** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 31,988,037,000.04/=** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Aidha **Sh. 12,187,455,000/=** zilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Sh. 12,070,200,000/=** ni fedha za ndani na **Sh. 117,255,000/=** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2024 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 42,553,500,154.77/=** sawa na **asilimia 52.2** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **Sh. 38,460,966,577.56/=** sawa na **asilimia 67.32** zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo **Sh. 22,257,174,244.60/=** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Sh. 16,203,792,332.96/=** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara (PE). Aidha, **Sh. 4,092,533,577.21/=** sawa na **asilimia 33.58** fedha za ndani zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**2.2.3 Fungu Na. 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 12,763,016,000**/= kati ya fedha hizo **Sh. 10,813,016,000/=** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 7,869,966,000/=** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Sh. 2,943,050,000/=** zilitengwa kwa ajili ya mishahara (PE). Aidha, **Sh. 1,950,000,000/=** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo **Sh. 1,500,000,000/=** ni fedha za ndani na **Sh. 450,000,000/=** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2024 Fungu hili lilipokea Jumla ya **Sh. 6,883,525,814.71/=** sawa na **asilimia 54** ya fedha iliyoidhinishwa, kati ya fedha hizo **Sh. 6,716,566,814.71/=** sawa na **asilimia 52.62** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 4,934,682,233.2/=** sawa na **asilimia 62.7** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Sh. 1,781,884,581.51/=** sawa na **asilimia 60.54** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara (PE). Aidha, **Sh. 166,959,000/=** sawa na **asilimia 8.56** fedha za nje zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**2.2.4 Fungu Na. 67 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 13,711,815,000/=** kati ya fedha hizo **Sh. 10,139,298,000/=** sawa na **asilimia 74** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 8,393,156,000/=** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Sh. 1,746,142,000/=** zilitengwa kwa ajili ya Mishahara (PE). Aidha, **Sh. 3,572,517,000/=** sawa na **asilimia 26** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2024 Fungu hili lilipokea Jumla ya **Sh. 7,528,580,298.5/=** sawa na **asilimia 55** ya fedha iliyoidhinishwa, kati ya fedha hizo **Sh. 6,111,525,227.86/=** sawa na **asilimia 60.28** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 1,326,787,850.24/=** sawa na **asilimia 21.71** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 4,784,737,377.62/=** sawa na **asilimia 78.29** ni kwa ajili ya

matumizi ya Kawaida (OC). Aidha, **Sh. 1,417,055,070.64/=** sawa na **asilimia 39.67** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

### 2.2.5 Fungu Na. 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 8,624,091,000/=** kati ya fedha hizo **Sh. 8,324,091,000/=** sawa na **asilimia 97** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 5,751,455,000/=** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **Sh. 2,572,636,000/=** zilitengwa kwa ajili ya mishahara (PE). Aidha, **Sh. 300,000,000** sawa na **asilimia 3** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2024 Fungu hili lilipokea Jumla ya **Sh. 5,366,919,773.53/=** sawa na **asilimia 62.23** ya fedha iliyoidhinishwa, kati ya fedha hizo **Sh. 5,066,919,773.53/=** sawa na **asilimia 60.87** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 1,470,592,534.38/=** sawa na **asilimia 57.2** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 3,596,327,239.15/=** sawa na **asilimia 62.5** ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida (OC). Aidha, **Sh. 300,000,000/=** sawa na **asilimia 100** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

### 2.2.6 Fungu Na. 04 – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh.4,347,811,000/=**. Kati ya fedha hizo **Sh. 3,897,811,000/=** sawa na **asilimia 90** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 2,575,000,000/=** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **Sh. 1,322,811,000/=** zilitengwa kwa ajili ya Mishahara (PE). Aidha, **Sh. 450,000,000/=** sawa na **asilimia 10** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2024 Fungu hili lilipokea Jumla ya **Sh. 2,209,478,359.9/=** sawa na **asilimia 50.8** ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **Sh. 2,035,594,923.9/=** sawa na **asilimia 52.22** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 890,170,574/=** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 1,145,425,349.96/=** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 173,883,436/=** sawa na **asilimia 39** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, Fungu hili lilioongezewa kiasi cha **Sh.**

**2,641,856,907.66/=** fedha za ndani nje ya bajeti iliyoiidhinishwa kutoka Wizara ya Fedha kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa Jengoo la Utawala la Makao Makuu ya Idara – Dodoma. Kwa sababu hiyo Fungu hili lilipokkea Jumla ya **Sh. 4,851,335,267.56/=** sawa na **asilimia 112** ya fedha zilizoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa sababu zilizopelekea Fungu hili kupata bajeti pungufu ya matarajio kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni matarajio ya ofisi hii kuwa na ajira mpya na upandishaji vyeo ambao hadi Februari, 2024 hawakupokea Watumishi wapya wala Watumishi waliopandishiwa vyeo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba:

(a) kwa ujumla, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliidhinishiwa **Sh. 1,013,295,508,000/=** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, hadi kufikia Februari, 2024 Ofisi hii ilipokea Jumla ya **Sh. 696,984,551,132.61/=** sawa na **asilimia 68.78** ya bajeti iliyo idhinishiwa na Bunge.

(b) Taasisi moja mbili kati ya saba za Ofisi hii ndiyo iliyofanikiwa kupata kiasi cha fedha ambacho kinaendana na uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa **asilimia 66.6** hadi kufikia Februari, 2024.

(c) Ofisi hii ingeweza kukusanya Maduhuli kupitia taasisi zinazofanya biashara kama vile Wakala wa Ndege za Serikali anaekodisha ndege zake kwa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL).

(d) Kwa ujumla Kamati ilielezwa kuwa sababu zilizopelekea kuwa Taasisi chini ya Ofisi hii kuonekana kuwa zimepokea bajeti pungufu ya matarajio kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni Watumishi walipaswa kuajiriwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kutoajiriwa wote na Watumishi kuhamia kwenye taasisi zingine. Aidha, upungufu wa bajeti kwenye miradi ya maendeleo umesababishwa na ucheleweshaji wa kuanza kwa miradi hususani miradi inayotekelezwa kwa feedha za ndani hivyo kupelekea ucheleweshaji wa kupata hati za malipo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ujumla si wa kuridhisha.

Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kwamba fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Ofisi hii zinapatikana kabla ya kuisha kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 1** na **Jedwali Na. 2**

**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2023/2024**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2023/2024 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 20** – Ofisi ya Rais (Ikulu) | 32,157,384,000/= | 21,502,957,031.40/= | 58.47 |
| **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri | 678,193,941,000/= | 490,375,635,583.92/= | 72.12 |
| **Fungu 32** – Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | 69,317,460,000/= | 38,460,966,577.56/= | 67.32 |
| **Fungu 33** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 10,813,016,000/= | 6,716,566,814.71/= | 52.62 |
| **Fungu 67** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma | 10,139,298,000/= | 6,111,525,227.86/= | 60.28 |
| **Fungu 94** – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma | 8,324,091,000/= | 5,066,919,773.53/= | 60.87 |
| **Fungu 04** – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 3,897,811,000/= | 2,035,594,923.9/= | 52.22 |
| **JUMLA KUU** | **812,843,001,000/=** | **570,270,165,932.88/=** | **70.15** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, 2024.*

**Jedwali Na. 2: Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2023/2024**

| FUNGU | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2023/2024 | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2024 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri | 181,992,535,000/= | 117,922,097,208.22/= | 64.8 |
| **Fungu 32** – Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | 12,187,455,000/= | 4,092,533,577.21/= | 33.58 |
| **Fungu 33** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 1,950,000,000/= | 166,959,000/= | 8.56 |
| **Fungu 67** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma | 3,572,517,000/= | 1,417,055,070.64/= | 39.67 |
| **Fungu 94** – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma | 300,000,000/= | 300,000,000/= | 100 |
| **Fungu 04** – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 450,000,000/= | 2,815,740,343.66 | 625.72 |
| **JUMLA KUU** | **200,452,507,000/=** | **126,714,385,199.73/=** | **63.21** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, 2024.*

## 2.3 Utekelezaji wa Mipango na Majukumu ya Ofisi ya Rais

**Mheshimiwa Spika**, bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ililenga kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu ya Ofisi ya Rais, Menjimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na taasisi zilizopo chini ya Ofisi hiyo. Ili kuliwezesha Bunge kujiridhisha na mwenendo wa Matumizi unayoakisi madhumuni ya kuidhinishwa kwa bajeti hiyo, Kamati ilichambua utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi huo umebaini mambo yafuatayo:

**2.3.1 Fungu Na. 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.**

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Februari, 2024 Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Fungu hili pamoja na mambo mengine imewezesha utekelezaji wa mambo yafuatayo:

(a) Usimamizi wa utekelezaji wa Ikama na Bajeti ya Mishahara kwa Waajiri 433 wanaotumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara umefanyika ambapo kiasi cha **Sh. 4,534,427,452,604.79**/= kimetumika kulipa mishahara na posho mbalimbali za kimshahara kwa Watumishi wa Umma wa kada mbalimbali;

(b) Madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma **26,331** yenye jumla ya **Sh. 39,055,480,683.58/=** kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika na Taasisi za Umma yamehakikiwa na kulipwa kwa watumishi stahiki;

(c) Madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma waliokoma utumishi wao kwa sababu mbalimbali kutoka katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Taasisi mbalimbali za umma yamehakikiwa na kuidhinishwa, ambapo jumla ya madai ya watumishi **1,664** yenye jumla ya **Sh. 6,074,166,982.99**/= yamelipwa;

(d) Miundo na Mgawanyo wa Majukumu wa Taasisi za Umma 80 kati ya 120 imepitiwa na kuhuishwa ili kuziwezesha taasisi hizo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi;

(e) Mfumo wa Tathmini ya Watumishi wa Umma (*HR Assessment Sytem*) umejengwa ili kufanya uchambuzi wa Mahitaji ya watumishi, ambapo kuanzia Novemba 2023 hadi Februari 2024, mfumo huo umetumika kufanya **uchambuzi wa mahitaji ya watumishi kwa Taasisi za Umma 571**; na

(f) Taasisi za Umma 570 zimejengewa uwezo na kuwezeshwa kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma (PEPMIS & PIPMIS) ambapo Watumishi wa Umma **587,656** kati ya **603,699** ambao ni sawa na **asilimia 97.3** wamesajiliwa katika mfumo wa Huduma Binafsi kwa Mtumishi (*Employment Self Service*)

kwa ajili ya kuwawezesha kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma (PEPMIS na PIPMIS). Aidha, jumla ya Watumishi wa Umma **560,652** kati ya **603,699** ambao ni sawa na **asilimia 92.9** wameweka Mipango ya Utendaji Kazi katika mfumo wa PEPMIS/PIPMIS inayojumuisha majukumu yanayotekelezwa na watumishi katika taasisi husika.

**2.3.2 Fungu Na. 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.**

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Februari, 2024 Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Fungu hili pamoja na mambo mengine imewezesha usikilizawaji wa malalamiko 164 ya maadili kutoka kwenye Kanda tisa (9). kati ya malalamiko yaliyopokelewa, malalamiko 113 yalihusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili na malalamiko 51 hayakuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Aidha, malalamiko 17 uchunguzi umekamilika na malalamiko 96 uchunguzi wake unaendelea. Malalamiko yaliyosalia yalitolewa ushauri. Malalamiko 51 yasiyohusu Sheria ya Maadili yamepelekwa katika Mamlaka au Taasisi husika zikijumuisha; Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Polisi, Halmashauri, Mabaraza ya Ardhi na kadhalika.

**2.3.3 Fungu Na. 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma**

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia Februari, 2024 Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Fungu hili pamoja na mambo mengine imewezesha utekelezaji wa mambo yafuatayo:

(a) Usikilizaji wa Rufaa za migogoro ya Kiutumishi **482** kati ya Rufaa **580** zilizopokelewa sawa na **asilimia 83.1** ziliamuliwa na Tume. Rufaa 41 zinaendelea kuchambuliwa na rufaa 57 vielelezo vyake vinafuatiliwa kutoka Mamlaka husika;

(b) Malalamiko 236 sawa na asilimia 77.9 ya malalamiko 303 yaliyokuwepo yaliamuliwa na Tume. Uchambuzi wa malalamiko 14 unaendelea na malalamiko 53 vielelezo vyake bado vinafuatiliwa kutoka Mamlaka husika; na

(c) Kukamilika kwa ukaguzi wa Uzingatiaji wa Sheria katika Taasisi 180 kwenye Utumishi wa Umma ambao ulihusisha Taasisi za Serikali Kuu 51, Mamlaka za Serikali za Mitaa 51 na Taasisi za Umma 78.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa bajeti umezingatia mipango na majukumu yaliyoombewa fedha. Aidha, Ofisi hii ilitumia fedha zilizopatikana kusimamia na kuimarisha misingi ya Utawala Bora.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hiyo, Kamati inampongeza kwa dhati **Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu** kwa usimamizi madhubuti wa Utawala Bora. Ni maoni ya Kamati kuwa, usimamizi na uratibu wa shughuli za Utumishi wa Umma umeimarika sana katika misingi ya haki, uwajibikaji na utawala Bora, hali ambayo imeendelea kuipandisha nchi yetu katika medani za utawala Bora Afrika na Duniani kote.

### 2.4 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi hii ilitengewa jumla ya **Sh. 200,452,507,000/=** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **Sh. 181,992,535,000/=** ziliidhinishwa kwa **Fungo 30** Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, **Sh. 12,187,455,000/=** ziliidhinishwa kwa **Fungu 32** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawaala Bora, **Sh. 1,950,000,000/=** ziliidhinishwa kwa **Fungo 33** Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, **Sh. 3,572,517,000/=** ziliidhinishwa kwa **Fungo 67** Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma, **Sh. 300,000,000** ziliidhinishwa kwa **Fungo 94** Tume ya Utumishi wa Umma na **Sh. 450,000,000/=** ziliidhinishwa kwa **Fungo 04** Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa,

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea miradi tisa inayosimamiwa na Wizara na kuchambua utekelezaji wa miradi hiyo kama ifuatavyo:-

#### 2.4.1 Mradi Na. 6203: Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya TAKUKURU

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa gharama za mradi huu ni **Sh. 1,607,989,115/=** ambapo katika mwaka wa fedha 2022/2023 kiasi cha **Sh. 500,000,000/=** na **Sh. 1,107,989,115** zilitengwa katika mwaka wa fedha 2023/2024 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo ambao ni jengo la ghorofa moja (1).

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huo unatekelezwa na Mkandarasi *Prison Corporation Sole* ambalo ni Shirika la Jeshi la Magereza. Mradi

unatekelezwa katika Kata ya Gangilonga, Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Mkoa wa Iringa.

Hadi kufikia Februari, 2024 ameshalipwa jumla ya **Sh. 239,356,728.1** sawa na **asilimia 15** ya gharama ya mradi, Kamati ilielezwa kuwa hakuna madai yoyote ya Mkandarasi yaliyowasilishwa kwa Mshitiri. Aidha, Utekelezaji wa Ujenzi wa mradi huo mpaka wakati Kamati imetembelea uwandani umefikia **asilimia 30**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliridhishwa na uwezo mkubwa wa Mkandarasi katika utekelezaji wa mradi huo, kwa ujumla Kamati inaipongeza Serikali kwa utekelezaji Mzuri wa Mradi huo.

**2.4.2 Mradi Na. 6220: Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

(a) ***Mradi wa Upandaji wa Miti ya Parachichi 231 Kwenye Ekari 3 ili Kunusuru Kaya Maskini-Katika Kijiji cha Ibumila, Wilaya ya Iringa.***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa gharama za mradi huu ni **Sh. 8,163,000/=** ambapo **Sh. 6,579,000/=** ni kwa ajili ya malipo ya ujira wa wanufaika 44 wanaofanya kazi kwenye mradi huo na **Sh. 1,584,000/=** ni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya mradi ikiwemo miche ya Parachichi 231. Mradi huo umekamilika kwa **asilimia 100** ukiwa umeshatumia kiasi chote cha fedha kama ilivyoidhinishwa. Mradi huo umewezesha walengwa kuongeza ujuzi na kipato kupitia ujira waliopokea kupitia mradi huo lakini pia mradi huo umekuwa shamba darasa kwa jamii inayozunguka eneo hilo ambao wengi wao ni wakulima. Aidha, kamati ilielezwa kuwa kufuatia kukamilika kwa mradi huo, mradi umekabidhiwa kwa serikali ya kijiji chini ya uangalizi wa Shule ya Msingi Ibumila.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya Kamati kukagua mradi huu na kufanya mkutano wa wazi na wanufaika wa TASAF, kamati ilipokea malalamiko ya baadhi ya wanufaiika kucheweleshewa malipo yao ya kazi. Kamati ilibaini kuwa changamoto hiyo inasababishwa na wanufaika hao kuwa na mahudhurio hafifu wakati wa utekelezaji wa mradi huo. Kwa ujumla, Kamati inawapongeza Wananchi wa Kijiji cha Ibumila na Serikali kwa ujumla kwa utekelezaji mzuri wa mradi huo.

(b) **Mradi wa Ujenzi wa Wodi ya Mama na Mtoto Katika Hospitali ya Mji Njombe (Kibena)**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ujenzi wa wodi ya Mama na Mtoto umekusuudia kuwasaidia Wamama wajawazito kujifungua katika mazingira mazuri na salama lakini pia kwa Wamama wanaojifungua Watoto njiti kupatiwa huduma bora wao pamoja na watoto kwenye Hospitali ya Kibena.

Kamati ilielezwa kuwa mradi ulitumia jumla ya **Sh. 169,325,000** ambapo mchango wa TASAF ni **Sh. 150,055,000/=** na **Sh. 19,270,000/=** ni mchango wa Wananchi pamoja na Wadau mbalimbali, hii ni kutokana na masharti ya mradi inayotaka Jamiii kuchangia asilimia 10 ya gharama za mradi kwa kutoa fedha au mahitaji yanayopatikana kwa urahisi katika eneo husika. Mradi huo umekamilika kwa **asilimia 100** na umekabidhiwa kwa Halmashauri ya Mji wa Njombe ukiwa umeshatumia kiasi chote cha fedha kama ilivyoidhinishwa. Mradi umekabidhiwa kwa serikali ya kijiji chini ya uangalizi wa Shule ya Msingi Ibumila.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inawapongeza Wananchi wa Mji ya Njombe na Serikali kwa ujumla kwa utekelezaji mzuri wa mradi huo.

(c) **Mradi wa Ujenzi wa Stendi ya Mabasi Kijiji cha Lundusi Kata ya Peramiho Katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea na Ujenzi wa Soko, Vyoo na Vizimba Kijiji cha Lituta Halmashauri ya Wilaya ya Madaba.**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Ujenzi wa Stendi ya Mabasi kijiji cha Lundusi ni mradi unaohusisha ujenzi wa Stendi, Maduka thelathini na sita (36), Jengo la Utawala, Vibanda viwili vya walinzi, Vyoo nane (8) na Uzio wa Stendi Jengo la Utawala. Kamati ilielezwa kuwa mradi huo una gharama ya **Sh. 434,657,802.68/=** ambao hadi kufikia Februari, 2024 mradi umeshatumia gharama ya **Sh. 277,728,381/=** sawa na asilimia 64 ya gharama za mradi. Aidha, mradi huo umefikia asilimia 50 ya ujenzi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia, ilitembelea mradi wa Ujenzi wa Soko, vyoo na vizimba unaotekelezwa katika Kijiji cha Lituta Halmashauri ya Wilaya ya Madaba wenye gharama ya **Sh. 171,176,339.29/=** ambao umefika **asilimia 70** ya ujenzi wa mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Kukamilika kwa miradi hiyo kutaleta tija kubwa kwa wakazi wa Lundusi, Lituta na Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla wake. Kamati inaipongeza Serikali kwa ujumla kwa utekelezaji mzuri wa miradi hiyo.

### 2.4.3 Mradi Na 6286: Ukarabati wa Jengo la Ofisi na Ghala Kuu la Nyaraka za Taifa

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa gharama za mradi huu ni **Sh. 450,000,000/=** ambapo **Sh. 150,000,000/=** ni kwa ajili ya kazi ya kuimarisha uhifadhi wa nyaraka katika teknolojia ya kisasa kwa kuingiza nyaraka katika mfumo wa kidigitali ujulikanao kama *Digitall Records Management and Preservation* System, **Sh. 23,883,436/=** ni kwa ajili ya gharama za ukarabati wa mashine za kudurufu nyaraka (*archival* scanners) na **Sh. 228,767,387/=** ni kwa ajili ya malipo ya malipo ya mwisho ya Mkandarasi (NHC) na Mshauri mwelekezi (ABECC) kwa ajii ya kazi ya ukarabati wa miundombinu ya nje ya jingo la Ofisi na Ghala Kuu la Nyaraka, Kanda Mashariki – Dar es salaam.

**Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Februari, 2024 idara ilipokea na kutumia jumla ya kiasi cha **Sh. 173,883,436/=** sawa na asilimia **38.64.** Kamati inaipongeza Serikali kwa utekelezaji mzuri wa mradi huo.

### 2.5 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri katika maeneo Kumi na Tano (15). Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa.

### 2.6 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni za Kudumu za Bunge zimetambua umuhimu wa uzoefu unaopatikana katika mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 117 (2) ya

Kanuni za Bunge. Kamati imezingatia umuhimu huo na masharti ya Kanuni za Bunge kwa kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kama ifuatavyo: -

### 2.6.1 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 922,755,472,000/=** Ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 42,592,485,000/=** ni kwa ajili ya Mishahara (PE), na **Sh. 880,162,117,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa **asilimia 13.52** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo bajeti ya Matumizi ya kawaida ilikuwa **Sh. 812,843,001,000/=** Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma.

Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri na ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Sheria. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 3**

**Jedwali Na. 3: Mchanganuo wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida 2023/2024 na Uwiano wa Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida 2024/2025**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2023/2024 | MAKADIRIO YA FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | ASILIMIA YA ONGEZEKO/ UPUNGUFU (-) |
|---|---|---|---|
| **Fungu 20** – Ofisi ya Rais (Ikulu) | 32,157,384,000/= | 33,544,557,000/= | 4.31 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri | 678,193,941,000/= | 805,676,639,000/= | 18.79 |
| **Fungu 32** – Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | 69,317,460,000/= | 48,254,069,000/= | -30.38 |
| **Fungu 33** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 10,813,016,000/= | 11,642,650,000/= | 7.67 |
| **Fungu 67** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma | 10,139,298,000/= | 10,831,831,000/= | 6.83 |
| **Fungu 94** – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma | 8,324,091,000/= | 8,740,713,000/= | 5 |
| **Fungu 04** – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 3,897,811,000/= | 4,065,013,000/= | 4.28 |
| **JUMLA KUU** | **812,843,001,000/=** | **922,755,472,000/=** | **13.52** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, 2024.*

### 2.6.2 Uchambuzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Ofisi ya Rais – Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 178,313,995,000/=** kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh. 125,016,338/=** ni fedha za ndani, na **Sh. 53,297,657,000/=** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepungua kwa **Sh. 22,138,512,000/=** sawa na **asilimia 11** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 4**

**Jedwali Na. 4: Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2024/2025**

| FUNGU | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | |
|---|---|---|
| | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE |
| **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri | 110,439,177,000/= | 53,169,907,000/= |
| **Fungu 32** – Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | 9,933,174,000/= | 127,750,000/= |
| **Fungu 33** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 1,500,000,000/= | - |
| **Fungu 67** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma | 2,348,047,000/= | - |
| **Fungu 94** – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma | 500,176,000/= | - |
| **Fungu 04** – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 295,764,000/= | - |
| **JUMLA KUU** | **178,313,995,000/=** | |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, 2024.*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maoni

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naomba kukamilisha uchambuzi kwa kubainisha Maoni ya Kamati yanayojenga mtazamo

ambao ni msingi wa Ushauri wa Kamati. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Serikali ihakikishe upatikanaji wa kiasi chote cha fedha ya bajeti kama iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii, ili kutekeleza mipango iliyokusudiwa kwa mwaka wa fedha unaoisha; na

(b) Kamati inaendelea kuishauri Serikali iharakishe mchakato wa uhamishaji wa Ndege zilizokodishwa kwa Shirika la Ndege (ATCL) kutoka kwa wakala wa ndege za Serikali;

### 3.2 Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kwa Maoni niliyobainisha kutokana na uchambuzi, naomba kutoa Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

(a) Serikali kupitia mfumo wa ki elektroniki (Human Resource Assessment) ihakikishe inafanya tathmini mahitaji ya Watumishi kwenye Taasisi za Umma ili kubaini taasisi zenye ziada ya Watumishi na zile zenye Upungufu wa Watumishi ili kuweka uwiano wa Watumishi;

(b) Serikali iboreshe mfumo wa mtandao ikiwa ni pamoja na ugawaji wa vitendea kazi kama vile kompyuta ama vishkwambi kwa Watumishi hususani kwenye maeneo ya vijijini ili kuwezesha utekelezaji fanisi wa ujazaji wa taarifa za kazi kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji kazi katika Utumishi wa Umma (PEPMIS & PIPMIS);

(c) Serikali ihamishe umiliki wa ndege zilizokodishwa kwa Kampuni ya Ndege Tanzania, kutoka kwa Wakala wa Ndege za Serikali kwenda kwa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL);

(d) Serikali ihakikishe kuwa fedha inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii na Taasisi zake inapatikana ipasavyo ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa;

(e) Serikali iendelee kuimarisha misingi ya Utawala Bora pamoja na Kuboresha mifumo ya utendaji kazi katika Utumishi wa Umma sambamba na kuboresha mishahara na maslahi ya Watumishi;

(f) Serikali iendelee kusimamia na kutoa mafunzo maalumu ya mara kwa mara kwa Watumishi wa Umma ili kuwezesha utendaji kazi unaozingatia weledi na ustadi mkubwa; na

(g) Tume ya Utumishi wa Umma iweke muda maalum (Speed truck) ya usikilizaji na utatuzi wa Rufaa za Watumishi.

**SEHEMU YA NNE**

## 4.0 HITIMISHO

**Maelezo ya Kuhitimisha**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb. – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb.
4. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb.
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.
7. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb.
8. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb.
9. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb.
10. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb.
11. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb.
12. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb.
13. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.
14. Mhe. Yahya Omary Massare, Mb.
15. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb.
16. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb.
17. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb.
18. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb.

19. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb.
20. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb.
21. Mhe. Aziza Seylum Ally, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb) Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano mkubwa ambao ameendelea kuipa Kamati pamoja na Naibu Waziri wake Mhe. Ridhiwani Kikwete.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Makatibu Wakuu wa Ofisi hiyo Ndg. Juma Selemani Mkomi Katibu Mkuu Ofisi ya Rais – Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Ndg Majula Mahendeka Katibu Mkuu Ikulu.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, kiupekee nawashukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**
**YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
19 Aprili, 2024

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ambao ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge:-

Tuna wageni 67 wa Mheshimiwa Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wakurugenzi na Maafisa Waandamizi, Wasaidizi wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, wanafunzi kutoka kaya walengwa wa *TASAF* wanaosoma elimu ya juu pamoja na maafisa wa *TASAF* karibuni. *(Makofi)*

Wageni waliotutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wageni 64 wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi, UVCCM, Tawi la Chuo cha Afya *City* kutoka Jiji la Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Waheshimiwa tunaanza sasa mjadala, mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Janejelly James, wa pili atakuwa ni Mheshimiwa Shangazi na wa tatu atakuwa Mheshimiwa Yahaya Omary Massare.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa wasaa huu, lakini nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa mchangiaji wa kwanza kwenye Wizara nyeti inayohusika na watumishi. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amedhihirisha yeye ni mwajiri namba moja kwa alivyoshughulika na masuala ya watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wote wao ndiyo wanatekeleza maono ya Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda kwenye nukuu aliyosema Mheshimiwa Waziri ya Mheshimiwa Rais akihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021 katika Bunge la Kumi na Mbili aliposema, nanukuu; "Tutawapima viongozi na watumishi wa umma kwa namna wanavyotimia majukumu yao, hatutawaonea aibu viongozi na watumishi wazembe, wezi na wabadhirifu wa mali za umma. Tutaendeleza pia juhudi za kupambana na rushwa kwenye utumishi wa umma. Wajibu wa watumishi wa umma ni lazima uendane na haki zao."

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nataka niongelee haki ya mtumishi wa umma katika mafunzo, maana mafunzo ndio kila kitu, mafunzo

ndio msingi, mafunzo ndiyo yatawafanya watumishi wetu watumike sawasawa ipasavyo. Kwa utumishi wetu wa umma kuna itifaki ya mafunzo ya hatua sita, mafunzo ya kwanza mtumishi huyapata anapoingia kazini inaitwa *induction entry course*. Mtumishi hapa atafundishwa nini maana ya Serikali, anaenda kufanya nini ndani ya Serikali, aitumikieje Serikali, atofautisheje na familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya mafunzo sasa hivi hayaendi ipasavyo, tukiajiri watumishi tunawakusanya wiki moja tunasema tumewapa *induction course,* hiyo haitoshi na ndiyo maana huu mwanya unafanya watumishi wa umma anaweza akashindwa kutofautisha ni mambo gani ya Kiserikali hayatakiwi kusemwa hadharani na ni mambo gani ya Kiserikali ambayo familia yake haitakiwi kuyajua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mafunzo namba mbili, haya huwa ni mafunzo ya awali, mafunzo elekezi ya msasa *orientation training,* hii nayo tumelegea. *Orientation training* ilikuwa mtumishi akiajiriwa hata kama zipo idara sita ndani ya taasisi atazungushwa kwenye zile idara ili azijue na lengo lake na yeye awe mmiliki sawasawa na kujua kila kitu kinachoendana na taasisi yake. Leo hii mtumishi anaweza akaajiriwa, akawekwa idara moja mpaka anastaafu, kwa hiyo huyu hawezi kujua taarifa zingine zinazoendelea ndani ya taasisi. Ukimuuliza habari za idara nyingine anaweza akashindwa kusimama na kuielezea taasisi yake ikoje, inafanya nini na kwa wakati gani. Niwaombe hilo twende tuliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na mafunzo namba tatu, mitihani ya umahiri na hii mitihani ya umahiri sana waliobaki wanaendana nayo ni Wizara ya Ulinzi. Sisi kwetu huku aidha ni bajeti au ni kitu gani hii mitihani ya umahiri haipo. Ili mtu aende kwenye na nafasi nyingine lazima afanye mitihani ya umahiri, lazima ajue nikienda kwenye *position* hii nyingine natakiwa nifanye nini. Hii imebaki kwa maafisa utumishi ndiyo naona wanafanya mitihani ya umahiri, lakini huku kwenye kada zingine mitihani ya umahiri kama imesahaulika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mafunzo namba nne, haya yalikuwa yanahusu misingi ya utumishi wa umma, hapa mtumishi ndiyo unafundishwa misingi ya utumishi wa umma, unatakiwa ufanye nini

ndani ya utumishi wa umma. Hapa unafundishwa hata kutoa rushwa na kupokea ni dhambi, hata unafundishwa kutoa siri za Serikali ni dhambi, lakini nani leo hii anayefundishwa hayo mafunzo ya misingi ya utumishi wa umma? Ndiyo maana si ajabu watu hamjamaliza kikao taarifa zote zipo nje kwa sababu misingi ile tumeisahau, msingi ya utumishi wa umma tumeisahau.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba tano, ilikuwa ni mafunzo ya viongozi wanaochipukia, watumishi wetu wakiwa ni Maafisa Wakuu wanaanza kupelekwa chuoni, mwanzoni ilikuwa ni *IDM* Mzumbe, lakini baadaye majukumu haya yakakabidhiwa Chuo cha Utumishi wa Umma, tusibaki kwenye kwamba viongozi wanazaliwa bali viongozi wanajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ndiyo Maafisa Wakuu walikuwa wanafundishwa namna ya kuwa kiongozi, namna ya kuwa mwadilifu, namna ya kuwa mvumilivu, namna ya kuwa msikivu na namna ya utendaji kazi. Tuna mifano, leo hii tunaona Mheshimiwa Rais wetu anabagazwa, anasemwa, anavumilia kwa sababu amepita *IDM* Mzumbe amefundishwa uvumilivu na ustahimilivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna Katibu Mkuu wetu wa Chama Cha Mapinduzi amepita *IDM* Mzumbe, aangalie *style* yake ya kusema hata kuikosoa Serikali, hata kuwaambia nyie Waheshimiwa Mawaziri anasema kwa staha kwa sababu amefundishwa kuwavumilia wenzake. Hiyo ndiyo ilikuwa kazi ya *IDM* Mzumbe, ndiyo ilikuwa kazi ya kufundisha viongozi wanaochipukia. Sasa wakishafundishwa hivyo ndiyo mle wanatolewa wateule, ndiyo anateuliwa mtu, anaenda akiwa ameshajengwa kwamba anaenda kufanya nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunaona watu wanateuliwa Wakurugenzi wetu, saa zingine wanakosea ni kwamba hawakupewa haya mafunzo, saa zingine wanakosea ni kwamba hawakutolewa kwenye kundi hili la maafisa wakuu, turudi nyuma, ya kale ni dhahabu, tukayafanyie kazi yatatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo namba sita ilikuwa hapa mstaafu anaandaliwa kustaafu, anafundishwa mafunzo ya kustaafu na alikuwa anafundishwa miaka mitano kabla ya kustaafu. Kulikuwa na Chuo kinaitwa *NIP- National Institute of Productivity,* ndiyo ilikuwa

kazi yake kufundisha wanaotaka kustaafu, wanamfundisha anaweza kufanya nini baada ya kustaafu na kama wewe utawaambia, nikistaafu nataka nifuge kuku, nifuge ng'ombe, niwe na biashara ya usafirishaji, wanakufundisha, wanakuandikia andiko, wao wenyewe unakopa sasa kwenye *pension*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unakopa *collateral* yako ni mshahara. Mpaka unamaliza miaka mitano umeshamaliza ule mkopo lakini wanaendelea kuangalia ule mradi wako ambao unaufanya. Leo hii ikifika miezi sita wamempa mtumishi barua ya miezi sita kwamba sasa jiandae utastaafu, ndiyo wananipeleka *course*. Sasa nikimaliza hapo wakinipa *pension* naenda kununua daladala linapinduka Mbezi, tayari nimekwisha, halafu tunasema maisha ya wastaafu yanakuwa magumu. Tunayafanya kuwa magumu sisi Serikali, tumesahau kuwaandaa hawa watu, hebu turudi tukaandae hawa watumishi wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anapohitimisha nitaomba anielezee hii hati iliyoanzisha Chuo cha Utumishi wa Umma kikaitwa *Public Service College,* mambo haya bado yapo, bado yanaendelea kufanyika kama hayapo kuna haja ya kuendelea kukiita Chuo cha Watumishi wa Umma? Leo hii ukienda pale unakuta imejaa *secretarial* na *record management,* ndiyo yalikuwa malengo, *record management* si ilikuwa Uhazili Tabora? Hiki chuo kilianzishwa kujenga watumishi, kuwajengea uwezo ambao wameshaajiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba wakati Waziri anahitimisha aniambie kama bado hiki chuo kinafanya kazi zake ipasavyo. Tunaweza tukawa tunalalamikia watumishi uadilifu umeshuka, wizi umekuwa mkubwa, amejengwa huyu mtu? Hebu turudi tukawajenge watumishi. Mheshimiwa Simbachawene amejengwa na ndiyo maana anaweza akapigwa mawe, ndiyo maana anaweza akasemwa, akavumilia kwa sababu amepita kwenye chuo amejengwa, Mheshimiwa Spika kajengwa, walikuwa wakifika mahali wanajengewa uwezo. Leo hii mtumishi gani anajengewa uwezo halafu tunawalaumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza tukawa tunavunja sisi wenyewe kwa mikono yetu wenyewe tunawavunja hawa watumishi halafu tunasema watumishi hawa hawafai, kizazi hiki kibovu, siyo

kibovu hakikujengewa uwezo. Turudi kwenye yale ya zamani tukayaangalie, tumepotea wapi na tulipopotea ni kila chuo kuacha malengo yake yaliyokianzisha tukaanza biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ukienda *IDM* Mzumbe siyo *IDM* Mzumbe ile ambayo Afisa Mkuu alikuwa akitoka *IDM* Mzumbe mnasema kweli huyu katoka *IDM* Mzumbe. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwishwa kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante kengele ya pili hiyo.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, niongezee dakika moja nimalizie nakuomba na hili ndiyo jimbo langu.

**NAIBU SPIKA:** Sasa utakuwa unachukua Mheshimiwa...

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba waende wakayafanye hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia Mheshimiwa Waziri leo ametambulisha viongozi wake pale, ina maana siku hizi hakuna wanawake wenye uwezo, nimeshangaa na nimeandika ki-*memo* lakini hakikufika kwake kwa sababu alishakuwa pale na kwa Mheshimiwa Ridhiwani hakikufika, aende nalo wakalifanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, vipi jamani kuna vita huko?

Mheshimiwa Shangazi jiandae Mheshimiwa Massare, jiandae Mheshimiwa Francis Mtinga.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi, nianze alipoishia Mheshimiwa Janejelly kwamba wanawake wanaweza na wapewe nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Rais ambaye ndiye Waziri kwenye Ofisi hii ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kipekee Waziri wa Nchi, Ofisi hii Mheshimiwa George Boniface Simbachawene pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete pamoja na Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara zote zinazounda Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwa kweli wanafanya kazi kubwa na kazi nzuri, kwa bahati mbaya hii ni Wizara ambayo mambo yake hayaonekani sana hadharani. Lakini itoshe tu kusema kila jema tunaloliona katika nchi hii linafanyika basi linatoka katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeanza mchango wangu katika Fungu 32 - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora. Mwaka 2014 wakati wa Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Mheshimiwa Jakaya Kikwete zilitangazwa ajira takribani 29,000 za walimu, lakini walimu wale wamekumbana na changamoto ya kutopanda madaraja kwa mtiririko vile ambavyo inapaswa kuwa. Kwa mfano mwaka 2014 wakati wanaajiriwa waliingia kama walimu wa daraja la 3A walipaswa kuthibitishwa mwaka 2015 na mwaka 2018 ilipaswa waanze kupanda daraja la kwanza ili waende daraja la 2A ambayo pia hata mshahara ungeongezeka lakini hilo halikufanyika. Baadaye wakapandishwa mwaka 2021, maana yake hapa kuna miaka miwili wamekopesha nguvu bure Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa mtiririko huo ilipofika mwaka 2022 walipaswa kupanda daraja kutoka daraja la 2A na kwenda daraja la 1A, lakini ukiona hapo ni takribani miaka 10 wamepanda ngazi moja moja. Kwa hiyo, tunadhani kwamba ni vizuri hili likatazamwa na tukaweza kuwasaidia kwa sababu kimsingi walipaswa kuwa wamepanda aidha mara mbili au mara tatu. Kwa hiyo, wanaona hiyo ni dhuluma kwamba Serikali yao inawadhulumu, lakini tunaamini Serikali hii siyo ya dhuluma bali inawezekana kuna jambo halikuangaliwa vizuri. Naomba litazamwe vizuri, waweze kurekebishiwa hizo taratibu zao ili waweze kupata stahiki kwa mujibu wa utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapongeza pia kazi nzuri ya upandishaji wa madaraja ambayo inaendelea. Sasa hivi tunashukuru kwamba, angalau malalamiko yamepungua sana, lakini tunaomba Maafisa Utumishi chini ya Wizara hii ambayo ndio inawasimamia, hilo

zoezi lifanyike kwa haki kwa sababu, bado kuna ambao wana zile kasumba za kibinadamu za kuendelea kushikilia ma-*file* ambapo hata hapastahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana eneo hili liweze kufanyiwa kazi maana lisipofanyiwa kazi, hili ndilo linaloenda kuathiri hata ile hatua ya mwisho ya mafao, kwa sababu, unakuta kuna mtumishi mwingine anapokwenda kuanza kudai mafao yake anagundua kwamba, kwa kucheleweshwa kupandishwa madaraja hata viwango vya mafao vilivyowekwa havilingani na hali ile ambayo anaikuta wakati wa kustaafu. Kwa hiyo, hili ni muhimu sana na lenyewe lifanyiwe kazi kwa wakati ili lisiathiri ile hatua ya mwisho ya kwenda kupata mafao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kulipa malimbikizo. Serikali inajitahidi sana katika eneo hili, lakini ni ukweli usiofichika kwamba, bado yako maeneo kuna malimbikizo ambayo hawajalipa. Tunaomba sana tuongeze kasi ya ulipaji wa malimbikizo ili tuwaongezee ari ya kufanya kazi. Miongoni mwa *motivation* katika utumishi wa umma ni pamoja na kulipa haya malimbikizo. Tunaamini hilo likifanyika litatusaidia sana kuongeza ufanisi wa watumishi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala zima la masuala ya nidhamu, hapa nazungumzia Tume ya Utumishi wa Umma. Tunafarijika kuona kwamba hata pesa tumeongeza na sisi pia, kama Kamati, juzi kuna mafungu tumeyaongeza hapa. Tunataka kesi zote ambazo zinasimamia malalamiko katika utumishi wa umma zifanyike kwa wakati. Haki yoyote ambayo inacheleweshwa ni haki ambayo inanyimwa. Kwa hiyo, tunaona kwamba, wako watumishi wanaanza kupata viharusi na wengine wanapata madhara mbalimbali ya afya ya akili kwa sababu, mashauri yao mbalimbali yaliyoko katika ngazi hii ya utumishi hayakufanyiwa kazi kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haipendezi sana kuona kwamba, kesi ya mtumishi inakaa zaidi ya miaka mitatu haijatafutiwa ufumbuzi. Kwa hiyo, tunaomba sana tuongeze kasi katika Tume hii ya Utumishi wa Umma na pia, tuongeze kasi katika kusikiliza mashauri na migogoro yote ya utumishi ili haki iweze kupatikana kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni kwa wale ambao wanakaimu. Bado tunaona kwamba, kuna ukiritimba mkubwa katika kutoa vibali kwa watu ambao wanakaimu ama kuwapandisha ama kuwathibitisha kwenye kazi. Kwa mujibu wa sheria mtu anatakiwa akaimu kwa muda usiozidi miezi sita, lakini bado tunaona kwamba, kuna maeneo ambayo watu wanakaimu kwa muda mrefu sana. Hapa nitatoa mfano na inabidi nimtaje tu huyo mtumishi kwa sababu, kinachofanyika siyo haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mtumishi anakaimu ukurugenzi katika Ofisi ya *TACAIDS* kwa muda wa miaka saba na ni mwanamke huyu, anaitwa Adrieli Njelekela, miaka saba anakaimu ukurugenzi. Sasa hapa kama hana uwezo anawezaje kukaimu kwa miaka saba? Maana yake ni kuna tatizo. Kama ni *vetting* miaka saba tunasubiri *vetting,* hiyo *vetting* ni ya kutoka mbinguni au ni hapa hapa duniani? Ndio maana wakati mwingine tunaonekana kwamba, labda nchi hii bado kuna mfumo dume ambao unawafanya wanawake wasiwe katika nafasi ambazo wanastahili kuwa nazo, kwa hiyo, naomba hili litazamwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu *Watumishi Housing.*

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

## TAARIFA

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hoja ya kukaimu, mzungumzaji ameisema vizuri sana. Nataka nimpe tu Taarifa kwamba, niliwahi kutoa Taarifa ndani ya Bunge hili kwamba, yupo mtumishi aliyekaimu zaidi ya miaka kumi ndani ya Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro, lakini baada ya miezi miwili wakamwondoa na kumshusha kabisa wakampeleka Mkoa mwingine. Kwa hiyo, ni Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hiyo naipokea, lakini huyu tutamwangalia kwamba, watampeleka wapi na tutaendelea kumfuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ni *Watumishi Housing*. Tumeboresha bajeti yao vizuri, wakatujengee nyumba za watumishi. Kipekee Mheshimiwa Waziri naomba sana, mimi natoka Wilaya ya Lushoto ambayo sehemu kubwa ni milima, imetawanyika mno na ndio maana sisi shida yetu kubwa kwenye eneo la utumishi ni watumishi kuendelea kuhama kutoka Halmashauri ya Lushoto kwa visingizio mbalimbali vikiwemo umbali, milima na kadhalika. Kwa hiyo, tunaomba, tunazo shule ambazo ziko pembezoni mno, kuna Shule ya Mhindulo ambayo iko kule Mbaramo na Shule inaitwa Nkombo iko huko Kata ya Mbaramo ni mbali sana zaidi ya kilometa 127 mpaka kufika makao makuu ya halmashauri. Kwa hiyo, tunaomba haya maeneo yote ya pembezoni hizi nyumba za watumishi na sisi ziweze kutufikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Wakala wa Serikali Mtandao. Tunaomba na wenyewe waboreshe, bado kuna maeneo mengi mtandao haujakaa sawa, hata ndani ya Serikali bado kuna taasisi nyingi hazizungumzi. Kwa hiyo, tunaamini kwamba, kwa zama hii ya teknolojia ambayo tunayo ni vizuri Wakala wa Serikali Mtandao nao ukaimarishwa ili mifumo mbalimbali ndani ya Serikali ikiwemo hii ya utumishi iweze kuonana na kusomana kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Massare. Jiandae Mheshimiwa Francis Mtinga na Mheshimiwa Maimuna Pathan.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi ili nichangie katika Hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Utumishi na Utawala Bora. Napongeza utendaji wa Serikali, kwa kiasi kikubwa umekuwa unaonesha kujali watumishi kwa kuwapandisha vyeo wale ambao walisimama kwa muda mrefu na kulipa malimbikizo ya watumishi wengi ambao walikuwa na madai, sasa kiasi fulani yamerekebishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali, nampongeza Mheshimiwa Rais na timu yake kwa kuona kwamba, uhitaji wa watumishi, hasa walimu, bado ni mkubwa sana. Hapa katikati Serikali imekuwa ikileta pesa nyingi katika halmashauri zetu na tumejenga mindombinu mbalimbali ya elimu na afya, changamoto iliyobaki ni watumishi hasa wa kada hii ya elimu. Kwa bahati nzuri Serikali imesikia kilio chetu sisi watumishi wa wananchi na sasa imetangaza ajira karibu 46,000. Naamini zitafika katika maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, majimbo yetu ya vijijini yana uhitaji mkubwa sana na hata walimu wanaohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine hawaombi kwenda vijijini, wanaomba kwenda mijini kuungana na familia zao maana familia nyingi ziko mijini. Huku vijijini sijui hakuna watu, lakini naomba hata uhamisho basi uzingatiwe, watu wanapopangiwa katika vijiji waweze kufanya kazi kwa muda wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imefanya kazi kubwa sana hasa katika Jimbo langu. Kuna maeneo kijiji kimoja kina shule nane, kutoka shule mbili sasa zipo nane, kwingine saba. Sasa walimu wanahitajika sana na kwa kweli katika jambo la kuzingatiwa ambalo tunaona kuwa ni changamoto sana, ni walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu hii Serikali mtandao. Serikali Mtandao kazi yao ni nzuri sana, lakini kuna changamoto kadhaa. Pamoja na kujenga mifumo mingi ambayo inafanya kazi bora bado ziko changamoto ambazo zinatakiwa zifanyiwe kazi. Mifumo hii haisomani kwa asilimia kubwa na changamoto hii inasababisha baadhi ya vitu kukwama, tunarudi katika *manual* ya ma-*file* wakati tulikuwa tumeshatoka. Mifumo hii ikisomana ni rahisi hata kwa Serikali yenyewe, Wizara na Wizara zikazungumza katika jambo mahususi ambalo linahusiana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalamu wa mifumo hii wanaohudumu ni wachache sana. Tunaiomba Serikali iongeze kuwasomesha vijana wetu ili waweze kumudu na hata inapotokea changamoto ya wengine kutoka kwa namna yoyote, basi mwingine aweze kuchukua nafasi hiyo. Jambo hili bado lina ugumu, watumishi wenye taaluma ambao wanasimamia mifumo hii ni wachache sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado siri zinavuja, siri za Serikali unazikuta mtaani mtu anazo. Kwa kweli, jambo hili linatakiwa liangaliwe kwa umakini sana. Zamani jambo la Serikali lilikuwa linabaki Serikalini, lakini sasa jambo la Serikali unakuta mtu wa mtaani kabisa analo, hata unashangaa siri hii imetokaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kidogo nizungumzie *TASAF*. *TASAF* wamefanya kazi nzuri kweli kweli, lakini bado zipo changamoto ambazo nadhani zikifanyiwa kazi zitafanya mradi huu wa *TASAF* ambao dhamira yake ni kuondoa umaskini uondoe umaskini kweli kweli. Unapowapa watu pesa ndogo sana, matokeo yake anakula halafu zinakwisha. Nashauri kutafuta miradi katika halmashauri ambayo itakuwa ni miradi endelevu, mfano miradi ya masoko, ili watu ambao wana uhitaji wapewe meza sokoni, watazungusha gurudumu na maisha yataenda. Tumeona baadhi ya maeneo yamejengwa masoko, natamani kuona hata kwenye halmashauri yangu ya Itigi waje wajenge kitu kimojawapo ambacho na sisi tutajivunia kutoka katika mradi huu wa kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Ndege za Serikali na *ATCL*. Hapa kuna vitu vinaleta mtafaruku kidogo, Wakala wa Ndege za Serikali ndiye mmiliki wa zile ndege, anapomkodisha *ATCL, ATCL* anailipa Serikali. Mmiliki wa *ATCL* kwa 100% ni Serikali, sasa hii ikoje? Natamani kuona hapa kuwe na mfumo ambao utaifanya *ATCL* imiliki hizi ndege na Wakala wa Ndege za Serikali amiliki zile ndege za viongozi tu. Sasa unapokodisha, ndege imenunuliwa na Serikali, Shirika ni la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie jambo moja, ndege ya Serikali inapokuwa kwa Wakala wa Serikali, deni la Serikali linafanya zile ndege zikamatwe. Hapa majuzi tumekamatiwa ndege na ninyi ni mashahidi kwa sababu, ndege zinasoma ni mali ya Serikali, lakini zingekuwa za *ATCL* isingekuwa rahisi kuzikamata kwa sababu, ni mali ya shirika japo mwenye lile shirika ni Serikali. Kwa hiyo, hili jambo tunatakiwa tulione ili tuepuke makandokando haya ambayo yanatukuta kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka pia nizungumze jambo kidogo kuhusu *Watumishi Housing*. Shirika hili limefanya kazi nzuri, lakini liko mijini. Halmashauri zetu za vijijini hatujaona *effort*, nataka niwaone

katika Halmashauri ya Itigi. Tutawapa viwanja bure wajenge nyumba za watumishi wetu ili waweze kukopa na tusaidie dhamira halisi ya shirika hili ambalo linafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina maneno mengi sana kwa sababu, bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri ni nzuri sana. Naunga mkono hoja ili wapewe hizi pesa wakafanye kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Francis Mtinga, wajiandae Mheshimiwa Maimuna Ahmad Pathan na Mheshimiwa Londo.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii inayoshughulikia watumishi ambao ni *engine* ya maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Kaka yangu Simbachawene, kwa kazi nzuri anayoitendea Wizara hii. Vilevile, nampongeza Naibu Waziri ambaye ni Mjumbe wangu wa Kamati ya Utekelezaji ya Vijana mimi nikiwa Katibu Mkuu wa Vijana kwa jinsi ambavyo anatenda haki katika kumsaidia Waziri na kuisaidia Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa nampongeza Rais wetu wa nchi hii. Rais huyu katika kila idara ya nchi hii amefanya mambo makubwa kwa muda mfupi sana na naomba Watanzania watuelewe tunapompongeza Mheshimiwa Rais. Katika kipindi cha miaka mitatu tu ya Mheshimiwa Rais, ameongeza ajira, jambo ambalo lilisimama kwa muda mrefu. Mwaka 2021 aliajiri watu 80,000, mwaka 2022 watu 32,000, mwaka 2023 watu 45,000 na baadaye watu 47,000 na hivi tunavyoongea kwa kipindi kifupi cha miaka mitatu Mheshimiwa Rais ameajiri watu 155,008. Hili si jambo dogo kwa muda mfupi kiasi hicho na tunaposema ajira, *implication* yake ni bajeti, kwa hiyo, tunapompongeza mama tunamaanisha amefanya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo ajira tu, mama huyu Mungu ampe maisha, amepandisha madaraja watumishi 513,490, jambo ambalo lilisimama kwa muda mrefu. Hii inamaanisha ameongeza kwenye bajeti shilingi 252,700,000,000. Kwa hiyo, Watanzania mnaotusikiliza tunaposema tunampongeza mama tunamaanisha amefanya makubwa na shukurani yetu Watanzania ni kumpa kura mama

mwaka 2025. Siyo kura tu, kura zitakazovunja rekodi ya nchi hii ambazo wamewahi kupata Marais, angalau hapo tutakuwa tumetenda haki maana hatuna kingine zaidi ya hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka mchango wangu ujikite kwenye suala zima la walimu. Pamoja na mama kufanya haya makubwa, lakini bado kuna tatizo kubwa sana kwenye utumishi hasa walimu. Urithi pekee ambao tuna uhakika wa kuwaachia watoto wetu pamoja na ugumu wa ajira ni suala zima la elimu, kwa sababu, elimu ni suala mtambuka, ukishakuwa na elimu unaweza kufanya mambo mengi na unaweza kujisimamia. Kwa hiyo, ni vizuri watoto wetu wakapata elimu bora na njia ya kwanza kabisa ya msingi ya kupata elimu bora ni kuwa na walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa bado tatizo la walimu ni kubwa kwa hiyo, niombe Wizara hii hizi ajira ambazo mama anazitoa tuziweke vizuri kwa sababu, pamoja na kuwa tatizo ni kubwa, lakini pia kuna tatizo kubwa katika mgawanyo wa hawa walimu. Kuna maeneo yana upungufu mkubwa na kuna maeneo walimu wamejaa, ule msawazo haupo. Kwa hiyo, Waziri atuelewe, tunaposimama na kusema upungufu hili jambo lisichukuliwe kijumla jumla, yapo maeneo yana hali mbaya sana. Nitatoa mfano kwa jimbo langu na najua utakuwa umegusa majimbo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jimbo langu linahitaji kuwa na walimu 1,376, lakini waliopo ni walimu 741 tu, ina maana kuna upungufu wa walimu 635. Huu ni upungufu mkubwa. Hata hivyo, nikiupeleka kiujumla hivyo bado meseji haitafika vizuri, naomba nitoe mifano tu kwa baadhi ya shule. Kwa mfano, nina Shule ya Msingi inaitwa Mwandu, iko Kata ya Iguguno, ina wanafunzi 1,102, ina upungufu wa walimu 24. Nina Shule ya Msingi Nkungi, iko Kata ya Ilunda, ina wanafunzi 1,043, ina upungufu wa walimu 23. Kuna Shule inaitwa Kikhonda, ina wanafunzi 1,285, ina upungufu wa walimu 29. Ipo Shule inaitwa Mwanigwe ipo Kata ya Kinampundu, ina wanafunzi 1,417, ina upungufu wa walimu 31. Tuna Shule inaitwa Mwangeza, ina wanafunzi 1,177, ina upungufu wa walimu 26, vilevile ipo Shule inaitwa Kinyamburi iko Kata ya Nkinto, ina wanafunzi 1,271, ina upungufu wa walimu 28 na mwisho, tena nimeamua tu kuishia hapo, Shule ya Msingi Tumuli ina wanafunzi 1,367 na ina upungufu wa walimu 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kwa upungufu wa namna hii katika hizi shule chache tu, hawa watoto wanapata elimu kweli, wanapata elimu bora kweli ili wakajitegemee? Hawa watajiajiri kweli kwa upungufu wa namna hii? Kwa hiyo ningeomba sana Mheshimiwa Waziri aelewe, hizi ajira zilizotangazwa juzi, wanapozigawa waangalie wanapeleka wapi na upungufu uko kwa kiasi gani. Tukisema tu kijumla jumla tu kwamba nchi ina upungufu bila kuangalia wapi pana upungufu kwa kiasi gani na athari kiasi gani, kuna watu wataumia na kukosa elimu ambapo tunazidi kusababisha umaskini wa kutosha katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niseme kidogo kwenye suala la *interview*. Utumishi wamekuwa na tabia ya kufanya *interview* nchi nzima. Nafasi 200 wanaitwa watu 40,000 Dodoma. Hili tatizo limekuwa likiumiza sana vijana. Watu 40,000 wanakuja kugombania nafasi 200 na hawa watu hawana kazi na wametoka huko kijijini, wamekopa nauli, akija hapa atakaa *guest* siku tatu. Halafu mwisho wa siku kwa sababu nafasi ni chache, wakiondoka wengi wamekosa, ndiyo inajengeka dhana kwamba kuna rushwa, kuna mwingine mpaka uwe na *referee*, mpaka ujuane na Mbunge, sijui mpaka ujuane na nani, tunapata tabu sana. Sababu kubwa ni hii ya kuita watu wengi namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Wizara ya Utumishi, wakishaita watu mara moja kufanya *interview* kwenye kada, waweke benki ya hawa watu. Naamini wanakuwa wame-*qualify* watu wengi zaidi ya ile nafasi wanayotaka. Waweke hii kwenye *list* ili nafasi zinapopatikana wampigie tu mtu simu, kwamba, wewe fulani uko wapi? Uko Mkalama? Umeajiriwa tayari? Bado. Nenda ukaripoti Nkenge kuna kazi kule. Kwa sababu alikwishafanya *interview* na wamekwishamweka kwenye benki

Mheshimiwa Naibu Spika, hii kuita watu kila siku, nafasi ni chache na watu ni wengi, wazazi wanahangaika nauli na vitu vingine, inasumbua sana. Angalau baada ya miaka mitatu minne, wana-*review* tena ili kuweka ile benki yao vizuri, kama watakuwa wamepungua au vinginevyo. Hii itatusaidia sana, lakini kuita watu wengi katika nafasi chache (watu sijui wangapi) inatutesa, inaleta *implication* mbaya na inaonekana kuna watu wachache wanaopata ajira kwa sababu wana *referees* kumbe wala siyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ni suala la wakuu wa idara kwenye halmashauri. Leo hii ili mtu athibitishwe kuwa mkuu wa idara awe ametumika kwa miaka 10 na ndiyo anaruhusiwa kwamba huyu sasa amekomaa. Hapo hapo *boss* wao ambaye ni mkurugenzi anaweza akateuliwa kutoka *private sector,* anaweza akatoka kwenye ualimu ameanza kazi juzi lakini anaonekana ni kijana mzuri na msomi, anaajiriwa na anapelekwa kwenye wilaya anakuwa mkurugenzi na kazi zinaenda. Sasa, *boss* wao anaweza kuajiriwa wakati wowote lakini wakuu wa idara mpaka wakae miaka 10. Niombe kitu kimoja. Aidha, Utumishi wabadilishe hiki kitu waachane na habari ya miaka kumi, watu wapate tu ukuu wa idara wakati wowote au mamlaka ya uteuzi iwe inapelekewa majina ya hawa wakuu wa wilaya ili kuwe na *succession*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtinga, hiyo ni kengele ya pili, ahsante.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie sana suala la walimu Mkalama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna, wajiandae Mheshimiwa Londo na Mheshimiwa Dkt. Kaijage.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii leo ya kuchangia kwenye Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala bora. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi ya uzima na wenzangu wote tulioko humu ndani tunatakiwa tumshukuru Mungu kwa sababu ametupatia uzima kwa siku ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kumshukuru Rais wetu, Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya katika nchi yetu. Miradi mingi ambayo anaifanya inaonekana, kazi kubwa

anazozifanya zinaonekana. Tunatakiwa tumpongeze sana Mama yetu Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Waziri wa Utumishi, Naibu Waziri na jopo lake lote la Utumishi kwa kazi kubwa wanayoifanya na kwa kutuletea bajeti nzuri inayoonesha mwanga endapo itatekelezwa vizuri kwa watumishi wetu wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina masuala machache kidogo. Suala langu la kwanza ni malipo ya wastaafu. Naongelea hili suala kwa huzuni kubwa na kwa uchungu mkubwa sana, kwa sababu kuna watumishi wengi wameitumikia Serikali yetu tukufu kwa weledi mkubwa, wamefanya kazi vizuri sana, lakini wamestaafu wametupwa na mpaka leo hawajapata haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana, nina baadhi ya watu na nina *evidence* za kutosha. Nina mtu wa kwanza hapa alikuwa ni dereva wa Chuo cha Ualimu Nachingwea, anaitwa Hamis Mnali. Huyu baba amefanya kazi yake vizuri, amestaafu mwaka 2009. Jamani, mtu amestaafu mwaka 2009 mpaka leo hajapata mafao yake. Hebu tuangalie hapo utu upo kweli? Ukitaka hii hali iume, hebu jaribu kurudisha vidole mikononi mwako wewe. Ufanye kazi, utumikie, halafu umalize utumishi wako mwaka 2009 mpaka leo hujapata mafao yako. Jamani tunakwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mama yetu Samia Suluhu anafanya kazi kubwa sana na inaonekana. Pia, viongozi wetu wakubwa wanafanya kazi kubwa sana, lakini huku chini kuna watu wanamwangusha. Nina mifano mingi na hata Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, tukimaliza hapa tutaonana. Huyu baba amestaafu 2009, amezungushwa na nina *evidence* ya barua zake zote hapa alizoandika utumishi, akaambiwa sijui leta nini, akapeleka. Mpaka baadaye akaamua kuandika barua ya kulalamika. Barua nyingine ikarudi kwenye kile Chuo cha Ualimu Nachingwea, huyo mtu afuatiliwe kisha majibu yarudishwe imefikia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo aliyoyafanya huyu baba mpaka leo hii ninavyongea na hili Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 19 Aprili, 2024 huyu baba hajapata mafao yake. Hii ni haki kweli? Tunakwama wapi Serikali yetu ya

Tanzania? Tunawafanyia nini wananchi wetu? Huyu baba mshahara wake ulikuwa ni mdogo tu, ni dereva wa Chuo cha Ualimu Nachingwea, lakini mpaka leo hajapata haki yake. Amefuatilia amemaliza, amekopa hela kwa watu, amehangaika, aliwatumia mpaka Wabunge na barua ziko humu ndani. Kitu cha kushangaza hajapata haki yake. Apate wapi na huyu ni Mtanzania halali? *Documents* ninazo, Waziri na Naibu Waziri, nikitoka naomba hapa tuonane ili tufuatilie suala la huyu baba, apate haki yake. Pia, wapo wengine wengi nitampa Waziri *evidence* zao. Inasikitisha sana na inaumiza sana. Nitapeleka hizi barua, vithibitisho na mambo mengine kwa Waheshimiwa Mawaziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la kuhakiki watumishi mkoani. Hili suala nilishaliongelea kwenye Bunge na nikauliza swali. Unapostaafu uchumi unakuwa umerudi chini, umri unakuwa umesogea na hauna nguvu. Kwa nini tusiwafuate hawa watu kwenda kuwahakiki kule kila mwaka? Nilijibiwa kwamba, wanakwenda kuwafuata wilayani, hawajaanza hicho kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaamini sana viongozi, Waziri na Naibu Mawaziri waliopo kwenye Wizara hii. Naomba walishughulikie hilo ili watu waende wakahakikiwe huko, hawana uwezo wa kutoka. Hivi umtoe mtu Kilimarondo au Liwale aende akahakikiwe Lindi, hivi jamani mnajua kilometa zilizopo? Mnajua nauli ni kiasi gani? Kwa kweli hatuwatendei haki ndugu zetu kwa sababu na sisi pia ni wastaafu wajao hapo mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine tulikuwa watumishi wa umma, hii hali tunaijua. Tunaomba kuhakikiwa kusiwe mikoani, tuwafuate hawa watu. Ni bora ukamlipa mtendaji wako akaenda kuwafuata hawa watu kwenye kila wilaya akahakiki ili kuwasaidia hawa watu. Watu wazima maradhi yako mengi, uwezo wa kifedha hamna, leo wakahakikiwe mkoani? Hatuwatendei haki na naomba hii ibadilishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la ajira, hili suala la ajira ndiyo kizungumkuti kabisa kusema ukweli. Wabunge wenzangu wameshaongelea hapa, unawaita watu wanatoka Liwale, wanatoka huko, wanatoka wapi, wanakuja kufanya *interview* Dodoma. Anakuja hapa mzazi wake hali yenyewe ya maisha ni ngumu. Wanakopa hela

huko wanakuja hapa wanakaa hata wiki kwenye hoteli. Hebu tuifikirie hii kwa kweli, inaleta msingi kweli? Naomba tubadilishe hili suala la ajira sasa hivi liwe linafanyika kiwilaya. Tena ikiwezekana tunaomba na mgawanyo wa kiwilaya, kwa sababu ajira zinafanyika kwenye *system,* tunaomba tugawane kiwilaya ili na wilaya nyingine zisikose. Inaonekana kuna wilaya nyingine wanapata watumishi wengi na wilaya nyingine hazipati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la lingine linaniumiza sana kichwa na *evidence* pia ninazo. Kuna baadhi ya askari polisi walifukuzwa kazi kwa uonevu. Nina *evidence* popote nitakaposimama na nitawaita na wenyewe. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, naomba walifuatilie hili suala. Mmoja alikuwa ni polisi anafanya kazi Kigamboni katika Kitengo cha *Anti-Robbery*, mmoja alikuwa anafanya kazi *central* pale kwenye Kitengo cha *Rider* (wale waendesha pikipiki). Siku moja wakiwa kazini usiku walikamata dawa za kulevya (ni siku nyingi kidogo mwaka 2013). Walipokamata dawa ya kulevya na gari wakaamua kuongea kwenye zile simu zao kutoa taarifa makao makuu kwamba kuna gari tumelikamata na lina madawa ya kulevya, kwa uhakika kabisa na kwa uaminifu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamejipalia makaa. Siwezi kuthibitisha kwamba zile dawa zilikuwa ni za wakubwa, ila naomba wani-*quote,* "Inawezekana zilikuwa dawa za wakubwa au dawa ya watu wenye pesa sana". Hali ilikuwa mbaya kwao, kilichofuatia waligeuziwa kesi na wakabambikiwa kesi za ajabu. Baada ya siku mbili, tatu walikwenda kukamatwa wakawekewa kesi ya kwanza kwamba, wameiba kwa Wachina, kesi ya pili wameiba *bar*. Mtu amekamata dawa za kulevya ameokoa vijana wetu ambao wanaharibika na madawa ya kulevya, leo wanakuja kubambikiwa kesi kubwa kama hizo? Inasikitisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilichofuatia ni kwamba kesi ilikwenda mpaka 2016 ikaonekana hawana hatia na wenye hatia walikamatwa wakafungwa. Kibaya zaidi, baada ya kesi kwisha wale walianza kuandika barua ili waweze kupata stahiki zao za miaka yote ambayo walikuwa wamewekwa ndani na kurudishwa kazini, inasikitisha. Wamepigwa danadana na kibaya zaidi kuna baadhi ya watu wakaanza kuwafanya mtaji wao kwa kuwachukulia hela ya kuishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha, watu wamejitolea kutetea Taifa letu, leo hii ndiyo wanaambiwa ndiyo wametenda yale madhambi…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maimuna Pathan, muda wako umekwisha kaa chini…

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, lakini naomba hizi kesi ambazo nawapa, Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, niwaone ili hawa watu wasaidiwe, warudishwe kazini, walipwe haki zao za msingi. Hii ni Tanzania, wako kwenye nchi zao, wana… *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pathan utaratibu ni kwamba kama una mengine ya ziada unaandika kwa Waziri.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nimekusikia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Londo, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Kaijage na Mheshimiwa Mohamed Monni.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi. Bajeti hii ni muhimu sana kwa sababu suala la utumishi ni suala *sensitive* na ni suala ambalo ni muhimu sana katika utawala wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye imempendeza yeye sisi waja wake kujadili bajeti hii muhimu katika utekelezaji wa moja kwa moja wa majukumu ya Serikali kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa nimshukuru Rais wetu, Mama yetu Samia Suluhu Hassan, kwa maboresho makubwa ya utumishi ndani ya Serikali. Pia, itoshe kusema kwamba, utumishi kwa

maana ya utawala ilikuwa ni sehemu ya Kamati ya kile kilichoitwa USEMI. Kwa hiyo, tulikuwa na maslahi ya karibu sana katika kuifuatilia na naweza kusema kwamba kuna maboresho makubwa katika utumishi ndani ya Serikali yetu. Sifa kubwa zimwendee Rais wetu, Mama yetu Samia Suluhu Hassan pamoja na timu yake katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaweza kuona kero na kadhia nyingi za watumishi wetu hasa kero ya upandishwaji daraja kwa watumishi, malimbikizo na madai mbalimbali ya watumishi wetu yakichukuliwa hatua; kwa maana ya kuangalia jinsi gani ya kutoa *solution* ya changamoto kwa kuwapandisha madaraja, kulipa malimbikizo na madai mbalimbali ya watumishi wetu. Jambo hili haliwezi kupita kimya kimya, ni wajibu wetu kupongeza pale ambapo Rais wetu na Serikali yake inafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo naomba kutumia nafasi hii kuipongeza sana Serikali hasa kupitia tangazo la Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi, kaka yetu Mheshimiwa George Simbachawene lililosema kwamba Serikali na Mama yetu Samia Suluhu Hassan, ameridhia ajira mpya za watumishi 46,000. Kilio cha upungufu wa watumishi ndani ya Serikali ni kilio kikubwa miongoni mwa Wabunge na wananchi wetu. Kwa hiyo, tangazo hili limetupa faraja sana sisi wawakilishi wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa kuliko yote ni ubunifu wa Wizara kusema kwamba hizi ajira zinakwenda mikoani. Hii inaweza kupunguza gharama kwa wazazi za kutuma watoto kwenda kwenye vituo vya Dodoma na Dar es Salaam kwa ajili ya *interview*. Pia, inaweza kuongeza uwazi katika suala zima la ajira. Kubwa kuliko yote ni msawazo wa ajira hizi kuwa wa haki kwa Tanzania nzima kwa sababu tunajua mahitaji ni makubwa. Nafasi ni chache lakini ni lazima kuwe na uwakilishi wa Kitaifa na ndiyo maana nasema kwamba suala la utumishi ni suala *sensitive*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utumishi wa umma kama dhana, ni dhana muhimu sana, lakini umma ni nini? Mtumishi wa umma ni nani? Ni huyu Mtanzania ambaye ana *check number* ambaye ameajiriwa na Serikali ama ni huyu kijana ambaye amejiajiri kama dereva wa daladala ambaye anaamka saa 10 alfajiri na analala saa tano usiku

akihakikisha kwamba watumishi na waajiriwa wa Serikali wanafika ofisini kwa muda, wanafanya kazi kwa muda na anahakikisha wanarudi nyumbani salama?

Mheshimiwa Naibu Spika, mtumishi wa umma ni nani? Ni huyu ambaye anaingia saa moja na nusu ofisini na anatoka saa kumi ama ni huyu mama lishe ambaye anahakikisha watu wote ambao wameajiriwa na ambao hawajaajiriwa wanakunywa chai asubuhi, wanakula chakula cha mchana na cha usiku na afya zao zinalindwa? Mtumishi wa umma ni nani katika nchi hii? Ni nani ambaye ana jukumu la kulinda maslahi ya umma? Ni hawa ambao wana *check number* ya Serikali ama hawa Watanzania ambao kila mmoja kwa nafasi yake anawajibika katika ujenzi wa Taifa letu?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nazungumza hivi? Kuna *concept* inaitwa *tragedy of the commons* (chochote cha umma hakina mwenyewe). Tunaweza tukaliona hili katika namna ya usimamizi na udhibiti wa mali za umma. Changamoto bado ni nyingi, bado changamoto ni kubwa na Serikali inaingia gharama kubwa ya usimamizi wa mali zake pamoja na uchakavu wa mali zake kutokana na usimamizi mbaya kwa sababu hakuna mtu ambaye anaona umuhimu wa kulinda mali za umma. Sasa wakati umefika kwa Watanzania wote kujiona kwamba ni watumishi wa umma. Kila mmoja kwa nafasi yake anawajibika kulinda maslahi ya umma, kulinda mali za umma na kuhakikisha umma unafaidika na kile ambacho unastahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la dhana ya utumishi linanipelekea kuona kwamba, ni muhimu kulinda haiba ya Serikali kwenye macho ya wananchi. Kulinda haiba ya Serikali ni jukumu la Watanzania wote ambao ni watumishi kwa namna moja ama nyingine. Mwalimu Nyerere alisema; "*It can be done, play your part.*" Inawezekana kila mmoja akitimiza wajibu wake kwenye eneo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kijijini kwenye *level* ya chini kabisa Serikali kule inaonekana kupitia waajiriwa wa Serikali kwa maana ya muuguzi, daktari, mtendaji wa kata. Mwananchi wa kule kijijini anaweza asikutane hata siku moja kwenye maisha yake na mkurugenzi, *DAS* ama *DC*, kwake yeye Serikali inaishia kwa mtendaji wa kijiji akienda juu sana mtendaji wa kata, hawa ndiyo sura ya

Serikali, hawa ndiyo vioo vya Serikali. Mwananchi akisema Serikali ni mbaya ni kwa sababu amehudumiwa vibaya na muuguzi kwenye zahanati ya kijiji, akisema Serikali ni nzuri maana yake amepata huduma safi kwa mtendaji wa kijiji, lakini utendaji wao wa kazi na haiba yao inafanana na dhana ya utumishi wa umma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili naomba nguvu kubwa ielekezwe kwenye kujenga dhana ya utumishi, kuboresha haiba ya utumishi katika ngazi za chini kwenye vijiji na kata zetu. Serikali yetu imekuwa ikibeba lawama nyingi ambazo zinatokana na utendaji mbovu wa watu katika maeneo ya chini, si wote, ni wachache lakini wanaharibu taswira nzuri ya Serikali. Mara nyingine si makosa yao, mara nyingine ni kukata tamaa, mara nyingine na wao kuona hawatendewi haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kuwekeza sana kwenye kuboresha ofisi, kuwapa vitendea kazi wengine mapikipiki, pale wilayani, magari, ofisi nzuri lakini bado kuna kitu ambacho kinakosekana na chenyewe kiko kwenye *software* siyo *hardware,* ni lazima sasa jitihada ziwekezwe katika kuboresha maisha ya mtumishi ajione kwamba anawakilisha Serikali, anawakilisha nchi kwa maslahi ya nchi katika maisha ya wananchi, katika ngazi ya chini. Kwa kufanya hivi tutakuwa tumeitendea haki na kuisaidia sana Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vema tukatambua utendaji mbovu wowote katika ngazi ya chini unapunguza imani ya wananchi kwa Serikali yao. Suala hili ni muhimu sana, *deficit* ya *public trust* kwa Serikali si jambo dogo, ni jambo kubwa sana, mwananchi ni lazima aamini kwamba akifika katika ofisi ya kijiji atatendewa haki na mtendaji wa kijiji. Mwenyekiti wa kijiji ni lazima asimamie maslahi ya Serikali ya kijiji kwa kulinda *interest* za wananchi wake katika ngazi ya kijiji na lazima mtendaji wa kijiji ajue kwamba yuko pale kwa ajili ya kuiwakilisha Serikali na yeye ni mwakilishi wa Serikali. Tukiboresha hayo, malalamiko ya wananchi wetu yatapungua, wataendelea kupenda Serikali yao na wataendelea kushiriki katika ujenzi wa Taifa lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, langu ni kumshukuru Rais wetu kwa sababu amewekeza sana katika kuboresha maisha ya watumishi katika ngazi za vijiji, kata na katika halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kaijage, wajiandae Mheshimiwa Mohamed Monni na Mheshimiwa George Kakunda.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Nami naendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo ameendelea kufanya kazi kwa umakini mkubwa kwenye Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kuwapongeza viongozi wangu kwa maana ya Waziri wetu Mheshimiwa George Simbachawene, amekuwa akifanya kazi kwa bidii sana bila kumsahau Ndugu yangu Naibu Waziri, Mheshimiwa Ridhiwan Jakaya Mrisho Kikwete kwa muda mfupi sana ambao amekaa kwenye ofisi hiyo ameonesha umahiri mkubwa, wenzangu wataniunga mkono tunampongeza sana ndugu yangu. Pia nawapongeza watendaji wote wa ofisi hii bila kusahau watumishi ambao wako chini ya ofisi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba niwapongeze watumishi wote ambao wako katika maeneo mbalimbali ambao wamekumbwa na kadhia au changamoto iliyosababishwa na mvua nyingi sana zinazonyesha katika nchi yetu. Wale watumishi wa maeneo yale wanafanya kazi siyo masaa 24, ni masaa yote, wanafanya kazi masaa yote, wanafanya vikao usiku na mchana, ni mazingira mengi sana yamepata mafuriko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikisema maeneo machache kwa maana Rufiji na Kibiti watumishi wa maeneo yale hawana kupumzika, unaona mpaka wanatembea wanasinzia na hii ni *spirit* ya watumishi wetu wa Tanzania. Hatukatai kuna watumishi wana mapungufu lakini watumishi wa Tanzania wameendelea kufanya kazi katika ari na

uzalendo mkubwa, Wabunge tukiwa mashahidi mazingira yetu kule vijijini kwenye halmashauri tunayaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona mazingira wanayoishi watumishi wetu watendaji wa kata, watumishi wetu ambao ni maafisa maendeleo ya jamii, watumishi wote katika halmashauri zetu vijijini wanaishi mazingira ambayo sisi tunayafahamu lakini watumishi hawa hatujawaona wakiingia barabarani wakifanya maandamano, wakibeba mabango kama nchi jirani. Kwa hiyo, watumishi wa Tanzania pamoja na kwamba wanapitia mazingira mbalimbali wameendelea kusimamia taratibu, sheria na kanuni za utumishi, wameendelea kuwa wazalendo, wanastahili kupokea maua yao watumishi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumnukuu Mheshimiwa Mama yangu kipenzi Dkt. Samia Suluhu Hassan ili kuunganisha sifa hizi ninazozitoa wapate kujua ndiyo moyo wa Mheshimiwa Rais alisema: "*Kwa kila Taifa linalokua kuna nguvu ya wafanyakazi kwa kiasi kikubwa mno.*" Hakuishia hapo Mheshimiwa Rais alisema, anatambua mchango wa wafanyakazi kwenye uchumi na ustawi wa Taifa la Tanzania. Pia hakuishia hapo Mheshimiwa Rais alisema, anatoa shukrani zake za dhati kwa wafanyakazi kwa kazi wanayofanya kwa Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema wafanyakazi wa Tanzania wanafanya kazi kwa uzalendo, hatukatai kuna watu wenye mapungufu, kwa hivyo naomba hilo lijulikane, wafanyakazi wa Tanzania wanastahili kupokea maua yao, tumeona wafanyakazi wa nchi zingine wako barabarani, siyo kwamba hawana changamoto, wana changamoto, lakini wamekuwa wavumilivu wamekuwa wazalendo kwa Taifa lao watumishi wa nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda Fungu 32 ambalo ni Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Nimezungumza mara nyingi kwenye Bunge lako Tukufu jinsi ambavyo ndani ya miaka mitatu Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amejali eneo la utumishi, amejali maslahi ya utumishi kwa mapana yake, siwezi kurudia nimeshasema kwa idadi na kwa gharama iliyotumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu Ofisi ya Rais ambayo ndiyo Wizara yake mwenyewe Mheshimiwa Rais, imeendelea kuumba mifumo mbalimbali ambayo inaleta ufanisi katika Utumishi wa Umma. Tumeona kuna miundo na mgawanyo wa majukumu ya Taasisi mbalimbali ambako mpaka sasa imehuishwa miundo 80 kati ya miundo 120. Naipongeza ofisi hii, lakini nijielekeze, ukienda kukutana na watumishi, kama kuna *top five* yaani kama kuna changamoto tano basi kati ya hizo tano miundo haikosekani. Wanalalamikia sana suala la miundo, miundo ya maendeleo ya utumishi yaani *scheme of service*. Najua kwamba ukigusa muundo unagusa *wage bill* sijakataa, lakini miundo imeendelea kuwa changamoto, inapelekea watumishi kule chini kupunguza morali ya utumishi wao wa kazi, kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mtumishi ameshafanya kazi katika kada yake, amefikia *TGS* ya juu sana, niseme mfano ni mwalimu lakini alikuwa na *ambition* maishani kuwa mwanasheria, akaenda kusoma sheria, sikatai kwamba akija kwenye Idara ya Sheria hawezi kupanda wakati huo huo, lakini basi kama hawezi kupanda wakati huo huo, hata ahame na mshahara wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama inawezekana waweke kanuni na taratibu au mwongozo kwamba mtumishi akitoka kusoma asishuke akaanza tena *TGS* ya chini, inawafanya wasiende kusoma, watu wana ndoto zao, eneo hilo limekuwa likilalamikiwa sana. Pia kuna kada zingine ili kuwa Mkuu wa Idara lazima awe ni *principal* lakini zingine si lazima awe ni *principal,* lakini watumishi wanafanya kazi eneo moja hii imekaaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kuna Miundo Mikuu ya Serikali na kuna Miundo ya Taasisi na Wakala mbalimbali, hebu tuendelee kuwasiliana ili watumishi wale ambao wameendelea kufanya kazi, kuna jambo kubwa watumishi wa Tanzania wanalisema, ukienda kuwasikiliza jambo la kwanza wanamshukuru sana Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wanasema pamoja na keki ndogo anayopata pamoja na kwamba amezingatia sekta zote, awamu hii hajawaacha watumishi ameendelea kuwajali, hiyo inawapa moyo kuendelea kufanya kazi. Pamoja na kwamba tunasema haki inatokana na wajibu, huo wajibu wanaofanya, basi na haki zao wapate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakwenda kupitisha bajeti yao, lakini pamoja na Wizara ya Fedha linapokuja suala la rasilimali watu, suala la watumishi, naomba tuliangalie kwa jicho la tofauti na bajeti yao tuipeleke kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda Fungu 67 kwenye Sekretariati ya Ajira. Nimezungumza mara nyingi kuhusu suala zima la Sekretarieti ya Ajira, nawapongeza kwanza kwa jinsi ambavyo wameendelea sasa Serikali kuweka mifumo ambayo sasa hivi waajiri au wanaoitwa kwa ajili ya ajira hawaendi sehemu moja tena. Walianza kwa *zonal* kwa maana ya Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kati, kote kuna *center* za kufanya mitihani, nawapongeza sana Serikali. Sasa hivi wameenda kiwilaya, sisi kama Kamati tumeona wamefungua *center* kwenye wilaya zote, sasa wanaokuja kufanya *interview* hawaendi tena kwenye mikoa wanaenda kwenye *zonal wise,* kwenye vyuo na kadhalika, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo moja naenda kulirudia, siyo siri kwamba miaka mitano iliyopita ajira hazikuwa nyingi sana na sasa Mama amefunguka, lakini wakumbuke narudia tena, kila mwaka vyuo vilikuwa vinatoa *graduates,* watoto wako nyumbani tunao, umri wao unakwenda. Wanapofanya *interview* sasa hivi na hawa ambao wametoka shule mwaka jana, tusitegemee kwamba watafaulu sawasawa na wale ambao wameshakaa nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisemi aende mtu aliyefeli, lakini kama *pass mark,* kwa sababu sasa wanafaulu sana watoto, kama ajira wanataka watu 200 na wamepata 100, 200 au 90 wote kuna watu wana 80 au 70 tuangalie mwaka wao wamemaliza lini shule, kama ana 80 amemaliza shule 2017, hebu tufanye *consideration,* ameshaingia mtaani amefanya shughuli nyingi, hatutegemei afaulu kama amemaliza shule juzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wanajua nini maana ya kukaa mtaani, wanakosa watu ambao watakuwa watumishi waadilifu kwa sababu wanajua nini maana ya kukaa mtaani, hebu na hawa wengine wasubiri au tuchukue 50 kwa 50. Tumewafanya hawa watu waichukie Serikali yao, wajione kama siyo sehemu ya Tanzania. Nakubali kwamba si wote ambao watapata ajira, lakini wale ambao wamekaa muda mrefu miaka mitano siyo kosa lao, naomba

wanapokuja mwisho kuhitimisha waniambie hili suala limekaaje maana ni mara ya tatu nalizungumza katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la makazi, mtendaji kata kule kwenye kata, kijiji, kule kwenye mtaa au mtendaji wa kijiji heshima yake na usalama wake ni makazi pia. Naipongeza Serikali inaendelea kujenga nyumba za watumishi na tunajua sasa hivi kwenye Halmashauri zetu wamehamia kwenye makazi maalum, Halmashauri nyingi zimehamia maeneo mapya ambapo ni mbali na kule ambako wanakaa watumishi wale na hakuna makazi ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kupitia Utumishi *Housing*, wameendelea kujenga nyumba, lakini kiuhalisia mtendaji kata anashindwa kununua ile nyumba ya Watumishi *Housing*, wamekuja na mawazo wamesema kama inawezekana kumjengea mtumishi kila siku nyumba ya bure basi jenga piga *flat* moja eneo la halmashauri fulani, angalau kila mwezi akatwe shilingi 10,000, akitoka halmashauri akahamishwa, akienda nyingine kuna uhakika wa nyumba, usimpe basi nyumba ya bure kama ni kazi namna hiyo. Naamini *National Housing* pamoja na Watumishi *Housing* pia wanafanya kazi kibiashara, lakini watumishi hawa anamkamata mtu kwenye kata, mtu huyu aliyemkamata amepanga nyumba ya mjomba wake, yaani yeye mtendaji amepanga nyumba ya mjomba wake huyo mtu, heshima iko wapi? Kwa hiyo suala la makazi ni muhimu sana, nampongeza Mheshimiwa Rais anafanya, lakini tuliangalie kwa umakini wake, kujenga nyumba za bure zote kwa kuwa Serikali inajua, inanielewa hebu tufanye.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Kaijage.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni, wajiandae Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Mpina.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu ya watumishi wetu wa Tanzania. Kwanza kabisa nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia afya njema, amenijalia uhai na nimepata fursa ya kuchangia hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wenzangu waliotangulia kusema kwamba tuna kila sababu za kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mama yetu kwa mema ambayo anayafanya kwa Watanzania. Kipekee kabisa nimshukuru pia kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene, Waziri na Naibu Waziri wake kwa kazi kubwa wanayoifanya kwenye ofisi hii. Niwashukuru na kuwapongeza pia watendaji wa ofisi hii kwa kazi wanazozifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa miaka mitatu Wilaya yetu ya Chemba imepata watumishi zaidi ya 550, kati ya hao 300 ni wa elimu, 250 ni wa kada zingine. Nachukua nafasi hii kuishukuru Serikali, nakumbuka mwaka 2021 nilisimama hapa kueleza namna Chemba ambavyo ilikuwa na upungufu wa watumishi, kwa hiyo nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuhakikisha wanatutendea wema Chemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuletewa watumishi wa kutosha hawa, bado changamoto ni kubwa sana Chemba, mahitaji ni zaidi ya 3,052, lakini waliopo ni 1,700, maana yake kitakwimu zaidi ya 43% ni upungufu. Katika mazingira hayo unaweza ukaona ni namna gani watumishi wa Chemba wanavyolazimika kufanya kazi za watu wengine. Nimwombe Mheshimiwa Waziri Kaka yangu Simbachawene aendelee kuiangalia Chemba kwa namna ya kipekee ili walau tuwe na watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nifafanue kidogo kwa mfano kwenye afya. Tunao upungufu wa zaidi ya 70% kwenye afya, kwa hakika ni takwimu za kutisha kidogo pengine kwenye Mkoa wa Dodoma au na wenzangu wengi, kwenye kada ya afya mimi ndiyo nina kiwango kidogo cha watumishi. Kwa hiyo, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Utumishi aangalie namna ambavyo anaweza akatusaidia na mwezi Juni tunaenda kufungua zahanati nne ambazo nina hakika

hatutakuwa na watumishi. Kwa hiyo, naomba katika watumishi hawa ambao wanaenda kuajiriwa tuiangalie kipekee Chemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika elimu tunayo changamoto zaidi kwenye elimu ya msingi na wenzangu wamesema. Kwangu pia watumishi waliopo ni 52% tu, 48% ni upungufu. Hali hii inaweza ikachangia pia matokeo mabaya, matokeo hasi. Wakati mwingine tunaweza kukaa tukalaumiana amesema ndugu yangu Mheshimiwa Mtenga, hizi shule zetu za vijijini mnaweza mkakaa mnalaumiana kwamba watoto hawafaulu, lakini je, tumewahi kuangalia uwiano uliopo wa wanafunzi ulioko kule na walimu? Ukweli ni kwamba kuna upungufu mkubwa sana wa walimu na waliopo wanafanya kazi kubwa, wanajitahidi lakini ukweli unabaki palepale na matokeo hayo yanakuwa hivyo kwa sababu ya upungufu huo wa walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kumwomba Mheshimiwa Simbachawene, kaka yangu aangalie pia kwenye sekta hiyo ya elimu ya msingi. Nashukuru sekondari kidogo hali imetengamaa, kuna upungufu lakini ni upungufu ambao unakubalika wa 20%, lakini huku kwenye *primary school,* nawaomba sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niongelee kuhusu watendaji wa kata. Wenzangu hapa watakubaliana kwamba majimbo ya vijijini au wilaya za vijijini kwangu kote ni vijijini, watendaji wa kata na vijiji ni watu muhimu sana, si tu wanafanya kazi za majukumu yao waliyopewa, lakini wanafanya kazi nyingi, wanafanya kazi nje na zile ambazo wamepangiwa. Wanafanya kazi za kukusanya mapato, wanafanya kazi za kusimamia miradi ya Serikali, wanafanya kazi ya kuchangisha michango kwa ajili ya miradi ya Serikali. Kwa hiyo wanafanya kazi nyingi sana, ndiyo wasuluhishi wa migogoro, ndiyo mahakama, kwa hiyo katika mazingira hayo tunaweza tukaona watendaji wa kata walivyo muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu kuna kata 26, lakini watendaji waliopo ni wa kata 19 tu, mnaweza mkaona kuna kata saba hazina watendaji. Nina vijiji 113, watendaji waliopo ni wa vijiji 85 tu, kwa hiyo tuna vijiji zaidi ya 28 ambavyo havina watendaji. Kwa hiyo nakuomba sana pia ndugu yangu, kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene, tuangalie ni namna gani tunaweza kuwasaidia hawa, kwa sababu ukweli ni kwamba makusanyo yote ya vijijini huko yanafanywa na

watendaji wa vijiji, yanafanywa na watendaji wa kata. Maana yake ni kwamba kama kijiji hakina mtendaji tafsiri yake ni kwamba, hata mapato ya Serikali hayawezi kukusanywa, hakuna chochote kinachoweza kukusanywa na hivyo inapelekea upungufu mkubwa wa makusanyo ya mapato. Kwa hiyo niwaombe sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nawashukuru sana watumishi wa Wilaya ya Chemba, nawashukuru kwa sababu moja tu, upungufu mkubwa huu, lakini kwa Mkoa wa Dodoma Chemba tunaongoza kwa kukusanya mapato vizuri, nafikiri ndugu zangu wa Mkoa wa Dodoma wanafahamu. Kwa hiyo nimshukuru sana Mkurugenzi wetu Ndugu Siwema Hamoud Jumaa kwa kazi kubwa anayofanya pamoja na upungufu mkubwa huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu mara kadhaa tumekuwa tukijadili ni namna gani tutafanya shule zetu zifanye vizuri, lakini mara kadhaa amekuwa akihangaika kufikiri namna gani anaweza akaweka vizuri ikama ya walimu. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri ndugu yetu aangalie namna ambavyo anaweza kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme jambo la mwisho ambalo ni muhimu sana kuhusu pikipiki za watendaji. Tulikubaliana hapa kwamba watendaji wote wa kata wawe na pikipiki. Jografia ya Chemba ni *complex,* kipo kijiji ambacho kitongoji chake kiko kilometa 50. Ili mtu atoke kwenye kitongoji aje apate saini ya Mtendaji wa Kijiji lazima asafiri na alale huko. Sasa tunaweza kuangalia hali halisi ilivyo. Mtendaji wa Kata hana usafiri. Mnaweza kuangalia namna gani wanaweza kufanya kazi. Ni kazi ngumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, zililetwa pikipiki nane wakati watendaji wapo 26. Unaweza ukaona zaidi ya watendaji 18 hawana pikipiki na hawana usafiri nao ndio wanaofanya kazi zote na jiografia ni mbaya. Kwa hiyo, nawaomba sana kwenye hiyo bajeti ambayo imewekwa kwa ajili ya vifaa, naomba na Chemba walau tununuliwe pikipiki kwa ajili ya watendaji wetu ili nao wafanye kazi ya Serikali vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nachukua nafasi hii kuwashukuru sana kwa nafasi. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa George Kakunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Mpina na Mheshimiwa Waitara ajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili nami nitoe mchango wangu wa mawazo ya namna ya kuendeleza Sekta hii ya Utumishi na Utawala Bora. Kwanza, nianze kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anaendeleza amani, utulivu, mshikamano, umoja, uhusiano wa kimataifa pamoja na kuendeleza miradi mikubwa na miradi midogo katika nchi hii. Majimbo yetu yote yana ahueni kubwa, na sekta zote Mheshimiwa Rais anazigusa.

Mheshimiwa Naibu Spika, umahiri wa Mheshimiwa Dkt. Samia katika uongozi ni wa kupigiwa mfano siyo katika nchi ya Tanzania tu, bali duniani. Ndiyo maana siku ya tarehe 10/10/2023 katika Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru cha India kilimtunukia Mheshimiwa Rais Samia Shahada ya Heshima ya Udaktari wa Falsafa kwa kutambua mchango wake katika maendeleo ya Tanzania. Huyu alikuwa ni kiongozi wetu wa pili kupewa heshima hiyo baada ya Rais Dkt. Julius Kambarage Nyerere mwaka 1995.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana tarehe 18/04/2024 katika Chuo Kikuu cha Ankara Uturuki, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alitunukiwa *Ph.D* ya heshima kwa kutambua jitihada zake katika kuendeleza mageuzi ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kupitia zile *4R* zake, zimetambulika Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukashangaa kwamba kuna baadhi ya watu hapa hapa nchini wanaweza wakawa hawatambui umuhimu wa uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini dunia inatambua. Kuna watu hapa Tanzania walikuwa hawapumui kisiasa. Sasa hivi wanapumua, wanafanya mikutano na kila kitu, na wamekiri hadharani. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kumpongeza Rais wetu kwa namna ambavyo anatimiza majukumu yake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na timu yote ya Wizara hii kwa

namna ambavyo wanaendeleza weledi, umakini, uadilifu na uaminifu kwa Rais pamoja na nchi yetu. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushauri katika maeneo machache. Eneo la kwanza ni kwenye Serikali mtandao. Katika Serikali mtandao nimkumbushe Mheshimiwa Waziri na Serikali kwamba, mwaka 2003 Serikali ilipitisha *secular* kwamba watumishi wote wa Serikali lazima wawe na anuani ya barua pepe ya *internet* kwa ajili ya mawasiliano ya Serikalini ili kutunza siri za Serikali hasa wanapo-*share documents.*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hilo bado tumeonesha udhaifu mkubwa. Watumishi wengi wa Serikali bado wanatumia anuani za *Gmail* na *Yahoo* kwa ajili ya matumizi ya ofisi. Ni jambo ambalo Serikali inatakiwa ifanye tathmini kuona ni kwa nini nchi nyingine zimeweza na kwa nini sisi tumeshindwa kudhibiti hali hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka nilizungumze kuhusiana na Serikali Mtandao ni mifumo ya kuratibu utendaji Serikalini. Kuna wakati hata Mheshimiwa Rais aliagiza ipunguzwe, lakini bado ipo mingi. Mfano, mifumo ya ununuzi, mifumo ya mapato, mifumo ya ufuatiliaji na tathmini na mifumo ya kupeana taarifa. Iko mingi sana, kila sekta ina mifumo yake tena ni mingi, ndani ya sekta mifumo mingi. Mratibu wa suala hili ni Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Sasa mifumo hii itapunguzwa lini na isomane? Hili ni jambo ambalo naamini Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atatueleza mikakati iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo ambalo napenda nichangie ni kuhusu utumishi wa umma. Kwenye eneo la ajira, kwa jinsi tunavyoajiri wale wanaoomba ajira Serikalini na kwenye vyombo vyetu vya umma, kuna tatizo ambalo linatakiwa lifanyiwe kazi. Kidogo wale wanaoomba ajira wanalalamika kwamba uwazi ni mdogo, ndiyo maana mpaka Wabunge wamelalamikiwa kwamba Mbunge fulani hajanisaidia mimi kupata kazi. Ni kwa sababu uwazi ni mdogo, wanahisi kwamba Mbunge anaweza akamwambia Waziri, bwana, kijana wangu huyu mpe kazi akapata kazi. Kumbe siyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, eneo hili la ajira naomba, licha ya juhudi mbalimbali ambazo zimefanyika lifanyiwe mapitio makubwa ili kuongeza uwazi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu mikataba ya utendaji wa kazi, *OPRAS*. Wakati wa kuanzisha *OPRAS* ilipigiwa debe sana na ilikuwa nzuri sana. Wakurugenzi walikuwa wanasaini na watumishi wao na Makatibu Wakuu walikuwa wanasaini na Wakurugenzi. Ilifikia wakati mpaka Mawaziri walitaka kusaini hiyo mikataba ya kazi. Sasa *OPRAS* baada ya miaka mingi, je, ni ni lini ilifanyiwa tathmini kubwa? Je, imekuwa na tija na ufanisi gani katika utendaji wa kazi? Ni jambo ambalo natoa wito Serikalini wafanye mapitio makubwa ili kuhakikisha kwamba hii mikataba ya kazi inakuwa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la tatu ambalo napenda kushauri ni kusimamia maadili ya utumishi wa umma. Tunayo Sekretarieti ya Maadili, hivi kazi yake ni kutusimamia tu sisi kujaza fomu za maadili? Kwa hiyo, tukishajaza fomu za maadili, basi! Kwa nini wasiende mpaka kwenye sehemu za kazi wakaangalia, hivi maadili yanaendeleaje kwenye sehemu ya kazi? Nadhani lazime kuwe na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ambao utahakikisha kwamba mambo haya yanakuwa yanasimamiwa kwa maadili tangu ujaze fomu na jinsi unavyofanya kazi za kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili kuhusiana na suala la maadili ni TAKUKURU. Kupitia sheria TAKUKURU tuliwapa meno makubwa sana, lakini kadiri siku zinavyoenda wale watu wetu wa TAKUKURU ni kama vile wanapotea potea hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, anaonekana Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU Kitaifa, lakini Mkuu wa TAKUKURU wa Wilaya na Mkuu wa TAKUKURU wa Mkoa ni kama vile wanapotea hivi kiasi ambacho inakuja kuonekana kwamba kunapokuwa na *issue* imetokea unakuta amekuja Waziri Mkuu, ndiye anayeibua mambo, lakini TAKUKURU wapo. Anakuja *CAG* ndiye anayeibua mambo, lakini TAKUKURU wapo. Zinakuja Mbio za Mwenge ndizo zinaibua mambo ilhali TAKUKURU wapo. Je, kwa nini wanapotea? Ni jambo ambalo inatakiwa Mheshimiwa Waziri aliangalie ili kama wanahitaji msaada, basi waweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la nne ni *TASAF*. Bila kupepesa macho, hata Waheshimiwa Wabunge wengi walilizungumzia wakati wa kuchangia kwenye hotuba ya Waziri Mkuu kwamba kwenye eneo hili la *TASAF* kuna malalamiko mengi sana. Watu wengi wanaolalamika ukiwakuta, ni kweli walistahili kuwemo kwenye mpango wa *TASAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichunguza kwa undani, unakuta kweli kuna watu wengi ambao hawakustahili kuwemo kwenye mpango wa *TASAF* lakini wamo. Kwa hiyo, ni jambo ambalo naomba Serikali isitishe mpango wa *TASAF* mpaka wafanye mapitio makubwa nchi nzima ili kuangalia nani alistahili na nani hakustahili, kisha waweke utaratibu mpya ambao utaondoa hayo malalamiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni kuhusu usimamizi wa uwiano wa watumishi katika maeneo yetu mpaka leo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ni kengele ya kwanza. *(Makofi/Vicheko)*

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo kuna baadhi ya mikoa ina ziada ya watumishi na kuna baadhi ya mikoa ina upungufu mkubwa wa watumishi. Kuna baadhi ya halmashauri zina ziada ya watumishi, kwa mfano walimu. Hivi ni nani anasimamia uwiano wa watumishi hapa Tanzania? Ni Wizara hii! Naomba ifanywe *study* kubwa kuangalia mtawanyiko wa watumishi katika nchi yetu ili baadaye wapendekeze namna ya kuweka *balance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa, huko nyuma kulikuwa na mipango mikakati *(Strategic Plans)* na mabingwa wa *strategic plan* walikuwa wanatoka Ofisi ya Rais, Utumishi. Wanasimamia *strategic plan* kila Wizara, halmashauri na mkoa, lakini sasa hivi ni kama vile wamepotea, kama hawapo. Naomba, kwa sababu jambo hilo ni zuri katika tija ya utendaji kazi Serikalini, ni muhimu nalo lirudiwe kama lilivyokuwa zamani ili mambo yetu yaende kuwa mazuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mpina, atafuatiwa na Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Kanyasu ajiandae.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipa ili niweze kuchangia hii hotuba muhimu sana ya Ofisi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambapo kwa kweli ndiyo *engine* ya utekelezaji wa shughuli zote za Serikali na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wenzangu wote ambao wamewapongeza sana watumishi wa umma wa nchi hii kwa kazi nzuri sana wanayoifanya wakiongozwa na mtumishi namba moja, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo anaendelea na shughuli za umma usiku na mchana. Pamoja na changamoto zote wanazozipata, tunawaombea na tunawatakia kila la heri katika majukumu ya kuliongoza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto nyingi katika mifumo ya utekelezaji wa shughuli za umma na dhana ya utawala bora. Ukisoma Ilani ya Uchaguzi ile sura ya sita halafu ukaangalia na utekelezaji wa shughuli za Serikali zinavyoenda, utaridhika na utabaini kabisa kwamba matukio haya yote yanathibitisha nchi yetu tayari ilishaacha utekelezaji na uzingatiaji wa dhana ya utawala bora. Kwa sababu gani? Unaweza kuona kabisa matukio mengi ya uvunjaji wa katiba wa moja kwa moja na uvunjaji wa sera na kanuni na kutokuzingatia haki za binadamu unafanyika kwa uwazi kabisa halafu kila kitu kinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona kwamba kama Taifa ni lazima tuitafakari upya mifumo yetu ya kiutumishi wa umma na utekelezaji na uzingatiaji wa utawala bora ili tuweze kuona kwamba tuko wapi. Kwa kweli tusikubali hali hii ikaendelea kwa sababu kama itaendelea, nchi yetu hii ambayo inastawi vizuri, itaenda kuanguka na itakuwa *failed state*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni vita. Mwalimu Nyerere wakati anatangaza vita ya kumng'oa Nduli Idi Amin alisema maneno haya; "Tunayo kazi moja tu sasa Watanzania, ni kumpiga Nduli Idi Amin. Uwezo wa kumpiga tunao, sababu za kumpiga tunazo na nia ya kumpiga tunayo. Tunataka dunia ituelewe hivyo kwamba hatuna kazi nyingine na tunawaomba marafiki zetu wanaotuambia maneno ya suluhu waache maneno hayo."

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi katika kuirekebisha nchi yetu na kuiweka kwenye misingi ya utawala bora, ni vita ambayo ni lazima tuipigane sasa. Hatuwezi kuendelea kuruhusu dhuluma, wizi, ufisadi na rushwa hizo vikaendelea kufanyika. Dhuluma na uonevu wa baadhi ya sekta ambao unafanywa hapa nchini hauwezi ukavumilika. Watanzania wenzetu wanauawa na kuteswa halafu maisha yanaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkanganyiko wa mifumo ya utumishi wa umma, kuna mkanganyiko mkubwa sana wa mifumo ya utumishi wa umma. Hivi sasa, kwanza kuwepo kwa *parallel system* kunafanya kila mtu kuwa ni mkubwa na hivyo kunakosekana hata nani amwagize mwenzake. Kuna mwingiliano mkubwa sana wa madaraka katika utekelezaji. Hakuna *clear separation of power* ya watu, hatimaye watumishi wetu wanalumbana tu kule, hakuna mkubwa. *DC* analumbana na Mkurugenzi, Mkurugenzi analumbana na Mbunge, Mbunge analumbana na Mkuu wa Mkoa, Mawaziri na Makatibu Wakuu hivyo hivyo. Hatimaye tunakuwa na mfumo ambao ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia teuzi na baadhi ya ajira kutolewa bila kufanyika kwa ushindani, inatufanya kupata viongozi na watendaji dhaifu ambao wanashindwa kutekeleza majukumu yao na kumpa kazi kubwa Mheshimiwa Rais kila leo kutengua na kuteua. Ni kazi kubwa kusoma *CV* za watu ilhali kazi hizi zingeweza kutangazwa, Watanzania wenye uwezo wakapata hizo kazi. Kwa nini Waziri ateuliwe? Kwa nini asishindane tu kwenye *interview*? Kwa nini Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Wakuu wa Wilaya, na Wakuu wa Mikoa nao wasishindanishwe? Mwisho wa siku tungeweza kupata viongozi wazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata huu mfumo wa *vetting* hau-*guarantee* kuwapata Watanzania wote milioni 60. Huwezi ku-*guarantee vetting* unampata wapi? Unapendekeza huyu awe *DC* au Mkuu wa Wilaya, umempata wapi? Nani ameanzisha maombi? Yamepatikanaje kwa Mheshimiwa Rais maombi hayo? Kwa hiyo, tunajenga taifa ambalo hatuwezi kupata viongozi wazuri. Pia, mpaka sasa watu wamepewa nafasi, mfano nafasi ya ukurugenzi, baadaye anakuja kutenguliwa...

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** ...mshahara unabaki ule ule.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya mambo yanatupa tabu sana, lakini mfumo huu wa utumishi...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina kuna Taarifa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** ...umetufanya pia hata kupata watumishi ambao siyo raia wa Tanzania.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina Kiti kikizungumza wewe unakaa kimya. Kuna Taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango mzuri wa Mheshimiwa Luhaga Mpina pamoja na mambo mengine amegusia kwamba Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wakuu wa Wilaya wanateuliwa teuliwa tu. Nataka nimpe taarifa kwamba Mamlaka ya Uteuzi kwa nafasi ambazo anataja ambazo naye amewahi kuteuliwa ni za Kikatiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tofauti kati ya kuhoji Katiba na kuhoji matendo, anachokihoji ni Katiba. Namtaarifu tu kwamba mamlaka hayo ambayo anayazungumzia kwa Mheshimiwa Rais ni

mamlaka ya Kikatiba, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika,...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpina si mpaka nikuite? Mheshimiwa Mpina taarifa hiyo unaipokea? *(Kicheko)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu tu ya muda, kwanza taarifa yake siikubali. Mimi nachangia hapa naye akipata nafasi ya kuchangia, atazungumza yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mfumo wa utumishi ambao unaruhusu mpaka watumishi ambao siyo raia wa Tanzania, mpaka viongozi ambao siyo raia wa Tanzania. Taarifa hii imeshatolewa na vyombo vyetu vya dola, na Jenerali Jacob John Mkunda Mkuu wa Majeshi ameshatoa taarifa hii, lakini Waziri wa Utumishi na Utawala Bora kwake hajaona kama hii ni changamoto wala hata hajazungumza. Suluhisho la tatizo hili ni nini? Hawa waliotajwa kuajiriwa na kuteuliwa na siyo raia wa Tanzania ni akina nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa changamoto ya muda, nizungumzie kuhusu kupuuzwa kwa maagizo ya viongozi. Viongozi wetu sasa hivi wanapuuzwa. Viongozi walioko juu wanaweza kuagizwa na kiongozi yeyote na wakapuuza maagizo yake. Mfano mzuri Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa aliwahi kuagiza hapa maelekezo 12 katika Bunge hili kwa watendaji wa Serikali hasa wale wa uhifadhi. Mpaka nikaja hapa Bungeni na vielelezo ikathibitishwa kwamba maelekezo ya Waziri Mkuu yamepuuzwa, lakini yale niliyoyakataa na yale ambayo hata Ofisi ya Spika ilithibitisha kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu inapuuzwa yanaendelea mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea kwamba baada ya kupuuzwa kwa maelekezo haya ya Waziri Mkuu, moja, walioyapuuza wangekuwa wamefukuzwa au Waziri Mkuu mwenyewe angekuwa ameshajiuzulu kwa sababu huwezi ukawa Waziri Mkuu halafu maelekezo yako yanapuuzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Esther Matiko na Mheshimiwa Emmanuel yule Mbunge wa Ngorongoro kweli mliongea kwa hisia kubwa sana na mchango wenu ulibubujisha machozi hapa Bungeni. Hongereni sana na Mwenyezi Mungu awabariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kuhusu kutokuwiana kwa taarifa ya uchunguzi na taarifa ya ukaguzi. Kumekuwa na shida kubwa *PCCB, DCI* na *DPP* wana taarifa zao na wakaguzi wana taarifa zao. Wakaguzi wanakagua na kubaini kila aina ya dalili ya wizi katika maeneo husika. Unaenda kwenye taarifa ya *PCCB* hakuna hizo taarifa za wizi. Hazijafanyiwa kazi mahali popote na hawasemi kama ni wizi au nini kilitokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2023 hapa, tuliona maeneo mengi ambayo yalikuwa yana ishara kubwa sana za ufisadi na rushwa kubwa kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere na hata *IPTL,* zaidi ya shilingi trilioni 1.4; tuliona kwenye *SGR* zaidi ya shilingi trilioni 3.4; tuliona kwenye deni la Taifa mikopo inachukuliwa bila ya kufuata sheria, zaidi ya shilingi trilioni 2.5; tuliona kwenye mikataba mingine ambayo fedha za umma zimetumika na mamilioni ya fedha yamepotea na wahusika wote wanajulikana. Ukienda kusoma taarifa ya *PCCB,* hakuna taarifa hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma malalamiko yanayowasilishwa na taarifa ambayo *PCCB* wanaifanyia kazi, ni kama asilimia sita tu ya malalamiko yaliyowasilishwa. Sasa hapo utazungumzia utawala bora! Hapo utazungumzia ushughulikiwaji wa rushwa? Kama kwa mwaka unapokea malalamiko halafu unashughulikia kati ya 6.7% mpaka 23%, utazungumzia utawala bora pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kesi tunazoshindwa mahakamani ni wastani wa 43% yaani kesi ambayo imechunguzwa, ina Ushahidi, *PCCB* wakajiridhisha, *DPP* akaidhinisha kwamba ni kweli tuna madai ya halali, mnaendaje kushindwa kesi mahakamani? Mpaka 43% ya kesi tunapoteza Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumeendelea kuwepo na mikataba ya siri, mikataba ya siri inafungwa hapa nchini, zaidi tuliambiwa hapa

kuna mikataba ya rasilimali 43 ambayo ilifungwa hapa, lakini Watanzania hatujaelezwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Mpina, ni kengele ya pili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko na Waziri wa Nishati anaomba kuwatangazia Wabunge wote kuwa leo saa 7.00 mchana pale tunapoahirisha Bunge, maonesho ya Wizara yake ya Nishati yanafungwa na mgeni rasmi ni Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria shughuli hiyo kwa umuhimu kwa namna Wizara hii ilivyosimamia na kutoa elimu kwa Wabunge na kusaidia na kupokea kero na kuzitatua kero za Waheshimiwa Wabunge papo hapo. Kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge tujumuike kwa pamoja kumsindikiza Waziri Mkuu kwenye kufunga maonyesho haya. *(Makofi)*

Sasa namwita Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Kanyasu hayupo, ajiandae Mheshimiwa Husna Sekiboko.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia katika Wizara ya Ofisi ya Rais, Utumishi. Nawapongeza Mheshimiwa Simbachawene na wenzake wote kwenye Wizara hiyo kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo muhimu ambayo nataka kupitia kwa haraka haraka. Eneo la kwanza ni TAKUKURU. TAKUKURU wamepewa jukumu kubwa sana la kwanza kuzuia rushwa, kuchunguza na kudhibitisha na hatimaye wale watuhumiwa waweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na uchunguzi usioisha katika maeneo mbalimbali, yaani siku hizi ikitokea kuna mradi fulani unashukiwa kwamba kuna rushwa, TAKUKURU wanaingilia kati, wanachukua mafaili, wanakaa nayo hata miezi sita mpaka mwaka mzima. Kwa hiyo, kazi imesimama, mradi hauendelei na uchunguzi hauishi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunaomba eneo hili ni vizuri

likafanyiwa kazi vizuri ili kama kuna tatizo mahali, hatua zichukuliwe, uchunguzi uishe, wanaowajibishwa wawajibishwe ili mradi uweze kuendelee na wananchi wetu waweze kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengi sana pale kwangu yako namna hiyo, yako *stranded* mpaka leo tunasubiri ripoti ambayo haijawahi kukamilika. Nadhani hilo ni muhimu sana kulifanyia kazi. TAKUKURU ndiyo ambao wangesaidia huu uchafuzi wa mazingira wa hali ya hewa ya kazi nzuri ya Serikali ya kwamba kila ripoti ya *CAG* ikitoka maana yake inasema kuna ulafi wa fedha, kuna fedha imeibiwa mahali fulani. TAKUKURU wanaweza pia kusaidia kupunguza hiyo. Tunajua anafanya kazi yake vizuri, tunamfahamu Mkurugenzi Mkuu ni kachero aliyebobea, tunamfahamu tulikuwa naye, ameanzia ngazi ya chini mpaka ngazi ya juu. Afanye kazi yake vizuri ili aweze kupunguza hayo malalamiko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni taasisi ya uongozi. Katika eneo hili tulitarajia taasisi hii ndiyo isaidie namna ya kutengeneza viongozi wa nchi. Sasa tunapoona kuna watu ambao wanapewa mamlaka makubwa baadhi ya maeneo, halafu ana-*mess up* katika utendaji, tunaanza kuona kuna ombwe katika eneo hili. Tunatarajia kwamba viongozi wetu kabla ya kupewa madaraka makubwa, nimeona kwenye ripoti hapa, kuna mafunzo kwa Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wanalalamika sana ugomvi uliopo kati ya ma-*DC* na Wabunge; na mgongano/ugomvi uliopo kati ya Wakurugenzi na Watendaji wengine katika maeneo yale. Yaani mtu anachukuliwa wa kawaida kabisa. Sawa, ana vyeti, amesoma, lakini kazi ya Ukurugenzi hakuwahi kuifanya. Tunatarajia kabla ya kukabidhiwa ofisi ya umma ni vizuri akapata *A, B, C* kupitia taasisi ya uongozi ili akienda pale atambue kwamba kuna wananchi wana haki zao. Waheshimiwa Wabunge ni viongozi wawakilishi katika maeneo yale, hivyo washirikishwe, ma-*DC* kila mtu afanye kazi yake vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba hawa watu wafanye kazi yao. Ni muhimu mtu amepata fursa ya kuteuliwa, lakini ni vizuri akapewa *A, B, C* huko anapoenda ili akafanye kazi vizuri katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ni eneo la *TASAF*. Wamesema wenzangu, lakini nataka niseme kwamba mimi sioni sababu kwa nini *TASAF* iendelee kubaki hapa Utumishi. Kwa nini isiende TAMISEMI? Kwa sababu watu wote ambao wanasimamia miradi ile, kwenda ku-*disburse* zile fedha na kadhalika, ni watu wa TAMISEMI. Kwa hiyo, mkienda kule kunakuwa na shida ya usimamizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza wananchi wanalalamika namna ambavyo wanapewa fedha zao. Wanachanganywa, wakati mwingine wanaambiwa kwamba fedha ipitia benki, wakati mwingine kwenye simu, simu wanaibiwa, wakati mwingine wanapewa kwa njia ya *cash*, wale ambao wanapewa fedha wanazikata makato. Sasa hili jambo ni muhimu likafanyiwa kazi. Hiki ni kitu ambacho kinasaidia watu ambao ni maskini wa hali ya chini sana, sasa umempa fursa ya kusaidiwa, lakini katika utekelezaji wake wanapata changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka tufanye ziada. Kuna upotoshaji mkubwa. Kuna mpango mmeupeleka kwamba wale watu wasaidiwe fedha ile ya *TASAF,* lakini wanafanya miradi ya kijamii. Sasa wanasema, inawezekanaje mtu ambaye ni mgonjwa, mtu ambaye ni maskini unamfanyisha kazi? Mimi naelewa kwamba analipwa fedha yake stahiki ile ya msaada, lakini pia kama ana nguvu ya ziada, au msaidizi wake atafanya kazi ya ziada apate fedha ya ziada. Kwa hiyo, watu wanapotosha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atoke ofisini na watu wake, watoe elimu, kwamba wanaofanya kazi miradi ya kijamii wala hawalazimishwi na kwamba fedha ambayo wanapata ya mradi, haina uhusiano na fedha ya kawaida ya ku-*qualify* ile ya mradi wa *TASAF*. Wanachanganya watu, tunaonekana sisi Serikali tunawatumikisha wagonjwa wa *TB*, wagonjwa wa Ukimwi, wazee sana, kitu ambacho wanapotosha. Kwa hiyo, ni vizuri hiyo ikawekwa *very clear* ili ikawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili pia la *TASAF,* ni vizuri Mheshimiwa Waziri na watu wake waende wakatambue wanaostahiki kupata hiyo fedha. Kuna wizi mkubwa, kuna majina hewa mengi, yaani wale watu ambao wana uwezo, wenye dhamana

wamechukua ndugu zao wamewaingiza kwenye Mfuko wa *TASAF,* wao ndio wanalipwa. Kila ukienda kwenye Mkutano wa Kijiji, Mbunge akifanya mkutano wanakuja maskini, vikongwe wanakuuliza hebu niambie Mheshimiwa Mbunge mimi na huyu ambaye anapata fedha, nani ana ahueni na afadhali? Ni vizuri hilo Mheshimiwa Waziri akalifanyia kazi. Wale ambao wanastahiki wapate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwamba, kama mtu amepata miaka mitano au miaka kumi a-*qualify*. Wahitaji ni wengi, hatuna uwezo wa kumlipa kila mtu. Mtu amekaa miaka kumi amejiendeleza, amejenga nyumba, ajengewe uwezo a-*qualify* ili wengine waweze kuingizwa kwenye mfuko na waweze kunufaika katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la nne ni ajira katika utumishi wa umma. Nataka kumwambia Mheshimiwa Waziri, ukweli ni kwamba unazungumza kwamba ajira ni *fair* lakini nataka kukwambia, tunapozunguka na kusoma watu wenye dhamana, kuanzia ngazi ya juu kabisa, tunaangalia hilo Baraza la Mawaziri, tunaangalia Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala, Wakurugenzi, ma-*DC*, *CMT*, na watumishi wengine kama Watendaji wa Kata, utaona kwamba kuna maeneo fulani; yaani kuna Mbunge hapa katika hizi nafasi zote za nchi hii ambazo kwenye Katiba zimetengenezwa, hakuna mtu katika wilaya yake au jimbo lake. Huo ndiyo ukweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kutuambia kwamba kuna u-*balance* wa utumishi, mlifanyie kazi. Kila Mbunge anataka watu wake wapate ajira. Kama ni kupata ajira ya jumla, kila nikienda mahali naona mbona ni eneo fulani wamejazana hapa. Kuna mjomba, shangazi, bibi, kaka; wao peke yao ndiyo wamesoma. Lazima tupeane nafasi hizi. Kwa hiyo, msaidie Mheshimiwa Rais na mamlaka kwamba watu wako wengi, mnapotoa zile ajira, kwa mfano mtu ameomba ajira ana miaka kumi mpaka leo ana-*apply,* ametembea mikoa yote hajawahi kupata ajira na wanalalamika mitaani. Hata mfumo mliotengeneza, Mheshimiwa Waziri katika jambo ambalo utakumbukwa na kuheshimika ni ku-*balance*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeomba hapa Bungeni, kama una ajira 17,000, si unipe watu 20 kwenye jimbo langu. Usinipe majina, lakini wapate kule na ndiyo maana hapo kuna shida ya utumishi. Kuna

watu sasa hivi wanaandika *address* kwa sababu wanataka ajira, anakuja unampa ajira. Mbunge anaambiwa umepata watumishi 20, baada ya miezi sita wote wamehama wanarudi nyumbani kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwenye majimbo ya vijijini imekuwa ni *address* ya kupatia ajira na Mbunge hana *say*. Sasa mtu anakwambia nimemfuata mume wangu, nimemfuata mke wangu, unafanyaje? Unanipa *figure* ya watu kufanya kazi, nawatangazia wananchi mtapata daktari, mtapata mwalimu katika eneo hili, baada ya miezi sita wote wamehama wamerudi nyumbani kwao. Sasa kumbe ungetakiwa ugawe tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli unabaki kwamba tunataka watu wapate ajira na vijana wengi wanalalamika. Tunataka ukitangaza ajira hizo, hebu tuone wametokea maeneo gani ili tuone kweli hiyo hali imekuwa sawa sawa. Mheshimiwa Waziri, huwezi kuwa unaajiri watu wanafanya kazi mpaka wanastaafu. Ukiajiri unakabidhi idara mbalimbali kwa mfano unapeleka TAMISEMI, unapeleka hapo Utumishi na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kushauri vizuri, kwa heshima, jambo la kikokotoo ni bomu. Nataka kurudia, suala la kikokotoo ni bomu. Ulipokee kwa heshima na Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba nisikilize hapa. Pokea jambo la kikokotoo na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na sisi Wabunge, mpelekee Mheshimiwa Rais ushauri wa kitaalam atoe *statement* kwa Watanzania, hilo ni bomu, mimi nimewashauri kwa sababu…*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, kengele ya pili.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Naam!

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, shikamoo. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tutakaporudi jioni panapo majaaliwa tutaanza na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, watafuatia Mheshimiwa Omar Ali Omar na Mheshimiwa Mohamed Said Issa.

Mheshimiwa Husna Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru sana kwa kupata fursa ya kuchangia kwenye Wizara hii muhimu kuhusu Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Naanza moja kwa moja kwa kuchangia upande wa utawala bora. Wote tutakuwa mashahidi namna ambavyo Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameleta mapinduzi makubwa katika utawala bora katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ni ile *philosophy* ya *4R* za Mheshimiwa Rais; *Reconciliation, Resilience, Reform* na *Rebuild*. Mheshimiwa Rais amekuja na falsafa ya kuhakikisha kwamba kwanza panakuwa na maridhiano kwenye nchi yetu. Pili, *resilience* kwa maana kunakuwa na umadhubuti na kuvumiliana. Vilevile, kunakuwa na mageuzi makubwa katika maeneo yenye uhitaji, na pia kunakuwa na kujenga upya yale maeneo yanayohitaji kujengwa upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa natoa mfano mmoja. Wakati Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anaingia madarakani, vyama vya siasa vilikuwa vimezuiwa kufanya mikutano, lakini baada ya muda mfupi Mheshimiwa Rais alikubali watu kufanya mikutano, vyama vyote vilianza kufanya mikutano, hata wale ambao wanapenda kuandamana wanapoomba kuandamana Mheshimiwa Rais amewaruhusu na wanafanya maandamano, japokuwa, muda mwingine wanashindwa hata kufanya maandamano yenyewe kutokana na kazi nzuri anayoifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hii inaonesha ni namna gani Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa katika kuhakikisha kwamba anasimamia utawala bora katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo napenda kuchangia ni kuhusu utumishi wa Umma kwa ujumla. Hapa, naanza kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. Ilani ya Uchaguzi ya 2025 inatamka dhahiri kwamba Chama Cha Mapinduzi kimewaahidi

wananchi kuhakikisha kwamba kitatetea, kitalinda na kujenga mtaji watu *(human resource/human capital)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa namnukuu mwanafalsafa mmoja anaitwa Claudia Goldin wa Havard University anasema; "*Human capital consists of knowledge, skills and health*," kwamba, mtajiwatu una vitu vitatu. Cha kwanza ni elimu, cha pili ni ujuzi, na cha tatu ni afya. Hapa nataka kueleza kwa namna hii, kwanza kwa nini *knowledge*? Kwa sababu tunahitaji mafunzo kwa watumishi waliopo makazini. Kuajiri mtumishi ni jambo moja, hata kama amefanyiwa *interview* namna gani, lakini muda unakwenda, mambo yanabadilika, mambo yanakwenda, yanakua.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtumishi huyu anapaswa kupewa elimu na ujuzi kuhakikisha kwamba anandelea kuenenda kulingana na uhitaji. Ujuzi wake unasaidia kuleta mabadiliko katika eneo ambalo anafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali, kwenye eneo hili tuhimize mafunzo kazini. Juzi wakati nachangia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, nilieleza hapa kwamba tunahitaji kuhakikisha hata wale ambao tunategemea kuwaajiri; kwa sababu, kwa mfano kwa sekta ya elimu, walimu tunaohitaji ni wengi kuliko walimu ambao wamehitimu, walioko mtaani. Sasa wakiendelea kuwa kwenye eneo ambalo ama wana-*practice*, wanajifunza au wanapewa *knowledge* ya namna fulani, tunakuwa na uhakika wa kupata watumishi ambao watakwenda kuleta tija inayokusudiwa kwenye Taifa letu. Pia wale ambao wameajiriwa, wanahitaji kupewa elimu *(knowledge)* ili waweze kufanya vema na waweze kuleta tija ambayo inakusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo hilo hilo, kwanini tunahitaji *health* kwa watumishi? Tunahitaji maslahi kwa watumishi ili angalau aweze kumudu maisha yake, aweze kusaidia familia yake, aweze kuwa na utulivu wa akili *(settled mind)* na utulivu wa mwili na nafsi ili aweze kutekeleza vizuri majukumu yake. Sasa hapa pamoja na kwamba Serikali imefanya vizuri katika kima cha chini cha mshahara, bado zipo kada ambazo kusema kweli ukiziangalia, ukiwalinganisha, wengine wanafanya kazi moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Polisi na Magereza; Polisi ana nafuu wanavyodai kwamba mshahara wake kidogo ana nafuu, lakini Askari Magereza ni kama amesahaulika kabisa. Sasa tuangalie namna ya kuoanisha kuleta usawa kidogo kwenye maslahi ya watumishi ili kuwatengenezea afya *(health)* na amani waweze ku-*settle* kwa ajili ya kutekeleza vizuri majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo kuna suala ambalo kadiri muda unavyozidi kwenda naona linazidi kuwa baya na pengine mwisho wa siku likatuletea athari kubwa zaidi kama Taifa. Uhamisho; ni kweli yapo maeneo ambayo tunafanya msawazo, maeneo mengine yana watumishi wachache mengine yana watumishi wengi. Lazima tufanye hivyo, lakini dunia na nchi yetu kwa sasa tuna janga kubwa la mmomonyoko wa maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya sehemu ambayo imechangia kwa kiasi kikubwa ni watoto ama kulelewa na mzazi mmoja au kulelewa na ndugu. Kukosa malezi ya pande zote mbili au wazazi wote wawili ni hali ambayo inaathiri sana watoto katika ukuaji wao na maadili yao na hata namna ambavyo wanaweza kukua na kwenda kujitegemea baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ushauri wangu kwenye eneo hili ni kwamba, kwa kuwa watumishi wetu na wenza wao, wanalazimika kuishi pamoja ili kuendeleza familia zilizo bora kwa ajili ya kutengeneza Taifa la kesho. Tusizuie uhamisho wa watumishi ambao wanawafuata wenza wao. Kumfuata mwenza iwe ni sehemu muhimu ya kuhakikisha kwamba mtumishi analindwa kwa lengo la kwenda kukisaidia kizazi kijacho kuwa na Taifa lililo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa mtumishi, tena wa ngazi ya chini kabisa, lakini nataka kukwambia, nimeanza kuishi na mume wangu baada ya kuchaguliwa kuwa Mbunge. Utumishi wangu wote zaidi ya miaka kumi mimi naishi Nachingwea, naishi Korogwe, na kadhalika, mwanaume yuko Dar es Salaam. *Imagine*, tulikuwa tunajenga familia ya namna gani? Kwa hiyo, hii haijanitokea mimi peke yangu, inawatokea watumishi wengi Tanzania. Watumishi wengi wanalea watoto wao ama na mzazi mmoja au na ndugu. Muda mwingine inafika mahali wanawatupia *boarding,* watoto wanaishi

kwenye mazingira ambayo hata hawana mahusiano mazuri na wazazi wao. *(Makofi)*

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Husna, kuna Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mchango mzuri wa Mheshimiwa Husna, lakini suala la uhamisho basi liwe pande zote mbili, kwamba pia wakati mwingine mwanaume naye ahame kumfuata mke wake. Ilivyo sasa ni wake tu wanahama kuwafuata wanaume. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Husna, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa naipokea na wakati mwingine hata mimi mume wangu angekuwa tayari kunifuata Nachingwea ningefurahi na ningeendelea na maisha Nachingwea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la…

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Taya, Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kufahamu, kwa sasa mume wa Mheshimiwa Mbunge amehamia hapa Dodoma na wewe au yuko Dar es Salaam? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Husna, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu *TASAF*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Husna mbona unacheka sana? *(Kicheko)*

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TASAF*.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Husna endelea. Mheshimiwa Waitara kaa chini unachukua muda wake.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kuzungumza na Naibu Waziri, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, nikamweleza kuhusu hali mbaya ya upatikanaji wa wanufaika wa *TASAF* kwenye Mkoa wa Tanga hususan kwenye Wilaya ya Korogwe. Nikamwonesha mpaka picha ya wazee wa zaidi ya miaka 90 ambao kwa bahati mbaya wale wazee hawakuwahi kuwa na watoto kabisa, lakini ndugu zao wote wameshatangulia mbele ya haki.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge pamoja na Wabunge watatu niliowataja mwanzo tutaongeza wengine jioni ambao watakuwa ni Mheshimiwa Eric Shigongo, Mheshimiwa Khadija Taya na Mheshimiwa Kanyasu baada ya wale watatu ambao niliwatangaza awali.

Nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Kama nilivyotaja asubuhi, tunaanza na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Omar Ali Omar na Mheshimiwa Mohamed Said Issa.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana nami kuweza kuwa mmoja kati ya wanaochangia katika Wizara hii. Nitazungumzia sana suala la ajira za Watanzania. Ninafahamu kabisa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri ninyi ndio mawakili namba moja wa kutetea haki za wafanyakazi. Mheshimiwa Waziri changamoto kubwa sana katika ajira ni shida kubwa ya walimu. Tumejenga shule, zahanati na hospitali, lakini bado tuna shida kubwa sana katika ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna vijana tunaowazalisha katika vyuo vikuu vya nchi hii ambao wengi hatujawaingiza katika soko la ajira. Ninafahamu kwa zaidi ya miaka mitano iliyopita huko nyuma ajira zilipungua kidogo, lakini tunashukuru kwamba mmeanza japo *speed* ni ndogo. Kuna shida kubwa sana ya ajira na bado nafasi za kazi zimekuwa chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu mwalimu anao wastani wa kufundisha watoto kiasi kadhaa katika darasa, lakini inafika mahali mwalimu ambaye anatakiwa afundishe watoto 25 anafundisha mpaka watoto 200 kwenye baadhi ya madarasa. Wenzangu wamezungumza hapa, wamesema kuna uwiano tofauti ambao haueleweki mmeupangaje, ipo mikoa mingine ina ziada ya walimu, ukienda maeneo ya mijini unakuta walimu wamezidi, lakini vijijini hawapo. Mheshimiwa Waziri tunaomba sana ulisimamie hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo walimu pamoja na wafanyakazi wa kada ya afya ambao wanajitolea kwa muda mrefu, yaani miaka miwili, mitatu mpaka mitano kwa sehemu nyingine. Tumewahi kuuliza swali hapa Bungeni kwamba, inakuwaje mtu anayejitolea kwa miaka minne au miaka mitano mnapoajiri ajira mpya yeye mfumo unamkataa? Tukatoa mawazo kwamba, ni lazima mtengeneze mifumo yenu. Kwa yule aliyejitolea, ajira inapokuja awe wa kwanza kuwa *considered* kwa sababu, kama angekuwa hafanyi vizuri, basi asingejitolea katika shule hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina mfano katika shule moja Wilayani Rungwe. Shule ya Ikuti, kuna walimu zaidi ya watano wanajitolea, wana mwaka wa nne sasa hadi watano. Tunaomba inapokuja ajira mpya mwafikirie kwa sababu tayari Afisa Elimu anawafahamu, Mkuu wa Shule anawafahamu, na wazazi tunawafahamu. Tunaomba mwapatie ajira hiyo waendelee kuliko anakuja mtu ambaye amesoma nyuma yake anapata, yeye mnamwacha.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumwongezea Taarifa mchangiaji kwamba, walimu hawa wengi ambao wamekuwa wakijitolea kwa asilimia zaidi ya 90 ndiyo ambao masomo yao yamekuwa yakifanya vizuri kufaulisha kuliko walimu ambao wako kwenye ajira rasmi. Kwa hiyo, ni kundi la kutazamwa kwa ajili ya kukuza uzalendo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipokea taarifa hiyo kwa kuwa ndiyo maisha halisi tuliyonayo katika vijiji vyetu, majimbo yetu na maeneo tunayotoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu malimbikizo ya madeni kwa walimu, maaskari na watu wengine wote ambao

wanahusika katika mambo ya ajira. Mheshimiwa Waziri, tunaomba mtu anayekuwa amefanya kazi, amehamishwa au amepandishwa daraja, alipwe sawasawa na stahiki yake anayostahili. Kuna watu toka 2013 wamepandishwa madaraja, wanaenda daraja la pili, wanaenda mpaka daraja la tatu, bado wanapata mshahara ule wa daraja walilokuwa mara ya kwanza. Tunaomba sana hili lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumelalamikia suala la upandishaji wa madaraja, mmeanza kupandisha madaraja. Basi ongezeni stahiki zao. Pia wanapokwenda likizo, kuna wakati mwingine mnawakopa, mnasema tutawalipa, inaenda mwaka wa kwanza, wa pili mpaka wa tatu. Hii siyo sawa kabisa. Tunaomba lisimamiwe hilo na watu hawa wapate stahiki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala la uhamisho. Leo hii imekuwa shida sana kwa wanandoa. Mwanandoa mmoja anaweza akawa yuko Dodoma, lakini familia yake kaiacha Kigoma. Tunapinga UKIMWI, tunapinga magonjwa ya kuambukiza, basi tunaomba watu wapewe nafasi ya kuungana na familia zao, waweze kutunza watoto. Maadili yanaharibika kwa sababu ya kutunzwa na familia upande mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba uhamisho uwe wa haki maadamu tu *documents* zinaonesha na vigezo vyote vinasimamiwa. Leo hii kupata uhamisho imekuwa ni shida sana. Inaonekana kama ni makosa. Ajira ni baraka na wala siyo laana. Tunaomba mwapatie watu hawa uhamisho, waungane na familia zao waweze kuendeleza Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Watanzania wengi wanalalamika kuhusu suala la kikokotoo. Japokuwa ni sisi tulipitisha hili suala la kikokotoo humu ndani, lakini leo hii lawama inakuja kwako Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri. Tunaomba mlitazame upya kwa sababu mwisho wa siku wananchi hawa hawa ndiyo ambao wanatupigia kura na ndio ambao wanaongeza uchumi wa Taifa hili. Basi mtoke kule mlikozidisha kwenye 33 angalau basi turudi kwenye 50 hawa watu waweze kupata haki yao kwa sababu tuliwahifadhia tukimaanisha kwamba mwisho wa siku hawa watu watakuja kupata uzeeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi leo hii nikistaafu nilipwe hela yangu, maisha yangu nitayajua mwenyewe, lakini ukiniambia utakuwa na maisha magumu baadaye, huko ni kuwafanya Watanzania hawawezi kujisimamia wenyewe. Tunaomba kikokotoo kirekebishwe, mkitengeneze kiwasaidie wanaotakiwa kupata hiyo stahiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utendaji kazi wa zamani, mtu alikuwa anafanya kazi anahamishwa baada ya muda fulani, lakini sasa hivi mtu anazoea anakaa miaka 20 sehemu moja ya kazi, anajijengea ufalme, anafanya mambo yasiyofaa kwa ajili ya mazoea. Tunaomba zile Sheria na Kanuni mlizokuwa mkizitumia zamani zirudi ili hawa watu wasizoee. Sijui ni kwa sababu ya kuogopa kuwalipa, lakini mwisho wa siku ufanisi unakuwa mbovu kwa sababu ni kijiwe, mtu anakuwa amekaa kwa muda mrefu sana. Tunaomba tafadhali sana msimamie hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, nitaunga mkono pale ambapo nitapata majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na Waziri. Kama yataniridhisha nitaunga mkono, yasiponiridhisha nitashika shilingi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Omar Ali Omar, jiandae Mheshimiwa Mohamed Said Issa.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nami kwa kunipa fursa ya kuchangia katika Wizara yetu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwanza sina budi kumshukuru *Allah Subhanahu Wa Ta'ala* aliyetuwezesha kufika hapa katika Bunge hili jioni hii tukiwa wazima na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kujielekeza kwenye mchango wangu kwa kuanza kuzungumza kuhusu mshairi mmoja ambaye alitunga shairi linasema Jeraha la Moyo. Alisema kwamba:-

"Moyo uliojeruhiwa, mengi huyafikiria,
Hufikia kuzidiwa, zitawalapo hisia,
Unaweza kuamua, lolote kujifanyia,
Ni rahisi kupagawa na kutoka kwenye njia."

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumza hivi kwa hisia kali. Nazungumza kwa hisia kali kwa sababu ya kikokotoo. Kikokotoo kama jina lake lilivyo, lakini kwa kweli linawakokotoa wafanyakazi ambao tumewatumia kwa muda mrefu sana. Wafanyakazi wamefanya kazi kwa miaka 30, 35, wengine ni waajiriwa wa Polisi, wengine ni Madaktari, Walimu kama mimi, kwa kweli wako katika hali mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wengine sasa hivi tunavyozungumza, kwa sababu ya kikokotoo, wanapumulia mashine, kuna wengine sasa hivi sukari inapanda kiasi cha kwamba, hawana maisha, lakini kuna wengine sasa hivi hawajui maisha yao yatakuwa yako wapi, wamebaki kuwa ombaomba hata chakula hawana, hawana cha kuvaa. Ukiwaangalia, unaweza ukamkuta mwalimu, daktari au mfanyakazi, anavaa kiatu kimoja chekundu kimoja cheupe. Unajiuliza, shida ni nini? Shida ni kikokotoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, hapa tumefanya kitu kibaya kabisa, ingawa tulipitisha sisi katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuna haja ya kuhakikisha kwamba sheria hii inaletwa tena kufanyiwa mabadiliko, tena mabadiliko ambayo yanaweza kusaidia kuhakikisha kwamba wafanyakazi hawa wanaishi katika hali ya raha na starehe. Unashangaa na unajiuliza, hivi kweli Mkurugenzi wa Manispaa au Mkurugenzi wa Halmashauri ambaye umemtumia miaka 30 ashindwe kuzitunza fedha zake ambazo umempa kiinua mgongo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni fedha yake, kweli ashindwe kuitumia wakati wewe ulikuwa unampa posho, unampa stahiki mbalimbali za wafanyakazi, lakini zile alikuwa anazitunza na anahakikisha kwamba zinafanya kazi vizuri na hakuna ubadhirifu wa aina yeyote. Aje ashindwe kutumia hela ambayo anaiendeshea familia yake? Naomba fedha hizi zirejeshwe kwa wafanyakazi ambao wametumika katika Taifa hili na kuhakikisha kwamba maisha yao na wao yanakuwa katika hali nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia Polisi sasa hivi, ndiyo ambao wanalinda nchi hii. Kwa kweli utawashangaa, nenda kaangalie hali walizonazo Polisi sasa hivi, ni mbaya. Ni wastaafu ambao wamekuwa ombaomba. Leo Kamishna wa Polisi analipwa kiinua mgongo chake shilingi 200,000,000, unampa shilingi milioni 60, kweli hii ni halali? Hii ni

haki? Shilingi 140,000,000 unazo wewe mfukoni, unamtunzia nani jamani? Mtu mzima anatunziwa pesa. Ikitokea akifa fedha ndiyo zimepotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi kweli ni mtu mzima gani mwenye akili timamu aliye na umri wa miaka 60 bado akili inafanya kazi, halafu unachukua hela unakwenda kumtunzia wewe? Serikali inatunza fedha za wafanyakazi ambao wamestaafu, kwa kweli hili ndiyo tunalolisema ndiyo hilo jeraha la moyo ambalo wafanyakazi wetu wanalo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niondoke hapo. Sasa naenda kwenye suala zima la ajira. Dada yangu Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kazungumza sana kuhusu ajira. Kwa kweli, tunasema kuna upendeleo wa ajira. Kwa nini tunasema hivyo? Kuna vijana wetu ambao wamemaliza chuo, wanatumikia Wizara ya Elimu, kwa mfano, wanajitolea. Vijana hawa hawalali, hawanywi, wanafanya kazi na watoto wetu, matokeo yanakuja mazuri na Tanzania tunajivunia kwamba tuna elimu bora, lakini unashangaa anakaa miaka saba hapati ajira. Halafu anakuja mtu anatoka *university, fresh* kabisa, leo yeye ndiye anapewa ajira. Huu si ni upendeleo! Upendeleo huu unatupeleka wapi? Kwa kweli hili naomba tuliingilie kati kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ajira 46,000 zitatolewa, naomba Mheshimiwa Waziri uhakikishe kwamba vijana hawa wanaojitolea wanapata ajira ili nao mwaongezee motisha waweze kuona kwamba kweli wanaitumikia nchi yao kwa weledi na uaminifu na pia wanapata stahiki zinazowastahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naenda kwenye Mfuko wa *TASAF*. Hiki ni kizaazaa, kwa sababu nia ya Mheshimiwa Rais ni kuhakikisha kwamba anawafanya Watanzania wawe na maisha bora. Kila mmoja aishi maisha ambayo yanamsaidia katika familia yake. Tuna familia zilizo duni kabisa. Familia zetu ziko katika hali mbaya, lakini jambo la kushangaza ni kwamba, utaratibu unaotumika kupata kaya maskini ambazo zinasaidiwa na Mfuko wa *TASAF* siyo sahihi, umeingiliwa na Masheha kwa kule kwetu Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheha sasa ndiye mwenye *say* kwamba huyu mpe, huyu usimpe. Kuna watu wako katika hali mbaya zaidi

kuliko hawa ambao sasa hivi wanapata fedha kwenye Mfuko wa *TASAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine tena la kushangaza ambalo kwa kweli linakera zaidi ni kwamba, kila siku fedha zinapungua. Kaya maskini inapewa shilingi 70,000, kesho unakuta zile fedha zimekatwa, inalipwa shilingi 30,000. Je, wale vijana waliokuwa wakihudumiwa na hiyo kaya wamekufa? Kuna kigezo gani kinatumika kukata fedha? Ukiuliza, majibu yao wanakwambia, aah, nenda, mambo haya yanatoka Bara bwana, siyo huku Visiwani, yanatoka Bara. Sasa kwa kweli, hili haliko sahihi. Naomba na hili lifanyiwe marekebisho. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed Said Issa, jiandae Mheshimiwa Eric Shigongo.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Bajeti ya Wizara ya Utumishi na Utawala Bora. Mimi nitazungumzia mambo matatu tu kwa leo. La kwanza, ni suala la ajira. Ajira za Muungano utaratibu wake siyo sawa. Kwa nini nasema hivyo? Siku nyingi huwa nasikia kuna kero za Muungano, lakini sijui zimepatikana vipi, kwa sababu kuna mambo mengi ambayo ni kero. Moja ni suala hili la ajira za Muungano katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ninalotamani hasa, kama kuna jambo la kutatua, basi Wizara ya Utumishi nayo ingekuwa ni Wizara ya Muungano. Kwa nini nasema hivyo? Ajira ambazo zinatoka kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwenda Zanzibar hazina mfumo sahihi. Wazanzibari hawazifahamu, wanasikia tu zimekwenda na watu wameajiriwa. Sasa jambo hili siyo zuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wazanzibari tunahitaji mfumo huu wa ajira utokee huku huku Wizara ya Utumishi ili Wazanzibari wajue tuna mfumo fulani ambao unatokea Wizara ya Utumishi Tanzania ambao tunaomba kuliko kwenda kule, watu wanachaguana, hajulikani nani kapata, unasikia tu ajira zimetoka, siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nahamia suala lingine. Mwishoni mwa mwaka huu tunakwenda kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na

mwaka kesho Mungu akipenda tunakwenda kwenye Uchaguzi Mkuu. Suala la Utawala Bora hapo litatamalaki. Kwa nini nasema hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokuwa kwenye uchaguzi sheria nyingi zinakandamiza na siyo kwamba sheria ni mbaya, ila watendaji. Natoa mfano mmoja; wakati wa uchaguzi watu wengi sana wanakamatwa na wanapelekwa Mahakamani. Kadhia inayotokea ni kwamba, watu wanaokamatwa ni wa vyama vya upinzani. Sasa nauliza, hawa watu wa CCM ni Malaika? Hawafanyi makosa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli jambo hili siyo sahihi kwa wananchi wote. Watu wanauawa, watu wanapigwa wakati wa uchaguzi. Suala la Utawala Bora linatakiwa lifanye kazi yake, kuwe na mizani sawa, isiwe huku ni hivi na huku ni hivi, hasa hili suala la kwamba sisi upande wa Zanzibar tunakuwa na vikosi vingi sana. Juzi Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi amesema kwamba, Jeshi linalinda mipaka, lakini wakati wa uchaguzi, hasa kwenye Jimbo langu la Konde, wanakuwepo. Sasa sijui wanakuja kwa mantiki gani? Ni mpaka au wanalinda uchaguzi? Jambo hili liwekwe sawa. Kama huku wanaolinda ni Polisi na sisi kule tusimamiwe na Polisi. Isiwe kwamba, hapa kuna kikosi kimoja, kule kuna vikosi 70, jambo hili siyo sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikitokea mtu ameuawa, wanaambiana aah, siyo Polisi, siyo Jeshi, siyo KMKM. Sasa tunashindwa kuelewa. Jambo hili ni lazima Serikali ibebe lawama na ituwekee mfumo kamili ambao utatufanya sisi Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla tusione kwamba uchaguzi ni balaa. Ninavyosema sasa hivi wananchi wa Tanzania wamevunjika moyo wa kuingia kwenye uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mfanye tathmini, mtaona watu ambao wanajiandikisha kwa uchaguzi kama itafikia ile asilimia ambayo ilitokea mwaka wa kwanza ule wa 1995 na 2000. Naomba mfanye tathmini hiyo halafu mje mlieleze Bunge hapa, kwa sababu watu wamekosa imani na Serikali juu ya usimamizi wa uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda kwenye suala lingine la hawa wanaomtukana Mheshimiwa Rais. Kwa kweli jambo hili mimi binafsi nalichukia sana. Ningetamani sana sasa hivi ningesikia kwamba kuna

hatua ambazo zimechukuliwa kwa watu hawa. Kwa sababu huyu ni Rais wetu wote, huyu ni mama wa watu, ukimtukana Rais umetutukana sote. Sasa sisi tunashangaa mtu anatokea huko kwenye mitandao anamtukana Rais, halafu hatuoni hatua ambazo zinachukuliwa. Kwa kweli jambo hili siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie wazi, mimi ni mpenzi mkubwa wa Mheshimiwa Rais na kama chama changu hakitasimamisha mgombea na hakuna maelekezo, basi nampa kura yangu Mheshimiwa Rais. Pamoja na kwamba CCM siipendi, lakini nitampa kura Mheshimiwa Rais kwa sababu anafanya kazi nzuri, anawatumikia Watanzania. Mambo aliyofanya sasa hivi sijaona Rais yeyote ambaye amefanya. Mheshimiwa Rais anafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hili lililotokea, napeleka lawama kwa kijana wa CCM, Mwenyekiti wa UVCCM kule Kagera. Kwa kweli matamshi aliyoyasema kama utawala bora upo, ningetamani awe ameshachukuliwa hatua. Ni jambo la kufurahisha Katibu Mkuu wa CCM amelitolea maelekezo jambo hili…

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nimjibu mwongeaji na nimpe taarifa kwamba Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi amelikemea, huo ni uzembe wa kijana mwenyewe na siyo wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Taarifa hiyo.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa naelezea hivyo hivyo, kwamba tunamshukuru Mheshimiwa Katibu Mkuu wa CCM kwa kulikemea jambo hili. Sasa ilikuwa ni nafasi ya vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kuchukua hatua. Kwanza wameshapata kibali kwamba hakuna mkubwa. Maana yake tunajua

Serikali ya CCM ndiyo inatawala. Sasa kama kuna hofu kidogo, basi hofu ya nini tena hapa?

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu kijana ni wa kuchukuliwa hatua tukaona mfano, kwa sababu mambo haya haya ndiyo yanamchafua Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa, amewatoa watu magerezani, amewasaidia matibabu. Sasa leo huyu anakuja kutamka maneno haya. Huyu ni mtu ambaye inatakiwa alaaniwe katika nchi hii na achukuliwe hatua. Nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Shigongo, jiandae Mheshimiwa Khadija Taya.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai ambayo ameniwezesha kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu leo kuweza kuzungumza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile namshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa mambo mema anayolifanyia Taifa letu. Kama sijakosea hesabu zangu sawasawa, leo ninapozungumza, amesafiri angani masaa 402, akienda huku na kule kutafutia riziki Watanzania na kuiunganisha Tanzania na nchi za nje katika kutengeneza mahusiano. Hakika anafanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Buchosa, nasimama hapa kumpongeza sana Rais wangu kwa kazi nzuri anayoifanya. Kwa wanaoelewa maana ya kusafiri kwa ndege masaa yote hayo angani ni jambo linalochosha sana, lakini hivi ninavyoongea, anatarajia kurejea nchini kutoka Uturuki. Kwa hiyo, nina kila sababu ya kumpongeza Rais wangu kwa kazi njema anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu. Pia nampongeze sana Spika wetu wa Bunge kwa mambo mema na anavyotuwakilisha kila kona ya dunia. Ametuletea heshima kubwa sana. Mara kwa mara huwa namwambia binti yangu, anasema yeye ni *role model* wake. Kwa hiyo, kama mwanangu anaangalia hivi sasa, basi ajue ya kwamba anatakiwa

awe kama Spika. Nitakuwa mzazi mwenye kujivunia sana nikiwa na mtoto kama yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nina mambo mawili tu leo na ninaomba niongee kwa utaratibu na nimemwomba Mungu anisaidie niweze kueleweka. La kwanza ni upande wa wafanyakazi wa nchi hii kwa sababu leo tunajadili Bajeti ya Utumishi, na la pili ni suala la rushwa na ufisadi katika Taifa letu kwa sababu tunazungumzia watu wa TAKUKURU.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la TAKUKURU, muda ukitosha kule mbele nitakuja kwenye suala la watumishi, maana limeshaongelewa na watu wengi. Nilisimama hapa wakati fulani akiwa anawasilisha rafiki yangu Mheshimiwa Ndumbaro akiwa Waziri wa Sheria, nikazungumza juu ya TAKUKURU ambao wanafanya kazi kubwa sana. Kazi yao ni njema, nimesoma ripoti leo ya *Transparency International,* wamepanda kidogo kutoka nafasi ya 38 mpaka nafasi ya 40.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hivi duniani TAKUKURU ina nafasi ya 87 kwenye ubora wa kujiepusha na masuala ya rushwa. Kwa kweli nina kila sababu ya kuwapongeza. Katika Afrika Mashariki, Tanzania ni nchi ya pili ikiongozwa na Rwanda. Kwa hiyo nataka niwapongeze sana TAKUKURU kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote, leo nina jambo linaloitwa *Security of Tenure*. Nilizungumza mara ya mwisho hapa nikasema, tunahitaji kum-*protect*, tunahitaji kumkinga Mkurugenzi wa TAKUKURU kwa maana ya *Security of Tenure*. Jambo hili linafanyika kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kulinda ajira yake, ajira ya Majaji na ajira ya *CAG*, kwamba ukishamteua *CAG* huwezi kumwondoa, labda kuwe na sababu ambayo imetajwa katika Katiba. Hata Rais akimteua *CAG* hawezi kumwondoa tu hivi akaamka asubuhi akaamua kumtoa. Kwa nini waliamua kufanya hivyo kwa *CAG? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yao ilikuwa ni kumpa uhuru *(Independence)* wa kufanya kazi yake bila kuingiliwa. Ndiyo ilikuwa sababu tumpe nafasi, tuilinde ajira yake. Ukimteua leo, huwezi kumtoa

kesho asubuhi. Kuna mchakato mrefu sana mpaka utengeneze *tribunal* ndiyo uweze kumwondoa na ushauriwe kama Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini jambo hili halifanyiki kwa Mkurugenzi wa TAKUKURU? Nataka Mheshimiwa Waziri ukija hapa unijibu, kwa nini hutaki kum-*protect* Mkurugenzi wa TAKUKURU? Kwa nini Wabunge hatuitishi sheria ije hapa Bungeni tuweze kufanya marekebisho ya sheria tuweze kum-*protect?* Kwa nini ni muhimu kum-*protect?* Kwa nini ni muhimu kulinda ajira ya Mkurugenzi wa TAKUKURU? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano, umemkamata leo mtu kwenye halmashauri yako, amekuja *CAG* amekagua ambaye ana-*deal* na wanasheria, halafu unamwita mtu wa TAKUKURU amkamate akamhoji amfikishe Mahakamani. *CAG* ana *protection* analindwa, akishatoka pale huyu mtu anakabidhiwa kwa mtu ambaye halindwi na sheria ambaye ni Mkurugenzi wa TAKUKURU.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna uwezekano na simaanishi katika nchi yangu, kuna uwezekano katika nchi nyingine wakubwa au watu wenye ushawishi kupiga simu na kumwambia achana na hiyo kesi, lakini huwezi kumwambia hivyo *CAG* kwa sababu analindwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni rahisi sana kumpigia Mkurugenzi wa TAKUKURU na kumwambia achana na hiyo kesi. Mkubwa ametuma ki-*memo* kimekuja, anatetemeka, anakuwa na hofu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nani asiyependa maisha mazuri? Ukishateuliwa tu Mkurugenzi wa TAKURURU, heshima inaanza siku ile ile, *Land Cruiser V8*, ofisi nzuri mpaka mjukuu wako kijijini anaitwa huyu ni mjukuu wa Mkurugenzi wa TAKUKURU. Nani yuko tayari kupoteza hadhi hiyo? Ikija *memo* mtu anasema aah, bwana ee, bora mimi nibaki na familia yangu. Ndiyo maana nasema kama *CAG* ambaye anafanya kazi *similar* kabisa na anayofanya Mkurugenzi wa TAKUKURU, ni lazima tum-*protect,* ni lazima tuilinde ajira yake kwa sheria na kwa Katiba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili siyo geni. Nitakusomea hapa baadhi ya nchi ambazo zimefanya hivyo. Kabla sijasoma hizo nchi nikusomee Azimio la Umoja wa Mataifa Ibara ya 6 ambayo imetamka

katika Ibara ya 6 (2) inasema; *"Each state shall grant the body or bodies referred to in paragraph one of this article the necessary independence, in accordance with fundamental principles of its legal system, to enable the body or bodies to carry out its or their functions effectively and free from any undue influence*." Umoja wa Mataifa wamesema, kuwe na chombo ambacho kinalindwa na sheria ambacho ni TAKUKURU, ifanye kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuachane na Umoja wa Mataifa, twende moja kwa moja Ghana. Ghana sheria yao Kifungu cha 4 na 5 wametamka hivi, *"The procedure for removal of commissioner and deputy commissioners shall be the same as that provided for the removal of a Justice of the Court of Appeal and a Justice of the High Court respectively."* Ghana wamesema kumwondoa Mkurugenzi wa TAKUKURU iwe sawasawa na mchakato ule wa kumwondoa Jaji. Hao ni Ghana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Seychelles* sheria yao inatamka hivyo hivyo. *Senegal* sheria yao inatakamka hivyo, kwamba kumwondoa Mkurugenzi wa TAKUKURU iwe ni mchakato mrefu. Kwa nini wanamlinda? Ili asiingliwe na mwenye mamlaka ili asiingiliwe na wenye ushawishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa huko kote ni mbali, hebu twende kwa jirani zetu Zanzibar. Naomba univumilie kidogo. Zanzibar ambayo ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sheria yao inatamka katika *article* ya 5 Kifungu cha 5, mimi siyo Mwanasheria, najua kupita pita kidogo inasema, "*In order to protect the integrity and independence of the authority, the Director General shall not be removed…*"

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nirudie. "…*shall not be removed from office, except for reasons and procedures laid down for the removal of the High Court Judge according to the article 95 of the constitution.*" Hapo ni Zanzibar, ni sehemu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo sawa kutokum-*protect* Mkurugenzi wa TAKUKURU, ni kama vile tumejitengenezea kamlango kwamba tunabana hapa kwa *CAG* halafu tukibanwa sana tunaenda tunachomokea kwa Mkurugenzi wa TAKUKURU, haitakiwi, haiwezekani.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, nawaomba, tumeaminiwa na Watanzania na wizi, ubadhirifu, rushwa zimechelewesha maendeleo ya Taifa letu, zimechelewesha maendeleo ya Afrika. Tuhakikisheni tunapambana na adui rushwa kwa nguvu zote na tuanze na sheria. Kazi yetu sisi Wabunge tumeletwa hapa kutunga sheria na kuishauri Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sheria hii irejeshwe na sisi tuweke kipengele kama walichoweka ndugu zetu wa Zanzibar ili tum-*protect* Mkurugenzi wa TAKUKURU.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili. Maneno yako mengine ni ya muhimu yaandike mpe Waziri sasa hivi.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Taya, atafuatiwa na Mheshimiwa Kanyasu na Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata fursa ya kuchangia katika Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Awali ya yote naomba nimshukuru tena Mwenyezi Mungu kila siku kwa kutuamsha salama na tukiwa na afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa muda wake anaoutumia angeweza kuwa na familia yake, lakini muda mwingi anafanya kazi kwa ajili ya Watanzania na sote tunaona na tuna-*appreciate* sana, atambue hilo. Kwa nafasi yake tunamheshimu sana na tunasema tena tunasimama na Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nishukuru Mhimili wa Bunge; Mheshimiwa Spika na wewe Naibu Spika, nawashukuru sana kwa sababu mnaendesha Bunge letu vizuri, mnatupa nafasi na fursa vijana leo hii ni mara ya tatu nachangia. Ahsanteni sana na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kwenye Ofisi hii ya Utumishi na Utawala Bora au Wizara hii ya Utumishi na Utawala Bora nataka nichangie mambo kadhaa. Naomba kwanza niwapongeze sana, mmefanya kazi nzuri sana. Mimi nikiwa Mjumbe wa Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria, mna mipango mizuri sana kiasi kwamba natamani sana tupate pesa za kutosha. Tupate pesa za kutosha vipi? Tupate pesa za kutosha kwa ajili ya kutimiza yale ambayo tumeyapanga katika mipango yetu endelevu tunayoenda kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano tu TAKUKURU kwa mwaka 2023/2024 wameweza kujenga ofisi tatu za mikoa. TAKUKURU hao pia wameweza kujenga ofisi saba za wilaya katika kipindi cha Mama Samia. Ni kipindi cha mwaka mmoja tu, TAKUKURU hawa hawa wameweza kuajiri watu 350. Ni hatua kubwa sana hiyo ambayo Serikali inafanya na tunawashukuru sana kwa sababu hizi ajira ni za watu wetu, ni za wananchi wetu. Sisi kama Wabunge tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiachana na TAKUKURU kwa mambo ambayo imefanya, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imeweza kusimamia *promotions* mwaka 2021/2022 watumishi 91,841 wamepata promotions. Mwaka 2022/2023 *promotions* 120,210. Mwaka 2023/2024 *promotions* watumishi 81,515 lakini mwaka 2024/2025 tunakadiria tutaweza kuwapandisha watumishi 219,000. Hizi zote gharama yake ni shilingi 789,615,000 na kuendelea. Hii ni hatua kubwa sana ambayo mmeifanya naomba niwapongeze sana Utumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, mmeweza kuajiri katika hiyo miaka, mwaka wa kwanza ule 2021/2022 mmeajiri watu 32,000, mmeajiri tena watu 30,000 kwa mwaka unaofuatia, mmeajiri watu 47,000 na mmekadiria kuajiri watu katika mwaka huu wa bajeti 2024/2025 watu 45,000. Mwenyezi Mungu awatangulie sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana mwanzo nilianza kusema kwamba hizi pesa tunazopitisha hapa Bungeni zifike kwenye hii ofisi, kwa sababu tunaenda kuhakikisha ajira za Watanzania zinaenda kupatikana. Tumsaidie Mheshimiwa Rais, tuhakikishe vipaumbele vya ajira vinakuwepo kwa sababu nchi yetu hii changamoto kubwa

iliyopo ni ya ajira. Ndiyo maana sasa hivi Serikali imekuja na utaratibu mzuri wa kuanzisha vyuo vya mafunzo ili watu waweze kujisimamia na kujiajiri ambayo ni hatua nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu ambao wamesoma maeneo mbalimbali na wameshatumia muda mrefu sana kusoma lakini ajira hakuna. Kwa hiyo, ajira hizi bado tunazihitaji pamoja na vile vyuo ambavyo vipo, tunavihitaji pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka nigusie naomba zile rufaa zinazotolewa na watumishi mzifanyie kazi kwa haraka sana. Jambo lingine naomba Ofisi hii au Wizara hii ya Utumishi na Utawala Bora, hakikisheni mnafanya tathmini ya kujua ofisi gani kuna wafanyakazi kiasi gani na kuna uhaba wa kiasi gani? Kwa sababu kuna ofisi ambazo wafanyakazi ni wengi zaidi ya ofisi nyingine ili iwe rahisi ninyi ku-*reallocate* wafanyakazi waende kwenye maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja hayo, nataka pia nigusie suala la uhamisho ambalo kila mtu hapa ameligusia na amelizungumzia. Kusema ukweli mimi kwenye hili nitakuwa tofauti na wenzangu, mnisamehe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mhubiri wa kutokuhamisha watu. Kwa sababu gani? Kwa sababu watu wanakosa ajira kwa muda mrefu, wanapopata ajira wanapangiwa maeneo ambayo kule kuna wananchi na hao wananchi wanahitaji huduma yetu. Hao wananchi wanahitaji huduma yetu jamani. Hivyo basi, kama wananchi wanahitaji huduma yetu, tunahitaji kuwatendea kazi, tunahitaji kuwatumikia, isipokuwa tu pale ambapo mtu atakuwa na sababu za msingi zinazomfanya ahame kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nitakuwa nimeeleweka kwamba, mimi siyo muumini wa kutaka watu wahamishwe maeneo kwa sababu ya matakwa yao, ila wahamishwe maeneo kwa sababu za msingi zinazowahitaji wao wahame. Kuna sababu za ugonjwa ambazo zinahitaji hospitali kubwa, basi mtu ahamishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kushauri jambo kwamba katika zile ajira ambazo mnatangaza, kwa nini msiainishe kwamba ajira hizi ni za mikoa hii ili wale watu wanaoenda kuomba wajue kabisa wanaomba kwenda kwenye hiyo mikoa, wasiombe kwa ajili ya kutaka kuingia ili wahame? Waombe katika Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hata wale wenye matatizo, wanaotaka kuhama, kwa mfano juzi kati kulitokea kesi moja kuna mtu anataka kuhamia Manyara na mwingine anataka kuhamia Dar es Salaam, hawa watu wawili waliweza kuwasiliana wakabadilishana. Ikitokea fursa kama hiyo Utumishi, pitisheni tu kwa sababu hawahitaji gharama zenu, wanahitaji kuhama kwa matakwa yao basi, msiingie gharama kama Serikali ya kuwahamisha mtu kama huyo ambaye anataka kuhama kwenda sehemu nyingine ambayo yeye anaona kwamba inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusema hayo, naomba pia niwashukuru sana Ofisi ya Utumishi na Utawala Bora kwa kuwa mmeweza kutengeneza utaratibu mzuri ambao unaenda kusaidia watu wenye ulemavu kwenye usahili kwa urahisi zaidi. Namaanisha nini? Pale mnapowaita watu wengi sehemu moja, mnatakiwa mtambue mahitaji ya watu wenye ulemavu. Tayari mmeweza kuainisha katika Kamati yetu kwamba mtaweka utaratibu maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu, kwanza wawe ni *first priority* kwenye *interviews,* pia kuwawekea maeneo maalum kwa wao kupumzika ili wasipate ile *pressure* kutokana na hali zao na ugumu wa mazingira kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niwapongeze sana kwa kujali hilo, na kwa sababu hii ni Serikali ya Mama Samia, Serikali ya Mwanamke inatambua, inathamini watu wenye ulemavu, pia utu wa binadamu. Kwa hiyo, hongereni sana kwa hilo. Hongera sana Mheshimiwa Waziri Simbachawene kwa ushirikiano wako, umefanya kazi nzuri sana na unashirikiana vizuri na Kamati yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu, atafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii.

**NAIBU SPIKA:** Jiandae Mheshimiwa Michael Mwakamo.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kuendelea kutupa afya na uzima wa kuendelea kulitumikia Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaanza kwa kusema kwamba, katika historia ya nchi yetu tulijitambulisha kote duniani kwa sera na mielekeo yetu kwamba hii ni nchi ya wakulima na wafanyakazi. Katika kujitambulisha hivyo, tulisimamia kazi zote za wakulima na wafanyakazi kwa kiwango cha juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme hapa kwamba bahati nzuri tunaye Rais ambaye ni msikivu, tena ambaye anajali. Unaposikia tunazungumza habari ya *4R* za Rais, haziendi katika jambo moja tu. *4R* za Rais zinaenda kwenye kila jambo, maana kuna watu wengine wanafikiri hizi *4R* zipo kwa ajili ya siasa tu, Tume Huru ya Uchaguzi sijui na nini, Hapana. Ni katika kila jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunapozungumza suala la haki za watumishi, haki za wafanyakazi waliopo kazini na wanaostaafu, tunazungumza jambo kubwa kwa mustakabali wa nchi. Kwa maana hawa wafanyakazi ndio wanaotafsiri kwa vitendo maamuzi ya Bunge hili, maamuzi ya Serikali, na maamuzi ya Rais. Ni hawa hawa mpaka maamuzi ya Mahakama ikihukumu mtu kwenda jela, ni hawa hawa wanaotafsiri maamuzi hayo. Kwa hiyo, ni lazima tuendelee kujenga mazingira mazuri kwa wafanyakazi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo malalamiko mnaendelea kuyafanyia kazi kama Serikali, lakini bado hamjafikisha sehemu nzuri malalamiko hayo. Ni haki za watumishi kuhama kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Hivi kuna haja gani ya kumhamisha mtu kama hamna fedha? Sioni haja kama hamna fedha msimhamishe mtu, maana mkimhamisha mnatengeneza deni ambalo halina sababu isipokuwa tu kwa mtu mwenyewe ambaye kaamua kwamba mimi niko tayari kujihamisha mwenyewe, basi ahame na kwamba halipwi.

Mtumishi unamhamisha kwa mamlaka yenyewe ya Serikali kuamua halafu humlipi. Kwa hiyo, jambo hili nilitaka niseme kwamba katika kipindi hiki kinachoendelea, mjaribu kuendelea kuliweka sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hilo tu, mmefanya kazi nzuri katika suala la upandishaji madaraja watumishi, lakini bado wapo Maafisa Utumishi kwa makusudi anakwambia, jina la mtumishi fulani nililisahau. Ni lazima Wizara ichukue hatua kali kwa Maafisa Utumishi wa namna hii ambao wanafika mahali hawatendi haki kwa watumishi wengine. Mwingine anafanya kwa makusudi tu kwa sababu hawaelewani na mtumishi huyo, anasema jina lake lilisahaulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, heshima hii na hadhi ya mtumishi iende mpaka anapostaafu. Ni kweli tulikaa hapa tukaamua kwamba tukitazame kikokotoo tukakitazama, baada ya kuamua tumerudi kwa wananchi, tumerudi kupitia maamuzi yetu, tunaona kabisa kwamba maamuzi yetu haya kwa ujumla yana kasoro katika ustawi wa jamii ya wastaafu. Tumeliona hilo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais huyu ni msikivu na Serikali hii ni Sikivu. Zaidi ya hilo, sera zenyewe za Chama cha Mapinduzi zinataka kuwaangalia watumishi na wastaafu. Turudi tuyatazame yale maamuzi na kurekebisha. Najua Serikali hii haishindwi, tumeamua na kurekebisha mambo makubwa kama Azimio la Arusha, tumeamua na kurekebisha mambo makubwa kama sera yetu ya Serikali kumiliki njia kuu za uchumi, mpaka tukafika mahali tukasema Serikali sasa inabaki kuwa mhimili wa shughuli za uchumi, lakini njia kuu za uchumi zisimamiwe na sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeamua mambo hayo makubwa ya kisera, hatushindwi kurudi kutazama tena kikokotoo ili tukirudishe katika nafasi yake ya ustawi wa maisha ya wataafu. Jambo hili siyo jambo la kufumbia macho ni lazima tulichukulie hatua haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali kwa hatua iliyoichukua kuhusu *TASAF*. Kwa maana leo tunapozungumzia *TASAF,* ukimfufua mtu aliyekufa miaka 10 au 20 iliyopita, haijui *TASAF*. Ni Serikali hii imeona umuhimu wa kuwasaidia watu wa familia zenye kipato cha chini ndiyo ikaleta *TASAF*. Kwa hiyo, lazima tuishukuru

kwanza Serikali kwa kuileta. Hata hivyo, katika utekelezaji wa *TASAF,* tunakutana na changamoto ambazo lazima tukae kujadiliana na kuzirekebisha, lakini Serikali yenyewe kuleta jambo la *TASAF* ilifanya jambo kubwa na zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado kuna matatizo kwenye *TASAF* kwa upande wa ulipaji kwa wakati, vilevile ulipaji katika masuala ya usimamizi. Mwenyekiti wa Mtaa anasimamia kazi kubwa kwenye *TASAF,* lakini anazidiwa na mtu aliyeitwa kuja kusimamia kazi siku moja ya kuelekeza barabara. Kwa hiyo, lazima tuangalie katika ulipaji wa *TASAF,* namna gani tunawalipa hawa wasimamizi na namna gani tunalipa kwa wakati hawa ambao wanahusika na *TASAF* yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumzie, najua kwamba majeshi yetu kwa ujumla yanao utaratibu wake, lakini wanajeshi vilevile ni watumishi wa umma. Naomba Wizara hii ya Utumishi hebu jaribuni kukaa na Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara nyingine, muangalie hii kitu kinaiutwa *PGO*. *PGO* ipo tangu ukoloni, *Police General Order* kuna vitu mle vimepitwa na wakati kabisa. Askari wa cheo cha chini, nafasi yake katika kulitumikia Jeshi la Polisi kwa raha, ni ndogo sana. Anaambiwa kwenye *PGO* kwamba anapotaka kwenda likizo akabidhi nyumba. Sasa unakabidhije nyumba wakati familia yako ipo humo? Hayo yote bado yamo kwenye *PGO. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Askari anaambiwa, akiajiriwa ndani ya kipindi cha miaka mitatu asizae. Maana yake hata akipata mtu wa kumuoa leo hawezi kumuoa maana hatakiwi kuzaa ndani ya kipindi cha miaka mitatu. Haya mambo yote tuyatazame. Hivi yana ustawi katika utumishi wa sasa wa Jeshi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba sana Wizara ya Utumishi, ninyi ndio mnaobeba dhima kubwa ya masuala ya utumishi nchini, angalieni hizi Kanuni zote za Utumishi wa Umma ikiwa ni pamoja za majeshi, kwa sababu wanajeshi kwa nidhamu yao hawana mahali pa kulalamika, wasemaji wao ndio sisi. Mimi hapa hata nikisema sichukuliwi hatua na afande yeyote, niko huru. Kwa hiyo, tunawasemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni haki zao za uhamisho. Askari anakwenda uhamisho au likizo, anarudi, halipwi mwaka unaisha, mwingine unakuja. Hapa katikati tuliweka utaratibu mzuri kwamba Askari wawe na posho kila katikati ya mwezi ili kuwafanya wasipate dhiki, wakafikiria namna ya kuombaomba hela kwa wananchi. Nasikia ile posho mmeiondoa, mmeipeleka mwisho wa mwezi. Irudisheni katikati ya mwezi. Posho ile nia yake ilikuwa ni kumfanya Askari muda wote awe na pesa za matumizi ili asishawishike kuomba hela ndogo ndogo kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitaka Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara zinazohusika, watusaidie kurekebisha mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Michael Mwakamo, jiandae Mheshimiwa Ally Kassinge.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kwa kupata nafasi ya kuchangia leo Wizara ya Utumishi na Utawala Bora. Kwanza kabisa, nitoe shukrani kwa Waziri na Wasaidizi wake wote kwa namna ambavyo wanawajibika na kutekeleza majukumu ambayo wamekabidhiwa na Mheshimiwa Rais kwa niaba ya Watanzania. Hongereni sana, kazi mnazozifanya tunaziona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nina mambo machache sana. Jambo la kwanza, nina hakika kabisa jukumu la kupanga na kutumia rasilimali watu ni jukumu la Wizara hii japo wamekasimu majukumu haya kwenye Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kuwa jukumu mama la kupanga na kusimamia masuala ya kiutumishi yanakuwa kwao, japo wanayapeleka kule TAMISEMI kwa niaba ya kuwasaidia kusimamia, kuna mambo machache ningewaomba wayatazame kwa kina na waweze kutoa maelekezo ikiwezekana au kusaidiana na Wizara ya Utumishi kwenye kuyarekebisha ili mambo yakae vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo ningependa kabisa kulizungumza ni suala zima la kuwapanga watumishi kwenye vituo vya kazi. Leo nchi hii ina tatizo kubwa la watumishi kuwa wachache kuliko mahitaji yanayotakiwa nchini. Bado ukienda kwenye utaratibu mzima wa kupanga, yapo maeneo ya watumishi wengi zaidi kuliko maeneo mengine na madhara haya yanatukuta sana sisi wenye Halmashauri zinazoitwa za vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukaenda ukakuta vijijini huduma zile ambazo wanatakiwa wapewe wananchi katika maeneo yale, watumishi walio kwenye maeneo hayo ni wachache zaidi kuliko watumishi walioko kwenye maeneo mengine. Hii ni kwa sababu ya namna ambavyo wanapangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kwamba pamoja na uchache uliopo wa watumishi nchini, kama Wizara mbili hizi zitakaa chini na kupitia vizuri ikama za watumishi kwenye nchi yetu, wanao uwezo wa kuwapanga kwa mahitaji yalivyo na kukawa na uwiano unaoweza kufanana na ukasaidia utendaji wa kazi na hii kasi ya kuonekana kuna watumishi wachache ikawa ndogo sana. Kwa hiyo, naomba sana, kwa kuwa tunawaamini, ni imani yetu kabisa kwamba hili jukumu lao mama, kwa maana ya Utumishi wanaweza wakakaa chini wakaliweka vizuri na likaondoa changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli vibali vinatolewa na watumishi wanaajiriwa, lakini kila siku Wabunge tukisimama tunalia namna gani watumishi hawa bado wanaendelea kuonekana wachache kwenye maeneo yetu. Kwa hiyo, niwaombe sana watazame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwenye suala zima la kuwapanga, hapa ndugu yangu Naibu Waziri anaweza akawa na ushahidi. Wapo watumishi wanapangwa kwenye maeneo tofauti na *skills* walizonazo. Ushahidi huu Naibu Waziri anao, aliwahi kuja kufanya ziara jimboni kwangu, alikutana na vitu hata yeye alishangaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumkumbusha Naibu Waziri, lile ambalo alilishangaa Kibaha la kupangwa mtumishi ambaye kwa kweli mwenyewe ameona amepata taabu kufanya kazi kwenye halmashauri, walitazame na waweze kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nje ya hili la huyu wa Kibaha, nina hakika litakuwa lina watu wengi katika nchi hii ambao watakuwa wamewa-*site* katika maeneo ambayo hawawezi kuyafanyia kazi. Kwa hiyo, ni vizuri wawasikilize watumishi. Kama mtu wanamwona, maana unaweza ukafikiri kama mtu amepelekwa kwa adhabu, lakini mtu anaonekana ni mtaalamu wa masuala mazima ya manunuzi, anatolewa, anapelekwa kwenye eneo lingine ambalo hata ukimwuliza anashindwa kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri tunapozungumzia suala zima la kupanga watumishi, ni vema Wizara hii ya Utumishi kama jukumu lao mama, wawasilisane vizuri na TAMISEMI, wawapange watumishi kwenye maeneo ambayo wanaweza kuyafanyia kazi. Ipo mifano mingi na tunaweza tukaieleza hapa, na kwa kuwa bahati nzuri huu mfano ninaoutoa Mheshimiwa Naibu Waziri anaufahamu, basi ni vizuri akaufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo kwa kweli linaondoa morali ya kazi, ni Serikali na Wizara hii ya Utumishi inayowashauri watumishi wajiendeleze kielimu. Mtumishi anaamua kujiendeleza kielimu, anajitoa kwenye sifa za kuwa mtumishi wa kada fulani, kwenda kada nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, anatakiwa afanyiwe *recategorization,* lakini ukirudi kwenye muundo mtu huyu kama atalazimika kufanyiwa *recategorization* analazimika kurudi madaraja ya chini hata kama ameshalitumikia Taifa kwa muda mrefu. Matokeo yake anapoteza sehemu ya maslahi yake, kwa sababu tu ameamua kubadilisha kada ya utumishi kwa sababu ya elimu aliyoamua kujiendeleza nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni vizuri kwa sababu shughuli nzima ya Wizara ya Utumishi ni kulinda maslahi, nao ndio walitoa huu mwamko wa watumishi kuamua kusoma vitu vingine ili waweze kujibadilishia kada. Kwa hiyo, ni vizuri wakapitia ile sheria waone ni namna gani wanaweza wakairekebisha ili iweze kuwapa morali watumishi, anayeamua kubadilisha fani, aende kwenye fani ile kwa mshahara ambao alikuwa nao ili maisha yake yaendelee katika kiwango kile kile, kwa sababu suala zima la mtu kubadilisha kada,

anaweza akafanya hivyo kwa maana ya yeye kuangalia *career* yake anapendelea wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, kama mtu anakwenda katika *career* ambayo atafanya vizuri, siyo vibaya akienda huko na akaendelea kulindwa mshahara wake ili aendelee kufanya kazi vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza kwenye maeneo haya ya utumishi, tunasikia Wabunge wengi tunalalamika juu ya suala zima la watumishi waliostaafu kupata tatizo la kufungashiwa mizigo kurudi makwao. Nazungumza kwenye Wizara hii kwa sababu tu wao ndio wana jukumu zima la utawala bora. Mambo haya yanawaumiza watumishi wengi kwa matendo wanayofanyiwa kule wanapofanyia kazi kwenye Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta mtumishi amefanya kazi halmashauri fulani, anafikia umri wa kustaafu, anafanikiwa kupata mambo yake mengine, lakini suala la kuondoka kurudishwa kwao, ambako ndiko alikoandika alijaza kwenye fomu ya ajira ni mtihani. Matokeo yake, mtu anakata tamaa, anabaki ugenini, anakuwa mzee wa ugenini, anashindwa kurudi kwao, mambo yanakuwa magumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mifano mingi ya kutosha. Hata kwangu Kibaha Vijijini kuna orodha kubwa ya watumishi ambao wamestaafu na hawajasafirishwa kurudi makwao. Imekuwa ni kazi wakiamka kuja kwenye Ofisi ya Mbunge kumwambia tusaidie Mkurugenzi atulipe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unajaribu kujiuliza, kwani wakati anaajiriwa mtu huyu Serikali haikujua imemtoa wapi? Serikali haikujua anapaswa kurudi wapi? Kwa hiyo, mimi nalizungumza kwenye Wizara ya Utumishi nikiwa na maana kwamba wao ndiyo wasimamizi wa masuala ya utawala bora, ni vema wakasimama na wakawatazama waliowakasimia majukumu kama jukumu lao hilo wanalitenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda kulielezea hapa ni la *TASAF*. Nimezungumza na hapa kwanza nitoe

pongezi kwa Wizara na Naibu Waziri naomba pongezi hizi uzifikishe kwa Waziri kama ambavyo uliagizwa na Wazee wa Kibaha Vijijini. Ulipofanya ziara pale walikushukuru sana namna ambavyo uliwasaidia kufanya ukarabati wa ukumbi wao. Pia wakawa na ombi mbele yako, nafikiri unakumbuka. Ni imani yangu wakati utakapokuwa unatoa majibu, utaniambia ni namna gani wazee hawa hili ombi lao unaenda kulitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, waliomba uwasaidie namna ya kumalizia kufanya ukarabati wa jengo ambalo kwao ni kitega uchumi. Hapa naomba nitoe ushauri kidogo kwa Wizara hii. Tunawahudumia wazee hawa sasa hivi katika ule mfumo wa kufanya yale majukumu mepesi, kwenye ile miradi ya barabara, miradi ya kupanda miti na miradi mingine ambayo inakuwa imechaguliwa kwenye maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke wale ambao wanaenda kuifanya ile kazi tayari tuliwatambua ni wazee ambao wameshaishiwa nguvu. Kwa hiyo, tunapokwenda kuwapa majukumu ndiyo wapate fedha, bado tunafanya kosa ambalo kwa kweli haliko katika dhana ile ambayo tumewasaidia. Ni vizuri tungeendelea kuwajengea msingi wa kuwatengenezea maeneo ya vitega uchumi ili kitega uchumi kiwe kinawaingizia kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nitatoa ule mfano wa pale Kibaha. Nafikiri ameuona Naibu Waziri alipokuja. Wale wazee mliwajengea ukumbi wa mikutano kwenye ile miradi ya mwanzo kabisa. Pamoja na uzee wao, ule ukumbi unafanya shughuli mbalimbali na wanaingiza kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri tungeweza kufikiria kufanya hivi kwenye maeneo mengi kuliko kuwapa majukumu ya kwenda kulima barabara na wakati mnajua kwamba tunaowasaidia ni watu wazima ambao pia wameshaishiwa nguvu. Kwa hiyo, wanakwenda asubuhi saa kumi na mbili, saa moja wanaisha. Matokeo yake barabara wanazozitengeneza ukienda kwenye hesabu ya kawaida zinatumia gharama kubwa, afadhali zile gharama zinazotumika kule zingesimamiwa na *TARURA* zingekuwa na uwezo mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wazee wetu kwa lengo la kuwatunza tuendelee kuwatafutia utaratibu mzuri wa kuwasaidia katika hizi fedha za Mfuko wa *TASAF* ili waweze kubadilisha hali yao ya kimaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hili, ningeweza kutoa ushauri ufuatao; nimezungumzia suala zima la re*categorization*, nawaomba sana, ipitieni vizuri tena ile sheria, kwani inaondoa morali kwa wale watu ambao wanaamua kwenda kujiendeleza na wanapokuwa wanaondoka morali, mtu yeyote yule ambaye hamu ya kazi ikimwondoka kwa sababu ya ugumu fulani wa utendaji anapoteza uwezo wa kuifanya ile kazi kwa ubora aliyonao. Kwa hiyo, nawaomba sana, tuzingatie mambo haya ili tuweze kuwasaidia watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ally Kassinge, jiandae Mheshimiwa Justin.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii jioni hii ili nami nichangie Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ambayo inaongozwa na Waziri nguli, kaka yangu, bosi wangu wa kipindi hicho akiwa TAMISEMI, mwanasheria msomi kabisa Mheshimiwa Boniface Simbachawene, pembeni yake akisaidiwa na wakili msomi, mjomba wangu Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani mamlaka haijafanya makosa kuwaweka wanasheria wote wawili katika Wizara hii. Tunapozungumzia utumishi wa umma na utawala bora, tafsiri yake ni kwamba tutaongozwa mahususi kabisa na Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 na kanuni zake za mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tutaongozwa na sheria, ninaamini kabisa Mheshimiwa Rais aliona kwamba Mawaziri wawili hawa; Mheshimiwa Simbachawene na Mheshimiwa Kikwete wataweza kusimamia vyema sheria zinazoongoza Wizara na

zinazoongoza utumishi wa umma katika Tanzania hii ili watumishi wa umma wapate haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, eneo langu la kwanza la uchangiaji niwakumbushe Wizara majukumu makubwa matatu ya uteuzi; ajira pamoja na nidhamu. Mamlaka za uteuzi, mamlaka za ajira na mamlaka za nidhamu wakati mwingine zinafanya kazi kwa kuingiliana, lakini wakati mwingine zinafanya kazi kila moja kwa nafasi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, naomba niweke wazi kabisa kwamba mtumishi wa umma anapoajiriwa, mamlaka yake ya ajira ndiyo inayotakiwa isimamie taratibu zake zote kuanzia kuajiriwa kwake, kuendelezwa kwake, haki zake, mpaka kustaafu. Hiyo haina mjadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma sura 298, ndani yake zipo mamlaka za nidhamu na mamlaka za ajira. Inatokea wakati mwingine kwa bahati njema kwa baadhi ya watumishi wanaofikia katika *principal levels*, wakati wengine hata katika *senior levels* za vyeo vyao wanapata bahati ya kuonwa na mamlaka za uteuzi wakateuliwa kwenye nafasi mbalimbali kutumikia utumishi wa umma, kwa nafasi kama vile Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri au Mamlaka za Serikali za Mitaa, Makatibu Tawala wa Wilaya na kadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa inapotokea mamlaka ya uteuzi ambapo katika hizo nilizozitaja nyingi katika hizo mamlaka zake za uteuzi ni Mheshimiwa Rais, zimeteua hao watu ambao wametoka katika utumishi wa umma wakatumikia hizo nafasi, utumishi wao wa umma unabaki pale pale na stahiki zao na haki zao zipo vilevile, haziwezi kubadilishwa kwa namna yeyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni bahati mbaya sana na ni masikitiko makubwa kwamba mamlaka za uteuzi, na hapa niseme tu Mheshimiwa Rais inapotokea kwamba anatengua nafasi za uteuzi za watumishi hawa walioteuliwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, imekuwa na kizungumkuti kwa kuhakikisha kwamba wanalinda ajira za watumishi hawa kuanzia mwanzo. Hii ni

changamoto kubwa. Imeonekana mtumishi wa umma anapoteuliwa kushika nafasi za uteuzi na baadaye mamlaka ikatengua, ni kana kwamba ameadhibiwa na hana haki nyingine yeyote ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuishukuru Serikali, tumelipigia kelele hili kwa uchache wameliona, wale wote ambao waliteuliwa na wakatenguliwa walirudishwa kazini, lakini nitoe ushauri kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ipitie *database*, bado wapo. Wengine imefikia hatua wanakaa *pending* baada ya kutenguliwa kwao zaidi ya mwaka mmoja, miaka miwili mpaka wanakwenda kutafuta haki zao Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifano tunayo na ndiyo maana tunasema kwamba bado wapo, na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ikapitie hizi *database*. Haipendezi mtumishi wa umma ambaye anaajiriwa kwa Sheria za Utumishi wa Umma ana haki zote halafu akatafute haki Mahakamani, haipendezi. Hilo ni eneo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni maslahi ya watumishi kuendana na majukumu yao. Hapa kwa upekee wake nakusudia kuzungumzia walimu. Kwa muktadha wa mchango wangu nakusudia kuzungumzia walimu wale ambao wapo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa maana ya walimu wa shule za msingi na walimu wa sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, tungekuwa tunaangalia maslahi ya utumishi kwa mujibu wa majukumu yao, nadhani walimu wangekumbukwa kama wanavyokumbukwa watumishi wengine. Imekuwa bahati mbaya sana kwamba watumishi wa kada ya ualimu kwa kiwango kikubwa wanakuwa wakiishi kwa mishahara tu, wanategemea mishahara pekee ambayo mwisho wa ajira yake ndiyo unakuja ule mzigo au msalaba ule wa kikokotoo. Hii kidogo inasikitisha kwa kada ya ualimu ilhali wa kada nyingine wanapata maslahi ya kujikimu ili siku ziende. Wapo watumishi ambao wanapata *Rational Allowance*, wapo watumishi ambao wanapata *Responsibility Allowance*, *On Call Allowance* na *allowance* kama hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwakumbushe kwa unyenyekevu mkubwa sana Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma,

tufanye kitu kinachoitwa *job analysis* kwa mwalimu, tuchanganue majukumu ya mwalimu. Mwalimu ana jukumu la kufundisha, lakini katika kufundisha huku kabla ya kuingia darasani ana jukumu la kuandaa Mpango Kazi wa Mwaka na wa Muhula; ana jukumu la kuandaa utaratibu wa kufundisha darasa hilo kwa siku hiyo ya kipindi husika ambayo ndiyo *Lesson Plan.* Pia kuna *document* zingine kadhaa za mapitio kwa mwalimu kama vile *Class Journal*, *Log Book*, anapitia *text books*, *reference books*, Kiongozi cha Mwalimu, kuandaa *teaching aid* na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiondoa majukumu ya msingi haya ya ufundishaji, Mwalimu pia amekuwa na majukumu mengine ya ziada ambayo naweza nikasema yamekuwa ni makubwa pengine hata kuliko kufundisha kwenyewe. Mwalimu anakuwa ni Mwalimu Mkuu. Mwalimu Mkuu tu peke yake ni jukumu tosha. Mwalimu anakuwa Mwalimu wa Zamu. Kusimamia zamu ni jukumu tosha. Mwalimu anakuwa Mwalimu wa Darasa, kusimamia darasa siyo mchezo. Mwalimu anakuwa Mwalimu wa Malezi, Mwalimu anakuwa Mwalimu wa Michezo. Kama ingekuwa walimu hawakufanya vyema katika kusimamia sekta ya michezo tangu shuleni, leo hii tusingewapata wachezaji mahiri tunaowategemea katika timu zetu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Mzamiru Yassin, Bakari Nondo Mwamnyeto, Fei Feisal Salum (Fei Toto); hawa wote wamekuwa wachezaji wanaotegemewa na timu zetu tunazozitegemea kwa sababu waliandaliwa vizuri tangu shuleni. Hayo ni majukumu ya walimu. Mwalimu amekuwa mwalimu wa uzalishaji; wote tumefundishwa hapa tulio wengi kwa umri wangu huu na wengi nikiwaangalia hapa tumefundishwa uzalishaji mali shuleni. Kwa hiyo, kwa ujumla wake Taifa lililopo sasa na Taifa lijalo ni matokeo ya kazi ya walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wanasimamia mpaka miradi. Wamekuwa na jukumu la kuwa wahandisi, wamekuwa na jukumu la kuwa mameneja; ni mzigo mkubwa kwa walimu. Sasa mimi naikumbusha Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Utawala Bora na Utumishi wa Umma, kwamba hebu wafanye *job analysis* ya majukumu ya mwalimu

na baadaye waje na kitu kinachoitwa *teaching allowance* kwa walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili kama sitapata maelezo ya mkakati wa Serikali kujiandaa na *teaching allowance* kwa walimu, nitakamata shilingi ya bosi wangu wa zamani Mheshimiwa Simbachawene. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nizungumzie kwa uchache sana kuhusu kikokotoo. Walimu hawakihitaji kikokotoo, na ndiyo kwanza wakati kimeanza walikuwa tayari kustaafu kwa hiari wakiwa na miaka 55 kwa kuchelea kikokotoo. Wengi walistaafu na miaka 55 wakati kinaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin, jiandae Mheshimiwa Waziri Katambi.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii nami kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa uhai nami niweze kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mambo mengi ambayo anaifanyia nchi yetu hata kwa kutangaza nafasi za ajira kwa vijana wetu ambayo itapunguza kwa kiwango fulani changamoto ya ajira kwa vijana wetu wengi waliopo kwenye maeneo tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, nawashukuru Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii. Hawa ni miongoni mwa wachache sana waliowahi kutembelea Kilolo tangu nimekuwa Mbunge kwa nyakati tofauti. Jimbo la Kilolo halipokei Mawaziri wengi wala Naibu Mawaziri, lakini hawa wawili wote wameshafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimkumbushe Mheshimiwa Naibu Waziri, alipokuja alikuwa na ahadi yake kwa kupitia *TASAF* kukamilisha ujenzi wa zahanati mbili ambazo wananchi wameziibua. Zahanati ya

Winome na Zahanati ya Kijiji cha Mkalanga. Nimkumbushe ndugu yangu kwamba wale wananchi wanakumbuka ziara yake na wanajua akitoa ahadi huwa anazitekeleza; na kwa hiyo, na hiyo nayo ataitekeleza kama alivyokuwa ameahidi. Mimi nitaendelea kumkumbusha kila tunapoonana mpaka hapo atakapotimiza ahadi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie dhana ya kujitolea na jinsi inavyofanywa hapa Tanzania na athari zake kwa vijana wetu ambao wanajitolea. Tanzania ina baadhi ya kada ambazo zina mfumo wa *internship* kama udaktari, na lengo lake huwa ni kupata uzoefu, ina mwongozo, ina namna ya kupata posho na kwa kweli imeundwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo kwamba Tanzania hatuna uzoefu wa jinsi ya kufanya *internship*, tunao na tungeweza kujifunza kupitia madaktari. Kwa bahati mbaya mfumo huo Serikali haijataka kuuchukua kwa kada nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu tumekuwa kwenye Kamati ya USEMI tuliomba kwamba mwongozo utakaotengenezwa utoe fursa ya *internship* iliyokuwa *organized* vizuri, tangu upatikanaji wa watu kwenda kwenye *internship,* kwamba wanapatikanaje ili kuondoa uwezekano wa watoto wa walimu wakuu wa shule na watoto wa wenyeviti peke yao kupata nafasi za *internship*. Ili kuondoa upendeleo lazima kuwe na namna bora ya kupata watoto wa kujitolea kwenye hayo maeneo kwa sababu hata kujitolea huwa ni fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ukishapata mwongozo huo lazima kuwe na muda maalumu wa kujitolea na namna ya kuwapa motisha wale wanaojitolea. Sasa kama kwa mfano, Tanzania tungeweza kufanya kila halmashauri iwe na vijana angalau 100 wanaojitolea, maana yake kila mwaka tungekuwa na vijana 18,400 kwenye maeneo mbalimbali wanajitolea. Hao ni wengi na kwa hiyo, ingetosheleza kwa angalau kuwapa nafasi ya kupata uzoefu. Jambo hili tumelizungumza muda mrefu, lakini utekelezaji wake umekuwa kwa kuchelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mkiwa na *data base* nzuri ya kujitolea, faida yake ni kwamba, inapokuja wakati wa ajira

tusingekuwa na kizungumkuti cha kusema kwamba hatuwezi kutumia hii nafasi ya vijana kujitolea kwa sababu hatufahamu. Kwa sababu siku za nyuma imesemwa kwamba haitumiki nafasi ya vijana wanaojitolea kwa sababu inaogopwa kwamba vijana wanaweza ku-*forge* au wanaweza wakafanyaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi madaktari wanapofanya *internship*, daktari anaweza aka-*forge*? Kwa nini kwa mfumo ule ule isitumike kwa watumishi wengine kama vile walimu, sekta za afya za chini? Ili tuwe na uhakika kwamba huyo amejitolea, *assessment* zimefanyika na kwa hiyo, inapofika wakati tunasema huyu aingie kwenye ajira kwa sababu amejitolea, inakuwa inajulikana kabisa kwamba kweli huyu amejitolea na tathmini zake zipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema kwamba mwongozo huo upo, azingatie haya mambo, wanapatikanaje? Wanasimamiwa na nani? *Assessment* inafanywa na nani? Wanalipwaje? Baadaye, uwezekano wa *acceleration* ya wao kuajiriwa unakuwaje ili tuweze kuondoa changamoto hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ningependa kuzungumza ni kuhusu watendaji wa kata na watendaji wa vijiji. Hawa ndio ambao wanaonwa kwenye vijiji. Serikali za Mitaa kwa kiwango kikubwa ndio wanaotegemewa kuwahudumia hawa wananchi kila siku. Hata hivyo, kwenye maeneo mengi kuna upungufu mkubwa sana wa Watendaji wa Vijiji na Watendaji wa Mitaa na badala yake wanaokaimu ni baadhi ya viongozi kama Wenyeviti wa Vitongoji au wananchi wanaojitolea ambao uelewa wao dhidi ya kazi hiyo siyo mkubwa. Tukumbuke kuwa hawa wanakuwa na mihuri, wanakuwa wanaweza kukusanya baadhi ya mapato, na kwa hiyo, wanapopata mafunzo kwenye hivi vyuo vyetu huwa wanapata uelewa wa jinsi ya kufanya haya mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja pale Iringa mjini na ninajua aliona upungufu ule ulivyokuwa, lakini afikirie, je, kwenye zile kata zote, ni nani alikuwa anakaimu wakati wale watu hawapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii namna ya kukaimu hata hakuna mwongozo wa jinsi ya kukaimu, kwamba kama kijiji hakina mtendaji awepo nani? Kwa hiyo, ni mtu yeyote yule ambaye Mwenyekiti wa Kijiji ataona anafaa, basi huyo huyo ndiye atakaimu. Kwa hiyo, ilitakiwa kwanza kuwe na maelekezo maalum kwamba kijiji kama hakina mtu ni nani anakaimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kufanya haraka kuhakikisha kwamba vijiji vyote vina watendaji kwa sababu wanafanya kazi kubwa na muhimu sana kwenye hayo maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, hawa watu wanatoka kwenye vyuo, na siku hizi angalau unakuta mzazi amejitahidi, amejichanga changa amepata shilingi 350,000 kamnunulia *laptop* ili afanyie kazi. Wanapofika sasa kwenye ofisi zenyewe za kata na za vijiji hakuna *laptop*, hakuna *printer*, barua zinaandikwa kwa mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ni kwamba je, tumeshindwa kweli kutengeneza mfumo mzuri wa angalau kuhakikisha kwamba kuna vitendea kazi na teknolojia inayofaa? Umefika wakati kwamba hata wao wenyewe jinsi ya kufanya vitu kwenye halmashauri wanatakiwa wafanye kwenye mfumo. Sasa, unafanyaje kazi kwenye mfumo wakati kitendea kazi hauna? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri kuna haja ya Wizara hii na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuzungumza ili kuhakikisha kwamba angalau hawa watumishi, Watendaji wa Kata, Watendaji wa Vijiji, wanapata *laptop*. Kama Serikali ikiona kwamba zile mpya ni gharama, zipo *used* tutawaonesha, tutaenda tutanunua wapewe maana hata wakiwa kwenye vyuo walitumia hizo. Kwa hiyo, sasa anaporudi huku hawezi kuchukua ya nyumbani kwake aje atumie huku, hilo litakuwa limeboresha sana utendaji wao wa kazi, wataandika hizo barua kwa kutumia hivyo, wataweza kufanya hivyo vitu kwenye mfumo, lakini pia tutakuwa tumeboresha mazingira yao ya utendaji kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo nataka nizungumzie ni hili suala la wastaafu na mafao yao, hasa wakati wanapokwenda kudai na kukuta kwamba Serikali haikupeleka michango na hii inaweza ikawa ni halmashauri au idara nyingine yoyote ya Serikali. Halafu yule mtumishi anaambiwa yeye atoe hela

zake ili mishahara itimie ndipo alipwe mafao. Hili linafanyika na ushahidi upo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachofikiri ni kwamba, na yule mzee unakuta anastaafu, anazunguka, anaenda anarudi, ataenda *NSSF* sasa hivi mifuko imeunganishwa, ataenda na kwingine. Mimi nafikiri ni wajibu wa yule ambaye kwenye lile eneo analostaafu yule anayemstaafisha kuhakikisha kwamba huyu mzee mstaafu mafao yake yanapatikana na michango yake yote inapatikana badala ya kuwaacha hawa wazee ambao wamelitumikia Taifa, wanateseka kwa muda mrefu wakitafuta namna bora ya kupata mafao. Jambo hili kwa kweli linawaumiza sana wazee wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sidhani kama Serikali imeshindwa, pengine ni vizuri kufanya tathmini ni wastaafu wangapi sasa hivi michango yao haijapelekwa na ni nani alizembea? Kwa hiyo, aliyezembea apeleke, na wastaafu wanapostaafu waweze kupata mafao yao bila shida. Pengine ni vizuri, ni kweli kuna namna ya kusema mtumishi awe anakwenda kwenye mfuko kuangalia mwenendo wa mafao yake kila wakati, lakini pia ni wajibu wa mwajiri kuhakikisha kwamba anapeleka ile michango yake kila wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kila upande utimize wajibu wake, lakini inapotokea Serikali haikupeleka michango, basi mara yule mtumishi anapostaafu pengine kutengenezwe mfuko maalum utakaolipa yale mafao ili huyu mtumishi alipwe halafu ninyi mwendelee kumtafuta yule ambaye alikuwa hakupeleka hayo mafao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ambalo ningependa kulizungumzia ni wakati ambapo inatokea watumishi wanaomba kuhama hasa wale wanaotaka kuhama kwa sababu ya ndoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kweli wapo watu ambao unakuta anataka kutoka kwenye mojawapo ya Wilaya za Kigoma kule Buhigwe kuja Kilolo, tena vijijini, kwa sababu anamfuata tu mke wake au mume wake. Sasa zipo nyingi ambazo ni halisi, nadhani kumetokea dhana kwamba ndoa inatumika kama kisingizio cha kuhama. Kwa hiyo, hata wale halali hawahudumiwi na hawapewi umuhimu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri sisi sote tunafahamu umuhimu wa familia na tunafahamu umuhimu wa kuhakikisha kwamba hawa watumishi wanakuwa eneo moja, hasa pale ambapo hizo sehemu zote zina upungufu, kwa sababu anayehama kutoka kwenye kijiji…*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Justin, ahsante sana.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni jioni hii ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 38 wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ambao ni wanafunzi wa Chuo cha Mt. Augustino kutoka Jijini Mwanza, karibuni. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kuwapongeza kwa kazi nzuri hasa kuhakikisha kuwa baada ya muda mrefu watumishi wanapanda madaraja na kulipwa stahiki zao. Pamoja na changamoto za hapa na pale, lakini kwa ujumla kazi nzuri imefanyika, nawapongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nina ushauri mahususi hasa kuhusu nafasi za Watanzania kufanya kazi katika Taasisi na Mashirika ya Kimataifa. Kumekuwepo na manung'uniko kwamba watumishi wanaopata nafasi za kwenda kufanya kazi katika Taasisi na Mashirika ya Kimataifa baada ya kumaliza mikataba wakirejea wanarudi katika ngazi ile ile aliyoondoka nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba, kwa kuwa mtumishi huyu alienda kufanya kazi kwa mfano kwa miaka mitatu, mitano au nane, akapata *exposure* na uzoefu zaidi, basi akirejea na akakuta wenzake wamepanda ngazi na yeye aendelee katika ngazi ile ambayo wenzake pia wameshapanda. Kwa kufanya hivi, itawamotisha wengi kuomba nafasi hizo katika Taasisi na Mashirika ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hili, naambiwa kwamba kuna nyakati hata zile nafasi ambazo ni kama *share* yetu katika baadhi ya taasisi ambazo nchi yetu ni wanachama kama vile *SADC* na kadhalika zinakosa watu (Watanzania) kwa kuwa tu ama watumishi wetu hawajaomba au kwa kukosa mwamko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu wa jumla ni kwamba Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje iwe na mkakati maalum wa kuwahamasisha watumishi wetu kuomba nafasi katika taasisi na mashirika ya Kimataifa, na ikibidi hata kuwajengea uwezo wa namna ya kupata nafasi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nina watumishi katika Halmashauri ya Mafinga Mji ambao wamekuwa wakikaimu, mmoja mwanasheria ambaye amekuwa akifanya kazi kama Mkuu wa Kitengo cha Sheria toka Halmashauri inaanzishwa mwaka 2015, kuna wakati aliletwa Mkuu wa Kitengo lakini hakukaa sana akaondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kanuni na taratibu za kiutumishi, nashauri watumishi wa aina hii wawe *rewarded* kwa kuzingatia uwezo wake kikazi na muda ambao amekaimu. Kwa mfano, mwanasheria huyu ametusaidia sana kuokoa mamilioni ya fedha kutokana na kushinda kesi za ardhi na za madai ambazo nyingi tulirithi kutoka Halmashauri mama ya *Mufindi DC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wa pili ni Kaimu Mweka Hazina wa Mafinga Mji, ambaye kupitia barua yenye Kumb. Na. HM/MAF/CS.20/PF.140/14 ya tarehe 04 Januari, 2024 aliombewa kuthibitishwa/kupandishiwa mshahara. Mtumishi huyu nilipomwuliza shida ni nini, alinifahamisha ana *CPA,* lakini hana *masters*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ufahamu wangu, akiwa na *CPA* kwa mhasibu ni sifa muhimu kuliko hata *masters.* Ushauri wangu, naomba watumishi wa aina hii Serikali iwatazame kwa macho mawili hasa kwa kuzingatia kwamba baadhi ya wenzao wenye sifa kama wao wanakuwa wamethibitishwa katika nafasi kama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa ni suala la *recategorization*. Ushauri wangu wa kila mwaka kwenu ni kwamba mtumishi akifanyiwa *recategorization,* basi walau abakie

na mshahara wake. Kwa mfano, mwalimu ambaye yuko kwenye *TGTS F,* akasoma na akafanyiwa *recategorization* akawa *HR,* ni wazi lazima aanzie *HR* Daraja la Pili, lakini mshahara wake abakie nao ule ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwahi kuongea na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete akafafanua kwamba mwajiri anaweza kumwombea mtumishi aliyefanyiwa *recategorization* mshahara binafsi, lakini mimi naliona gumu kiutekelezaji. Hivyo ni vyema ikawekwa *openly* kuwa mtumishi akifanyiwa *recategorization automatically* mshahara wake utabakia ule ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza tena maana katika lolote linalofanyika hapa nchini, *engine* ni utumishi wa umma. Mmebeba dhamana kubwa na Mwenyezi Mungu awasimamie katika utendaji wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi. Nichukue nafasi hii kuwapongeza watumishi wote wa umma wanaokadiriwa kufikia 1,000,000 kote nchini wakiongozwa na mtumishi wa umma namba moja, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna mnavyojitoa kuhudumia wananchi usiku na mchana pamoja na changamoto nyingi mnazozipitia, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa na kutangaza ajira mpya katika kada mbalimbali ambapo inatibu tatizo la upungufu wa watumishi, kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na kutoa ajira kwa vijana wetu nchini wakiwemo vijana wangu wa Jimbo la Kisesa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunajadili hotuba ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2024/2025, Wizara ambayo ni *engine* ya utekelezaji wa shughuli zote za Serikali na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kutokana na umuhimu huo, ni vyema kufahamu dhana ya utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, utumishi wa umma ni mfumo wa kiutawala na kimenejimenti uliokabidhiwa jukumu la kuhakikisha kuwa jamii inapata huduma inayokusudiwa kutoka kwa Serikali yao au taasisi yoyote kwa niaba ya Serikali kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili watumishi wa umma waweze kutoa huduma bora kwa wananchi, ni lazima kuwepo mazingira wezeshi katika kutekeleza jukumu hilo muhimu, lakini pia wazingatie misingi na nguzo za utawala bora ambazo ni uwazi *(transparency)* ambapo shughuli za umma huendeshwa kwa uwazi bila siri na kificho ili wananchi wawe na uwezo wa kupima utendaji na uzingatiaji wa kanuni, taratibu na sheria, uwajibikaji *(accountability)* ambapo kiongozi na mtendaji huwa tayari kujibu, kubeba dhamana na kutoa maelezo kwa wananchi juu ya maamuzi au matendo aliyoyafanya katika kutekeleza dhamana aliyopewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, misingi mingine ni pamoja na utawala wa sheria *(rule of law),* ushirikishwaji *(participation),* usawa *(equity),* ufanisi na tija *(effectiveness and efficiency),* mwitikio *(responsiveness),* maridhiano *(reconciliation)* na uadilifu *(integrity)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nguzo za utawala bora ni katiba, utawala wa sheria, uhuru wa mahakama, uhuru wa habari na vyombo vya habari, mgawanyo wa madaraka, kulinda na kuheshimu haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yoyote duniani isipozingatia nguzo na misingi ya utawala bora, hutokea athari kubwa ikiwemo matumizi mabaya ya rasilimali za nchi, kuongezeka kwa umasikini, ujinga na maradhi, kuongezeka kwa rushwa, huduma mbovu za jamii, kutoheshimiwa haki za binadamu na kuongezeka kwa dhuluma na uonevu.

Mheshimiwa Naibu Soika, kama Taifa ni lazima tujipime je, tunafuata na kutekeleza misingi ya utawala bora au tumebakiza kuuzungumza kwa nadharia tu, huku tunazisigina nguzo na misingi ya utawala bora?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Tanzania kuridhia mikataba mbalimbali ya kimataifa ya uwazi na uwajibikaji, lakini utekelezaji wa dhana ya utawala bora katika nchi yetu umeshuka na unatishia ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie changamoto za utekelezaji wa mifumo ya utumishi na dhana ya utawala bora. Ukisoma Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 Sura ya Sita ukurasa wa 161 mpaka 169, ukipitia utekelezaji wa shughuli za Serikali katika maeneo mbalimbali na baadhi ya matukio yanayoendelea nchini, utabaini kuwa nchi yetu kwa sehemu kubwa ilishaacha nguzo na misingi ya utawala bora, kwani kuvunja katiba, sera, sheria, kanuni na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu imekuwa ni jambo la kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiukwaji huu unafanyika kwa makusudi ili kufanikisha maslahi binafsi ikiwemo wizi, rushwa na ufisadi, uonevu na dhuluma kwa wananchi. Kama Taifa ni lazima tuitathmini upya mifumo ya utumishi wa umma na utekelezaji wa misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, tusikubali mambo haya yaendelee, kwani yanaweza kuua Taifa letu kutoka kuwa Taifa lililostawi hadi kwenda kuwa Taifa lililoanguka *(failed state)*. Hii ni vita kubwa, lakini ninaamini tutaishinda endapo kama Taifa tutaendelea kuunganisha nguvu kwa pamoja na kuviangamiza vyanzo vyote vinavyotishia uhai wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naib Spika, nakumbuka Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere siku alipokuwa akitangaza vita vya kupambana na uvamizi wa majeshi ya Nduli Idd Amini tarehe 02 Novemba, 1978 alisema na nanukuu; "...tunayo kazi moja tu, Watanzania sasa, ni kumpiga (Nduli Idi Amini), uwezo wa kumpiga tunao, sababu ya kumpiga tunayo na nia ya kumpiga tunayo. Tunataka dunia ituelewe, hivyo kwamba hatuna kazi nyingine, na tunawaomba marafiki zetu wanaotuambia maneno ya suluhu waache maneno hayo…" Mwisho wa kunukuu kauli ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu ilishapitia mitihani na vita nyingi na kuzishinda. Hivyo hatuwezi kushindwa kubadili hii mifumo ili

kurejesha heshima na uadilifu katika Taifa. Binafsi ninayo ndoto kuwa siku kasoro hizi zikitatuliwa, nchi yetu itaingia kwenye mageuzi makubwa ya uchumi na maendeleo. Katika kuweka msingi wa hoja yangu kuhusu changamoto ya mifumo ya utumishi na utekelezaji wa dhana ya utawala bora, nitatolea mifano katika maeneo nane kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni maslahi duni ya watumishi wa umma, mishahara midogo, madeni ya uhamisho na likizo, kutokulipwa kwa wakati masurufu ya kazi na safari ni mambo ambayo yanawaumiza sana watumishi wetu wa umma hali inayopelekea kukosa morali ya kazi na kutoa huduma duni kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kujiuliza, kama uchumi wetu unakua, mapato yanaongezeka, bajeti zinatengwa kila mwaka, je, kuna sababu gani ya kushindwa kuwalipa mishahara mizuri na kuwalipa stahiki zao kwa wakati? Mfumko mkubwa wa bei za bidhaa na chakula uliobuka miaka ya hivi karibuni umepelekea ugumu wa maisha kwa watumishi wetu wa umma hasa wale wa kada za chini za Ualimu, Uuguzi, Uganga, vyombo vya ulinzi na usalama, Watendaji wa Vijiji na Kata, Maafisa Misitu, Maafisa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Maafisa Maendeleo ya Jamii, Madereva, Wahudumu, Walinzi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha mishahara wanayolipwa watumishi wetu hakitoshi, kwani bei ya nishati ya mafuta, chakula, nauli na bidhaa nyingine muhimu zimepanda bei maradufu na kuwafanya washindwe kukidhi kupata mahitaji muhimu. Baadhi yao kutumbukia kwenye mzigo mkubwa wa madeni ya mikopo ikiwemo kausha damu, hali inayopelekea kuwaondolea ari na utulivu wa kufanya kazi za kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya changamoto hizi kubwa za watumishi wa umma, lakini Waziri wa Utumishi ameshindwa kueleza chochote juu ya hatua zinazochukuliwa na Serikali kutatua changamoto za watumishi. Hivyo basi, Bunge lichukue nafasi yake ili ikawe mwisho kwa watumishi wa umma kudhalilika na kunyanyasika katika Taifa lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni kuhusu kikotoo cha mafao kwa watumishi wa umma. Tangu Serikali itangaze kuanza kwa matumizi ya

kikotoo kipya, kumeibuka manung'uniko na malalamiko makubwa kwa watumishi wa umma. Pia nimesikia michango ya Waheshimiwa Wabunge wakilalamikia kikotoo kipya mara kwa mara hapa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, kama Bunge tuamue leo na kama Serikali itaendelea na msimamo wake wa kung'ang'ania hiki kikotoo kipya kinacholalamikiwa na watumishi, ikifika wakati wa kupitisha Bajeti Kuu ya Serikali kwa kupiga kura ya Ndiyo na Hapana, Wabunge wote tutoke nje ya Ukumbi wa Bunge tumwachie Waziri Mkuu na Mawaziri peke yao wapitishe bajeti ya Serikali ili Bunge hili Tukufu lisiingie kwenye dhambi ya kuwaangamiza watumishi wetu wa umma nchini wanaofanya kazi usiku na mchana na kwa uadilifu na uzalendo wa hali ya juu.

Tatu ni kuhusu mkanganyiko wa mifumo ya utumishi wa umma. Hivi sasa mfumo tulionao unaruhusu kuwepo mgongano wa kiutawala kutokana na kuwepo kwa mifumo sambamba ya kiutawala *(parallel system)* ambapo anakosekana nani mkubwa? Nani anayepaswa kumwagiza mwenzake?

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana kwa mgawanyo sahihi wa majukumu *(clear separation of power)* na kusababisha kuingiliana katika utendaji na kusababisha viongozi na watendaji wa Serikali kutumia muda mwingi kulumbana na kugombana kila uchao, badala ya kutekeleza majukumu ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira na uteuzi wa baadhi ya nafasi hufanyika bila ushindani, hali inayopelekea kupata viongozi na watendaji wasiokuwa na uwezo wa kumudu majukumu yao na ndiyo maana tunashuhudia teuzi na tenguzi kila mara. Mheshimiwa Rais amepewa kazi ngumu ya kuhangaika na teuzi za kila siku na kusoma *CVs* za watu huku akipokea mashinikizo kutoka kwa ma-*godfather* wa watu wanaowania teuzi mbalimbali Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo pia ni rahisi kundi fulani la watu kutengeneza utawala wenye mrengo fulani *(empire)*. Utaratibu wa upekuzi *(vetting)* unaotumika hivi sasa hauwezi kuhakikishia kutokuwepo kwa upendeleo na upatikanaji wa viongozi bora. Pia siyo rahisi kuwatendea haki Watanzania zaidi ya milioni 60 wenye ujuzi na taaluma mbalimbali kupitia utaratibu wa *vetting.*

Mheshimiwa Naibu Spika, binafsi sioni sababu ya kwa nini tuendelee kuwapata kwa njia ya uteuzi badala ya ushindani Mawaziri, Makatibu wa Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Bodi za Mashirika ya Umma na Wakurugenzi wa Mashirika na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa utumishi tulionao sasa ni rahisi kuwabeba watumishi wazembe na wasio waadilifu ambapo badala ya kuadhibiwa huishia kubadilishiwa vituo na kulipwa gharama za uhamisho. Pale inapotokea wametenguliwa katika nafasi zao za uteuzi, huendelea kulipwa mshahara huo huo hali iliyopelekea daftari la mshahara la Serikali *(payroll)* kuzidiwa na uzito wa malipo yanayojirudia na kuliingiza Taifa kwenye hasara kubwa. Wengine wanapokea mishahara mikubwa kuliko hata ya mabosi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado hatujasahau kipindi cha mwaka 2016 tulibaini kuwepo kwa ajira za watumishi wenye vyeti *fake* 15,508 na watumishi hewa 19,708 ajira zilizokuwa zinaligharimu Taifa shilingi bilioni 19.8 kila mwezi. Pia mfumo wa utumishi unaruhusu kuajiri watumishi wasio raia wa Tanzania hali inayopelekea kukosekana kwa uzalendo, kuziba nafasi za Watanzania wenye sifa stahiki na kuhatarisha usalama wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Taarifa ya *CAG* ya mwaka 2022/2023 inaonesha kuwa kupitia mfumo huu huu wa utumishi, Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* wameweza kuajiri watumishi sita bila tangazo na bila kufanya usaili wa ushindani na watumishi hao hawajulikani walipatikanaje hadi kuajiriwa na shirika hilo la umma na huu ni mfano mmoja tu ya yanayoendelea katika ajira za watumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna watumishi 190 kwenye taasisi mbalimbali za Serikali wanaokaimu katika nafasi mbalimbali kwa zaidi ya miaka miwili hadi sita, jambo ambalo ni kinyume na Kanuni za Utumishi wa Umma na inashusha ufanisi wa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne ni kuhusu kutokutolewa taarifa kamili ya kifo cha Rais Magufuli. Baada ya kusikiliza kwa kina maelezo ya Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Mstaafu, Jenerali Venance Salvatory

Mabeyo aliyoyatoa tarehe 16 Machi, 2024 nimeshawishika na ninalishauri Bunge kukubali iundwe Tume Huru ya kuchunguza utata wa kifo cha Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ili kumtendea haki Hayati Magufuli na watu wengine wanaohusishwa kwa mema au kwa ubaya kuhusiana na kifo hicho. Pia tume hiyo itabaini watu waliokataa kuapishwa kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati lilikuwa ni takwa la kikatiba.

Tano ni kuhusu kupuuzwa maagizo ya viongozi. Tumekuwa tukishuhudia kushuka kwa nidhamu na uwajibikaji Serikalini kiasi kwamba baadhi ya viongozi na watumishi wa umma wamekuwa wakikaidi hata maagizo ya viongozi wa juu.

(i) Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitangaza uamuzi wa kujiuzulu nafasi yake ya Makamu wa Rais ifikapo Juni, 2024 endapo mradi wa maji wa Same – Mwanga - Korogwe hautakamilika kama alivyoagiza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia. Mradi huo umechelewa na sasa ni zaidi ya miaka kumi, pamoja na Makamu wa Rais kufedheheshwa na kuamua kutangaza kuacha kazi, lakini hatujasikia hatua zilizochukuliwa dhidi ya watumishi na viongozi waliosababisha mradi huo kuchelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Taifa tusikubali viongozi wetu wakafikishwa hapo na baadhi ya watumishi wa umma wasiowajibika katika nafasi zao kwani kila mtu abebe msalaba wake, lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango kwa kuweka wazi msimamo wake na kuwa mfano bora wa uwajibikaji.

(ii) Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa akifanya majukumu mengi ya huku na kule *(multitasking ambassador)* lakini amekuwa akitoa maagizo ambayo kwa sehemu kubwa hayatekelezwi na watendaji wa Serikali walio chini yake, mfano maagizo 12 aliyoyatoa hapa Bungeni tarehe 27 Aprili, 2023 ya kupiga marufuku kukamata wananchi na mifugo kiholela bila kuzingatia sheria, kanuni na taratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maagizo 12 ya Waziri Mkuu yalipuuzwa na Mawaziri na watendaji wa sekta husika, kwani licha ya kupiga marufuku *operation* hizo ambazo hazizingatii sheria, kanuni na taratibu na pia kuwepo ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu, *operation* hizo ziliendelea na kuleta madhara makubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa tarehe 3 Mei, 2023 nikiwa Bungeni nililalamikia watendaji wa Mamlaka za Uhifadhi kupuuza maagizo ya Waziri Mkuu ambapo Mheshimiwa Spika Dkt. Tulia Ackson alinitaka kuleta ushahidi kuthibitisha madai yangu niliyoyatoa Bungeni kuhusu kupuuzwa kwa maagizo ya Waziri Mkuu ndani ya siku saba, kazi ambayo niliifanya na kukabidhi vielelezo na nyaraka zote kwa wakati kama ilivyoagizwa. (Kiambatisho Na. 1)

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 28 Juni, 2023 Spika wa Bunge, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson wakati wa kuhitimisha Bunge la Bajeti la mwaka 2023/2024 alitoa maamuzi na kukiri kuwa Mheshimiwa Mpina alikuwa sahihi, kwani ni kweli kuwa maagizo 12 aliyotoa Waziri Mkuu kuhusu migogoro baina ya wananchi na maeneo ya hifadhi aliyoyatoa Bungeni tarehe 27 Aprili, 2023 yalikuwa yamepuuzwa. (Kiambatisho Na. 2 na Kiambatisho Na. 3).

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Waziri Mkuu alitoa maagizo hayo tangu tarehe 27 Aprili, 2023 na hadi nilipolalamika Bungeni tarehe 3 Mei, 2023 wiki moja baadaye *operation* ziliendelea na hata baada ya Mwongozo wa Spika wa tarehe 28 Juni, 2023 na hadi leo Aprili, 2024, mwaka mzima sasa *operation* zinafanyika bila kuwashirikisha wananchi na viongozi wa maeneo husika, wananchi kupigwa, kuteswa, kujeruhiwa, kusababishiwa ulemavu wa kudumu na kuuawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wananchi hupigwa faini kinyume cha sheria, wananchi huvamiwa na kuharibiwa mazao yao na kunyang'anywa mifugo, mifugo kukamatwa na kuuzwa kiholela, mifugo kukosa matunzo na kufa ikiwa imeshikiliwa hifadhini na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi wa kamatakamata isiyozingatia sheria inaendelea na licha ya mimi kutoa vielelezo vya kujitosheleza vilivyothibitishwa na Ofisi ya Bunge kama nilivyotakiwa na

Spika wa Bunge, lakini hadi leo hatujaona hatua zozote mahususi zikichukuliwa na badala yake dhuluma na mauaji yanaendelea kwa wananchi wetu katika maeneo mbalimbali ya nchi. Mfano Meatu, Mbarali, Ngorongoro, Tarime, Kaliua na kadhalika hadi leo Wabunge wengi bado wanalalamikia *operation* hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisikiliza vizuri mchango wa Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Mara na Mheshimiwa Emmanuel Shangai, Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro, michango ambayo iliugusa moyo wangu na kutokwa na machozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitegemea kuwa baada ya maagizo 12 ya Waziri Mkuu kupuuzwa, mambo mawili yangefanyika. Mawaziri na Watendaji wa Serikali waliopuuza maagizo ya Waziri Mkuu wangekuwa wameshafukuzwa kazi na kuchukuliwa hatua kali za kisheria au Waziri Mkuu mwenyewe angekuwa alishajiuzulu kwa kushindwa kumudu majukumu ya Uwaziri Mkuu kama anavyotakiwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 51(3)(e) kuhusu ukomo wa kushika madaraka ya nafasi ya Waziri Mkuu na Ibara ya 52 kuhusu kazi na mamlaka ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika dhana ya utawala bora haiwezekani akakosekana mtu wa kuwajibika, leo damu za wananchi zinazoendelea kumwagika, mateso ambayo wananchi wanayapata kuishi kama wakimbizi kwenye nchi yao, dhuluma na uonevu unaoendelea, haiwezi kuwaacha salama wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya uwajibikaji ipo duniani kote na siyo jambo geni katika nchi yetu na tunayo mifano mingi ya viongozi waliowajibika kwa tuhuma mbalimbali. Tunakumbuka Hayati Mzee Ali Hassan Mwinyi akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi alijiuzulu kwa makosa yaliyofanywa na watendaji walio chini yake na kumwandikia barua Rais wa wakati huo Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye aliridhia kujiuzulu kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hayati Edward Ngoyai Lowassa, akiwa Waziri Mkuu wa Tanzania alijiuzulu nafasi yake kwa tuhuma tu. Pia Dkt. Emmanuel Nchimbi, akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambaye leo ni Katibu Mkuu wa CCM na Mawaziri wenzake sita

walijiuzulu nyadhifa zao kwa madhila yaliyotokana na *operation* Tokomeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa George Simbachawene ambaye leo ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora alijiuzulu nafasi yake ya Waziri wa TAMISEMI baada ya kutuhumiwa kwenye mikataba ya madini kipindi alipokuwa Waziri wa Nishati na Madini. Hapa pia Makamu wa Rais Dkt. Philip Mpango ameonesha njia kuwa huwezi kuendelea kuwepo kwenye nafasi ambayo huwezi kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko Uingereza nako aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza, Tony Blair alijiuzulu nafasi ya Waziri Mkuu baada ya kubainika kuwa sababu za kuivamia na kuipiga Iraq *(Casus belli)* hazikuwa na ukweli, kwani nchi hiyo haikuwa inamiliki silaha za maangamizi *(WMD Trinity)* kama ilivyokuwa imeelezwa awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita ni kuhusu kutowiana kwa taarifa za uchunguzi na taarifa za ukaguzi. Kumekuwepo kwa kukinzana kwa Taarifa za Uchunguzi na Ripoti za Ukaguzi. Taarifa za uchunguzi zinazotolewa na TAKUKURU, *DCI* na *DPP* zimekuwa haziakisi Ripoti za Wakaguzi za *CAG, PPRA, FIU, IAG* na Mbio za Mwenge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia Ripoti ya Wakaguzi na Wachunguzi ya mwaka 2020/2021, 2021/2022 na 2022/2023 na kubaini tofauti kubwa. Hii ina maana kuwa ripoti za wakaguzi hazifanyiwi kazi kikamilifu na mamlaka za uchunguzi hivyo kuchochea wizi, rushwa na ufisadi nchini. Mamlaka za uchunguzi zimekaa kimya katika maeneo mengi yaliyotolewa taarifa za viashiria vya kuwepo wizi, rushwa na ufisadi katika ripoti za wakaguzi. Iko mifano kadhaa katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, uchunguzi kutofanyika kwa wakati. Katika kipindi cha miaka miwili takwimu zinaonesha kuwa malalamiko yaliyopokelewa TAKUKURU ni 14,773 lakini majalada yaliyokamilika uchunguzi ni 993 tu, sawa na 6.7% tu, huku majalada 93.3% yakiachwa bila kufanyiwa kazi katika mwaka husika, lakini pia kati ya kesi 638 zilizopelekwa mahakamani Serikali ilishindwa kesi 275 sawa na 43%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu hizi, hivi kweli tunayo nia ya dhati ya kupambana na rushwa nchini kwetu? Uchunguzi umefanyika, 6.7% tu kwa malalamiko yote yaliyopokelewa katika mwaka husika, huku tukipoteza 43% ya kesi zote zilizofikishwa mahakamani, na hapa unajiuliza majalada yaliyofanyiwa uchunguzi na TAKUKURU na kuridhiwa na *DPP* yakiwa na ushahidi wa kutosha inawezekanaje mahakamani tushindwe kwa kiwango hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 inaonesha kuwa malalamiko yaliyopokelewa ni 7,225 lakini majalada yaliyokamilika uchunguzi ni 1,828 sawa na 25% huku kesi zilizoshindwa ikiwa ni 33%. Kila mahali watuhumiwa wa rushwa na ufisadi wamekingiwa kifua na mamlaka za Serikali ukienda *TRAB* na *TRAT* (kodi zilizoshikiliwa kwenye mapingamizi ni shilingi trilioni 10.48) bila sababu za msingi, *FIU* (kuwepo miamala shuku yenye thamani ya shilingi trilioni 280 ambayo haijakamilika kufanyiwa uchambuzi hadi sasa), vilevile katika Ripoti za *CAG, PPRA,* Mbio za Mwenge na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukipitia tovuti ya TAKUKURU unakuta waliohukumiwa kwa makosa ya rushwa kwa sehemu kubwa ni viongozi wa vijiji, kata, wilaya na bodaboda, huku watuhumiwa wakubwa wa rushwa na ufisadi wakiwa kwenye ofisi za umma na mitaani wanatamba. (Kiambatisho Na. 3)

Pili, ni kuhusu watuhumiwa wa rushwa na ufisadi kutofikishwa mahakamani licha ya mamlaka za ukaguzi kuibua tuhuma mbalimbali za rushwa na uhujumu uchumi, lakini ni idadi ndogo tu ya watuhumiwa wanaofikishwa mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa zinaonesha kuwa katika kipindi cha miaka miwili, ni kesi tisa tu za rushwa na uhujumu uchumi zilizofikishwa katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi licha ya kwamba watuhumiwa wengi wa rushwa na ufisadi hawakupelekwa mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hizo kesi tisa hazifahamiki kwa umma zinamhusu nani? Katika eneo gani? Huku TAKUKURU ikipambana kuwaficha watuhumiwa wa rushwa na uhujumu Uchumi, lakini Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar *(ZAECA)* inatawangaza hadharani kwa majina na nafasi zao.

(i) Taarifa ya *CAG* ya mwaka 2021/2022 inaonesha kuwa *TRC,* Wizara ya Fedha na Wizara ya Uchukuzi waliacha njia ya ushindani na kutumia njia ya *single source* katika zabuni ya ujenzi wa reli ya *SGR* kipande cha Makutupora - Tabora na kuisababishia hasara Serikali ya shilingi trilioni 1.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hata katika kipande cha Tabora - Kigoma Wizara hizo zilitumia njia ya *single source* bila sababu za msingi na kuisababishia hasara Serikali ya shilingi trilioni 1.7 na hivyo kufikia hasara ya shilingi trilioni 3.4. Matrilioni hayo ya Watanzania yamepotea, lakini watu waliohusika bado wako kwenye ofisi za umma na hawajafikishwa mahakamani. Taarifa ya TAKUKURU imekaa kimya kuhusu jambo hili.

(ii) Kwa mujibu wa taarifa ya *CAG* ya mwaka 2021/2022 Serikali Kuu, jedwali Na. 17 ukurasa wa 56 linaonesha kuwa Serikali imekopa nje ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na bila ridhaa ya Bunge kiasi cha shilingi trilioni 1.285. Pia jedwali hilo linaonesha kuwa kiasi cha shilingi trilioni 2.531 fedha za mikopo hazikupokelewa katika Mfuko Mkuu wa Serikali, kwani fedha hizo zilipokelewa kwenye akaunti za wafadhili na nyingine zilipokelewa moja kwa moja kwenye miradi. Hii ni kinyume na Katiba, sheria na dhana ya misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mara tumemtaka Waziri wa Fedha kuwasilisha Bungeni jedwali la matumizi ya mikopo hiyo bila mafanikio, hapa kinafichwa nini? Serikali inataka mpaka taarifa ya akaunti na majina yaliyotumiwa miamala ya fedha hizo yavuje mitandaoni ndiyo mtoe maelezo ya ufafanuzi? Kuendelea kuchukua mikopo hii kwa kificho na nje ya sheria kumelipelekea Taifa letu kutumbukia kwenye mzigo mkubwa wa madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufikia tarehe 30 Juni, 2023 deni la Serikali lilikuwa shilingi trilioni 82.2 ikilinganishwa na shilingi trilioni 71.3 mwaka 2022. Kuna ongezeko la shilingi trilioni 10.9 (15%) ikilinganishwa na ongezeko la shilingi trilioni 6.7 (10%) kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, deni la Taifa limekuwa likikua kwa kasi kubwa ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambapo lilikuwa likikua kwa wastani wa asilimia nne hadi tano tu. Usiri na kasi ya uchukuaji mikopo unaoendelea nchini, unatishia uhai na uhuru wa Taifa letu. Benki ya

Dunia *(WB)* imezionya nchi za Afrika kuacha kukimbilia kuchukua mikopo ya nje ili kurahisisha kutatua shinikizo la ukwasi *(liquidity pressures)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)*, Dkt. Akinumwi Adesina amezitahadharisha nchi za Afrika kuacha kutumia rasilimali zake za asili kama dhamana ya mikopo. Nchi nyingi za Afrika zimeanza kuchukua mikopo inayolindwa na dhamana ya maliasili za nchi kama madini, gesi, mafuta, bandari na kadhalika, hali inayopelekea kuingiliwa katika utungaji na usimamizi wa sera, sheria, kanuni, miongozo, programu na mikakati (kunyang'anywa uhuru wa kujiamulia mambo), mikopo kukosa uwazi, ulinganifu na yenye riba kubwa na masharti mengi ya kinyonyaji.

(iii) Mfano mwingine ni Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere *(JNHPP-2115)* ambapo fedha za faini ya ucheleweshaji, *CSR* na tozo ya Mahakama kwa *IPTL* kiasi cha shilingi trilioni 1.4 hadi leo haijadaiwa na Serikali. Hapo dhana ya utawala bora iliyojengwa katika misingi ya uwajibikaji na utawala wa sheria iko wapi? Taarifa ya *CAG* ya mwaka 2022/2023 inaendelea kulalamikia kutokulipwa fedha hizi lakini taarifa za uchunguzi ziko kimya na wahusika bado wako kwenye ofisi za umma na hawajafikishwa mahakamani hadi leo.

(iv) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imekuwa haitangazi hadharani majina ya watuhumiwa wa rushwa na ufisadi na imegeuza kuwa jambo la siri hali inayorudisha nyuma mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi nchini. Tofauti na upande wa Zanzibar, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar *(ZAECA)* imekuwa ikiwatangaza kwa majina, vyeo na hasara waliyoisababisha watuhumiwa wote wa rushwa na ufisadi wanaopelekwa mahakamani. (Kiambatisho Na. 4)

(v) Kila ripoti ya *CAG* inapowasilishwa haioneshi watuhumiwa waliofikishwa mahakamani wala hatua zilizochukuliwa. Sheria ya Ukaguzi inampa mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kuwapeleka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka *(DPP)* watuhumiwa wote aliojiridhisha pasipo mashaka kuwa kosa limetendeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 47(3) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008, nanukuu: " *47(3) When the Controller and Auditor General has reason to believe that an offence has occurred, he shall refer the matter to the Director of Public Prosecutions for appropriate action (The Public Audit Act),"* huku taarifa za wakaguzi zikionesha dalili za kuwepo wizi, rushwa na ufisadi wa matrilioni ya fedha za umma, lakini TAKUKURU inaripoti kuokoa fedha shilingi bilioni 15.5 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba ni kuhusu kuingia mikataba ya siri ya rasilimali za Taifa. Serikali hairuhusiwi kuingia mikataba ya rasilimali za umma kwa siri na badala yake inatakiwa kuweka wazi mikataba hiyo ili wananchi wawe na uwezo wa kupima utendaji na uzingatiaji wa kanuni, taratibu, sheria na utawala bora. Hivi sasa Serikali inaingia mikataba kinyume cha Katiba na sheria za nchi.

(i) Katika kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi 2022/2023, Serikali inakiri kuingia mikataba 43 ya rasilimali za nchi. Mikataba hii imeingiwa kwa siri na kwa kificho, hata tulipoomba kuletewa mikataba hiyo au kuelezwa inahusu nini, Serikali imekaidi agizo hilo na kuamua kukaa kimya. Mikataba hii imeingiwa kinyume na kifungu cha 16(1) cha Sheria ya *The Tanzania Extractive Industries (Transparency and Accountability) Act 2015,* pia kifungu cha 12 cha Sheria ya *The Natural Wealth and Resources (Permanent Sovereignty) Act No. 5 of 2017* ambazo zinataka mikataba yote ya rasilimali kuwekwa wazi kuanzia hatua za awali za makubaliano hadi kusaini mkataba na baadaye kuridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, usiri huu wa mikataba unaleta hofu kubwa sana kuhusu hatima ya rasilimali za Taifa letu. Hii mikataba 43 ya rasilimali inahusu kuuzwa, kukodisha, kuwekwa dhamana au kubinafsishwa? Hapa dhana ya utawala bora iko wapi? Waziri wa Utawala Bora yuko kimya au anasubiri mikataba hii yote 43 ivuje kwenye mitandao ndiyo ufafanuzi utolewe!

(ii) Serikali imesaini mikataba saba ya ujenzi wa barabara saba zenye jumla ya kilometa 2,035 kwa gharama ya shilingi trilioni 3.75 kwa kiwango cha lami kwa kutumia utaratibu wa *Engineering, Procurement, Construction and Financing (EPC + F)* bila kueleza kwa kina masharti yaliyoko kwenye mkataba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa ni takribani mwaka mmoja umepita miradi hiyo haijaanza. Mikataba ya *EPC+F* awali aliyekuwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mnyaa Mbarawa na Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba walieleza kwamba mkandarasi anakuja na fedha zake kujenga barabara hizo na baadaye Serikali kuanza kulipa kidogo kidogo, ghafla baada ya kusainiwa mikataba hiyo Serikali inabadilisha tena maelezo kwamba mkandarasi anatakiwa apewe 10% ambayo ni shilingi bilioni 375.51 ndiyo miradi iweze kuanza ujenzi wake. Hizi fedha hazimo katika bajeti ya mwaka 2023/2024 na siyo utaratibu wa *EPC+F*. Madai haya hayamo katika mkataba wa *EPC+F,* fedha hizi zinatotewa kwa ajili gani na tunapata unafuu gani kama Taifa kwa kutumia utaratibu huu wa *EPC+F?*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ripoti ya *CAG* ya mwaka 2022/2023 imethibitika kuwa mikataba hii ilisainiwa bila kuwa na ufadhili wa uhakika wa miradi hiyo na wakandarasi wameshindwa kuwasilisha dhamana ya benki ya utendaji kazi yenye thamani ya shilingi bilioni 375.51 kama matakwa ya mkataba na ndiyo sababu ya miradi hii kushindwa kuanza hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa wakandarasi walipatikanaje hadi wakasaini mikataba wakiwa hawana sifa na uwezo wa kifedha? Mkataba wa *EPC+F* uliwezaje kusainiwa bila kujiridhisha na masuala ya msingi ikiwemo ufadhili wa fedha za mradi? Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi – Prof. Mbarawa na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu wamekuwa wakitumia nguvu kubwa kulipotosha Bunge na umma wa Watanzania kwa makusudi kuhusu faida za miradi ya *EPC+F* huku ukweli wakiwa wanaujua.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni dhahiri kuwa Mawaziri hawa walijipanga kulihadaa Taifa ili kufanikisha maslahi yao binafsi na kulitumbuliza Taifa kwenye mzigo mkubwa wa madeni yasiyolipika. Haya yote yamefanyika Waziri wa Utawala Bora yupo na Waziri Mkuu yupo.

(iii) Mradi wa ujenzi wa barabara ya kulipia, ghafla tukasikia Serikali inasaini mkataba wa ujenzi wa barabara ya *express way* kutoka Kibaha hadi Chalinze yenye urefu wa kilometa 78.9 kwa njia ya ubia *(PPP)*. Mkataba huu umesainiwa bila kulieleza Bunge masharti

yaliyopo katika mkataba huo. Serikali haina mamlaka ya kutwaa ardhi ya umma ambayo ni hifadhi ya barabara na kuikabidhi kwa mwekezaji bila kibali cha Bunge. Hii ni kinyume cha Sheria ya Ardhi na Sheria ya Rasilimali, hapa utawala bora tunaozungumza uko wapi? Hakuna uwazi, hakuna ushirikishwaji wa wananchi wala uzingatiaji wa sheria. Haya yanafanyika Waziri wa Utawala Bora yupo na Waziri Mkuu yupo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane ni kuhusu Mawaziri kutoa taarifa za uongo kwa Mheshimiwa Rais na umma wa Watanzania. Katika siku za karibuni, kumeibuka tabia ya Mawaziri kutoa taarifa za uongo mbele ya Rais na mbele ya Watanzania bila hofu wala woga wowote, kinyume kabisa na misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona hapa majuzi Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba akimweleza Mheshimiwa Rais kwenye mkutano wa hadhara kwamba hakuna wizi Serikalini huku akijua fika kuwa kuna Ripoti ya *CAG* ya mwaka 2021/2022 aliyoiwasilisha Bungeni ikiwa imejaa tuhuma za wizi, ubadhirifu na ufisadi wa kila aina wa zaidi ya shilingi trilioni 30.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya TAKUKURU na Ripoti ya *CAG* ya mwaka 2022/2023 nazo zimejaa tuhuma za ubadhirifu wa kila aina. Pia tumeona Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa naye mbele ya Mheshimiwa Rais akimhadaa kuwa wizi unaosemwa mitandaoni ni wa miaka ya 2017 hadi 2021 huku akijua fika *CAG* katika ripoti yake ya mwaka 2021/2022 na 2022/2023 amebaini wizi na ubadhirifu wa kila aina kwenye Wizara yake ya TAMISEMI, halafu Waziri mbele ya Rais anaita taarifa za wizi zinazoibuliwa na *CAG* na TAKUKURU kwamba ni taarifa za kwenye mitandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkuu naye huko Mara alikutana na wizi mkubwa hadi fedha zinasafirishwa kwenye mabegi kama nguo kutoka Mara kuja Makao Makuu ya TAMISEMI Dodoma zaidi ya shilingi milioni 200. Hili dili limejulikana, je, ni madili mangapi ya aina hii yanayofanyika kwenye halmashauri zote nchini kwa kificho?

Mheshimiwa Naibu Spika, ujasiri huu wa Mawaziri hawa kusema uongo tena mchana kweupe mbele ya Mheshimiwa Rais na

Watanzania wanautoa wapi? Mawaziri hawa wanafanya hivyo ili kufanikisha nini? Hayo yanafanyika, lakini Waziri wa Utawala Bora na Waziri Mkuu wako kimya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa ni kuhusu kuwepo viongozi na watumishi wa umma ndani ya Serikali ambao siyo raia wa Tanzania. Zipo taarifa za uhakika kwamba baadhi ya nafasi za uongozi na watendaji wa Serikali zimechukuliwa na raia wa kigeni kinyume na Katiba na sheria za nchi yetu na kupelekea usalama wa nchi yetu kuwekwa rehani mwa wageni, kukosekana kwa uzalendo na uadilifu, ajira za Watanzania kuchukuliwa na raia wa kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi *(CDF)*, Jenerali Jacob John Mkunda wakati wa Mkutano wa Saba wa Mkuu wa Majeshi *(CDF)* na Makamanda wa mwaka 2023 uliofanyika tarehe 22 Januari, 2024 mbele ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alisema, nanukuu: "Taarifa zilizopo, baadhi ya waomba hifadhi hao au wakimbizi au familia zao wameajiriwa Serikalini kwa nafasi mbalimbali na wengine wamepewa teuzi Serikalini katika nafasi zenye maamuzi." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ina maana kwamba vyombo vya dola vimeshajiridhisha kuwepo kwa viongozi na watendaji ndani ya Serikali, tena katika ngazi ya maamuzi ambao siyo raia wa Tanzania na orodha ya majina hayo wameshaikabidhi Serikalini kwa hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Waziri wa Utumishi wa Utawala Bora kupitia hotuba hii ameshindwa kusema chochote juu ya hili jambo kubwa ambalo ni tishio la usalama wa nchi yetu. Hii ina maana kuwa, tangu vyombo vya dola vitangaze hadharani suala hili mwezi Januari, 2024 hadi sasa hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa na Serikali. Utawala bora uko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi ni kuhusu kuwepo kwa taarifa nyeti zisizothibitishwa. Katika siku za hivi karibuni kumekuwepo na taarifa nyeti zinazotolewa na baadhi ya viongozi waandamizi Serikalini kutoa matamko yanayotishia usalama wa nchi, lakini taarifa hizo zimekuwa hazikanushwi wala kuthibitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtakumbuka Mheshimiwa Albert John Chalamila wakati akiwa Mkuu wa Mkoa wa Kagera mwezi Oktoba, 2022 alisema baadhi ya Mawaziri wameacha majukumu ya kumsaidia Mheshimiwa Rais na kuhangaika nje ya nchi kusaka fedha za kuja kumng'oa mwaka 2025, lakini pia hivi majuzi Mheshimiwa Paul Christian Makonda, Mkuu wa Mkoa wa Arusha tarehe 12 Aprili, 2024 akiwa na viongozi wakuu wa nchi na wananchi wengine katika kumbukizi ya miaka 40 ya kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania, Hayati Edward Moringe Sokoine, Monduli alisemam ninanukuu: "Nitumie fursa hii kuwaambia hasa kaka zangu mnaotuma watu na kulipa kumchokoza mama yangu, ninawajua na ninyi mnanijua. Narudia tena, hasa kaka zangu mnaotuma na kulipa watu kumchokoza mama yangu Samia, mnanijua na ninyi nawajua. Mheshimiwa Rais, kwa majina yao nawajua, na leo tarehe 12 nataka iwe mwisho kuwatuma watu hao wanaokutukana kwenye mitandao ya kijamii. Jumatatu ikiendelea, nakutajia majina. Wwengine ni Mawaziri na wengine wanapewa nguvu na watu tunaowaheshimu. Naomba iwe mwisho, tumwache Daktari Samia afanye kazi aliyopewa na Mungu." Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha kuhusishwa baadhi ya Mawaziri kuwa sehemu ya mkakati wa kumpinga na kumkwamisha Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake na kushiriki njama za kumwondoa madarakani ni kosa la uhaini na kosa la kimaadili na hii ni kwa mujibu wa Ibara ya 54 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo ilitarajiwa baada ya kauli hizi kutolewa na viongozi hao waandamizi wa Serikali, vyombo vya dola vingeueleza umma usahihi wa taarifa hizo na hatua zilizochokuliwa dhidi ya wahusika. Tulitegemea Wakuu wa Mikoa hao wawili Chalamila na Makonda wangelazimishwa kuwataja kwa majina na nafasi zao Mawaziri wanaotuhumiwa kumsaliti Rais ambao wangekuwa wametenguliwa katika nafasi zao na kufikishwa mahakamani, lakini pia kama Wakuu wa Mikoa hao wametoa taarifa za uongo na wameshindwa kuwataja kwa majina wahusika, basi wao wakamatwe na washitakiwe kwa makosa ya uhaini. Rais ni taasisi nyeti, ni lazima tuilinde kwa wivu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ikilinganishwa na nchi nyingine katika dhana ya utawala bora; utoroshaji wa fedha nje ya nchi *(Illicit Financial Flows - IFFS)* umefikia wastani wa shilingi trilioni 3.5 kwa mwaka, Tanzania ni nchi pekee ambayo wahalifu wa makosa ya *transfer pricing* wamefutiwa adhabu, pia ripoti ya *Transparency International* ya mwaka 2023 kwenye kipengele cha *Corruption Perception Index (CPI)* Tanzania ilipata 40% na kushika nafasi ya 87 kati ya nchi 189 zilizopimwa. Kwa tathmini hii, nchi yetu inaonekana kufanya vibaya katika usimamizi wa dhana ya utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Mambo yanayofanyika hivi sasa nchini kwetu katika baadhi ya sekta hayaendani na misingi ya utawala bora. Kama nilivyosema awali kuwa Katiba, sheria, kanuni na miongozo na misingi ya utawala bora haifuatwi katika maeneo mengi ya utekelezaji wa shughuli za Serikali na hivyo kusababisha kuwepo matumizi mabaya ya rasilimali za nchi, kuongezeka kwa umaskini, ujinga na maradhi, kuongezeka kwa rushwa, huduma mbovu za jamii, kutoheshimiwa haki za binadamu na kuongezeka kwa dhuluma na uonevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**VIAMBATISHO**

Kiambatisho Na. 1, Maelezo ya Ushahidi ya Mbunge Luhaga Mpina
Kiambatisho Na. 2, Maagizo 12 ya Waziri Mkuu ya Tarehe 27 Aprili 2023
Kiambatisho Na. 3, Uamuzi wa Spika kuhusu kupuuzwa kwa Maagizo ya Waziri Mkuu
Kiambatisho Na. 4, Taarifa ya ZAECA ya kuwafikisha Mahakamani Watuhumiwa wa Rushwa na Ufisadi.

*(Hapa Mhe. Luhaga J. Mpina hakuweka viambatisho katika mchango wake wa maandishi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa namwita Mheshimiwa Katambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Kikwete.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa

George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuifanya. Mahususi nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuweza kuiongoza nchi kwa kufuata misingi ya utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninasema hivi kwa sababu misingi ya utawala bora imeainishwa kisheria na kikatiba kwa mambo yafuatayo; Kwanza, lazima kuwe na Utawala wa Sheria na ndiyo maana tunaona hatua zinachukuliwa na Mahakama inafanya kazi kwa kuhakikisha kwamba, inatoa hukumu au maamuzi na vyombo vya ulinzi na usalama vinafanya kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuna kuheshimu Katiba na tatu, msingi mwingine ni *independence of judiciary* kwa maana ya kuwa na uhuru wa Mahakama katika kufanya kazi zake bila kuingiliwa. Jambo lingine ni kuwa na heshima au kuheshimu haki za binadamu. Sambamba na hilo kuna suala la kuheshimu maamuzi yanayoamuliwa na Bunge lako Tukufu, hivyo hivyo, kuheshimu misingi ya kidemokrasia kwa mana ya *principle of democracy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote yamethibitika ndiyo maana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliunda Tume ya Haki Jinai kuhakikisha kwamba kutakuwa na Utawala wa Sheria. Pia aliweka uhuru katika vyombo vya maamuzi ikiwemo *PCCB* kwa maana ya TAKUKURU kuweza kufanya maamuzi yake pale ambapo hatua zimekuwa zikichukuliwa, na wapo watu wenye kesi Mahakamani, pia wapo ambao wamechukuliwa hatua mbalimbali. Kwa hiyo, kwenye msingi wa Utawala wa Sheria, nchi yetu imekuwa kielelezo na tutaendelea kusimamia hivyo na Katiba yetu tutaendelea kuiheshimu, kuitii na kuilinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ni muhimu niweze kulizungumzia ni hili la kikokotoo. Kumekuwa na *mixed feelings,* na ni kweli tunakubali katika upande wa Serikali kwamba suala la kikokotoo kulikuwa na changamoto kubwa. Lazima turudi kwenye historia. Nakumbuka changamoto hii imejitokeza kutokana na historia ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kupitia Bunge hili Tukufu tulitunga sheria ya kuanzisha Mfuko wa *LAPF,* tulitunga sheria ya kuanzisha Mfuko wa *PSPF*, tukatunga sheria ya kuanzisha Mfuko wa *PPF*, pia tulikuwa na Mfuko wa *GEPF* na hivyo hivyo tulikuwa na Mfuko wa *NSSF* katika kipindi cha nyuma. Tusisahau kwamba Bunge hili ndilo lilipitisha sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadaye katika uendeshaji wa mifuko hii zilitokea changamoto mbalimbali zikiwemo za uendeshaji na kuwa mzigo tena katika mfumo, kwa sababu ilikuwa inatengeneza mfumo wa kiushindani. Sasa kwenye masuala ya wafanyakazi, kwa sababu wanachokichangia ni kwa ajili ya maisha yao, ukiweka mfumo wa ushindani, matokeo yake kutakuwa hakuna uwiano wa mafao kwa wafanyakazi ambao walikuwa wakifikia hatua ya kustaafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika kutengeneza uwiano wa mafao na kupunguza hasara zilizokuwa zikijitokeza kama *Operational Cost* za uendeshaji wa mifuko, ndiyo yakafanyika maamuzi mwaka 2018 ya kuunganisha mifuko, tukawa na mifuko miwili. Mmoja wa *PSSSF* kwa ajili ya wafanyakazi wa sekta ya umma, pia kuwa na Mfuko wa *NSSF* ambao utashughulika na wafanyakazi wasio katika sekta ya umma au sekta rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo haya nini kilichofanyika? Kwanza, tulienda kwenye unafuu. Yapo mafao awali yalikuwa 25%. Katika kuingia kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tulifanya *actuarial evaluation* na katika tathmini hiyo ilitupeleka pamoja na kukaa vikao na Vyama vya Wafanyakazi wote nchini, Vyama vya Waajiri wote nchini na upande wa Serikali kuweza kuangalia na kutafuta ule unafuu, tukatoka 25% kwenda 33%.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa ninavyosema, hatua ni nzuri. Mheshimiwa Rais, alishatoa maelekezo zaidi ya mara mbili akiwa amekutana na Jeshi la Polisi Wastaafu, Wakuu wa Jeshi la Polisi, alitoa maagizo kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba, tufanye tathmini na kuangalia upya na kufanya mapitio kuona hiki kikokotoo cha sasa kama tunaweza tukakiboresha zaidi ili wastaafu wetu wasiweze kupata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshaanza kazi hiyo na pia sheria inatutaka tufanye *actuarial evaluation* kila baada ya miaka mitatu na tayari miaka mitatu imeshafika kuanzia mwaka 2023, na sasa tupo kwenye hatua hiyo. Tumefanya tafiti nchi nyingi, hatuwezi hata siku moja Serikali kufumba macho wala kuziba masikio katika suala ambalo linawahusu Watanzania ambao wamefanya kazi ya heshima kwa ajili ya ujenzi wa Taifa hili. Hatuwezi hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpe pole Mheshimiwa Neema Mwandabila ambaye kimsingi yeye alikuwa anaeleza kwa maana ya jinsi ambavyo tulimwelimisha kupitia mifuko lakini imeonekana kama mashambulizi yamekuwa mengi kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wamekuwa wakieleza kulingana na uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwape pole, lakini tuseme suala hili ni la kisayansi, linahitaji kufanya tafiti za kina ili kuweza kuhakikisha kwanza kunakuwa na uendelevu wa mifuko, na zaidi, katika tija kuangalia wastaafu hawa waweze kupata fedha na wawe na uhakika wa kulipwa mafao yao pale wanapostaafu kuliko vinginevyo ambavyo imekuwa. *(Makofi)*

Mheshemiwa Naibu Spika, tumefanya utafiti katika nchi za Afrika, tumeona Tanzania tupo tofauti sana katika nchi zote za Afrika katika utoaji wa mafao. Hata nchi za wenzetu kule nje, tena wao hawatoi kabisa ile fedha ya mkupuo. Wakati mwingine kuzitaja hapa inaweza isilete mahusiano mazuri ya kidiplomasia lakini tunafanya tafiti kuweza kuhakikisha watu wetu wanapata mafao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi mwenyewe nina maslahi, nina wazee wangu watatu sasa hivi wanaelekea kwenye kustaafu. Sasa ingekuwa ni mambo yangu binafsi, pengine au ni jambo la Mheshimiwa Waziri, au ni la mtu mwingine, maana yake angeangalia maslahi na upendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi tunachoangalia ni ile *sustainability* na nafuu ambayo ataipata mstaafu awaze kupata heshima ya kuwa na fedha nyingi ambazo anazipata baada ya kufanya kazi kwa kutumikia Taifa lake. Pili, ile mifuko iweze kuwaendeleza wale wengine ambao wanachangia. Kwa hiyo, ndiyo maana ilikuwa ni uamuzi wa

Serikali kuhakikisha tunakuwa na mifuko miwili sasa, usimamizi wake uweze kuwa mzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia 81% ya wanufaika kwa sasa imeongezeka, ukiacha ya awali 19% peke yake ndio ambao mkupuo umepungua, lakini 81% zimeongezeka hata yale mapato yao ya mwisho wa kila mwezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa sababu jambo hili limeshatolewa maelekezo na Mheshimiwa Rais, Bunge lako Tukufu limetuelekeza, tunalipokea kwa unyenyekevu mkubwa kwenda kulifanyia kazi na pengine tutasikia kauli ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan pale katika viwanja vya Sheikh Amri Abeid, Arusha Tarehe 01 Mei, ambapo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan rafiki wa Wafanyakazi na rafiki wa Waajiri atakutana nao na ataenda kueleza kuhusiana na suala hili. Kwa hiyo, tumelipa uzito unaostahili kuweza kuhakikisha tunaliweka sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala hili la uhamisho. Ni kweli uhamisho kwa mujibu wa sheria, kwanza unaanzia pale ambapo zinatangazwa ajira. Pili,

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika moja kwa ruhusa yako.

**NAIBU SPIKA:** Bado unazo dakika tatu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala hili la uhamisho, Mtanzania yeyote anapoomba ajira hasa hizi za Serikali, kuna kipengele na makubalino kwamba atakuwa tayari kufanya kazi popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Tanzania Bara au Tanzania Visiwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika kipengele hicho, anapopata ajira, changamoto ambazo tumekuwa tukizipata kwa upande wa Serikali ni pale ambapo anapata ajira, anaenda kufanya kazi na kuna sharti lingine katika sharti lake la ajira kwamba atafanya kazi kuhudumia Tanzania kwa kipindi cha miaka mitatu ili sasa baadaye katika miaka mitatu hiyo ikiisha, ndiyo aweze kuwa na uhuru wa kuweza kuhama kwenda eneo lingine lolote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *experience* inaonesha pale tu ajira zinapotolewa, mtu anakubali popote kwa sababu Serikali inatoa ajira pia kulinga na uhitaji na ikama kuweza ku-*balance* kwenye maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna maeneo ambayo ni ya pembezoni mwa Tanzania, hawapati wafanyakazi na Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiomba kwamba wakati wao wana upungufu wa Madaktari, Manesi na kadhalika, inapotokea Serikali imetoa ajira kwa ku-*balance* hiyo ikama na wale waliokubali kwamba wanaweza wakafanya kazi popote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa zaidi ya miaka mitatu bila kuhama, akishapata ajira, hatua ya pili inayofuata ni kuanza kuomba uhamisho. Anaomba uhamisho atoke Kigoma aende Dar es Salaam kwa sababu shangazi ni mgonjwa, mama ni mgonjwa, baba ni mgonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine kuna maeneo utakuta hata vyeti vya *forgery;* kumekuwa na sababu za kwenda masomoni, na wengine wamekuwa wakiingia hata kwenye ndoa hata zile mkeka wakati mwingine ili tu mwisho wa siku awe na ndoa ya kwenda kuthibitisha kwamba anahitaji kutoka kwenye eneo lile. Sasa hili ni sisi wenyewe katika sababu hizi ambazo zimekuwa zikitolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo sababu nyingine. Hata viongozi tuwe wa kweli kwa ajili ya Tanzania yetu. Hata sisi Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukiombwa uhamisho. Tunakuja tunaandika *memo* kwamba tunaweza kuwahimisha kutoka kwenye maeneo fulani tunaweka kwa *memo* kwamba wahamie kwenye Majiji au kwenye Halmashauri za Miji na Mikoa. Lazima tuseme ukweli kwa ajili ya Tanzania yetu. Sasa changamoto inakuja kwamba, mwingine anasema yupo tayari kuhama hata kama bila kupewa hela za uhamisho na hela za mizigo. Akishahama hatujafuta sheria, akirudi

anaenda kudai hela yake ya mzigo kwamba hakupewa. Yanarudi malimbikizo tena, huku wakati huo tunahitaji ku-*balance* ikama ya maeneo ambayo ni *remote area* na *difficult to reach*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna maeneo ambayo mengine kwa kweli hayapo *privileged* kulingana na ule umbali. Sasa wakishahama wote, tukajaa Dar es Salaam, wote tukajaa Dodoma na wote tukajaa Arusha, mwisho wa siku maeneo ya Tanganyika na maeneo mengine, hawapatikani. Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy anakubali hapa kwamba wapo Madaktari wanataka kuhama, watumishi wanataka kuhama. Lazima tufike sehemu tuitendee haki nchi yetu na tuseme kweli kulingana na changamoto ambazo tunazipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hatujakataa suala la kuhama, ni sahihi na vigezo vilivyowekewa kisheria vitakuwepo, lakini Serikali lazima itafanya uchunguzi na kuangalia na kufanya mapitio ya yule ambaye anastahili kuhama, atahama bila ajizi yoyote na bila mkwamo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hayo machache, naomba kuunga mkono hoja, lakini nikiendelea kusema kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan yupo makini katika kuhakikisha nchi yake na Serikali yake inafikia malengo ambayo amewaahidi Watanzania. Mpango wa Maendeleo tutautekeleza, na pia Ilani ya Chama cha Mapinduzi tutaendelea kuitekeleza bila ajizi. Ndiyo maana umeona miradi yote ya maendeleo tumeshafika 90% mpaka 98%, tunamaliza. Hakuna mwananchi au jimbo ambalo halijaweza kupelekewa miradi ya maendeleo na ushahidi huo wewe mwenyewe umezidi kuona.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, kama ni taarifa tutaipata baadaye muda wa taarifa ya habari saa mbili asubuhi. *(Makofi /Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kikwete.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na wote waliotangulia kusema, kwanza, kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia afya iliyo njema na hata leo tupo mbele yako ukituongoza, tukiwasilisha kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wangu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, *Comrade* Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, *GBS*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu mimi binafsi nianze pia kwa kukushukuru wewe, kwanza kwa kuongoza kikao chetu vizuri. Pia kwa upekee kabisa namshukuru Mheshimiwa Spika kwa kuongoza Bunge hili vizuri, ameendelea kuwa Spika wa mfano, Spika anayetupa heshima na kwa kweli Spika wa viwango vikubwa. Nasi kwa kweli tunaendelea kumshukuru sana kwa uongozi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, nami niungane na waliotangulia kusema kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri ambayo ameendelea kuifanya. Ni wazi kabisa kutokea kwenye michango ya Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia wamedhihirisha kabisa kwamba Mheshimiwa Rais wetu ni Rais wa mfano wa kuigwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nirudi katika maneno mazuri yaliyosemwa na ndugu yangu Mheshimiwa Mohamed Said Issa, Mbunge wa Konde, ambaye alisema, kwa kweli akipata nafasi ya kupiga kura atamchagua Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maneno haya ni maneno mazito, maneno ambayo hayapaswi kupuuzwa, na pia ni maneno ambayo yanaonesha wazi kwamba naye anakubali kazi nzuri inayofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa kweli huu ni mfano wa wazi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, nawashukuru sana wote ambao wanamsaidia ambao kwetu sisi; mimi na Mheshimiwa Waziri wangu wamekuwa ni viongozi wetu. Nikianza na Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dkt. Philip Isdor Mpango, yeye pamoja na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Dkt. Doto Mashaka Biteko, kwa kweli kazi nzuri inayofanyika ni wazi kabisa nchi yetu imepiga hatua kubwa ya kimaendeleo toka sehemu moja

kwenda sehemu nyingine na hili linashuhudiwa kwa vitendo kutokea kwenye kazi zao, usimamizi wao na maelekezo ambayo kila siku wamekuwa wanayatoa, nasi Mawaziri wao tunatekeleza kazi hizo kwa juhudi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siwezi katika salamu za shukurani nikamsahau Waziri wangu, ndugu yangu, *Doctor*…

**MBUNGE FULANI:** He, amekuwa *Doctor*?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetaja madaktari hapa nimeona, nikampa naye Mheshimiwa Dkt. George Boniface Simbachawene. Mwenyezi Mungu atamjalia atafika huko. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri mimi binafsi kwa niaba ya wenzangu wote ndani ya Wizara. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitumie nafasi hii kabla sijaingia kwenye michango hii mizuri ya Waheshimiwa Wabunge, kumshukuru sana, kwanza kwa uongozi wake, na pia mazingira mazuri ambayo anatengeneza ndani ya Ofisi yetu. Amefanya Ofisi imetulia, anatoa ushirikiano mkubwa, maelekezo yake, maangalizo yake, kwa kweli ni Waziri wa mfano na Mwenyezi Mungu amjalie katika safari yake ya uongozi, basi ampandishe madaraja. Mwenyezi Mungu ampe na mengineyo ndani ya nyumba yake ili tuweze kuyaona na sisi tulio chini yake tuendelee kufaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wa leo, tumepata bahati ya Waheshimiwa Wabunge 23 kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara yetu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Michango yote imejikita katika maeneo ya kimsingi kabisa ambayo yameelekezwa kuwa ndiyo kazi yetu ya msingi kabisa sisi ndani ya Ofisi ya Rais, inayosimamia Utumishi na Utawala Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, nataka kuanza kwa kulikumbusha Bunge lako kwamba, msingi mkubwa wa ofisi yetu ni usimamizi wa sheria, sera na taratibu ili kuweza kuisadia nchi katika

kuhakikisha kwamba Utawala Bora na Utumishi wa Umma unaendelea kustawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, yote yaliyozungumzwa hapa kwa mfano kwenye upande wa Utawala Bora, Waheshimiwa Wabunge wameeleza juu ya mambo ya msingi ambayo wao wanayaona kwamba yana changamoto kwa upande wao; siyo huko tu, pia hata katika eneo la Utumishi wa Umma, nalo pia wameeleza mambo ya msingi ambayo wanaona kwamba yana changamoto kwa upande wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, pia katika michango yao wametumia nafasi hiyo kuishauri Serikali juu ya maeneo ya kimsingi ambayo wanadhani yakifanyiwa kazi, yakiwekwa vizuri au yakiangaliwa kisera na kisheria mambo yatakuwa mazuri zaidi kuliko ilivyokuwa jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niendelee kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba, sisi ndani ya Serikali tukiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Waziri wetu, Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, kazi ya kuendelea kuangalia sera, sheria na taratibu kuendelea kuongoza nchi yetu, tumeshaanza kuifanya na tunaendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo ambayo kutokea kwenye michango ya Waheshimiwa Wabunge, imejidhihirisha wazi kwamba tunayo kazi ndani ya Wizara yetu ya kuendelea kutoa elimu kwa Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu yapo mambo yanafanyika ndani ya Wizara na kwa michango ya Waheshimiwa Wabunge ni wazi kabisa yanaonekana mawasiliano kutoka kwenye Wizara yetu kuja kwa Waheshimiwa Wabunge kwa maana ya wananchi, bado yamekuwa ni hafifu. Katika mchango wangu au katika uchambuzi wangu nitayagusia maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nianze kwa hoja ambazo zimeelezwa na Waheshimiwa Wabunge hasa katika eneo hili la *TASAF*. Katika hoja ambayo imeelezwa na Waheshimiwa Wabunge iliyochangiwa ni kwamba, Serikali iharakishe upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa ili kuwawezesha wananchi wenye sifa za kunufaika na mradi wa *TASAF* kupata fursa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nilihakikishie Bunge lako kwamba, *TASAF* imeingia kwenye mkataba wa makubalino *(MOU)* kwa kushirikiana na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* kufanya mazoezi maalum ya kusajili na utoaji wa Namba za Vitambulisho vya Taifa kwa wanufaika wa mradi huo. Mpaka sasa wanufaika wa *TASAF* 680,816, wameshasajiliwa na kupokea ruzuku zao kwa njia ya elektroniki, kigezo kikubwa kikiwa ni kupatikana kwa hivyo vitambulisho vya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge Omar Ali Omar yeye ameeleza na amesikitika sana juu ya utaratibu ambao unaonekana kwamba kuna baadhi ya watu wapo juu ya sheria, miongozo na taratibu zinazosimamia miradi miradi ya *TASAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naliambia Bunge lako kwamba, kama malalamiko hayo yapo, namwomba Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kwa ujumla waendelee kutuletea ili tuyashughulikie. Isitoshe katika hilo, miongozo inayosimamia mradi wa *TASAF* inaelekeza wazi njia ya ku-*deal* na malalamiko ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kama inatokea kuna tatizo katika ngazi ya shehia, basi kwanza malalamiko yanatakiwa yapelekwe katika Kamati ya Uchambuzi kwamba, sijafanyiwa haki na ninahitaji kufanyiwa haki hiyo, lakini kama ataona pale katika shehia ambapo ndiyo matatizo yametokea labda wale watu wamekusanyana kwa pamoja dhidi yake, basi utaratibu unaelekeza kwamba, malalamiko yapelekwe katika ngazi ya wilaya, hasa kwa Wakurugenzi ili waweze kusimamia na kuchambua vizuri malalamiko hayo. Pale watakapoona kweli mtu huyu ana haki, lakini hakupendekezwa katika mradi, basi uamuzi wa kumrudisha ili awe sehemu ya wafaidika utafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo mtu huyu ataona pia Mkurugenzi katika ngazi ya wilaya hajafanya haki, basi utaratibu wa kukata rufaa kwenda Makao Makuu inabidi ufanyike ili mfaidika huyu aweze kupata haki anayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako kwamba, utaratibu huo unafanyika na uko wazi. Naomba yeye aendelee na kama ataona mambo yanakwenda hovyo, basi Ofisi ya Waziri na Ofisi ya Naibu Waziri zipo wazi, tuletee tuyashughulikie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia *4R* alizosema Mheshimiwa Rais, moja ya kazi kubwa ni kuhakikisha kwamba sisi wasaidizi wake tunawafikia mara moja wananchi wetu na tunakutana na changamoto wanazokabiliana nazo ili kuweza kuzitatua. Katika kufanya hilo, nataka kulieleza Bunge lako kwamba, tumepokea malalamiko 52,376 na baada ya kudodosa kaya hizo, tumeridhika kwamba kaya 7,412 zinajitosheleza katika vigezo na zimerudishwa katika mpango, lakini kaya 44,964 ambazo hazijajitosheleza katika vigezo, zimetolewa baada ya rufaa zao kushindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mwingine ni Serikali ihahakikishe matokeo ya rufaa za waombaji wa kujiunga na mradi wa *TASAF* yanatolewa mara moja. Ushauri umepokelewa na kuzingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulieleza Bunge lako kuwa Serikali inaendelea kufanyia kazi rufaa zilizopokelewa kama ambavyo nimeeleza na ambapo sasa tunapozungumza kaya zile ambazo nimezitaja 7,412 ambazo zimeleta rufaa zake na kusikilizwa, zimeshajulishwa. Hapa tunapozungumza, watu wapatao 1,300,000 kutoka kwenye kaya hizo wanaendelea kufaidika na mradi huu wa *TASAF*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo pia wapo baadhi ya wajumbe ambao walizungumza na kuitaka Serikali iendelee kuimarisha misingi ya utawala bora pamoja na kuboresha mifumo ya utendaji kazi katika utumishi wa umma, sambamba na kuboresha mishahara na maslahi ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninataka nizungumzie eneo la watumishi na mishahara. Serikali imepokea ushauri huo na inaendelea kusimamia misingi ya utawala bora kwa kuzingatia uwajibikaji, uwazi na ushirikishwaji. Katika kuboresha mifumo ya utendaji kazi, Serikali imejenga mifumo ya kielektroniki katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya kusimamia utendaji katika utumishi wa umma, ukiwemo Mfumo wa

*PEPMIS* na *PIPMIS* ambao unawezesha kupima utumishi na ufanisi wa kazi wa watumishi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, kwa sasa mambo yote yanayohusu utumishi wa umma yanapimwa kwa kupitia vigezo ambavyo vimeainishwa na *PEPMIS* na *PIPMIS*. Kupitia Mfumo wa *PEPMIS* na *PIPMIS* wafanyakazi wanaweza kuorodhesha majukumu yao na vigezo vya kuwapima watumishi hawa vinatumika kwa kupitia vigezo vilivyowekwa katika utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wajumbe wengi wamezungumzia jambo la msawazo wa watumishi wa umma, hasa katika maeneo ambayo yanaonekana kwamba kuna shida kubwa ya watumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa maneno mazuri ambayo yameelezwa na Naibu Waziri, Mheshimiwa Katambi wakati anatoa mchango wake kuhusiana na hoja iliyowekwa Mezani. Nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa Serikali katika utaratibu wa kusimamia utendaji kazi, imebuni mfumo unaoitwa *HR Assessment*. Mfumo huu unaiwezesha Serikali kujua idadi ya watumishi katika maeneo yao, ni wapi ambapo kuna upungufu mkubwa na ni wapi pana uhitaji mkubwa ili kuwezesha mipango na misawazo ya utumishi wa umma kuweza kukaa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kueleza jambo hili, nataka nirudi katika maneno au hoja iliyoelezwa na Mheshimiwa Yahaya Massare, Mheshimiwa Francis Isack Mtinga na Mheshimiwa Lujuo Mohamed Monni ambao wamezungumza hasa katika eneo la hitaji la walimu na upungufu mkubwa wa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako kuwa, pamoja na changamoto hiyo, Serikali kupitia Mfumo wa *HR Assessment* inaendelea kupanga na kukamilisha zoezi la tathmini ya rasilimali watu ili kubaini upungufu au ziada ya walimu na watumishi wa kada mbalimbali katika Halmashauri zetu. Katika kufanya hivyo, Wilaya ya Mkalama na Wilaya ya Iramba zimetengenezwa nafasi za ajira mpya 86 na 70 za msawazo wa kada ya ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, pia nalikumbusha Bunge lako kwamba, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali ilitarajia kuajiri walimu 10,505 ili kupunguza changamoto ya upungufu wa walimu, lakini katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imetenga jumla ya nafasi za ajira mpya 10,590 za kada ya ualimu ili kuendelea kujaza nafasi katika maeneo yenye upungufu wa watumishi wa kada hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kwa upande wa Wilaya ya Mkalama na Iramba katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2021/2022 hadi sasa, walitengewa nafasi za ajira mpya 192 na 175 za mtawala wa kada ya ualimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi ameeleza masikitiko yake, hasa katika eneo la malimbikizo ya mishahara ya watumishi na kwamba bado kuna maeneo hawajalipwa malimbikizo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kulikumbusha Bunge lako juu ya kazi kubwa ambayo inafanywa na Serikali, hasa baada ya muundo mpya wa mfumo wa taarifa ambao unaitwa *HCMIS*. Mfumo huu unaiwezesha Serikali siyo tu kupata taarifa za watumishi, lakini pia katika kupanga vizuri mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, pia napenda kulieleza Bunge lako kwamba, mfumo huu kwa namna moja au nyingine umewezesha watumishi kutokuwa na malimbikizo ya madai kutokana na kupandishwa vyeo kutokana na mabadiliko ya miundo kwa sababu sasa, kupitia mfumo huu mfanyakazi au mtumishi wa umma anapopanda daraja pale pale mabadiliko ya mishahara na taarifa zake, ikiwemo posho zake anazostahili nayo pia yanabadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kueleza mbele ya Bunge lako kwamba, kwa mwaka 2021/2022 hadi 2023/2024 Serikali imelipa zaidi ya shilingi bilioni 193.15 kwa watumishi 118,584 wenye madai. Aidha, Serikali inaendelea na uhakiki wa madeni yaliyowasilishwa kwa waajiri kwa ajili ya malipo. Hadi sasa madai ya malimbikizo ya watumishi 21,660 yenye jumla ya shilingi bilioni 45 yamehakikiwa na yanasubiri kulipwa na Serikali kulingana na uwezo wa bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Joseph Kakunda amehimiza na kuikumbusha Serikali kufuatilia uzingatiaji wa maadili ya watumishi wa umma sehemu za kazi. Kwanza nalihakikishia Bunge lako kwamba mawazo mazuri yaliyotolewa na Mheshimiwa Mbunge tunayabeba na kwenda kuyafanyia kazi, lakini katika kufanya jambo hilo, Serikali inaendelea kutoa mafunzo ya maadili kwa watendaji na watumishi wa umma ili kuwakumbusha wajibu wao wa kazi pamoja na kutekeleza mipango na malengo ya Serikali. Mpaka sasa tunapozungumza jumla ya watumishi 24,922 wamepatiwa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya taasisi 92 zimefanyiwa ufuatiliaji na kubaini maeneo yenye upungufu katika kuzingatia maadili na kuchukua hatua stahiki. Jibu hili ninalotoa hapa ni sanjari na mazungumzo au kumbusho lililotolewa na Waheshimiwa Wabunge kwamba, Tume yetu ya Watumishi wa Umma siyo tu isubiri kesi na kufuatilia mienendo, pia iende katika taasisi na Idara za Serikali ili kuweza kujua ni nini ambacho kinatokea hasa katika stahiki na haki za watumishi hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, pia Mheshimiwa Kakunda ameeleza kuwa kuna wakati uanzishwaji wa *OPRAS* ulipigiwa debe sana, lakini hajui kiutendaji *OPRAS* hiyo imepimwa vipi na ni lini imefanyiwa tathmini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kulieleza Bunge lako kuwa, kwanza Mfumo wa *OPRAS* kwa sasa haupo. Sasa hivi mfumo unaotumika kupima utendaji kazi unaitwa *PEPMIS* na matokeo ya mtendaji mmoja mmoja wa *PEPMIS* ndiyo unaitwa *PIPMIS* kwa maana ya taarifa ya taasisi au ofisi ambayo inasimamia watumishi wa umma. Mfumo huu umeanza kutumika katika kupima utendaji kazi wa Watumishi wa Umma katika mwaka wa fedha 2023/2024, baada ya Serikali kutoa waraka na kufuta mfumo ule wa zamani wa *OPRAS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango mwingine umeelezwa na Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage, ambaye ametaka mtumishi anapobadili kada asianze katika cheo kipya au mshahara wake uweze kusomeka kama ulivyokuwa zamani, na kwamba, watumishi wa umma ambao wamejiendeleza kielimu ndiyo ambao wanakabiliana sana na changamoto hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nitumie mfano mmoja, hasa watu ambao wamesomea shahada ya kilimo. Kwa mtumishi wa umma ambaye ana Stashahada ya Kilimo ambayo ndiyo imemfanya aajiriwe katika kazi, pale anapokwenda kujiendeleza na kutunukiwa Shahada ya Kilimo kwa maana kwamba sasa ametoka katika stashahada, ameingia katika shahada, mara nyingi miundo ya kazi nayo hubadilika, kwa sababu, sasa huyu anakuwa ni Bwana Kilimo, lakini yule mwenye stashahada ya kazi kwa mujibu wa vyeo vya kimuundo anakuwa ni Afisa Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu hawa wawili wote wana vyeo tofauti, lakini anapofika kwenye ngazi ya juu kabisa katika ngazi ya cheti, kwa maana ya mtu mwenye stashahada, maana yake ni mshahara wake unaweza kuwa juu ya mshahara ambao akiwa na shahada anaenda kuanzanao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulieleza Bunge lako kwamba, inapotokea mtu ana mshahara mkubwa katika nafasi ya cheo anachoomba kubadilishwa, basi maombi kwa ajili ya kumwezesha kuondoka na mshahara wake ule ulio juu, yanafanyika kupitia Ofisi ya Katibu Mkuu Utumishi. Kibali kinapotolewa, utaratibu wa kumhamisha mtu huyo na mshahara wake unafanyika ili aweze ku-*enjoy* uwepo wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge pamoja na Bunge lako kwamba, taratibu zipo wazi. Tunachoomba ni watumishi wa umma mfuate taratibu ili mambo yaende vizuri katika stahiki zenu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hoja nzuri zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, lakini wapo baadhi yao ambao wametaka kujua juu ya mifumo mipya ya Sekretarieti ya Ajira inavyofanya kazi katika eneo zima la usaili wa vijana wetu. Mheshimiwa Francis Mtinga ameeleza kwamba, utaratibu uliopo unafanya baadhi ya vijana wasafiri umbali mrefu, kwa mfano, wapo ambao wanatoka Kigoma, Mwanza, Bagamoyo, Lindi na Mtwara kuja kufanya usaili katika Mji wa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelekezo yaliyotolewa na Kiti chako ya kutaka Sekretarieti ya Ajira iangalie tena utaratibu wa jinsi ambavyo watumishi wapya wa umma wanapatikana, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri George Boniface Simbachawene, naomba kuliarifu Bunge lako kwamba, tumeanza usajili kwa njia ya kidijitali ambapo sasa *online aptitude test* imeanza kufanya kazi na mara ya kwanza ilipotumika usaili ulifanyika Tanzania nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako kwamba, katika siku ulipofanyika usaili kwa mara ya kwanza kupitia utaratibu huu mpya, hatukupata lalamiko lolote. Baada ya utaratibu huu kuonekana umefanikiwa, malengo ya Serikali ni kuhakikisha taratibu nyingine za usaili wa vijana wetu katika kada zote unaingia katika utaratibu huu wa *online aptitude test system* ili waweze kupata nafasi ya kufanya usaili katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako kwamba, kwa wale vijana wanaotokea Singida, kwa utaratibu huu mpya maana yake ni watafanya usaili Singida. Hivyo ndivyo itakavyokuwa pia kwa watu wote wanaotokea katika kona zote za Tanzania, ikiwemo wale wenzetu wanaotokea upande wa Visiwani au Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, pia Mheshimiwa Mbunge Dkt. Alice Kaijage amezungumzia eneo la Sekretarieti ya Ajira, anapenda aone uwezekano wa kutoa kipaumbele kwa waombaji kazi waliohitimu vyuo muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendeshaji wa michakato ya ajira katika utumishi wa umma unazingatia Sera ya Menejimenti ya Ajira ya Mwaka 2008, Sheria ya Utumishi wa Ajira Sura ya 298, na Kanuni ya Uendeshaji wa Shughuli za Sekretarieti ya Ajira ya Mwaka 2021. Aidha, kanuni ya 18 (2), (c) inampa kipaumbele msailiwa mwenye umri mkubwa kupangiwa kazi pale inapoonekana amepata alama za ufaulu. Kwa hiyo, nalihakikishia Bunge lako kwamba, utaratibu huu unaendelea, lakini najua kwamba hapa kinachozungumzwa hasa ni watu ambao wamemaliza shule muda mrefu na hawajapata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka kulikumbusha Bunge lako kwamba, ndani ya vikao vya Bunge hili tumekubaliana kwamba, ajira

zote ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mujibu wa sheria, zitatolewa kwa njia ya ushindani. Kwa hiyo, sisi ndani ya Sekretarieti ya Ajira au ndani ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma tunachokifanya ni kusimamia sheria, sera na taratibu tulizokubaliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawahakikishia Waheshimiwa Wabunge, mijadala juu ya hao wenzetu ambao wamemaliza shule muda mrefu na hawajapata nafasi za kuajiriwa inaendelea kujadiliwa ndani ya ofisi yenu. Katika kufanya hivyo, chini ya uongozi wa Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, ninaamini kabisa kwamba majibu yatakapokuwa tayari tutayaleta mbele ya Bunge na huenda yakachagiza kubadilishwa kwa sera, sheria na mambo mengine. Haya yote yanayozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge tunayachukua na tunakwenda kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninazungumza juu ya ujenzi wa mifumo. Mheshimiwa Yahaya Massare amekuwa na tamaa ya kutaka kujua sana na ninadhani hili ni kwa Bunge lako lote, kwamba mifumo imekuwa inalalamikiwa kwamba haisomani. Hili limekuwa ni changamoto kubwa sana lakini pia Bunge lako limezungumza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie wewe na Bunge lako kwamba juhudi kubwa sana zimeendelea kufanyika ndani ya Serikali. Moja ya eneo kubwa ambalo limefanyiwa kazi ni kutengenezwa kwa mfumo wa kubadilishana taarifa ambao unaitwa *Government Enterprise Bus* au kwa lugha ya ki-TEHAMA inaitwa *GovESB*. Hadi sasa taasisi 122 ambazo zinatumia mifumo 132 zimeweza kuunganishwa na zinabadilishana taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuthibitisha hili, nataka nitoe mfano wa Mfumo wa Haki Jinai ambapo wenzetu wa Jeshi la Polisi, Mahakama, Ofisi ya *DPP* na wenzetu wa TAKUKURU, mifumo yao inabadilishana taarifa kwa sasa. Sasa hivi likifunguliwa jalada katika ofisi, labda katika Jeshi la Polisi, basi jalada lile likiwekwa tu ndani ya utaratibu, Ofisi ya *DPP* itapata taarifa, wenzetu wa TAKUKURU watapata taarifa, pia Mahakama nayo itapata taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hilo tu, pia mfumo huo umewezeshwa na mfumo mwingine wa malipo wa Serikali ambao unaitwa *GePG* ambapo mfumo huo umeunganishwa na mifumo yote ya watoa huduma wa simu. Ikiwemo hawa wenzetu wa *Vodacom, Tigo, Halotel*, *TTCL* na wengine wote ili kuwezesha mifumo yote kusomana. Leo hii mimi ninayetumia simu fulani ya kampuni fulani, nikitaka kufanya malipo kwa simu ya kampuni nyingine kupitia Mfumo wa *GePG,* malipo yanawezekana na mambo yanakwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niendelee tena kuishukuru Serikali yangu. Pili, namshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na wasaidizi wake wote wakiongozwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais, kwa kazi nzuri inayoendelea kufanyika ya kuwahudumia Watanzania; kuwahudumia watu wote ambao wana mahitaji bila kusahau kaya masikini zinazohudumiwa na *TASAF* ambapo Serikali imeendelea kuongeza pesa kila siku kuhakikisha kwamba tunawaondoa Watanzania katika umaskini, huku ikibuniwa miradi ya mfano wa kipekee kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa maelezo mazuri. Mheshimiwa Mtoa Hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda nimshukuru Mungu kwa namna ambavyo siku ya leo imeanza na inaenda kwisha na sasa umenipa nafasi ya kuhitimisha hoja ambayo niliitoa asubuhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yetu imepata wachangiaji wengi sana na ninakupongeza sana. Kwa siku moja kupata wachangiaji 23 pamoja na Kamati ni 24, ni wachangiaji wengi sana na michango ilikuwa ni mizuri sana. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla wale ambao mmechangia na wale ambao hamkuchangia, lakini kwa nyakati tofauti mmekuwa mkileta maoni yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi haya yote tunayachukua na pengine inaweza ikawa siyo rahisi sana kuyajibu yote, lakini tutafanya utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba kila hoja iliyotolewa hapa itajibiwa vizuri kwa maandishi na kila Mbunge ataipata kwa utaratibu ambao upo hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, niseme mwelekeo na dhamira ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kutaka kujenga utumishi wa umma unaowahudumia wananchi na ndiyo maana tumeomba fedha hizi. Tunataka kujenga utumishi wa umma unaowahudumia wananchi na ambao unachagizwa na matumizi ya teknolojia katika kuboresha huduma kwa wananchi na kupeleka huduma kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anayo dhamana ya Watanzania wote ambao wameweka dhamana yao kwake, lakini hawezi kufanya kazi yeye peke yake. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Katiba yetu amekasimu majukumu haya kwa wasaidizi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kazi kubwa ya sisi wasaidizi pamoja na watumishi wote wa umma ni kuhakikisha kwamba tunawahudumia wananchi na kufanya huduma hizo ziwe bora. Huduma hizo zinapaswa ziwe za heshima, zisizokuwa na rushwa na kusimamia uwajibikaji wa watumishi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana nasema suala la kuwahudumia Watanzania kwa msukumo wa teknolojia na hasa mifumo ambayo tumeijenga ni maelekezo yake Mheshimiwa Rais na ndiye atakayetutoa katika misukosuko ya kutokuwa na huduma stahiki kwa wananchi wetu. Ndiyo maana tunafikiri tangu tumeanza kutumia mifumo, kumekuwa kuna huduma bora na tutaendelea kuboresha hii mifumo kwa sababu tumeona ndiyo njia na nyenzo pekee ya kututoa hapa tulipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema asubuhi na nikanukuu maelezo ya Hotuba ya Mheshimiwa Rais ya tarehe 22 Aprili, 2021 wakati akihutubia Bunge la Kumi na Mbili, mstari ule wa mwisho amesema; "Wajibu wa Watumishi wa Umma ni lazima uendane na haki zao." Tangu ameingia Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu

Hassan, mabadiliko na mapinduzi makubwa katika utumishi wa umma yametokea, tena ni makubwa sana sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa kuna mkwamo wa kupanda madaraja kwa muda, kulikuwa kuna mkwamo wa kupanda kwa mishahara kwa muda, kulikuwa hakuna *annual salary increment* kwa muda na kulikuwa kuna madeni ya watumishi ya muda mrefu. Haya yote, kwa muda wa miaka mitatu toka alipoingia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alisema Hapana, lazima watumishi wa umma wapate haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *annual salary increments* kwa mwaka 2023/2024 ilichukua kiasi cha fedha ya bajeti ya Serikali shilingi bilioni 153.9, hizi zililipwa kwa mwaka ule. Katika mwaka huu wa fedha ambao tunakwenda nao, huu tunaokwenda kuuombea fedha 2024/2025, fedha zimeombwa kwa ajili ya kuwalipa hiyo *annual salary increment,* kwa sababu sasa *consistency* inaenda kila mwaka, kitu ambacho hakijawahi kutokea, tunaomba shilingi bilioni 150.8. Hali hii itaendelea *consistently* kwa *spirit* hii ya Mheshimiwa Rais kwamba hataki dhuluma kwa mtu, kila mtu apate anachostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, suala la madai ya malimbikizo ya mishahara kwa watumishi 26,331 yenye jumla ya shilingi bilioni 39.055 kutoka Wizara, idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika na taasisi za umma yamehakikiwa na kulipwa kwa watumishi stahiki. Kulipa fedha hizi kutoka kwenye bajeti katika mazingira tuliyokuwanayo, tumetoka kwenye *COVID* na uchumi umedorora duniani, ni utashi wa kiongozi wa nchi na siyo maamuzi mepesi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama vile haitoshi, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ya Awamu ya Sita imerejesha utaratibu wa kuwapandisha vyeo watumishi wenye sifa stahiki kila baada ya miaka mitatu, badala ya minne iliyokuwa inapigiwa kelele na watumishi. Sasa utaratibu wa kupanda vyeo ni baada ya miaka mitatu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi kama inavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameridhia kupandisha vyeo watumishi 81,515 waliokasimiwa katika bajeti ya mwaka 2023/2024 kwa gharama ya kiwango cha shilingi bilioni 130.47.

Hii siyo fedha ndogo. Pia, Serikali imepanga kuwapandisha vyeo watumishi 219,924 waliokasimiwa katika bajeti hii tunayoiomba na gharama yake ni shilingi bilioni 252.7. Fedha hizi ni nyingi, na unapokuwa Rais ukaamua kuzipeleka huku na nchi ina mahitaji mengi, maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba Rais huyu anawapenda watumishi wa umma wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, lazima watumishi wa nchi hii wamwone Mheshimiwa Rais ni mkombozi wao, lazima wamuunge mkono, na pia wamwombee kwa sababu ana changamoto katika meza ya matumizi mengi, lakini anawagawia wao anawaweka wa kwanza na mambo mengine yanafuata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imelipa mishahara ya wafanyakazi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa 113 zilizopo chini zenye jumla ya watumishi 691 kwa awamu. Kwa awamu ya kwanza Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya kugharamia mishahara ya watumishi 474 wa Mamlaka za Serikali za Mitaa 101 ambazo zimebainika zina uwezo mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka Waheshimiwa Wabunge na wengi wamechangia hapa, bila kutaja majina ya waliochangia kwa sababu ya muda, halmashauri zilizokuwa hazina uwezo zilikuwa zinashindwa kulipa watumishi hawa, lakini Serikali imechukua watumishi hawa kutoka halmashauri 101. Ninaamini kwenye awamu inayofuatia tutamalizia na wengine wote waliobakia ili walipwe kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na kule kwenye halmashauri tutaweka utaratibu mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisisitize, madeni ya watumishi hawa ambayo wanadai Mamlaka za Serikali za Mitaa ziwalipe. Sisi tutaanza kuchukua hatua kwa wale Wakurugenzi ambao tunawapelekea maelekezo ya kulipa stahiki za madeni yanayotokana na watumishi waliokuwa chini yao, halafu hawafanyi hivyo. Tutachukua hatua za kisheria ya kiutumishi kwa sababu sasa inakuwa kama mchezo. Watumishi wanakuja ofisini kwetu, wanalalamika, tukiwaambiwa walipwe na tunawandikia, lakini Wakurugenzi hawataki kuwalipa. Tutachukua hatua kali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mtiririko wa michango ambayo tumeipokea, mchango wa kwanza kabisa ni mchango wa Kamati. Kamati yetu pendwa, Kamati ya Utawala, Katiba na Sheria yenye Wajumbe makini sana. Nasema kwamba ni Wajumbe makini kwa sababu ya namna tunavyofanya nao kazi. Tunafanya nao kazi kitaalam sana. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote na maoni yenu yote sita, tunayachukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hili la msawazo wa watumishi. Ni kweli maelezo ya Waheshimiwa Wabunge yana ukweli ndani yake, kwamba yako maeneo ambayo yana upungufu wa watumishi, lakini yako maeneo mengine ambayo yana watumishi wengi kupita kiasi. Watumishi hawa wanang'ang'ania maeneo yale ambayo yana mazingira mazuri na kuacha yale maeneo ya pembezoni na vijiji yakiwa yana uhaba wa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali tumeshaamua, sisi Wizara ya Utumishi, TAMISEMI na wenzetu wa Wizara ya Fedha, tumemaliza kujadiliana na maamuzi yamefikiwa kwamba tukimaliza bajeti hii tutakuwa na fedha ya kuhakikisha kwamba tunaenda kufanya msawazo wa watumishi nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme hapa, Waheshimiwa Wabunge msirudi tena kuanza kulalamika kwa sababu tutakapoanza hii *operation* haitamwacha mtu na haitakuwa na upendeleo, lakini tutazingatia hali na sababu mahususi walizonazo watumishi wetu. Katika kufanya hili, liko suala limezungumzwa hapa la wenza kufanya kazi maeneo tofauti tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwajiri ni Serikali na Serikali tunahimiza maadili, lakini tunapenda sana na mpaka tuna Sera ya Magonjwa ya Kuambukiza ukiwemo UKIMWI. Tunapowaweka wenza maeneo tofauti kama kuna mambo ambayo mimi huwa yananiuma ni pamoja na jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme kwa kutumia nafasi hii ya msawazo, tutahakikisha kila mwenye mwenza wake wa kweli wanakwenda kufanya kazi katika eneo moja. Siyo lazima iwe kituo kimoja cha kazi. Kama ni walimu, basi huyu atafundisha shule hii na

huyu atafundisha shule hii, lakini ni maeneo ambapo jioni wanakwenda kulala pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwe wakweli, jambo hili limekuwa linatukera. Waheshimiwa Wabunge wote na wengi mna maombi na mnaleta kwa Mheshimiwa Mchengerwa na kwangu kwamba tusaidie hawa wamefunga ndoa. Ukiwa na cheti cha ndoa na umefunga ndoa ya kweli, maana kuna ndoa nyingine za uongo uongo, hili hatuwezi kulikubali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutahakikisha kwa kutumia mwanya huu wa msawazo, basi kila mtumishi ambaye mwenza wake yuko mbali, basi tunawaunganisha ili waweze kufanya kazi kwa raha na mustarehe. Mimi naamini hii itaongezea tija katika utendaji wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu akiwa na mwenza wake yuko mbali, kuna kesi tunazipokea. Mimi nina mwalimu wangu mmoja mwanamke katoka Kigoma, kamfuata mume wake Shule ya Sekondari Mbuga. Amefika pale, sasa likizo imeisha anatakiwa kurudi. Unamwona anavyosikitika kwamba anaacha mume wake anakwenda mbali ambako hawataonana kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu hiki hakikubaliki na inaweza ikawa ni kinyume cha haki za binadamu. Kwa hiyo, ni lazima tutakisimamia na tutahakikisha kwamba tunatumia fursa hii ya bajeti kuweza kuweka msawazo na kuhakikisha kwamba wenza wanakaa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, mmezungumzia suala la ndege za Serikali, kwamba suala la *TGFA*, zile ndege ambazo zimenunuliwa na Serikali na kwamba zipelekwe *ATCL* kwenye shirika letu la ndege ambalo linaendelea kufanya vizuri sana, hili jambo tumeshalizungumza kwenye Kamati na kwamba tuko kwenye hatua za mwisho za kumalizia kuhamisha hizi ndege kwenda *ATCL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhamisha ndege siyo sawasawa na kuhamisha gari au pikipiki. Ina mchakato wake wa kitaifa, lakini pia wa kimataifa. Kwa hiyo, kuna mambo mengi ya kuyaangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni vitendea kazi vya mifumo. Hili tunalichukua. Mifumo tuliyoijenga na hasa inayosajili watumishi ili waweze kuweka malengo yao, ili wapandishe *details* zao na kuweka malengo yao na mpango kazi na baadaye waweze kupimwa na mpango huo, unaoitwa *PEPMIS,* mfumo huu wala hauhitaji teknolojia kubwa, ni uwepo tu wa *internet,* na kama hakuna *internet,* basi unaweza ukasogea mahali ambapo inapatikana na ukaweza kuingiza takwimu zako.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni sababu tu zinatolewa na wala vishikwambi haviwezi kutusaidia sana. Kinachoweza kutusaidia ni watumishi wenyewe kuamua kuingiza *data* zao kwenye mfumo. Mfumo huu baadaye ndiyo utakaochuja na kupandisha vyeo na ndiyo utakaochuja na kupandisha madaraja. Sasa kama hawataki kuingia, mathalani, mpaka sasa hivi 4,700 na ushei wamegoma kujiingiza kwenye mfumo kwa sababu ambazo hazieleweki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia humo ndani tumegundua wako wengine hawana vyeti stahiki vya kuingiza. Vilevile, humo ndani tumegundua wako wengine ni watoro wa muda mrefu, na huko ndani tumegundua kuna watumishi hewa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mkiona mnapigiwa kelele, muulize tu nipe *details* zako, halafu mwambie twende nikupeleke, kisha mlete kwangu. Halafu tuingie tuangalie, aniletee vyeti, tuingize kwenye mfumo. Mimi nafikiri kwenye hili ikitokea mtu anasema mimi sijaingia, nimefungiwa mshahara, mwambie twende nikupeleke, utaona ananyamaza. Watumishi wana sababu nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la fedha kupatikana kwa wakati, tumelichukua hilo. Pia suala la kuboresha maslahi na mishahara, kama nilivyoeleza, huu ni mpango endelevu na Mheshimiwa Rais anayo *political will* katika hili, ameamua kupandisha mishahara. Amefanya hivyo kwa vitendo na anaendelea kufanya hivyo. Kwa hiyo, tuamini kwamba hakuna kitakachosimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la rufaa za watumishi, mmesema juu ya rufaa za watumishi na ninyi mnakumbuka kwamba mmetuongezea bajeti kwa ajili ya ile Tume ya Utumishi wa Umma. Kwa hiyo, tutaenda kuongeza vikao na kuhakikisha kwamba rufaa nyingi zinashughulikwa kwa kasi kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja zote ambazo zimetolewa, nyingi wamenisaidia kujibu na namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye amezijibu hoja nyingi. Pia Mheshimiwa Katambi naye kazungumzia kuhusu kikokotoo na mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie hili la kukaimu, ambalo Mheshimiwa Francis na Mheshimiwa Rashid Shangazi wamelizungumzia. Kwanza kabisa, kukaimu kuna sifa yake, siyo kwamba mwajiri anaamua kukukaimisha tu. Kukaimu kuna sifa yake na sifa ya kukaimu ni lazima uwe na sifa ambayo cheo hicho kikitaka kuthibitishwa kwako unakuwa una sifa za cheo hicho. Usikaimishwe na ukikaimishwa ni lazima taarifa itolewe kwa Katibu Mkuu Utumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa waajiri wengi na hasa Mamlaka za Serikali za Mitaa na hata taasisi zetu wanawakaimisha watu kwa mapenzi yao na urafiki wao. Hata mahali ambapo yuko mwenye sifa ya kukaimu nafasi hiyo hakaimishwi na anakaimishwa rafiki yake au jamaa yake ambaye hana sifa. Ukianza mchakato wa kumthibitisha unagoma na anapoambiwa kwamba huyu hana sifa, anaenda kukaa kimya na lile *file* au ile barua na yule anaendelea kukaimu, ndicho kinachotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa na uharaka katika kufanya *vetting* na kuhakikisha kwamba wataalamu hawa ambao wana sifa hawakaimu katika nafasi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo limezungumzwa ni hili linalohusiana na malimbikizo ya mishahara, amesema Mheshimiwa Shangazi, na hili tumeshalitolea majibu lakini mengine amejibu Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ajira kwa Watendaji wa Kata; *WEO, VEO* na *MEO,* ajira hizi kwanza zinatolewa kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa na wala hazitolewi na Sekretarieti ya Ajira. Mchakato ule unafanyika kwenye Halmashauri na Sekretarieti ya Ajira inakwenda kusimamia tu.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, ajira hizi ziko kwenu na Waheshimiwa Madiwani wetu wanashiriki kujua ziko kiasi gani, lakini Kamati za Ajira ndizo zinazofanya kazi ile

zikishirikiana na Kamati za Ulinzi na Usalama. Kwa hiyo, tunaweza tukauliza yanayofanyika kule, kama mnadhani siyo sahihi tunaweza kushauriana nini kifanyike zaidi, lakini kwa kweli zimepelekwa kule na wala haziko *central* kwa maana ya Sekretarieti ya Ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzingatiaji wa maadili sehemu za kazi, Mheshimiwa Kakunda hili limejibiwa na Naibu Waziri pia. Mheshimiwa Janejelly mmetambulishwa viongozi, lakini jinsia haikuzingatiwa. Tuangalie *standards* katika nchi. Kwenye nafasi nyingi za kitaifa kwa mwaka 2023, makatibu kwa mfano Makatibu Wakuu, wanawake walikuwa 22.2% lakini mwaka 2024 waliongezeka na kuwa 25.6%. Kwa hiyo, ni ongezeko kubwa la wanawake katika nafasi hizi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makatibu Tawala wa Mikoa Wanawake kwa Tanzania Bara kwa mwaka 2023 walikuwa 30.8%, lakini wapo mpaka mwaka 2024, hivi tunavyozungumza wameongezeka kwa 46.2%. Ongezeko hili ni kubwa sana. Kwa hiyo, nchi yetu ni *gender sensitive* na tunazingatia sana na Mheshimiwa Rais ni *champion* katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajira za uwiano kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, uwiano tuliuweka kwa *formular,* ni 79% kwa 21% kwa ajira zile za Taasisi za Kimuungano. Kwa hiyo, kama yanayotokea kule Zanzibar pengine hayako sawasawa, tutajaribu kuwasiliana na wenzetu, tuwaambie kwamba kuna hili na pengine tutapata zaidi kwamba changamoto ni nini, kwa sababu umesema Mheshimiwa Mbunge, hatuwezi kuacha ku-*respond*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Alice amezungumzia mtumishi anapobadili kada kwamba asianze na cheo cha chini, aanzie na cheo kile kile. Tumekusikia, lakini ipo changamoto kubwa, kwa sababu, kama watu watatakiwa kuhama kada, hata ile *career development* huwezi kuipata vizuri. Kuna watu wana-*struggle,* yaani kuna watu wengine mimi nawajua nimesomanao, toka nilivyosomanao wameshasoma vitu vitatu vya aina tofauti na mpaka leo hata hawaajiriki.

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani kuna watu wako hivyo, anapenda tu kusoma, hataki hata *career development*. Umeajiriwa

kama Mwalimu, soma kutoka Mwalimu wa Msingi, ukawe Mwalimu wa Sekondari, ukawe Mwalimu wa Chuo Kikuu. Sasa wewe unataka kuhama, umekuwa Mwalimu unataka ukawe Mhasibu, ulikuwa Mwalimu unataka ukawe Afisa Mipango na ndiyo inaleta *confusion*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiruhusu hii kiholela, ndiyo maana tumeweka *caveat* pale, kwamba ukisoma ujue unakuja kuanza na moja, kwa sababu uzoefu unaotizamwa ni wa kazi ile, siyo wa kazi nyingine. Kwenye kazi ile ya Afisa Manunuzi, wewe huna uzoefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mwanao uliyemsomesha utamkuta akiwa *boss* wako, wewe unakuja kuanza chini yake. Kwa hiyo, rai yangu kwa watumishi wa Tanzania, hebu tuchague *career* tunazozipenda tukiwa bado wadogo na tuendelee nazo kuelekea mpaka juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini Wakuu wa Vitengo, Idara na Mamlaka za Serikali za Mitaa wanakaa miaka mingi; saba hadi kumi lakini Wakurugenzi wanateuliwa kutoka kokote kule? Mamlaka ya kuteua nafasi za kuteuliwa ni Mamlaka ya Rais na yanatokana na Katiba, kwamba Rais ana uwezo wa kuunda chombo chochote, lakini Rais anao uwezo wa kumteua mtu yeyote kwa ajili ya kufanya jukumu lolote katika nchi kwa maslahi ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hii itabakia hivyo kwa sababu haijaleta tatizo. Kwani wakiwa wamepewa ule uongozi, wewe si unaendelea na utumishi wako na hawa wanaoteuliwa. Jamani, kuteuliwa siyo raha. Mkitaka mwaulize walioteuliwa, halafu baadaye uteuzi ukaondoka, ni mateso. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuteuliwa siyo jambo la kujisifusifu na kufurahia na pengine ukiteuliwa, ujiulize kama huwezi bora useme, nashukuru sana, lakini mimi naomba niendelee na *career* yangu. Kwa hiyo, itakuwa hivyo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya awali kwa Watumishi yanafanyika sana. Ni kweli kwamba Chuo cha Utumishi wa Umma hakija-*loose focus* ila kimeongeza zaidi, lakini zimeongezeka Taasisi nyingine zinazosaidiana na Chuo cha Utumishi wa Umma kuwajengea uwezo watumishi wa umma. Vyuo hivyo ni kama Chuo cha *NDC,*

kinafanya kazi hiyo, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo kinafanya kazi hiyo, Chuo cha Lushoto cha Mahakama kinafanya kazi hiyo, Chuo cha Uhusiano wa Kimataifa kinafanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, vyuo vimeongezeka siyo kwamba Chuo cha Utumishi wa Umma kimehama katika majukumu yake, vimeongezeka na vinafanya kazi ya kuwajengea uwezo watumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, mambo ni mengi, wenzangu wamenisaidia kuyajibu, yapo mengine ambayo yamepata majibu na mengine kama nilivyosema tutajaribu kuyajibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa liko jambo moja lilisemwa na Mheshimiwa Mpina, ni jambo zito na ukilichukulia kwa wepesi wepesi hivi unaona amezungumza kitu chepesi, lakini Mheshimiwa Mpina amezungumza kitu kizito na lazima tukijibu kama Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mpina anasema, Ilani na utekelezaji wa Serikali haviendani. Anasema pia kuna uvunjaji mkubwa wa sheria bila hatua kuchukuliwa, yaani utawala ambao hauna sheria *(no enforcement)*. Anazungumza kwamba Watanzania wanauawa, kuna wizi wa kutisha, *no separation of powers*, teuzi za ajira bila ushindani. Pia anasema kuna ufisadi na anatoa mifano ya Mradi wa *SGR*, *Nyerere Hydropower,* deni la Taifa halieleweki na viongozi hawaheshimiani.

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani ukaacha kwa sababu yeye ameshaipeleka kwenye mitandao. Sasa ni nchi gani hiyo ambayo ina sifa kama hizi ikabaki *stable* kama ilivyo nchi yetu? Hiyo nchi inaitwa Tanzania, nchi ambayo demokrasia chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan iko kwenye viwango vya juu kuliko wakati mwingine wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyombo vya habari viko huru, Vyama vya Siasa viko huru, vinafanya mikutano inavyotaka na kuandamana wanavyotaka. Wewe unasema nchi hii imevurugika. Unajua anachokisema hapa Mheshimiwa Mpina. Ni kwamba hapa kuna *a failed state.* Anataka kusema kwamba *there is a weak state*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa *weak state* ina *characteristics* zake. Moja ya *characteristic* ni hizi ninazozisema. Nchi ikiwa *failed state,* mipaka yake haidhibitiki, mipaka ya nchi hii niambieni katika ukanda huu kuna mipaka ya nchi inayodhibitika kama ya Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi haichezewi! Niambieni nchi ambayo ni *a failed state* kama kwa maneno haya anayoyasema Mheshimiwa Mpina inaweza ikawa na *GDP* inayokua *consistently* kati ya asilimia saba imeshuka pamoja na *COVID*, pamoja na mdororo wa uchumi wa dunia, lakini haikushuka *below 4.7* wakati kuna nchi zimeenda *negative*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi anayoisema kwamba imeshuka, ni *failed state* inatoa elimu bure kutoka shule ya msingi mpaka sekondari na ukimaliza kupata elimu bure hiyo unaenda kupata mkopo wa Chuo Kikuu. Unasema *it is a failed state*. Nchi anayoizungumza Mheshimiwa Mpina inatekeleza miradi mikubwa kama Mradi wa Mwalimu Nyerere *Hydropower* ambao una-*cost more than six trillion shillings*, mradi ambao hakuna nchi imeweza kuujenga kwa muda mchache kama tulivyojenga Tanzania, wewe unasema *is a failed state! (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi anayoizungumza Mheshimiwa Mpina kwamba imefeli, inaweza kutengeneza Mradi wa *SGR* ambao kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro ni kilometa 300, kutoka Morogoro mpaka Makutupora ni kilometa 422, zimefika 98% katika muda wa miaka chini ya mitano kwa gharama ambayo kilometa moja ni zaidi ya dola 3,000,000. Mradi huu ni mkubwa, nchi nyingine zikitekeleza mradi kama huu zinafilisika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hiyo ambayo unasema *it is a failed state,* inakusanya kodi kati ya shilingi trilioni moja mpaka shilingi trilioni tatu kwa mwezi na inatekeleza miradi yake, unasema *it is a failed state*! Nchi unayoisema imefeli leo *Moody's Credit is a Global Rating Agency* ambayo inaaminika duniani inasema Tanzania ni kati ya nchi ambazo ina uchumi *very stable* na kwamba uchumi wake umekua kwa viwango vyao, kutoka *B.2* mpaka *B.1*. Kwa hiyo, imekuwa *rated* kama ni nchi yenye uchumi unaokua na *stable* katika nchi za *East Africa* zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii imetolewa *Moody's*, tarehe 23 Machi, 2024, mwezi haujapita na kwamba, katika ku-*rate* hizi kwa sababu gani wametu-*rate* katika hii, ni kwamba tuna *diversified economy*, kwamba tuna uchumi ambao umekamata sekta zote na unashirikisha watu wote. Pili, wanasema *we have a strong export*. Tatu, wanasema *stable debt*. Wewe unazungumzia nchi ambayo ipo kwenye *stable debt*, haidaiwi ikapitiliza, nchi yake iko *stable* unasema *is a failed state*!

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme tusijidharau kiasi hicho. Ni dhambi kujidharau. Kama mtu una mambo yako, ni vema ukayazungumza kwa namna nyingine, lakini siyo mambo ya kitaalamu kama haya. Nchi yetu inaheshimika, Rais wetu anaheshimika na ndiyo maana kila anapokwenda duniani wanampa Shahada ya Udaktari. Ni heshima, wanampa zawadi zote za kubeba, wanaona hazifai, mpaka wanaamua kumpa zawadi ya kichwani. *This global appreciation to a Woman President,* haiwezekani ikadharauliwa na sisi wenyewe ndani ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tujenge tabia ya kujiamini na kuheshimiana. Huwezi ukaizungumzia *a failed State* halafu ukasema unamheshimu huyo Rais anayeongoza hiyo nchi. Hii ni *insubordination*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kuomba sana kwamba ni lazima nchi yetu katika kipindi hiki cha changamoto kubwa duniani, *COVID-19* imepiga, uchumi unadorora duniani, tunatekeleza miradi kila mahali. Mfano, miradi ya afya, miradi ya elimu kule Meatu kwake, *TARURA* wamepeleka pesa, *SEQUIP* wamepeleka shule mbili mpya kwa Mheshimiwa Mpina, *BOOST* wamempelekea madarasa chungu nzima, kapokea *ambulance* moja katika kituo cha afya kimoja. *You say this is a failed state?* Hapana! Nadhani pengine kuna *agenda*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, inaomba Waheshimiwa Wabunge waniidhinishie mimi na wenzangu katika Wizara yangu tukasimamie kiasi cha shilingi 1,101,069,467,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 4 – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*............................................Sh. 1,759,885,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*........................Sh. 210,520,000
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*..............................................Sh. 132,374,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaingia kwenye *guillotine*.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 4 – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*..........................................Sh. 1,759,885,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…...................Sh. 210,520,000

Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*……..............…….…..…..Sh. 132,374,000
Kifungu 1004 – *Information and Communication Technology Unit*……..............…….…..…..Sh. 245,600,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*……..............…….…..…..Sh. 108,774,000
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*……..............…….…..…..Sh. 68,780,000
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*……..............…….…..…..Sh. 99,140,000
Kifungu 4001 – *Archive Management Division*……..............…….…..…..Sh. 442,287,000
Kifungu 4002 – *Records Center Division*……..............…….…..…..Sh. 0
Kifungu 4003 – *Records Management Division*……..............…….…..…..Sh. 783,987,000
Kifungu 4004 – *Founders of the Nation, Presidential Libraries and Museum Division*...................Sh. 213,666,000
Kifungu 1004 – *Information and Communication Technology Unit*……..............…….…..…..Sh. 245,600,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*……..............…….…..…..Sh. 108,774,000
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*……..............…….…..…..Sh. 68,780,000
Kifungu 1008 – *Procurement Management Unit*……..............…….…..…..Sh. 99,140,000
Kifungu 4001 – *Archive Management Division*……..............…….…..…..Sh. 442,287,000
Kifungu 4002 – *Records Center Division*……..............…….…..…..Sh. 0
Kifungu 4003 – *Records Management Division*……..............…….…..…..Sh. 783,987,000
Kifungu 4004 – *Founders of the Nation, Presidential Libraries And Museum Division*..................Sh. 213,666,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 20 – Ofisi ya Rais, Ikulu**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.......................................Sh. 33,544,557,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.......................................Sh. 794,575,979,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*........................Sh. 843,086,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Coordination Division*...............................Sh. 1,148,382,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*.......................................Sh. 679,017,000
Kifungu 1005 – *Information and Communication Technology Unit*..........................................Sh. 529,173,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*………………….........................................Sh. 750,838,000
Kifungu 2001 – *Cabinet Secretariat*................................Sh. 3,671,686,000
Kifungu 2002 – *Government Communication*..................Sh. 381,840,000
Kifungu 2003 – *Good Governance and Reforms Coordination Division*...............................Sh. 1,218,018,000
Kifungu 2004 – *Public Service Administration and Complaints Division*...................................Sh. 1,230,344,000
Kifungu 2005 – *Monitoring and Evaluation Unit*…………….........................................Sh. 648,276,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 32 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*..........................................Sh. 25,496,756,432
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*........................Sh. 628,820,700
Kifungu 1003 – *Government Communication Unit*…...........................….Sh. 350,334,700
Kifungu 1004 – *Procurement Management Unit*………........................…........................Sh. 427,833,500
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*.........................................Sh. 283,276,500
Kifungu 1006 – *Planning Division*..........................................Sh. 902,542,500
Kifungu 1007 – *Legal Service Unit*........................................Sh. 381,805,500
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*..............................................................Sh. 633,931,008

Kifungu 2001 – *Policy Development Division*..................Sh. 2,281,100,600
Kifungu 2002 – *Management Services Division*..................Sh. 921,583,500
Kifungu 2003 – *Establishment Division*..................Sh. 1,543,469,000
Kifungu 2004 – *Ethic Promotion Division*..................Sh. 668,346,000
Kifungu 2005 – *Human Capital Division*..................Sh. 1,579,761,000
Kifungu 2006 – *Performance Contracting*..................Sh. 595,291,000
Kifungu 3001 – *Human Resource Development Division*..................Sh. 9,648,130,000
Kifungu 3004 – *Division of Salary and Remuneration*..................Sh. 838,266,000
Kifungu 4002 – *Management Information System Division*..................Sh. 1,072,821,060

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*..................Sh. 2,268,139,972
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*..................Sh. 458,210,440
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*..................Sh. 606,322,500
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*..................Sh. 313,157,800
Kifungu 1005 – *Procurement and Management Unit*..................Sh. 314,364,900
Kifungu 1006 – *Internal Audit Uni*..................Sh. 412,034,000
Kifungu 1007 – *Information and Communication Technology Unit*..................Sh. 612,487,028
Kifungu 1008 – *Legal Services Unit*..................Sh. 350,681,200
Kifungu 2001 – *Public Leaders Ethics Enforcement Division*..................Sh.803,408,200
Kifungu 2002 – *Public Leaders Ethics Promotion Division*..................Sh. 659,788,000
Kifungu 2004 – *Zonal Office – Northern Zone*..................Sh. 510,221,000
Kifungu 2005 – *Zonal Office – Southern Zone*..................Sh. 442,215,800
Kifungu 2006 – *Zonal Office – Central Zone*..................Sh. 580,802,000

Kifungu 2007 – *Zonal Office – Eastern Zone*......................Sh. 627,784,160
Kifungu 2008 – *Zonal Office – Southern Highlands*..........................................Sh. 652,698,000
Kifungu 2009 – *Zonal Office – Lake Zone*..........................Sh. 610,767,000
Kifungu 2010 – *Zonal Office – Western Zone*......................Sh. 483,764,000
Kifungu 2011 – *Zonal Office – Dar-es-Salaam*.....................Sh. 935,804,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 67 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.........................................Sh. 3,861,721,475
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*......................Sh. 538,254,800
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*.........................................Sh. 595,575,000
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*..................................................Sh. 333,336,000
Kifungu 1005 – *Legal Services Unit*..................................Sh. 296,973,340
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*..................................................Sh. 331,078,485
Kifungu 1007 – *Management Information Systems Unit*.........................................Sh. 938,453,000
Kifungu 1008 – *Internal Audit Unit*..................................Sh. 293,715,000
Kifungu 2001 – *Recruitment Management Unit*..............................................Sh. 1,961,332,900
Kifungu 2002 – *Quality Control*...................................Sh. 1,681,391,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*........................................Sh. 3,778,097,027
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.....................Sh. 310,649,784
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*...............................Sh. 633,058,541

Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*…………..................…....Sh. 193,471,270
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*………………………….............….....Sh. 155,642,270
Kifungu 1006 – *Legal Services Unit*…...............................Sh. 341,299,541
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*………………….............................Sh. 284,318,008
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*……………….................Sh. 236,514,270
Kifungu 1009 – *Guidelines Formulation, Dissemination and Research*...................….Sh. 414,642,770
Kifungu 2006 – *Appeals and Complains Department*..............................................Sh. 1,188,187,679
Kifungu 2007 – *HR Standards and Compliance Department*.....................................Sh. 1,204,831,840

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 4 – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa**

Kifungu 4001 – *Archive Management Division*...................Sh. 295,764,000
Kifungu 4002 – *Records Center Division*…..........................................…....Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*…...................Sh. 163,609,084,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## Fungu 32 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*...........................Sh. 2,500,000,000
Kifungu 1006 – *Planning Division*………..................………Sh. 2,757,750,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*……………………..................................Sh. 112,974,000
Kifungu 2001 – *Policy Development Division*………...……….........................……Sh. 3,190,200,000
Kifungu 2004 – *Ethic Promotion Division*…...............................…Sh. 0
Kifungu 2005 – *Human Capital Division*...............................................Sh. 0
Kifungu 2006 – *Performance Contracting*..........................................Sh. 0
Kifungu 3001 – *Human Resource Development Division*…..........................…....Sh. 1,500,000,000
Kifungu 4002 – *Management Information System Division*……….......................................….....……Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

## Fungu 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*..........................Sh. 1,480,000,000
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*….......................................…..Sh. 20,000,000
Kifungu 1007 – *Information and Communication Technology Unit*..........................................................Sh. 0
Kifungu 1008 – *Legal Services Unit*…....................................................Sh. 0

Kifungu 2001 – *Public Leaders Ethics Enforcement Division*.....................................................Sh. 0
Kifungu 2002 – *Public Leaders Ethics Promotion Division*……...................................................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 67 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**

Kifungu 1007 – *Management Information Systems Unit*…….........................................Sh. 2,348,047,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**Fungu 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma**

Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*…….................……......Sh. 500,176,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi zake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Mtoa hoja taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 ninaomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Sasa naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Yalipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Wote wameafiki. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wako pamoja na timu ya Katibu Mkuu na taasisi zote ambazo ziko chini yako hongereni sana. Kwa kweli mmefanya kazi vizuri chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais, Waziri Mkuu, Makamu wa Rais na Naibu Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri, *winding statements* zako umeonesha dhahiri umahiri wako kwa kujua umuhimu na utaifa wako kwa nchi yetu. Umesema maneno ya ukweli, yaliyonyooka ya namna Rais Samia anavyofanya kazi na anavyolipenda Taifa lake. Sasa kama kuna mtu mwingine anakuwa na hisia nyingine, hayo ni maradhi yake, hatuwezi kumwingilia na matatizo ambayo anayo yeye mwenyewe. Kwa hiyo, mimi ninakupongeza sana. *(Makofi)*

Pia ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa michango mizuri na Serikali imekubali, imeipokea na kwa kweli yatafanyiwa kazi na tuna uhakika kwa kipindi kifupi tu majibu mazuri yatatoka na mtaona mapendekezo yenu na maoni yenu yanavyokuwa *accommodated* na Serikali na kufanyiwa kazi vizuri sana.

Waheshimiwa Wabunge, ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 01.43 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 22 Aprili, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*